ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake

37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini

59.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

61.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

66.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

67.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

70.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

72.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Saba – Tarehe 24 Juni, 2013

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mahmoud Muhammed Mussa) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa mwaka 2013/2014. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mezani Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa mwaka 2013/2014. Naomba kuwasilisha.

TAARIFA YA MWENYEKITI

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kuna taarifa hapa kwamba yale mashindano yetu yanayoendelea ya Kombe la Mabenki na Taasisi za Fedha, jana yaliendelea na matokeo yalikuwa kama hivi ifuatavyo.

Baraza la Wawakilishi Sport Club ililicheza mchezo wake na Timu ya *ZSSF*, matokeo Baraza la Wawakilishi 2 na *ZSSF* 0 na wafungaji wetu kama kawaida alikuwa ni Mhe. Ussi Jecha Simai Mwakilishi wa Jimbo la Chaani pamoja na Mwanasheria wetu Khamis Hamad Haji. Naomba tuipongeze sana *Baraza la Wawakilishi Sport Club* kwa ushindi huo wa jana. *(Vicheko/Makofi)*

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 75

Posho Maalum kwa Vikosi vya SMZ

Mhe. Salim Abdalla Hamad (Kny. Mhe. Saleh Nassor Juma) – Aliuliza:-

Vikosi vya SMZ kwa maana ya JKU, KMKM pamoja na KVZ vimeanzishwa kisheria na vinasaidiana na Jeshi la Polisi katika kuimarisha ulinzi na usalama hapa nchini.

Kwa kuwa vijana wetu hawa kwa bidii kubwa, maana saa 24 wanaonekana wakilinda majengo ya serikali, majumba ya viongozi wetu usiku na mchana bila kujali muda, vifaa wala kipato. Kwa kuwa vikosi vingi vya ulinzi hata vile vya watu binafsi hulipa posho maalum kwa ajili ya ulinzi wa usiku (*night allowance*).

(a) Je, vikosi vyetu vya SMZ wanalipwa '*special allowance*' wanapoingia kazini usiku.

(b) Kama hawalipwi ni sababu gani za msingi.

(c) Kwa kuwa taasisi nyengine za ulinzi zinatoa posho hilo, kama SMZ haitoi si kuwarudisha nyuma vijana wetu hao.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 75 lenye sehemu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Watumishi wa Idara Maalum za SMZ kwa sasa hawalipwi posho maalum wanapoingia kazini usiku. Ulinzi kama mchana au usiku ndio kazi yao ya msingi. Hata hivyo, kwa wale Maaskari na Wapiganaji wote wanapoingia zamu ya usiku basi huwa wanakula chakula kambini, yaani wapiganaji wote wanaokuwa kazini wakati wa usiku wanapatiwa chakula kamili.

(b) Posho maalum kwa wapiganaji wanaoingia kazini wakati wa usiku halikuainishwa kati ya maposho ambayo yaliyotajwa katika Kanuni za Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ kufuatana na Sheria ya mwaka 2007. Aidha, mikataba ya ajira ya maaskari na wapiganaji

wa Idara Maalum za SMZ inawataka askari hao wawepo kazini wakati wote masaa 24.

(c) Serikali haina dhamira ya kuwakatisha tamaa au kuwarejesha nyuma askari wa Idara Maalum za SMZ. Nia ya kuboresha maposho mbali mbali yaliyopo sasa ipo, utekelezaji wa nia hiyo utafanywa kila hali ya kifedha itakaporuhusu kwa mujibu wa taratibu.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana aliyoyatoa Mhe. Waziri naomba nimuulize swali dogo sana la nyongeza.

Kwa kuwa wizara nyengine kwa mfano Wizara ya Afya wanapewa *night allowance* kwa madaktari au *call allowance*. Vile vile Wizara ya Afya Mhe. Waziri wanatoa *radiation allowance* kwa wale wanaofanya kazi katika mambo ya mionzi. Sasa kwa kuwa hawa vijana wetu wa JKU, KVZ pamoja na KMKM wanafanya kazi nzuri sana za ulinzi na hasa wakati wa usiku ni ku-*risk*.

(a) Kwa nini Mhe. Waziri ashindwe kutoa posho hili wakati vijana wetu wanapolinda usiku wana-*risk* na Wizara ya Afya waweze kutoa *risk allowance* kwenye *radiation allowance* na Mhe. Waziri ashindwe kutoa hii inayoitwa "*mbu allowance"* hii ya usiku.

(b) Kwa kuwa Jeshi la Polisi wanalipwa hizi *night allowance* wanapoingia kwenye *guard* za usiku. Pia kwa kuwa roho zimeumbwa na choyo, haoni kwamba Mhe. Waziri wakati wenzao wanalipwa hawa na wasipolipwa ni kuwarudisha nyuma wapiganaji wetu wa Vikosi vya SMZ. *(Vicheko/Makofi).*

Mhe. Waziri wa Nchi, **(OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:** Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme kwamba si muasisi tu isipokuwa nieleze ni mkereketwa. Mhe. Mwenyekiti, *nurse* ni muuguzaji na yule mwengine tumesema ni daktari, kwa hivyo kazi yao ni uguzaji na udaktari, kwa hivyo kuna *risks* za maisha yao na ninakubaliana na Mhe. Mjumbe kama alivyosema, yaani kwa *nature* ya kazi zao wameekewa hizo *risks allowance*.

Lakini kama nilivyosema kwa hawa maaskari kazi yao wao ni walinzi ndio *nature* ya kazi yao, yaani ulinzi na hiyo ndio nature ya kazi yao kwa sababu yule kazi yake ni *nurse* au daktari na huyu *nature* ya kazi yake ni mlinzi.

Sasa nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba kweli iko haja tuboreshe maslahi yao, yaani maslahi yao yawe mazuri zaidi kwa *nature* ya kazi yao ya ulinzi ambayo kweli inahatarisha na maisha yao. Kwa hivyo, hilo

tunalichukua Mhe. Mwakilishi na tutazidi kulifanyia kazi kama nilivyosema kwa mujibu wa hali itakavyoruhusu.

Mhe. Mwenyekiti, nimejaribu kufuatilia kwa Tanzania Bara na nimejuilishwa kwamba hata wao labda wanapokuwa kwenye *operation* maalum za kivita kule ndiko kunakuwa na posho maalum, lakini kwa kazi za kawaida nao pia hakuna posho maalum ya ulinzi.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza baada ya majibu mazuri sana. Kwa kweli hivi vikosi ni vya serikali na wakati mwengine wanalipwa na watu binafsi katika shughuli zao.

Je, kuna makubaliano gani baina ya watu binafsi na serikali katika kuwatoa watu hawa wafanyakazi wa serikali kwenda kulinda kwa watu binafsi na kama kwa bahati mbaya ikitokea majanga huwa ni nani ambaye anahusika, yaani kama kuna kupewa fidia itakuwa ni yule tajiri kwa sababu tukio lilitokea kwenye sehemu yake au serikali iliyotoa watu wake kupeleka kwa wale matajiri kwa kazi za watu binafsi.

Mhe. Waziri wa Nchi, **Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:** Mhe. Mwenyekiti, kama maaskari wale wameingia mkataba na kampuni binafsi au watu binafsi walioingia mkataba ni kampuni na vikosi sio na mtu binafsi. Kwa hivyo, kama kutatokea chochote basi dhamana ni kikosi chenyewe na wale ndio walioingia mkataba na wakawapeleka kule kwa ajili ya kwenda kufanyakazi. Mhe. Mwenyekiti, sijui kama nimelijibu na lile swali la (b) au vipi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, rudia tena swali lako la (b).

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, swali lilikuwa ni hilo hilo, isipokuwa amelijibu vibaya tu naomba nilirudie tena.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema kwamba vikosi hivi ni vya serikali na vinachukuliwa na taasisi binafsi kwa kazi ya ulinzi tena usiku. Lakini kwa bahati mbaya likitokea lolote hawa askari wetu wakapata matatizo, anayehusika na kuwashughulikia baada ya haya yanayowafika ni ile taasisi waliokodi au bado ni serikali yenyewe na jengine lilikuwa kuna mikataba yoyote kwa taasisi hii ya serikali kwenda kufanya kazi kwa taasisi binafsi. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, **Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:** Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba ile taasisi au mtu

binafsi wameingia mkataba na vikosi vya serikali ndio iliyoingia mkataba naye kwa ajili ya kumfanyia kazi.

Kwa hivyo, dhamana yote au matokeo yoyote kama fidia basi dhamana ni ile taasisi ya serikali kwa lolote lile litakalotokea. Lakini wakati mwengine kunakuwa na maelewano mazuri kama vile kusaidia yule anayefanyiwa kazi huchangia lakini dhamana ni ya taasisi ya serikali ndiyo yenye mkataba wa yule askari aliyekwenda kulinda pale.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza hili miaka yote hupitisha fedha nyingi sana kwa ajili ya maslahi ya askari wetu wa Vikosi vya SMZ ikiwemo mishahara na maposho mbali mbali. Lakini kadri Wawakilishi wanapozunguruka wamekuwa wakipata malalamiko ya maslahi ya vikosi vyetu kwamba ni madogo na haya uwazi, yaani askari anapodai taarifa ya fedha ndani ya idara au ofisi ya mhasibu hapati maelezo ya kina ya uwazi kwa maslahi yake.

(a) Je, Mhe. Waziri atuambie ni lini sasa ataweka utaratibu wa wazi wa askari wetu wa vikosi ili wanapodai taarifa ya fedha za maslahi yao isiwe ni adhabu kwa askari wetu.

(b) Tumegundua kwamba kuna askari wa mafunzo wanafanya kazi za ujenzi wa Gereza la Hanyegwa Mchana na wametengewa shilingi 1500/= kama ni posho la nauli ni sawa na shilingi 50 ya Tanzania kwa siku. Je, hivi si kuwadhalilisha askari wetu. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, **Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:** Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba baadhi ya vijana au maaskari wetu wamekuwa na manung'uniko na nimefanya ziara mimi katika vikosi kadhaa na nikizunguka huwa ninajaribu kukutana na *private* wale bila maofisa na hilo wamelizungumza ni kweli.

Lakini fursa ipo wazi, yaani ule uwazi aliousema Mhe. Mwakilishi upo na tumewaagiza yeyote yule, kwa sababu tumeona kidogo ni vigumu kuchapishwa ile *salary slip* kwa wote si chini ya *volumes* za makaratasi kama 70 kila mwezi.

Sasa ile mishahara inayotengenezwa kwenye Kalamazuu zao ndani ya vikosi vyao na kila mmoja na tumewaagiza sana Maafisa Utumishi wale wa Vikosi wawape, yaani kila askari apewe ajuilishwe, kwa sababu mshahara wote

unapoelekwa benki kwa ajili ya wanaopokelea benki wawajuilishe na kila mwenye *querry* yoyote ni ruhusa aulize. Mhe. Mwenyekiti, tatizo hilo halipo.

Kwa kweli jambo liliopo ni kwamba baadhi ya maaskari wanakopa vitu vingi, yaani wanakopa sehemu nyingi kwa hiyo kidogo wanasahau zile hesabu zenyewe walizokopa zinawatinga. Sasa kwa upande huo huwa kidogo hawauoni sana. Mhe. Mwenyekiti, nataka kumhakikishia Mhe. Mjumbe kwamba ukweli na uwazi upo na tutajitahidi kuzidi kuwaelimisha maaskari wetu.

Mhe. Mwenyekiti, sijui kama nimemjibu vizuri pamoja na swali (b) na kama bado naomba areje swali lake la (b).

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, swali la (b) ni kwamba askari wa Kikosi cha Mafunzo ambao wamepangiwa kazi ya kujenga Gereza la Hanyegwa Mchana na wamepangiwa posho la shilingi 1500/= kwa mwezi sawa na shilingi 50 ya Tanzania kama nauli ya kutoka mjini hadi Hanyegwa Mchana na hiyo si kuwadhalilisha askari wetu.

Mhe. Waziri wa Nchi, **Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:** Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu swali hili ni *very specific*, basi naomba nilichukue na nikalifanyie kazi nipate ukweli wake na halafu nitakuja kumjibu Mhe. Mwakilishi. *(Makofi)*

Nam. 39

Ununuzi wa Meli Mpya ya Abiria

Mhe. Salim Abdalla Hamad – Aliuliza:-

Serikali kwa makusudi iliazimia kuwaondelea usumbufu wananchi katika suala zima la usafiri wa baharini kwa kununua meli mpya. Serikali ilipunguza kiasi fulani cha fedha kutoka kila wizara.

(a) Ni kiasi gani cha fedha kilichopatikana na kiasi gani kilichohitajika kugharamia meli hiyo.

(b) Fedha ya ziada kama ilihitajika ilikuwa kiasi gani na ilipatikana kutoka wapi.

(c) Meli hiyo inatarajiwa kufika lini hapa Zanzibar.

Mhe.Waziri wa Nchi, (OR), Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa na ruhusa yako kabla ya kujibu swali la Mhe. Mwakilishi lenye vifungu (a), (b) na (c) naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kweli kuwa serikali imo katika jitihada za kununua meli mpya ya abiria na mizigo, kwa lengo la kuhakikisha usalama wa usafiri kwa wananchi na mali zao, kwa kuzingatia kuwa nchi yetu ni visiwa na usafiri huo ndio unaotumiwa na wananchi wetu wengi.

Maandalizi juu ya ununuzi wa meli mpya mnamo mwezi wa Julai mwaka 2012 yalitolewa maelekezo na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein, kuwa meli hiyo iwe ya kubeba abiria wasiopungua 1200 na ichukue tani 200 za mizigo.

Ili kutimiza azma hiyo, serikali iliamua kutenga fedha kutoka kwenye bajeti yake ya mwaka 2012/2013 kwa ajili ya kuanza hatua za ununuzi wa meli hiyo. Mhe. Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuwashukuru wataalamu wetu wa ndani kwa kufanikisha zoezi la kuandaa *specifications* ambazo zimeweza kusaidia sana kutambua aina ya meli tunayoitaka.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

a) Kiasi cha fedha kilichotengwa katika bajeti ya mwaka 2012/2013 ni shilingi 17.166 billioni na fedha zote hizo zitatumika kama kitangulizi (*advance payment*). Kwa ujumla meli mpya itakayopakia abiria 1200 inatarajiwa kugharimu dola za Kimarekani 30.4 milioni sawa na shilingi 48.6 bilioni.

b) Kwa kuzingatia kiasi cha kitangulizi, fedha za ziada ni shilingi 31.4 billioni na zinapatikana kupitia Bajeti ya Serikali. *(Makofi)*

c) Ujenzi wa meli unatarajiwa kuchukua si zaidi ya miezi 24 na hivyo meli hiyo inatakrajiwa kuwasili nchini kabla ya mwezi Juni mwaka 2015.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Kwa kuwa azma ya kununua meli ya serikali ipo na kwa kuwa meli hii ilisababishwa na matokeo yaliyotokea ya kupata ajali mara kwa mara na tukailaumu serikali, kwa sababu Zanzibar ni visiwa na kutakuwa na meli madhubuti ya serikali.

Vile vile serikali iliitikia wito huo na ikakubali lakini Mhe. Mwenyekiti, huu ni mwaka wa tatu tangu kutokea matokeo hayo na Mhe. Waziri anatuambia meli inatarajiwa kupatikana Juni mwaka 2015.

Je, Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa gharama za meli zinajulikana na idadi ya fedha amesema, sasa kucheleweshe mpaka mwaka 2015 wakati gharama za maisha kila siku zinapanda hawaoni kwamba hizo fedha walizozitenga baadae zitazidi.

Je, kwa kuwa mpaka hivi sasa hiyo saini yenyewe bado haijatiwa ni lini hasa wananchi wa Zanzibar watarajie kupata meli ya serikali. *(Makofi)*

Mhe.Waziri wa Nchi, (OR), Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimhakikishie tukimaliza kutiliana saini hata kama gharama zitapanda zitakuwa ni kwa upande wa kampuni sio kwa upande wa serikali. Sisi wajibu wetu kulipa zile fedha zitakazokuwemo ndani ya mkataba na kama nilivyoeleza makubaliano yetu ya awali ni kusaini meli yenye gharama ya dola 30.4 milioni.

Kwa hivyo, katika hilo asiwe na wasi wasi kwetu sisi gharama hazitopanda tena na wakicheleweshe ujenzi katika kipindi hicho itakuwa ni kwa gharama zao na wao itawapasa kutulipa sisi kwa kucheleweshe.

Pili nataka nimhakikishie Mhe. Mjumbe pamoja na Waheshimiwa Wawakilishi wote kwa jumla, moja katika kipengele tulichokiweka ndani ya mkataba nataka nimhakikishie meli hiyo inajengwa Korea na kipengele chetu ni kwamba kabla ya kusaini tukaone *shipyard* ambayo itakayojengwa meli hiyo na wenzetu wanazo *shipyard* na lazima kwenye makubaliano museme munataka ijengwe kwenye *shipyard* hii.

Timu ya wataalamu inatarajia kuondoka tarehe 28 mwezi huu na baada ya kukamilisha taratibu zote za kuona *shipyard* zote walizonazo na kuteua *shipyard* moja, basi saini itatiwa na hatimaye ujenzi utaanza.

Mhe. Mwenyekiti, ni matarajio yetu kwa mujibu wa program ilivyopangwa matarajio ya saini yatafanyika tarehe 7 Julai.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na ninaomba nimuulize kaka yangu mpenzi Mhe. Waziri wa Fedha swali la nyongeza kama ifuatavyo.
Kwa kuwa bajeti ya mwaka jana serikali ilitamka wazi kwamba meli hiyo itajengwa si zaidi ya miezi 18 na fedha ikatengwa kupitia vifungu mbali mbali

ndani ya wizara tofauti. Vile vile hivi sasa inaonekana itazidi mieizi 18 na itakuwa ni miezi 24.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Wazanzibari kupitia Wawakilishi wao hawa wamejenga wasi wasi kwamba meli inaweza kufika mwaka 2016. Pia wataalamu wataondoka tarehe 28 mwezi huu kwa ajili ya kuangalia shughuli nzima ya meli.

Hivi kwa nini haoni busara kuwachagua baadhi ya Wawakilishi hasa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi wafuatane na wataalamu kwa ajili ya kwenda kujiridhisha kwamba kweli meli inajengwa, kwa sababu tuliwahi kuambiwa uongo kwamba tayari mkuku umenzishwa jambo ambalo hakuna hata saini, kwa nini hawachaguliwi baadhi ya Wawakilishi wakafuatana pamoja na wataalamu kwa ajili ya kwenda kuona ukweli wa serikali. *(Vicheko/Makofi).*

Mhe.Waziri wa Nchi, (OR), Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, nilieleza mwaka jana kwamba utaratibu wa ujenzi wa meli tuachieni serikali na kama kutakuwa na tatizo lolote litakalotokea sisi Wajumbe wa Baraza lako tukufu tufike pahala tuwahoji serikali, lakini tukianza kuwashirikisha Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika huu mchakato hata wa kwenda kuangalia tu likija kutokezea tatizo nani atakayemuhoji mwenziwe.

Kwa kweli mimi nakubaliana na hoja ya Mhe. Hija lakini sio katika *stage* hii, nadhani tusubiri katika hatua zijazo tunaweza wawili au watatu wakenda wakaichungulia meli jinsi inavyojengwa huko. *(Makofi).*

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa hivi sasa suala la ununuzi wa meli liko katika hatua ya mikataba na serikali yetu hii imekuwa na matatizo makubwa hasa katika maeneo haya ya utiliaji mikataba jambo ambalo huisababishia serikali hasara. Vile vile kuhusu mkataba wa ujenzi wa barabara za Wete Konde serikali inagharamika kulipwa zaidi ya shilingi milioni 10 kwa siku kutokana na mikataba mibovu.

Je, Mhe. Waziri mkataba huu katika hatua ya awali umeweza kumshirikisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali kama sheria iliyopitishwa hapa na Baraza hili tukufu. *(Makofi).*

Mhe.Waziri wa Nchi, (OR), Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nitoe taarifa kwamba Mhe. Rais ameunda Kamati hii ya Kusimamia Ujenzi wa Meli, katika tamko la Mhe. Rais alisema Mwenyekiti atakuwa Waziri anayesimamia Masuala ya Fedha, Mwenyekiti

Mwenza Waziri wa Miundombinu na awemo na Mwanasheria Mkuu wa serikali na hilo ndilo agizo la Mhe. Rais na wataalamu wengine.

Kwa hivyo, kuhusu wataalamu wengine amemuachia Mhe. Waziri ambaye ni mwenyekiti awatafute, tukatafuta *engineers* wa meli na kadhalika. Lakini huyu Mwanasheria tulihakikisha ni Mwanasheria Mkuu ambaye anaingia ndani ya hiyo Kamati. Kwa maana hiyo Mhe. Dokta Salmin mikataba yote, mikataba ya fedha na mikataba ya ujenzi imeandaliwa kwa ushirikiano baina ya kampuni zinazojenga na Mwanasheria Mkuu wetu. Na hivi ninavyokwambia kwamba mkataba ule anao Mwanasheria Mkuu na yeye ataondoka nao kuelekea nao Korea kwa ajili ya saini.

Nam. 26

Ujenzi wa Barabara Wete – Konde na Wete – Gando Kutokamilika.

Mhe. Hassan Hamad Omar – Aliuliza:

Kwa kuwa ujenzi wa barabara ya Wete, Konde na Wete, Gando ni miaka mitatu sasa toka kuanza kwake na mpaka sasa haujakamilika, jambo la kusikitisha ni kuwa utiaji wa lami barabara ya Wete, Konde umesimama kabisa.

(a) Je, ni sababu gani ya msingi iliyopelekea kusimama katika kipindi hiki cha jua kunakosababisha kuchimbika kwa barabara hiyo na kupelekea ujenzi wa mara kwa mara uliotia Serikali hasara.

(b) Je, ni mwaka gani ujenzi wa barabara hizo utakamilika na kuweze kutumika rasmi.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako kabla sijamjibu Mhe. Mwakilishi swali lake naomba kidogo niweke sawa kuhusiana na swali la nyongeza aliloniuliza Mhe. Salmin Awadh kwa sababu swali lilikuwa linahusu huu ujenzi wa barabara ya Wete/Konde na Wete/Gando kama ambavyo nitajibu.

Tatizo lilotokea kama nilivyolieleza sivyo alivyolitoa leo, kwa hivyo nataka niliweke sawa. Tatizo lilotokea kucheleweshe ni kuchelewashwa kulipwa fidia nyumba na mambo mengine yaliyoko katika eneo la ujenzi wa barabara na sio mikataba mibovu. Mikataba ya barabara ya ujenzi wa barabara ni mizima, safi na haina tatizo. Lakini kucheleweshwa kulipwa fidia ndio

kulikosababishwa kucheleweshwa kujenga ile barabara na kulazimisha kampuni kudai fidia ya ziada kwa muda ulioongezeka.

Baada ya hilo Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam 26 lenye kifungua (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, kuchelewa kwa malipo ya fidia ya nyumba, hali hii imesababisha mkandarasi kukosa eneo la kufanyia kazi kwa wakati. Sababu iliyopelekea malipo hayo kuchelewa ni kutokupatikana fedha kwa wakati kutoka Serikalini, hata hivyo fedha iliyokuwa inapatikana ilikuwa haitoshi kulipia fidia za vizuizi vyote vya ujenzi wa barabara kama nyumba na miti.

- Kuchelewa kwa malipo ya mkandarasi kutoka serikalini pamoja na wafadhili. Hali hii imesababishwa na kutokuwepo kwa msimamizi wa ujenzi ambaye kwa mujibu wa mkataba ndiye anayethibnitisha malipo ya mkandarasi kwa kazi aliyoifanya kwa kipindi husika. Wizara ilichukua juhudi ya kumtaka mshauri kurudi Pemba kwa ajili ya kuzihakiki na kuziidhinisha nyaraka za malipo ya mkandarasi. Msimamizi huyo alirudi na kuyathibitisha malipo hayo ambayo kwa sasa yanafanyiwa taratibu za kumlipa mkandarasi. Na kwa taarifa niliyonayo ya jana ni kwamba taratibu hizo zimekamilika na mkandarasi wakati wowote anapewa pesa zake kutoka *BADEA* na kutoka *SAUD FUND*.

- Mhe. Mwenyekiti, mkandarasi aliposimamisha shughuli yake ni kutokana na kutokuwepo kwa Mhandisi Mkaazi kutoka Kampuni ya *J. Burrow* ambaye ndiye anayethibitisha malipo kimkataba na hatimae mkandarasi kulipwa malipo hayo baada ya kufanyakazi. Mnamo mwanzo wa mwezi wa Machi 2013 mkandarasi alitoa kusudio la kusimamisha kazi kwa siku 21 kama mkataba unavyomtaka kufanya, na mwisho mwa mwezi huo huo mkandarasi huyo alitimiza azma yake hiyo na kusimamisha kazi rasmi.

- Hata hivyo wizara ilichukua juhudi ya kumtaka mshauri kurudi Pemba kwa ajili ya kuzihakiki na kuziidhinisha nyaraka za malipo ya mkandarasi. Msimamizi huyo alirudi na kuyathibitisha malipo hayo ambayo na kama nilivyosema taarifa iliyopo sasa ni kwamba *BADEA* wameshatoa malipo hayo na *SAUD FUND* inatangulia.

(b) Mhe. Mwenyekiti, pamoja na matatizo yote yaliyokuwepo imani kubwa ya wizara kwamba kabla ya kumalizika mwaka huu barabara hizo mbili zitakuwa zimekamilika. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Waziri atakubaliana na miye barabara hii imeanza kwa muda mrefu sana na yeye kabla hajawa Waziri alikuwa Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi n mimi nilikuwa mjumbe wake mmoja wapo. Mhe. Waziri alikuwa na *challenges* sana kwa sababu ya barabara ile na akaiona hali yake ni ngumu na mimi nikipita barabara ile naona siku hadi siku inachimbika.

a) Je, kwa sababu barabara hii imechelewa na hatuoni shughuli zile kufanyika je, hamuoni ni kutia serikali hasara.

b) Kwa sababu barabara ile imekuwa ya muda mrefu na kuna tetesi hata wasimamizi walikuwa wanakula madafu kutokana na udhaifu kuwa hawapati pesa. Sasa nataka Waziri atwambie rasmi hapa barabara ile itaanza kazi siku gani na itamaliza lini, kwa sababu muda umepitilia kiasi. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli barabara hizi mbili hasa ile ya Konde imekaa muda mrefu sana lakini kama nilivyoeleza mwanzo matatizo yalikuwa yanatofautiana. La mwanzo ilikuwa ni kuondosha vizuizi yaani kubomoa nyumba na mambo mengine yaliyopo kwenye eneo la ujenzi. Hili lilikuwa ni jukumu la serikali kuwalipa fidia wale ambao wanaohusika.

Fedha zilikuwa zinapatikana kidogo kidogo sana ukilinganisha na ukubwa wa eneo lenyewe. Kama tujuavyo kwamba watu wetu wengi sana wanajenga barabarani au karibu na barabara na barabara zinazojengwa zinatanuliwa. Kwa hivyo ilikuwa hakuna njia isipokuwa kama ambavyo wizara iliamua kwamba haiwezi kuvunja nyumba ya mtu yeyote kabla ya kulipa. Kwa hivyo kutokana na sera hiyo iliyokuwa inakwenda nayo ndio maana baadhi ya maeneo yakachelewa kuvunjwa nyumba na kukosa kumpa mkandarasi eneo la ujenzi hilo ni eneo la mwanzo.

Lakini kwa barabara hizi zilipata bahati mbaya vile vile kwamba kulikuwa na matatizo ya ulipaji kwa baadhi ya wafadhili. Hii ilisababishwa na mambo ya kiofisi huko ambako inatoka hii mikopo na mambo mengineyo. Matatizo haya yalichanganyika na la mwisho kama nilivyosema juzi kwamba mkandarasi kutokana na kuondoka kwa Kampuni ya *PRISMO* na kulazimika yeye kujenga ile barabara aliyoondoka *PRISMO* ikabidi abebe mzigo wa deni ambalo lipo serikalini na hilo amechukulia *advantage* kwamba ni mtaji wake ambao hauna nafasi ya kujitanua kwa sababu kakosa mtaji.

Sasa kwa yote haya yaliyochanganyika Wizara imepiga hatua ya kuyatatua moja baada ya jengine. Suala la ulipaji fidia limekamilika, suala la malipo ya wafadhili au watu wa mkopo wa benki limekamilika, sasa iliyobaki ni mkandarasi kurudi katika *site* baada ya kupewa malipo yake ya mwisho ya bilioni 1.6 na serikali...

UTARATIBU

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mimi nilimuomba Mhe. Waziri ni lini barabara ile itaanza tena na kumalizika, hilo ndio ninalolitaka, hakuna jengine.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, nimemjibu lakini naomba nimjibu tena kwamba kwa imani ya Wizara mambo yanavyokwenda wakati wowote kuanzia mwezi huu tulionao au mwanzo wa mwezi wa Julai mkandarasi atarudi na barabara zinatarajia kukamilika kabla ya mwisho wa mwaka huu 2013. Lakini kwa sababu tuna bajeti yetu tarehe 18 pale ndio tutakuja kutoa hasa kitu gani halisi kitatokea. Kwa sababu katika siku mbili hizi tatu za mwezi, hizi wiki moja au wiki mbili kuna mambo ambayo yanashughulikiwa ili mkandarasi arudi katika *site*.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi nimuulize Mhe. Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Waziri ni kwa nini serikali ikaingia mikataba huku ikijua kwa kusema hivyo bila ya kuwa na fedha za kulipia fidia ni kwenda kinyume na mkataba.

b) Ni kiasi gani cha fedha ambacho serikali imekula hasara ambayo mkandarasi amedai kutokana na kadhia hiyo.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, hamu ya kupata maendeleo na barabara ni sehemu moja ya kiashiria cha maendeleo. Kwa hivyo ukiwa na hamu ya kupata maendeleo unaweza ukapanga mipango yako lakini makisio yanayofanywa katika gharama za kulipa fidia huwa mara nyingi yanapindukia yale makisio ambayo yaliyokuwa yametarajiwa.

Katika kuendeleza hii mikataba na mashirika ya nje ya mikopo kuna wakati maalum ambao wao wanashughulikia. Sasa mkikosana na wao wakati ule mnabidi msubiri tena mwaka mzima kabla hamjenda tena kutia mkataba. Lakini kwa sababu makosa hayo tayari yameshaonekane yamefanyika, nasisitiza tena kusema kwamba mikataba yote na njia zote zinazoanzwa

kujengwa kuanzia sasa hivi fidia itakuwa haichelewi tena. Huo mfano umetolewa kwa njia ya Jendele /Cheju.

Kama nilivyosema kuna njia karibu itajengwa ya Ole/Kengeja. Tutahakikisha kwamba kabla haijatiwa mkataba kupewa yule mjenzi, uwanda ule unatayarishwa na wanalipwa fidia. Hilo mimi nalikiri kwamba kosa lilifanyika lakini wizara imeshasoma.

Ama kima cha hasara kilichoingizwa hii nitaleta kwa maandishi kwa sababu hasara kama nilivyosema zimeingia katika mafungu mawili. Moja ni sisi serikali kuchelewesha kumpa yule mkandarasi eneo lake. Lakini na wale benki kuchelewa kulipa, kwa hivyo hii ni mafungu mawili tofauti na hilo nitalileta kwa maandishi katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi fursa nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa barabara hii ya Konde imechukua muda mkubwa mno kwa kuwa barabara hii ilikuwa na mkataba maalum wa kuanza kujengwa na kumalizika.

a) Ni mara ngapi sasa ameongezewa muda mjenzi wa barabara hiyo baada ya muda wake wa mwanzo.

b) Na kwa kuwa barabara ile Mhe. Waziri anasema ilikuwa ikizuilika kwa sababu ya kuwa kulikuwa na majumba yalikuwa hayajalipwa. Je, Mhe. Waziri haoni kama yeye akiwa kama Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na mimi nikiwa mjumbe wake tumepita zaidi ya mara tatu na tukaona kama barabara yote ya Konde nyumba zilikuwa tayari zimeshaondoshwa.

c) Je, atakubaliana na mimi kwamba wametekeleza barabara yote mpaka kiwango cha kutia lami, mara ya kwanza imeachwa imeharibika, imetengenezwa tena mara ya pili imeachwa imeharibika na hivi sasa inatengenezwa tena mara ya tatu. Je, ni nani atagharamamia gharama hizo ni Kampuni au ni serikali.

d) Na kama mtu hakutimiza ule muda aliyetakiwa wa kujenga je, mkataba ule unakuwa umeshavunjia au unakuwa unaendelea.

Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema katika majibu yangu kwamba makosa ya ucheleweshaji wa barabara zile yalitokana na sehemu nyingi, upande wa serikali lakini na

upande wa wafadhili ambao walitoa mkopo ule wa ucheleweshaji wa malipo. Kwa hivyo kulikuwa na mambo mengi zaidi kuliko vile ilivyofikiriwa.

Lakini kama nilivyosema tena kwamba Wizara imeshasoma kutokana na tatizo lililojitokeza pale katika sehemu nyengine kutotokea tena. Lakini lile hatuna budi twende nalo. Wengine wanasema lisilobudi hutendwa. Sasa tukisema mkandarasi ondoka barabara haitojengwa tena. Kwa hivyo tunakwenda nalo ili tuweze kuhakikisha kwamba kabla ya mwisho wa mwaka huu barabara zile zinakamilika na hilo ndio lengo letu na ndio azma yetu, tukijaaliwa.

UTARATIBU

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nilitaka Mhe. Waziri atwambie ni mara ngapi kishaongezewa muda katika barabara ya Konde mkandarasi.

Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu: Mhe. Mwenyekiti, ni mara ngapi sina uhakika lakini najua hiyo imetokezea zaidi ya mara mbili. Kwa hivyo mimi nitamjibu kwa maandishi. Najua imetokea zaidi ya mara mbili kuongezewa muda lakini uhakika hasa ni mara ngapi sina uhakika, kwa hivyo nitamjibu kwa maandishi.

Nam. 30

Tatizo la Jaa Katika Eneo la Skuli ya Jang'ombe

Mhe. Asha Abdu Haji - Aliuliza:-

Skuli ya Jang'ombe inakabiliana na changamoto ya uvamizi wa maeneo ya skuli na kuwepo kwa jaa ndani ya eneo la skuli, tatizo hilo limekuwa sugu na linahatarisha afya za walimu na wanafunzi.

Skuli ya Jang'ombe inakabiliana na changamoto ya uvamizi wa maeneo ya skuli na kuwepo kwa jaa ndani ya eneo la skuli, tatizo hilo limekuwa sugu na linahatarisha afya za walimu na wanafunzi.

a) Je, Wizara inachukua jitihada gani ya kuliondoa jaa hilo katika maeneo ya skuli.

b) Je, suala la kudhibiti uvamizi wa maeneo ya skuli unashughulikiwa au kusimamiwa vipi.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwenyekiti swali lake Nam. 30 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako kabla ya kumjibu Mheshimiwa naomba kutoa taarifa za nyongeza au za utangulizi kama hivi ifuatavyo:-

Ni kweli ubavuni mwa skuli ya Sekondari ya Jang'ombe kuna jaa la taka ambalo baadhi ya wakati hutoa harufu na kuhatarisha afya za wanafunzi na walimu. Lakini baadhi ya nyakati Baraza la Manispaa au Baraza la Mji huzikusanya na kuzoa taka hizo. Lakini baadhi ya nyakati taka hizo huachwa kwa muda mrefu na zikaanza kuleta uvundo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:-

a) Wizara yangu imefuatilia na imezungumza na Mkurugenzi wa Baraza la Mji la Zanzibar kumtaka kuchukua hatua za kuliondosha au kuliondosha jaa hilo hapo karibu ya Skuli ya Jang'ombe. Kwa bahati mbaya hatua hizo za kuliondosha jaa hilo bado hazijachukuliwa.

b) Pia Wizara yangu ikishirikiana na Kamati ya Skuli na Afisa wa Elimu wa Wilaya pamoja na Mkuu wa Wilaya, tumefanya mazungumzo mara kadhaa kuhakikisha jaa hilo linaondolewa, pamoja na kuzuia uvamizi wa eneo lile la Jang'ombe na maeneo mengine ya skuli. Hivi sasa wizara yangu inachukua juhudi ya kuwasiliana na Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, katika kutupatia hati miliki na sio eneo hilo tu lakini na maeneo mengine ya skuli ili kuondosha tatizo la uvamizi wa maeneo ya skuli.

Mhe. Asha Abdu Haji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali la nyongeza.

a) Kwa kuwa wanaosababisha kuwepo kwa jaa hilo ni Manispaa wa Mji wa Zanzibar.

b) Na kwa kuwa jaa hilo linaleta athari kwa wanafunzi, walimu pamoja na wana kijiji. Je, serikali ipo tayari kufidia gharama za matibabu ambayo athari yoyote itakapotokea.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema taka za jaa hilo zinawekwa pale na wananchi

wanaokaa katika eneo la Jang'ombe iliyoizunguka hiyo skuli. Taka hizo haziwekwi na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Kwa sababu hiyo, kama kutakuwa na utaratibu wa kuwalipa watakaoathirika na afya katika eneo hilo basi hilo ni suala la mtambuka. Tutashirikiana Wizara ya Elimu, Tawala za Mikoa, Mwananchi, Kamati za Skuli, kufanya tathmini hizo na kuwalipa, lakini sioni kama hili litahitajika.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba na mimi nimuulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa skuli huwa zinahitaji mazingira mazuri yenye utulivu na inaonekana ni skuli nyingi ambazo zimeachiwa maeneo yake kuvamiwa na watu wengine.

Je, ni lini serikali italiondoa tatizo hilo kwa kuzijengea skuli hizi uzio ili zibaki katika mazingira mazuri.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, swali hili tumelizungumza mara nyingi na uzio una gharama zake na kuziwekea skuli zote za nchi hii ni gharama kubwa sana. Gharama iliyokuwa rahisi kwanza kuzipatia skuli zetu hati miliki ili tuweze kuzuwia uvamizi kisheria. Maana wakati ule eneo hili la skuli tunazo hati miliki. Tukiweza kufaulu kufanya hivyo tutaweza kuyajengea mazingira mazuri skuli zetu bila ya kugharamika kuweka uzio pale itakapo lazimika na pale ambapo hali yetu ya kifedha itakaporuhusu tutaweka uzio.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu yake mazuri Mhe. Waziri niseme kwa kuwa Baraza lililopita tuliahidiwa kuwa jaa lile litaondolewa. Lakini katika majibu yake mama Mhe. Waziri amesema kwamba atawasiliana na Manispaa ili kuliondoa jaa lile.

Je, Mhe. Waziri huoni hii ni dharau kwa matatizo kwa watoto wetu na afya zao.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nilivyosema sio hivyo alivyosema Mhe. Mwakilishi, nimesema nimeshawasiliana na nimeshawaandikia si mara moja si mara mbili si mara tatu, Baraza la Manispaa kuliondosha jaa hilo. Sio kwamba nitawasiliana, hapana, nimeshawasiliana nao.

Lakini la pili ninalolisema pindi tukipata hatimiliki ya eneo lile kama kuna eneo linahitaji kujengwa uwa au kujengwa eneo la kuzuia uvamizi basi lile ni eneo namba moja ambalo tutalichukulia hatua hizo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali naomba kumjibu Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli tulitoa ahadi ya kuliondosha jaa lile na kama alivyozungumza Mhe. Waziri kwamba ameshamuona Mkurugenzi wa Manispaa mara nyingi tu. Tatizo linalotukwaza ni pakuliweka jaa jengine hilo ndio tatizo litu. Tumehangaika sana, tumeshirikiana na Sheha wa Jang'ombe, atutafutie sehemu nyengine imeshindikana. Sasa juhudi za haraka haraka tunavyojitahidi pale taka zisilale wala zisikae zikitupwa tu tunaondoa, tofauti zamani kwamba zinarundikana, zinakera harufu kwa wanafunzi wetu. Wakati juhudi zinaendelea za kupata sehemu nyengine ya kujenga hilo jaa kwa sababu hata ukiweka kibao Mhe. Mwenyekiti, usitupe taka hapa basi watu habari hawana, hicho kibao watakichukua, watakirembea na wataendelea kutupa taka. Sasa juhudi kama alivyosema Mhe. Waziri tunashirikiana kwa pamoja ili lile jaa tutafute mahali pengine tujenge lile jaa tena kwa muundo mpya. Sasa tunajenga kama banda kubwa hivi tayari tumeshaanza kujenga ambapo inaweza kuingia gari likachukua na likaondoka. Tayari mifano mingi ipo na kazi hiyo imeshaanza na tunaomba sana Waheshimiwa walioiuliza hili swali watusaidie kupata hilo eneo sehemu ya Jang'ombe tuweze kujenga hilo jaa jipya. Hatuna tatizo Mheshimiwa tuko tayari leo kuliondoa. Ahsante.

Nam. 33

Matumizi ya Dawa Feki za *ARVs*

Mhe. Wanu Hafidh Ameir – Aliuliza:

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hivi karibuni iligundua kuwepo kwa *ARVs* bandia ambapo Serikali hiyo iliwasimamisha kazi viongozi wa Idara ya Bohari ya Madawa na kusimamisha kufanya kazi kiwanda cha *Tanzania Pharmoceutical Industry* (*TPI*) kilichopo Arusha kwa kusemekana kutengeneza dawa hizo bandia za kupunguza makali ya ugonjwa wa UKIMWI (ARVs).

(a) Je, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imechukua juhudi gani kuhakikisha kuwa dawa za *ARVs* zinatolewa Zanzibar ni salama na zenye viwango.

(b) Je, ni kwa kiasi gani dawa hizi bandia za *ARVs* ambazo zilitengenezwa Tanzania Bara ziliwaathiri watumiaji wa dawa hizo hapa kwetu Zanzibar.

(c) Ni vituo vingapi Zanzibar vimeruhusika kutoa huduma kwa wagonjwa ambao hutumia dawa hizi za *ARVs*

Mhe. Waziri Afya – Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 33 lenye vifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:

Ni kweli Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iligundua kuwepo kwa *ARVs* bandia zilizotengenezwa na kiwanda cha *Tanzania Pharmaceutical Industry* (TPI) cha Arusha.

Mradi wa Ukimwi ni mradi wa Taifa, kwa hiyo Zanzibar inapata mgao wake wa dawa kutoka ghala kuu la madawa Dar es Salaam ambalo *MSD* pale unapohitaji na kutiwa mahesabu yake katika mradi wa Taifa.

Lilipotokea tatizo la dawa feki za ukimwi, Zanzibar ilikuwa na dawa za kutosha kwa hiyo mkumbo wa dawa hizo haukufika Zanzibar. Kwa kawaida kila mkumbo wa dawa unapotengenezwa unakuwa na namba yake (*betch No*.) Mradi wa Ukimwi Zanzibar umehakisha katika vituo vyake vyote vinavyotoa dawa za kupunguza makali ya ukimwi, pamoja ghala kuu na kwenye buku zake ambako wanarikodi uingiaji na utoaji wa dawa na wakajiridhisha kwamba dawa hizo wao hawana yaani hizo zinazo upungufa. Kwa hiyo hakuna mtumiaji aliyeathirika hapa Zanzibar kwa sababu dawa hizo hazikuwepo.

Vituo vinavotoa dawa za *ARVs* Zanzibar ni 10 na kimoja kimeruhusika kutoa huduma kwa wagonjwa ambao hutumia dawa hizi na kimoja ambacho ni tofauti na vyengine ni kituo cha matibabu ya *TB* na ukimwi pamoja.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti ninamshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nilikuwa naomba kumuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifautavyo:

Kwa hivi sasa ni asilimia ngapi ya wananchi wa Zanzibar walioathirika wanaotumia dawa hizi za *ARVs*.

Pili, je huduma ya *ARVs* inayotokewa inakidhi asilimia ya wagonjwa wanaotumia dawa hizi.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, nilipojibu swali mama nimesema tuna dawa za kutosha kwa wagonjwa wanaopata matatizo hayo. Kwa hivyo hakuna suala la kuwa na asilimia na vituo vinavyotoa dawa hizo ni 10.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Nimetaka kujua ni asilimia ngapi ya wagonjwa wanaotumia dawa hizi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, ninasikitika kwa sasa siwezi kujibu ni asilimia ngapi ya wagonjwa wanaotumia dawa hizo. Kwa sababu mambo haya ni ya siri na kila mgonjwa hutaka ajistiri anapotumia dawa hizi, wengine huwa hawapendi kujidhihirisha. Kwa hivyo huwezi ukasema kwamba hawa ndio hawa sio, wale wanaokuja tunawapatia bila ya matatizo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, Mhe. Mjumbe swali lake alitaka takwimu hataki majina kwamba ni fulani na fulani.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti nakubali, lakini huwezi ukajua ni wangapi wanatumia maana wengine hawaji wala hawataki kujulikana. Kwa hivyo utaipataje asilimia kama wengine huwajui.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii kuuliza swali moja la nyongeza kama hivi ifuatavyo. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba nimuulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa dawa hizi siku nyingi zimetumika, je, kuna utafiti unaonesha kuwa dawa hizi zinaweza kurejesha maisha ya watumiaji. Lakini kama kuna utafiti, utafiti huo ulifanywa mwaka gani.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, ninavyoelewa kwamba dawa hizi hazijatibu kumaliza kuwa mtu kuwa hana ukimwi akawa kapona zinapunguza makali ya ukimwi na mpaka sasa ndio dawa inayoaminika kuwasaidia wagonjwa wa aina hiyo. Sijapata utafiti unaoonesha kuwa dawa hizi zinaponyesha au vipi. Lakini ndizo zinazowasaidia wagonjwa na wengi wanaendelea kuishi kwa kutegemea *ARVs.*

Nam. 4

Gharama za Kuunganisha Umeme kutoka Tanzania Bara

Mhe. Nassor Salim Ali: (Kny:Mhe. Jaku Hashim Ayoub) - Aliuliza:

Kabla swali la Mhe. Jaku Hashim Ayoub kujibiwa naomba nitoe maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo: Kwa niaba ya wananchi wa Zanzibar kwa heshima kubwa na unyenyekevu wa hali ya juu napenda nitoe pongezi sana kwa Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mwakilishi wa Jimbo la Muyuni kwa kile ambacho anakifanya yaani cha kuwatetea wananchi akiwa ndani na nje ya Baraza hili. Kwa hivyo kwa niaba ya Wazanzibari ninampongeza sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub:

Gharama ya kuunganisha umeme kwa Tanzania Bara zimeshuka kutoka shilingi 480,000 hadi shilingi 117,000 lakini kwa upande wa Zanzibar bado bei hiyo haijashuka na inaendelea kuwaumiza wananchi masikini.

(a) Je, ni lini *TANESCO* itaipunguzia bei Shirika la Umeme Zanzibar (*ZECO*) ili liweze kuwapunguzia bei wateja wake ambao wengi wao ni wa kipato cha chini na kuweza kumudu huduma hiyo muhimu.

(b) Katika kupunguza makali ya bei ya huduma ya umeme kwa wananchi ni Serikali kuwa na umeme wake yenyewe; Je, mkakati huu umefikia wapi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 4 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Lakini kabla sijajibu naomba kufanya masahihisho kidogo katika swali lake ni kwamba sio milioni 480 nadhani kategemea 480,000 na 117,000. Kwa hapa kwetu gharama za kuunga umeme ni 365,000 kuanzia mita moja hadi mita 30, *distance* ikiongozeka basi na gharama inapanda. Baada ya hayo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama hivi ifuatavyo.

(a) *Tanesco* huwa inapandisha bei yake ya kuuza umeme kwa *ZECO* kulingana na gharama wanazozipata kutuletea umeme Zanzíbar, hivyo mara zote *TANESCO* wanapotundishia umeme Wizara yangu ikishirikiana na Shirika la Umeme inahakikisha kuwa bei inayotozwa ni gharama halisi ambazo *TANESCO* wanazitoa kutuuzia umeme.

(b) Serikali bado inafuatilia kwa makini sana juu ya suala zima la kuwa na umeme mbadala utakaozalishwa hapa nchini na hatua iliyofikiwa hadi sasa ni matayarisho ya kufanya utafiti yakinifu utakaoweza kubainisha ni njia ipi muafaka itakayoweza kutumika kupata umeme wa uhakika na wenye bei nafuu. Aidha wapo wawekezaji binafsi waliojitokeza kutaka kuzalisha umeme mbadala lakini bei walizopendekeza zimekuwa kubwa sana kuliko tunazonunua kutoka *TANESCO* na hiyo itapelekea mwananchi kutoweza kumudu bei ya umeme.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Ninakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti kunipa fursa nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri kakiri kama bei inayotumika ni bei sahihi kutoka *TANESCO* na *ZECO* inaendesha bei hiyo kwa sababu ya kuwa ndio bei sahihi. Sasa namuuliza

Mhe. Waziri je, haoni kama *TANESCO* wamepunguza bei Bara, kama wamepunguza je na wao hawaoni kama kuna haja ya kuonana na *TANESCO* ili kuwapunguzia mzigo wananchi.

Swali la pili, kwa kuwa serikali inasema suala la kupata umeme Zanzibar wa kujitegemea binafsi yaani wapo katika hatua ya upembuzi yakinifu na suala hili kila siku tunaambiwa kwamba wanafanya upembuzi yakinifu ni lini hasa serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itakusudia kwa dhati kupata umeme wake binafsi bila ya kutegemea umeme kutoka Tanzania Bara.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli *TANESCO* kule wamepunguza bei kama lilivyoulizwa swali lakini pia tutizame na sisi wanavyotuuzia hapa Zanzibar. Nadhani Mheshimiwa anakumbuka kwamba walikuwa wakituuzia umeme kwa bei kubwa sana asilimia 168 ya bei ya ongezeko walikuwa wakituuzia hapa, tumekwenda nao na kuzungumza nao hadi sasa wamekubali kuishusha bei ile na tunashukuru sana kwamba hili limefanikiwa kwa kiasi fulani. Bei hii imewawezesha *ZECO* kupata kama wanachokitumia lakini bado hawajaweza kupata faida. Kazi tunayofanya hivi sasa ni kuhakikisha kwamba wanaodaiwa wote wanalipa madeni yao na hili ni tatizo sugu ambalo tunaendelea kulishughulikia kwamba wanaodaiwa walipe madeni ili *TANESCO* iweze kupata faida katika kuendesha biashara yake.

La pili ni suala la upembuzi yakinifu, suala hili tulikwisha fanya *pre-feasibility study* ya awali ambayo imeshaonesha maeneo ambayo yanaweza yakatumika kwa ajili ya kutuo cha umeme. Lakini hata hivyo sasa hivi tunataka tufanye ile *study* hasa kwa uhakika kujua hasa ni maeneo yepi hasa tunaweza tukayatumia na umeme wa namna gani, wa jua, mawimbi, wa taka hiyo ndio kazi inayoendelea hivi sasa hivi. Sasa kama alikuwa ameambiwa siku nyingi, suala la kufanya *study* ni suala la muda mrefu hasa katika suala la kutafuta umeme wa uhakika lazima litachukua muda.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, nilivyomfahamu Mhe. Waziri ni kuwa wamekubaliana na *TANESCO* katika mambo ya kupunguza bei, lakini kitabu cha bajeti ambacho hivi sasa ndio tunachojadili, ukurasa 61 katika kero za muungano kinasema kuwa, kuna tatizo hili la ongezeko la gharama za umeme kutoka *TANESCO* kwenda *ZECO* ambalo bado limo katika mjadala. Je, makubaliano haya waliokubaliana ni kinyume na utaratibu wa ile Tume iliyopelekwa kule kwa kuondoa kero za muungano.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, hicho kitabu anachokisoma sasa kilipoandikwa bado mjadala haujamalizika juu ya suala hili. Lakini jana tu tumethibitisha kwamba makubalioano haya yamefikiwa kabisa kupunguza bei kutoka asilimia 168.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia na mimi fursa ya mwisho kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti pamoja na gharama kubwa wanazozipata wananchi wa Zanzibar katika kupambana na bei kubwa za umeme, lakini vile vile wananchi hao wanapata hasara kubwa pale *ZECO* wanapounganisha umeme kutoka sehemu moja hadi nyengine kwa kukatiwa matawi yao ya kudumu kama vile miembe, mikaratusi, minazi na kadhalika na kadhalika. Kama ilivyotokea kutoka Darajani pale Vitongoji hadi Makaani ambapo mamilioni ya mali za wananchi zimeathiriwa kutokana na kuunganisha umeme katika eneo hilo.

Je, ni lini serikali itawalipa fidia wakulima wa Vitongoji kuanzia Umangani, Kibokoni, Udusini, Vumba, Uwandani kutokana na kukatiwa mazao yao kwa kuunganisha umeme kutoka pale Darajani mpaka Makaani

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, *TANESCO* wana jitihada kubwa sana ya kuwalipa fidia wananchi wanapopitisha umeme katika maeneo mbali mbali. Suala analozungumza Mheshimiwa ni suala kidogo lina utata, ambao ni vizuri yeye na mimi tukakutana tukapata ufumbuzi zaidi juu ya masuala haya. Kwa sababu kishawahi kuyaleta hata ofisini kwangu suala hili. Kwa hivyo tukutane zaidi tumtambulishe ule utata uliokuwepo kwenye suala hili.

Nam. 5

Mpango Endelevu wa Kuwa na Maji ya Uhakika

Mhe. Saleh Nassor Juma: (Kny. Mhe. Jaku Hashim Ayoub) - Aliuliza:

Licha ya nchi yetu kuwa ya visiwa na kuzungukwa na bahari pande zote pamoja na kuwa na misitu ya asili ya kuvutia mvua za kutosha na vyanzo vya maji, bado hali ya upatikanaji wa maji ya uhakika kwa wananchi imekuwa kitendawili kilichokosa uteguzi licha ya kupata maji. Kama kauli ya “maji ni uhai” ni ya kweli, na tunaisema kutoka ndani ya mioyo yetu na siyo midomoni tu.

(a) Je, kwa nini Serikali imeshindwa kuwa na mpango unaotekelezeka wa kupeleka maji kwa wananchi wa Unguja na Pemba.

(b) Kwa vile tumezungukwa na bahari ni lini Serikali itatafuta utaalamu wa kuyatibu maji chumvi ili yaweze kutumika kama wanavyofanya nchi nyengine duniani.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 5 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, wizara haijashindwa kuwa na mpango unaotekelezeka wa kupeleka maji kwa wananchi wa Unguja na Pemba. Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji inatekeleza kazi zake kwa kufuata Mwelekeo wa 2020 (*Vision 2020*), Malengo ya Maendeleo ya Milenia (*Mellenium Development Goals*), Malengo Makuu ya Mkakati wa Miaka mitano Mamlaka ya Maji Zanzíbar mipango yote hii inayotekelezwa kuhusiana na suala zima la upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama hapa Zanzibar. Hiyo ni mipango madhubuti ambayo Wizara yangu inayo katika kuhakikisha inawapelekea maji wananchi.

(b) Naomba kukubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba ni kweli tumezungukwa na maji ya bahari ila tatizo liliopo ni gharama kubwa ambazo zinagharimu kazi ya ubadilishaji wa maji ya chumvi kuwa maji matamu kama ambavyo nchi nyengine duniani zinafanya na Serikali yetu bado haijaweza kumudu gharama hizo. Hata hivyo naomba kutoa ufafanuzi mbele ya Baraza lako tukufu kwamba Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji ina lengo hilo na tayari imeshafanya jitihada mbali mbali katika kukabiliana na tatizo sugu la maji nchini kwa kufanya upembuzi yakinifu (*Feasibility study*) katika maeneo ambayo maji yake yana kiwango kikubwa cha chumvi.

Vile vile Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji kwa kushirikiana na Serikali ya Ujarumani, Kampuni ya *DON* na *Mork Water Solution* tayari wameshafanya majaribio ya kuyachuja maji ya bahari *(Desalination Process)* katika eneo la Chuo cha Usimamizi wa Fedha Chwaka kwa matumizi ya chuoni hapo na maeneo ya jirani.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti katika Mkoa wa Mjini/Magharibi wananchi wamekuwa na tatizo kubwa la maji safi na salama. Miaka miwili iliyopita serikali chini ya Wizara hii imetumia zaidi ya bilioni 32.5 kwa ajili

ya maji Mjini/Magharibi, lakini bila ya matunda yaliyokusudiwa na bajeti serikali imetenga zaidi ya bilioni 48 kwa ajili ya maji kwa Mkoa huu wa Mjini/ Magharibi. Kwa ujumla Mkoa wa Mjini/Magharibi utakuwa umetumia bilioni 80.5 kwa tatizo la maji. Hebu atwambie zaidi yale maji ambayo yanapatikana kutokana na juhudi za Wabunge na Wawakilishi wa Mjini/Magharibi, na bilioni yenyewe 80 ambazo zimetengwa na serikali kwa miaka miwili, nini matarajio ya Wazanzibari kwa sekta hii ya maji.

Lakini pili, Mhe. Waziri aliwahi kutwambia kwamba utafiti umeonesha kwamba Zanzibar kiwango cha maji kimepungua katika ardhi ya Zanzibar, lakini zipo tafiti ambazo zinaonesha za nyuma kwamba Zanzibar tuna maji mengi katika visiwa vyetu. Hebu atwambie utafiti wa karibu ambao yeye Wizara yake anauamini ni upi, kwamba maji yamepungua katika ardhi au maji bado yapo lakini ni uzembe na kutokuwa makini na Wizara yake.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli katika Mkoa wa Mjini/Magharibi kuna tatizo la maji na tatizo la maji la Mkoa wa Mjini/Magharibi nimeshawahi kulizungumza katika Baraza hili linasababishwa na upungufu wa maji katika chemchem ya Mwanyanya na Mtopepo. Kwa sababu hiyo Wizara hiyo Wizara yangu imechukua hatua ya kuhakikisha kwamba lile pengo la maji yaliyokuwa yakipatikana Mwanyanya na Mtopepo hivi sasa linazibwa kwa kuchimba visima virefu na tumeanza kufanya jitihada hiyo katika eneo lililokuwa lina mitambo ya radio hapo Chumbuni na tumeanza kuchimba visima 3 na tuna lengo la kuchimba visima vitano pale ili kuweza kupata maji kwa ajili ya Mkoa wa Mjini/Magharibi kuweza kutosheleza kwa ajili ya maji. Jitihada hiyo inaendele na kwa wale wanaoishi Mji Mkongwe, wataona kuwa visima 3 ambavyo tayari vipo tatizo la maji Mji Mkongwe halijakwisha kabisa lakini limepungua.
Tatizo la pili katika maji kwenye Mkoa wa Mjini/Magharbi ni suala la uchakavu wa miundombinu. Juzi tu Mhe. Mwenyekiti tumetia saini mradi mwengine wa *IDF* wa kutengeneza mabomba chakavu katika mji wa Unguja ili kupunguza tatizo la maji katika mji wa Unguja.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2012/2013 -Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujaanza kutoa fursa ya kuchangia hadi sasa nina orodha ya wachangiaji 35. Katika watu 35 ni wachangiaji ni 8 tu ambao tayari wamemaliza na shughuli hii tunatakiwa leo

mchana saa 7.00 tuwe tumeimaliza katika upande wa uchangiaji. Lakini pia ningependa kuchukua fursa hii vile vile kuwaomba baadhi yetu watoe michango yao kwa maandishi ili waweze kumpelekea Waziri husika na aweze kuifanyia majumuisho kwa ujumla wetu. tutaendelea na utaratibu wetu na kwa kuanzia tutamkaribisha Omar Ali Shehe, baadae atafuatia na Mhe. Hija Hassan Hija.

Utaratibu

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, Baraza hili lipo kwa mujibu wa Kanuni na Kanuni imeeleza wazi kwamba Baraza hili litajadili bajeti yake kwa mjumbe....

Mhe. Mwenyekiti: Taja kifungu cha Kanuni.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, Kifungu 58 cha Kanuni hoja yangu ni kwamba Kanuni ipo wazi kwamba Wajumbe katika kipindi cha bajeti wachangie bajeti ile kwa dakika ambazo hazipungui 30. Sasa imekuwa ni mazoea ya serikali kila mwaka kwamba Kamati ya Uongozi inaamua kwa mujibu wa kalenda yake. Lakini tukifika humu sasa serikali hutuburura na kuamua wanavyotaka wao. Sasa mimi naomba kwamba utupe fursa tuchangie na usitulazimishe kwamba watu waandike wakati muda upo. Kama muda hapana basi twende hata usiku lakini Wajumbe angalau nusu wafike kuchangia. Leo ukinita mimi na Mhe. Omar watakosa Wajumbe wengi jambo ambalo si sahihi Mhe. Mwenyekiti, naomba uzingatie.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe, Mwenyekiti, kwanza ningependa mjumbe aelewe kwamba sio serikali inaweka muda wa kufanya ratiba ya bajeti ni Baraza lenyewe kutokana na hali ya muda. Kwa hivyo abadilishe usemi wake wa kusema serikali na aseme kwamba ni Baraza ndio limeweka muda huo.

Mhe. Mwenyekiti: Ninafikiria Mhe. Mjumbe tusiendelee na malumbano kilichopo ni kwamba tuna taratibu. Kanuni inatuongoza kwamba muda wa kuchangia ni dakika 30 kwa kila mjumbe katika suala la bajeti. Lakini vile vile katika utaratibu wa kuweza kuchangia katika bajeti za serikali tuna muda maalum wa kufanya kazi na muda ule utakapopindukia hatuna namna nyengine ya kuweza kufanya.

Sasa katika taratibu za kuchangia kuna njia mbili zinaweza kutumika, aidha iwe njia ya kuzungumza au njia ya maandishi yote ni katika michango ya serikali. Lakini kama hilo halitoshi ni wajibu wetu sisi ambao tunataka

kuchangia tuchangie yale maeneo ambayo wenzetu hawajachangia ili na wao waweze kupata nafasi na ili tuwe zaidi katika uchangiaji. Naomba tuendelee.

Utaratibu

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi na kwa sababu muungwana siku zote ni kukubali kosa naomba radhi kwamba sio serikali. Mimi ni mjumbe wa Tume ya Bajeti ya Baraza, Wawakilishi hawa walichagua kwamba tuwapangie bajeti kwa maslahi ya vikao vyao na tumefanya hivyo. Hakuna sababu ya kupunguza muda angalau kwa leo na kuwanyima wajumbe. Serikali wametuwezesha, uwezo upo waachewatu wachangie ili wananchi waone kwamba Wawakilishi wao wanawajibika. Hivi sasa imejengwa picha kwamba Wawakilishi humu ni 7 tu. Mhe. Salmin Awadh, Mhe. Hamza, Mhe. Hija, Mhe. Jussa si utaratibu mzuri, kwa hivyo nadhani Mwenyekiti, tuwape fursa Wajumbe wachangie na kama Wajumbe watasema hawana basi watanyamaza. Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba uzingatie, usichague watu wachache ikaonekana kama hili Baraza ni la watu 7, ni Baraza la wananchi wote wajumbe 82 wapewe fursa na hasa serikali imetuwezesha na wako tayari kusikiliza.

Mhe. Mwenyekiti, naomba utumie busara hiyo, tusibanwe kuchangia na tukiona kwamba muda hautoshi sisi ni waungwana tuko tayari kuwaachia serikali watoe majibu.

Utaratibu

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, lazima tukubaliane kwamba ofisi tatu ni ofisi kubwa sana kwa Zanzibar na ni muhimu sana kwa Wazanzibari na watu wake. Ukiachilia mbali ile ya bajeti ambayo imeshapita lakini tuna Ofisi ya Rais, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Ofisi ya Makamo wa Kwanza hizi ndio Ofisi nyeti na muhimu sana. Na zilitakiwa Ofisi hizi zipate maelekezo, zipate michango kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao ndio mawazo ya wananchi wa nchi hii. Kwa kuwa kuna watu zaidi ya 30 wameomba kuchangia Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ambao wewe unasema hawa haitowezekana kuchangia, mimi nadhani sio kuwatendea haki wananchi wa Zanzibar. Katika hili basi ikiwa suala ni gharama, gharama hii kwa sababu Wazanzibari wanataka kutoa mawazo yao na pesa zinatoka kwa kodi zao basi ongezeni siku.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe majadiliano haya tukiendelea nayo tutakwenda nayo muda mrefu naomba muda tusiutumie katika utaratibu huo tuendelee kuchangia mengine tutafahamiana baadae.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia na kutuwezesha siku ya leo tukaweza kukutana hapa lakini vile vile niitumie fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kuwa ni mchangiaji wa kwanza kwa siku hii ya leo.

Naomba nianze kwa pongezi kwa Makamo wa Pili wa Rais kwa namna anavyosimamia na kutekeleza vyema majukumu yake. Lakini pia naomba nimpongeze Waziri katika Ofisi ya Makamo wa Pili kwa namna anavyomsaidia Makamo wa Pili Rais katika kusimamia na kutekeleza majukumu yake.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara hii kama walivyotangulia wenzangu kwamba ni wizara muhimu sana katika nchi yetu, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ni Wizara muhimu na Wizara nyeti sana katika nchi yetu. Ni wizara muhimu kwa sababu kwanza inaongozwa na mwenyewe Makamo wa Pili wa Rais kwa mujibu wa Katiba yetu ni mshauri mkuu wa Mhe. Rais, lakini Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa mujibu wa Katiba yetu pia ni mtendaji mkuu wa shughuli za serikali katika Baraza la Wawakilishi.

Kwa sababu hizo za uwepo kwa Makamo wa Pili wa Rais katika kuiongoza Wizara hii, lakini vile vile Wizara hii ina majukumu ya kusimamia vyombo muhimu, Wizara hii kwanza inasimamia Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, Wizara hii inasimamia Baraza la Wawakilishi, lakini Wizara hii vile vile inaratibu masuala mazima ya muungano ya Jamhuri ya Muungao wa Tanzania. Juzi nilipata jengine hapa kwamba Wizara hii ndio inayoratibu utekelezajiwa Ilani na kuripoti katika Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo ukichukuwa uwepo wa Makamo wa Pili wa Rais katika kuiongoza Wizara hii na ukichukuwa majukumu yaliyomo ndani ya Wizara hii utabaini kuwa Wizara hii ina umuhimu wa kipekee. Kwa mnasaba huu naomba nianze kwa Tume ya Uchaguzi wa Zanzibar ambayo imezungumzwa katika ukurasa wa 49 katika ripoti ya bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ina jukumu la Kikatiba la kusimamia na kuendesha uchaguzi wa Rais, Madiwani pamoja na Waheshimiwa Wawakilishi. Pia Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ina jukumu la kusajili wapiga kura wapya kila hatua inapofikia.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti ya Tume iliyomaliza muda wake ninaomba kwa ruhusa yako uniruhusu nisome katika ukurasa wa 34 katika kifungu cha 6.4 kinasema matumizi ya kitambulisho cha Wazanzibari wakati wa uandikishaji, naomba kwa ruhusa yako niisome.

"Wakati wa uandikishaji wa mwaka 2009/10 Tume ililazimika kutumia vifungu vya 12(b) cha sheria ya uchaguzi ya 1984 kinachotaka mtu anayeomba kuandikishwa kuonesha kitambulisho cha uzanzibari mkaazi na katika hapa ripoti ya Tume imeeleza changamoto ambapo imesemwa kwamba wajibu wa kisheria wa kuonesha kitambulisho cha MzanzibariMkaazi katika uandikisha umewakosesha, ninaomba nirejee Mhe. Mwenyekiti, wajibu wa kisheria wa kuonesha kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi katika uandikishaji umewakosesha baadhi ya watu wenye sifa kuandikishwa na baadhi ya wapiga kura waliokuwemo katika daftari la 2005 walikosa kurekebishiwa taarifa zao na kushindwa kuonesha kitambulisho hicho".

Hiyo ni taarifa ya Tume ya uchaguzi Mhe. Mwenyekiti kwamba walilalamika kwamba uchaguzi wao uliathirika sana na kwamba kuna watu wengi sana walishindwa kuwa wapiga kura kwa sababu tu ya kukosa ZID. Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, naomba nirudie yale ambayo yalinukuliwa katika rasimu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano imeelezwa kwamba, sasa hivi taifa linafikiria kuwaruhusu Watanzania walioko nje kupiga kura zao wakati wa uchaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, ikiwa sasa hivi wenzetu wanafikiria kuwaruhusu Watanzania walioko nje ili wapige kura wakati wa uchaguzi wakiwa nje, lakini vile vile malalamiko ya Tume ya Uchaguzi iliyopita walilalamika kwamba kuna Wazanzibari wengi walikosa haki yako ya msingi ya kupiga kura kwa sababu ya kutokuwa na kitambulisho. Sasa Mhe. Mwenyekiti, tunapata tatizo hasa katika suala zima la Tume ya Uchaguzi na wakati wa uchaguzi, kwamba tuna watu wengi sana wananyimwa haki zao za kupiga kura kwa sababu ya kutokuwa na kitambulisho. Na sababu hiyo kwa kweli iliwekwa sheria ile inayolazimisha kwamba lazima mtu awe na kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza hili liko kwa sababu moja tu, kazi yake kubwa ni kutunga sheria, lakini vile vile Baraza hili lipo kwa maana na kwa sababu ya kubadili sheria kila hali inapotokea kila wakati. Sasa imeonekana kwamba kuna Wazanzibari wengi sana wanakosa haki yao kimsingi kabisa ya kuchagua kwa sababu ya kutotimiza masharti ya sheria.

Mhe. Mwenyekiti, kinachoonekana kwamba Serikali kwa makusudi haitaki kuleta mabadiliko yanayohusiana kuondosha kipengele hichi. Wakati tunajadili vitambulisho vya Mtanzania vile, Mhe. Waziri anayehusika na Wizara hii tulikuwa katika *interview* moja ya *ZBC* na pale ikaja hoja hii na yeye mwenyewe akathibitisha kwamba karibuni tutakuwa na mabadiliko ya Katiba, mimi nikwamwambia sasa hivi kuja haja ya kubadilisha sheria ili iwape fursa watu waandikishwe kuwa wapiga, minajili kwa sababu tunajua

kwamba watu wetu wengi hasa wa vijijini haya mambo haya ya umuhimu wa vyeti yanaonekana katika siku za karibuni tu, lakini siku za nyuma takriban wazee wetu walikuwa na matatizo makubwa ya kutokutilia maanani. Na hasa tukizingatia kwamba sasa hivi kitambulisho cha Mzanzibari ndio maisha ya sasa, suala la kuhusika kwenye uchaguzi ni kitu kidogo tu. Mhe. Waziri, akaahidi kwamba sheria italetwa Barazani na kipengele hichi kitaondoshwa, mimi nikamwambia minalfaidhina tukifanya hivyo. Lakini bahati mbaya sheria ililetwa katika Baraza bila ya kuweko kwa kipengele hichi.

Mhe. Mwenyekiti, inavyoonesha ni kwamba Serikali haitaki kubadili kipengele hichi ili kuwapa watu haki na fursa ya kuchagua. Tuulize sasa kwa sababu gani, Serikali inakuwa ina *interest* gani kuhakikisha watu hawapigi kura nchi hii, naomba Mhe. Waziri atakapokuja pamoja na majibu mengine lakini hususan aje anijibu kwa nini Serikali inakuwa ina-*interest* ya kuwanyima watu haki ya kupiga kura kwa sababu ya kutokuwa na kitambulisho cha *ZID*, kitu ambacho kinafanywa kwa makusudi. Unapomnyima mtu kitambulisho za *ZID* kwa minajili kwamba asipike kura *interest* yako ni nini au hatima ya watu hawa ni nini tuwapeleke pahala gani, watu hawa ni wa taifa gani, watafutieni watu nchi waende wakakae kwa sababu inaonekana hawa si Wazanzibar watafutieni nchi wakakae na unapomnyima mtu inategemea na yeye achukuwe hatua gani.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sana ninaomba kwa moyo wa dhati Serikali ikae itafakari tena suala hili. Ikiwa leo Jamhuri ya Muungano inafikiria kuwapa watu haki walioko nje ya nchi wapige kura iweje leo tuwe na *shortlist*, maana utaratibu wa sasa inavyoonesha kuwa kunakuwa na *shortlist* ya wapiga kura katika Zanzibar, wengine wawemo wengine wasiwemo, hichi ni kitendo ambacho hakikubaliki na wala hakivumiliki, tuwapeni watu fursa wachague mtu anayemtaka. Kwa hiyo naomba Mhe. Waziri, atakapokuja aje anipe jawabu ni kitu gani na sababu gani zilizopelekea Serikali ikawa haina interest au ina intrest ya kuwanyima baadhi ya watu leo Wazanzibari ni Wazanzibari wazaliwa wa nchi hii unawanyima kwa makusudi kwa sababu ya kuwekwa sheria hii, ni lini Serikali italeta mabadiliko ya sheria kuondosha vipingamizi, kwa sababu mimi naita hivi kama ni vipingamizi vya makusudi na Baraza hili lipo kwa ajili ya kufanya *amendment* ya sheria naomba Mhe. Waziri, atapokuja aje anijibu hilo.

Mhe. Mwenyekiti, katika Tume ya Uchaguzi na katika hili tutalazimika sasa kuleta majina ya watu, kwa sababu ninavyowaambia sasa hivi kuna wameshafikia umri wa miaka 18 kama maamuru ya katiba yalivyo watu hawa wananyimwa kwa sababu tu hawana vitambulisho, kuna watu sasa hivi wameshapiga picha lakini hawapewi vitambulisho, kuna watu sasa hivi wana vyeti vya kuzaliwa, kuna watu sasa hivi wana barua za Sheha lakini hawapewi

vitambulisho, sasa hivi tutaendelea na utaratibu kama huu hadi lini, na wananchi hawa waende wakalalamike wapi, na wananchi hawa waende wakaishi nchi gani na nchi yao waliozaliwa ndio hii, ni mambo ambayo hayakubaliki, hatuwezi tukaendelea tena kuyavumilia mambo kama haya.

Mhe. Mwenyekiti, athari ya mambo kama haya ni kutokea fujo kitu ambacho sisi tunakipinga kwa nguvu zetu zote Zanzibar kutokea fujo hatupendi, tunataka tuishi kwa amani wachia tuendelee kuishi kwa amani, tumechoka na matatizo ya kisiasa katika nchi hii. Naomba niishie na suala la Tume ya Uchaguzi kuomba ufafanuzi wa matumizi ya elfu nne mia tatu na tisini na nne milioni, naomba Mhe. Waziri atakapoja anipe ufafanuzi kwamba kumetengwa bilioni nne mia tatu na tisini na nne kwa ajili ya kuendesha kura ya maoni, SMZ imetenga fedha hizo. Lakini tunavyojua kwamba kura ya maoni ya katiba ya Jamhuri ya Muungano itaendeshwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano, iweje fedha hizi tutenge katika mfuko wa SMZ, ninaomba atakapokuja anipe ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile ninaomba ufafanuzi wa matumizi ya milioni 80 katika kufanya mapitio ya ugawaji wa majimbo, atakapokuja Mhe. Waziri, naomba aje anipe uchanganuzi mapitio ya ugawaji wa majimbo haya mapitio yake yatafanywaje kiasi cha kwamba, kwa sababu ninavyoamini Tume ipo, Sekretarieti ipo, na fungu la uendeshaji wa shughuli zao lipo, sasa hizi milioni 80 zitafanye vipi na vipi na vipi hadi tutenge katika bajeti ya Serikali. Naomba kwa Tume ya Uchaguzi niishie hapo.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Wawakilishi ambalo limetajwa katika ukurasa wa 51. Baraza letu hili la Wawakilishi Mhe. Mwenyekiti, ni moja katika mihimili mitatu ya nchi hii ya dola la Zanzibar, ambapo shughuli yake kubwa iliainishwa katika katiba yetu ya ibara 5 kwamba ni kusimamia shughuli za utendaji wa umma. Sasa Mhe. Mwenyekiti, kadri Baraza litakapokuwa makini na Serikali nayo itakuwa makini, na Baraza lisipokuwa makini na Serikali nayo itakuwa ni goi goi, na Serikali ikiwa ni goi goi maana yake wananchi watafika pahala kwa kweli watavunjika moyo.

Mhe. Mwenyekiti, matokeo katika kipindi cha miaka miwili na nusu yanaonesha kwamba ndani ya Serikali bado kuna matumizi makubwa mabaya ya fedha za umma, katika Serikali inaonekana kwamba kuna kutokuwajibika kwa viongozi pamoja watendaji. Mhe. Mwenyekiti, kilichodhihirika katika kipindi cha karibuni ni kwamba maagizo yanayotokana na Baraza hili Serikali inakataa kuyatekeleza. Kilichodhihirika ni kwamba Baraza letu linaendelea kuporwa mamlaka yake na Serikali, kitu ambacho ni kinyume kabisa na matakwa ya Katiba yetu. Kama nilivyosema mwanzo kwamba Mtendaji Mkuu wa Shughuli za Serikali katika Baraza hili ni Mhe. Makamo wa Pili wa

Rais, ambaye tunaye katika Baraza hili. Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, kama haya yanatokea na yeye yupo, sasa sijui tujiulize kunakuwa kuna mapungufu gani, kwamba kadri ninavyomuelewa Mhe. Balozi Seif Ali Idd, kwanza ni mtu makini sana. Ninaomba nitaje sifa za Mhe. Balozi Seif Ali Idd.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Balozi Seif Ali Idd, ni mtu makini sana, halafu ni mtu mzima, ni mtu ambaye ana uwezo mkubwa sana wa kiutendaji, vile vile ni mwanadiplomasia makini na mahiri na ameiwakilisha Tanzania katika sehemu mbali mbali ulimwenguni. Mhe. Balozi hapendi majungu, Mhe. Balozi hapendi madaraka, hizo ni sifa ambazo ni za Mhe. Balozi. Lakini pamoja na sifa hizi kwa nini kunakuwa na mambo haya, kwa nini maamuzi ya Baraza hili ikiwa pamoja na yeye ni sehemu ya Baraza, Serikali inashindwa kuyatekeleza, kwa nini?. Lakini vile vile kama yeye Mshauri Mkuu wa Rais, kwa nini katika Serikali kuwe na mapungufu makubwa katika suala zima la utendaji kazi.

Ninamuomba Mhe. Balozi kwa sababu hii ndio Wizara yake na hapa ndio pahala pake, azidi kuwa makini katika kumshauri vizuri sana Mhe. Rais ili asifike pahala; kwa sababu nilisema mwanzo kwamba moja katika kazi yake ni kuratibu utekelezaji wa ilani, haingefurahisha kumuona Pinda kule Tanzania Bara Mhe. Waziri Mkuu anakuwa na *package* kubwa katika utekelezaji katika Chama chake anapokwenda katika mikutano mikuu, yeye ikawa kwa kweli anarudia na anazunguka hapo hapo, haileti picha nzuri, haileti picha nzuri kwake yeye na haileti picha nzuri kwa Baraza hili ambalo ndilo linasimamia Serikali. Namuomba sana Mhe. Balozi azidi kuwa makini zaidi kama alivyo ili tufike pahala aweze kutekeleza majukumu yake vizuri na yeye tumpe heshima na sifa ambayo anastahiki kuwa nayo
.
Mhe. Mwenyekiti, katika hili vile vile mbali ya madaraka ya Baraza kuporwa kuna suala lile ambalo tunalizungumza kwa sababu ili Baraza lisimamie vizuri majukumu yake ni lazima liwe na uwezo wa kufanya kazi. Tumekuwa tukizungumza mara kwa mara suala zima linalohusiana na kuletwa kwa sheria linalohusu Baraza kuwa na mfuko wake, lakini hapa ni pahala pekee ninaomba Mhe. Waziri, atakapokuja aje atupe ahadi ni lini na kikao gani ambacho Serikali italeta sheria ile katika Baraza hili, lakini vile vile Baraza ni Taasisi ambayo tunasema kwamba lazima kuwe na Tume pekee ya Baraza la Wawakilishi ambayo ina mamlaka kamili. Hili hatutaki tulisemee sana kwa wakati huu tutakuja kusema wakati wa Wizara inayohusika, lakini tunaomba kutoa tahadhari kwamba Baraza kama moja ya Taasisi muhimu, moja kama muhimili wa dola ni lazima iwe ni Tume inayojitegemea ya Baraza letu la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoka kwenye Baraza la Wawakilishi, sasa ninaomba niende kwenye mambo ya muungano kama tulivyosema kwamba Ofisi hii kazi yake kubwa ni kuratibu masuala yanayohusiana na muungano na Mhe. Mwenyekiti, tunapozungumzia bajeti, kwa maana tunapozungumzia uchumi hatuwezi tukatenganisha baina ya bajeti ama uchumi wa Zanzibar na suala zima linalohusiana na mfumo wa muungano tulionao. Mara kwa mara Mhe. Mwenyekiti, tulikuwa tunalizungumza suala hili na katika nukta hii naomba nirejee tena kwa mara nyengine kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano kuruhusu wananchi waendelee kujadili mambo haya kwa uwazi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile niwashukuru wananchi wa Zanzibar kwa namna walivyojitokeza na kwa asilimia zaidi 66 kuelezea namna gani ya mfumo wa muungano wanaouhitaji, lengo lao likiwa ni moja tu kutaka kuondosha kero kwa maana ya kero ili basi Zanzibar tujinasue tulipo na tupige hatua zaidi katika masuala mazima ya kiuchumi ili bajeti zetu zitengemae.

Mhe. Mwenyekiti, ninaomba tu nirejee katika hili, kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba wawe makini zaidi katika hatua hii, wawe makini katika kuona kwamba tunafanya marekebisho yanayostahiki katika mfumo wa muungano ili tufike pahala kwa kweli tuweze kujinasua kiuchumi katika Zanzibar yetu.

Mhe. Mwenyekiti, katika nukta hiyo ninaomba nitoe rai kwamba kwa vile kwa kipindi kirefu tumekuwa tuna orodha ya vikao vya kero za muungano na kwa kuwa kwa sasa inaonekana tukapata suluhu ya kudumu kupitia mchakato huu wa katiba mpya, ningeshauri kwamba zile fedha zilizotengwa kwa ajili ya kuendesha vikao hivi vya kero za muungano zikawa fedha hizo zisitumike na vikao hivyo visiendelee kwa sababu kuendelea kwa vikao hivyo sasa hivi ni kupoteza fedha bure za umma. Kwa sababu kuna suluhisho karibu litafika pendekezo langu kwamba vikao hivi visitishwe ili tutoe fursa sasa kwa wananchi pomoja na Tume ya Marekebisho ya Katiba pamoja na Bunge la Katiba linalokuja liweze kukamilisha kazi yake ambayo hiyo itakuwa ina maana zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho naomba nizungumze hali ya siasa ambayo ilizungumzwa katika ukurasa wa 4 katika ripoti ya bajeti. Mhe. Mwenyekiti, hali ya siasa ni nzuri kwa sasa, hasa baada ya kuwepo kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Tunakumbuka kwamba kabla ya hapo sote ni mashahidi kwamba tulikuwa tuna migogoro mikubwa ya kisiasa, ndugu kwa ndugu walikuwa hawazikani, majirani walikuwa hawazikani, kulikuwa kuna mtafaruku ambao kwa kweli ulikuwa haumfanyi mwananchi wa kawaida kuhisi kwamba jua litakuchwa bila ya kupata hatari ya aina yoyote. Sasa kwa kweli hali hii ni

nzuri ya kuwepo kwa Serikali hii na niwapongeze wananchi kwamba kwa ridhaa zao ndio waliokubali kuwepo kwa Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa, wananchi wenyewe ndio waliokubali na wale waasisi wetu Mhe. Dkt. Amani Karume pamoja na Maalim Seif pamoja na wengine waliofanye juhudi hizo hatuna budi lazima tuwapongeze kwa dhati na tuwaombee kwa Mwenyezi Mungu awape afya njema na waliotanguliwa mbele ya haki awape malazi mema

.

Mhe. Mwenyekiti, katika hilo ninaomba nitoe tahadhari kwa watendaji kwa sababu tumekuwa na Serikali ya Umoja wa Kitafa ambayo imeleta utengamano mzuri katika Zanzibar yetu, kuna baadhi ya wanasiasa au kuna baadhi ya watendaji wakifanya choko choko za hapa na pale katika kuona kwamba tunarudia tena kule kule. Masalan ni hilo nililolitaja kwamba kuna watu ambao ni Wazanzibari wameshafikia miaka 18 na hawapewi vitambulisho na hawaandikishwi katika buku. Sasa ninaomba kutoa tahadhari kwa watendaji kwamba watendaji wanapaswa wawe makini sana hasa kwa wana siasa. Wanasiasa ni watu ambao ni wepesi sana kugombana lakini wanasiasa ni watu wepesi sana wa kupatana. Watendaji wazingatie hilo kwamba sisi wanasiasa ni watu wepesi sana katika kugombana lakini pia wanasiasa ni watu wepesi sana wa kukaa pamoja na kupatana dakika moja tu wanapatana. Sasa wasichokonoe na wakafanya mambo ambayo hayastahiki kuwafanyia watu kwa sababu mwisho wa siku wanasiasa watakapokaa pamoja vidole vyote vitawageukia wao, watekeleze sheria, watekeleze wajibu wao katika kutoa haki kwa wananchi, wasitumike kabisa kabisa katika kuona kwamba wanaleta vurufu katika nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ningelitoa rai kwa viongozi kwamba viongozi tuwe makini sana katika kukemea viashiria vinavyopelekea kuashiria kuleta migogoro, Watanzania na Wazanzibari mara zote tumekuwa ni wepesi sana wa kulaani matokeo. Mhe. Mwenyekiti, Watanzania na Wazanzibari na Waafrika tumekuwa ni wepesi sana wa kulaani matokeo lakini hatuko wepesi katika kulaani viashiria vinavyopelekea kutokea matokeo hayo. Mhe. Mwenyekiti, naomba katika hili nirudie tena kwamba tunahitaji tuione Zanzibar katika kipindi hiki ikiendelea kuwa ya amani ya utulivu, tunahitaji tuione Serikali yetu ya Umoja wa Kitaifa ikidumu daima milele, lakini tunahitaji kuona kwamba ili tuepushe migogoro tunahitaji kwamba kila mwenye haki apewe haki yake ili tuone matokeo mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, chanzo cha migogoro ni msingi wa kuwanyima watu haki. Askofu wa Afrika wa kusini kule alisema, '*there is no piece because there is no justice*, pahala ikiwa hapana haki hapana amani. Kwa hivyo na sisi viongozi tufanyeni haki ili tuwe na amani ya kudumu. Mungu ibariki Zanzibar, nakushukuru Mwenyekiti.

Mhe. Hijja Hassan Hijja: Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii ili nitoe mchango wangu mfupi sana wa hotuba hii ambayo Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais ameiwasilisha Barazani juzi kwa niaba ya Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, nitangulie na mimi nikushukuru kwa kukupongeza kwa jinsi unavyotuendesha katika Baraza hili na ninajua kwamba ni sehemu nzito ambayo inahitaji changamoto, kwa hivyo nikupongeze kwa jinsi unavyotuongoza na Mungu akujaalie utuongoze vizuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nianze pale Waheshimiwa wengi wamezungumzia kwamba Ofisi hii ya Makamo wa Pili wa Rais, ndio yenye jukumu la kuendesha Serikali. Kwa hiyo kama kuna udhaifu wa Serikali basi utakuwa upo kwenye ofisi hii, kama kuna umakini wa Serikali utakuwa upo kwenye ofisi hii na kila jema na baya litakuwa limo ndani ya ofisi hii, kwa sababu ndio waratibu wa Serikali nzuri. Kwa hivyo Wawakilishi wao watakaposifu Serikali maana yake imesifiwa Wizara hii kwa niaba ya Serikali, na pale ambapo Wawakilishi watagundua uovu basi Wizara hii ndiyo ilisababisha kwa makusudi ama kwa bahati mbaya lakini Wizara hii ndio iliyosimamia maeneo yote ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nimeanza hivyo kwa sababu ni muhimu Wawakilishi tukajikumbusha kwamba Katiba imezungumzwa na kama ni mbali mbali zinasema kwamba Wizara hii chini ya Makamo wa Pili wa Rais ndiyo Wizara ambayo inasimamia utendaji mzima wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa maana ya Wizara zote na Ofisi zake zote.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ya muda na nataka niheshimu maelekezo yako naomba niseme kwamba niungane na Mhe. Jussa, kwamba vifungu vyote vyenye matumizi wa bajeti hii nachangia kwa jumla kwamba nitahitaji maelezo ya ufafanuzi hasa vile ambavyo ukurasa wa kitabu hiki Mhe. Waziri, amevitaja ikiwemo mafungu ya maafa, mafungu ya mchango wa muungano, sherehe za mapinduzi na kadhalika, tunaomba ufafanuzi. Kwa nini kwa sababu pamekuwa na tabia fungu bila ya maelezo kwa mfano, unapotuambia kwamba Serikali imetenga bilioni 17.5 kwa ajili ya ajira bila ya kutuambia utaajiri watu wangapi, bila ya kutuambia mshahara utaongeza kiasi gani ni takwimu ambayo kidogo inaleta mashaka, kwa hivyo lazima uwe wazi ili kila mtu anayesikia ajue kwamba fungu lile limetengwa kwa ufafanuzi huu. Kwa hivyo kwa ujumla Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme hivyo kwamba wakati wa vifungu nitajaribu kuomba maelezo katika vifungu mbali mbali ambavyo Mhe. Waziri, ametuomba fedha ili kujiridhisha kwamba fedha hizo zimetengwa kwa madhumuni ya Wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, niseme tena kwamba Wizara hii kwa sababu kuna usimamizi niwakumbushe kwamba wao ndio wenye dhamana ya kulinda heshima ya Serikali, wao ndio wenye dhamana ya kulinda uwajibikaji wa Serikali. Juzi nilipita maeneo fulani pale Mwanakwerekwe nikaona vijana wanalalamika kwamba wakati wanapovamiwa na vikosi vya SMZ kwa misingi kwamba wanauza biashara katika maeneo yasiyohusika, wananchi wanauliza nani katoa amri hii, wakati sheria zile kwamba anayefanya kosa yeyote yule basi sheria inasema adhibitiwe na kupelekwa Mahakamani, lakini badala ya Mahakama basi wakati mwengine vikosi wanachukua bidhaa za wananchi, nimeona pale wanawake wanafukuzwa na maboksi yao ya samaki huku wakidhalilika, majibu ya askari wale basi wanasema kwamba haya ni maagizo ya Seif Sharif, na pengine kesho watasema haya ni maagizo ya Shein, na pengine kesho watasema ni maagizo ya Balozi. Sasa huo si utendaji mzuri wa Serikali, lazima ni viongozi wetu wajenge imani, nikiachiwa mimi kumdharau mmoja na mwenzangu anaweza akamdharau mwengine hatimae itakuwa hakuna nidhamu ya viongozi wetu. Na tumebahatika sisi Wazanzibari tumepata viongozi watatu wote watu wazima, maana yake ingelikuwa viongozi hawa ni chini ya umri wa miaka 40 tungesema vijana hali zao kidogo nyepesi, maana ndio msingi wa ujana lakini watatu ni *over 40 years*.

Sasa kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani nasema kwamba viongozi wetu watatu ni watu wazima na lazima waheshimike, ni watu wazima wana busara zao, watu wazima wenye heshima zao lazima Wawakilishi tuwapigie debe tuwatetee viongozi wetu watatu kwamba hawa lazima waheshimike. Naamini Mhe. Waziri ujenge nidhamu ya watendaji wa Serikali pamoja na askari wetu kwamba waheshimu viongozi wetu watatu kwa misingi yoyote ile.

Mhe. Mwenyekiti, tukizungumza lugha kwenye watu wa kawaida tutaonekana dhahiri kwamba Serikali haiheshimu viongozi wetu watatu. Ningeliomba hilo nilianzie kwa heshima kubwa na niseme kwamba Mhe. Waziri ulichukulie hatua. Mhe. Mwenyekiti, mimi ni miongoni mwa mtu nisiyekubaliana na nimeamini kwamba na nilisema mara nyingi kwamba Serikali hii haina uchungu wa fedha, Serikali hii ya awamu ya saba kila ukiiba ndio unakuwa mtu mzuri barabara, ukitaka usifiwe na uonekane kidume basi wewe iba tu Serikalini, utapewa mapumziko ya mwezi mmoja baadae uende upande mwengine.

Mimi ninazungumza hapa au sisi tunaozungumza humu tunaonekana wakorofi, wabaya sana wale, hao wanaozungumza ni wakorofi lakini watu wanaoiba ni watu wema, si tabia nzuri ya Serikali, na kigezo cha hayo hiki, haiwezekani kwamba tangu awamu hii ya saba imeingia tumesema mengi humu zaidi ya hoja 2000 tumesema, 1900 zote ni uongo basi hata moja

hakuna iliyokuwa sahihi. Serikali imeshindwa kuchukua hatua na tumefanya utafiti Mhe. Mwenyekiti, tunagundua kwamba baadhi ya Mawaziri wanawatetea watendaji kwa sababu ya maslahi yao na ikifika siku ya kusema tutasema, kwa sababu ndio wajibu wetu wa kusema, hatuwezi kuona fedha zinapotea Serikali ipo, hatimae wananchi wanadhalilika.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali hii haina uchungu wa fedha na niungane nae moja kwa moja Mhe. Omar ule ushawishi kwamba kila alipo akunje, ale mkutano kiamani, kwamba tunafanya dhambi tunafanya halali. Mhe. Mwenyekiti, Serikali inaibiwa na kwa kadri Baraza letu la Wawakilishi sisi si wataalamu lakini tunajaribu serikali kuwaambia kwamba wanaibiwa. Ninasema hayo mbele ya Mhe. Balozi Mkuu wa Serikali, tunasema hayo mbele ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kama ni mnadhimu wa serikali, tunasema hayo mbele ya mawaziri kwamba serikali inaibiwa. Wakati mwengine huashirii kama maeneo haya yanaibiwa lakini kadri ukisema ndio watu wanatia pamba masikioni hatimaye mwisho wa mwaka unamalizika Wazanzibari waungwana hawalalamiki, hawaandamani wanamuachia Mwenyezi Mungu siku ya mwisho kwenye mkunazi lakini wananchi wanateseka sana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba niseme kwamba uungwana ni kitendo. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais si mara moja wala mbili umewahi kuchukua fomu ya Urais hapa Zanzibar, naambiwa mara moja. Umewahi kuchukua fomu ya Urais kwamba unaomba Wazanzibari wakuchague na mimi nilikuwa tayari kukuchagua lakini bahati mbaya hukupita. Lakini inaonesha kwamba wewe ungekuwa Rais ungekuwa makini, keshokutwa tutachagua tena mwaka 2015 hii nishawishi kwamba ukichukua fomu onesha kwamba mimi niko makini, watendaji hawa baadhi yao ni safi sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa taarifa yake baadhi ya Makatibu Wakuu wanalalamika hawasemi tu kwa sababu hata wakisema hakuna liwalo, *business as usually*. Sasa wanalalamika kwamba serikali inaibiwa lakini wao wakisema basi watapata adabu. Kwa hivyo, utuoneshe kwamba wewe ni mtu uliyewahi kuchukua fomu na kuomba Urais, kama wewe ungekuwa vipi? Tusaidie Mhe. Mwenyekiti, serikali inaibiwa. Serikali inaibiwa na wakati nawaziri 17 mpo lakini hamjali au mnaogopa, mnaogopa nini wakati sisi ndio walinzi wenu Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani kila wizara tunaitaja sisi Wawakilishi maeneo ambayo yanayoibiwa lakini kwa nini Mhe. Waziri anashindwa kuchukua hatua, aje atujibu. Kuna mtu yuko juu ya nyinyi, au kuna mshauri nambari nne au tano ana nguvu zaidi kwa nini wanashindwa kuchukua hatua, au nini

malengo ya serikali juu ya wizi wa mali za umma. Kwa nini tumfunge mtu aliyeiba dafu lakini tumlinde aliyeiba pesa, kwa nini.

Mhe. Mwenyekiti, si haki inayofanyika na kama hatutaki kusema kweli hapa duniani basi kuna siku tutasema ukweli mbele ya Mwenyezi Mungu. Nadhani tusisubiri huko tuchukue hatua kwa yale mambo ambayo yako dhahiri yanafanywa kwa msingi wa kudhalilisha taifa letu. Mhe. Mwenyekiti, serikali inaibiwa na lazima Mhe. Waziri achukue hatua.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu utawala bora nimepata malalamiko juzi kuna eneo moja sitaki nilitaje Mhe. Waziri wewe wizara yako ndio mdhamini wa serikali. Kuna wana maskani fulani hivi sikusudii kwamba CCM au *CUF*, ni vijana wanaokusanyika wengine wanaita baraza, wengine maskani lakini ni makundi ya vijana kwa ajili ya mazungumzo au michezo mbali mbali. Kuna bango moja au mabango mawili yako jirani, bango moja limeandikwa 'kila bangi na kichwa chake' ni bango la vijana hilo, na jirani yake limeandikwa 'tuacheni tupumue' ni lugha mbili za mabango mawili ya vijana, ambapo moja kila kichwa na bangi yake na jengine tuacheni tupumue. Lakini inaonekana hili bango la tuacheni tupumue ni kero kubwa kwa serikali wakaendewa likavunjwa wakafurushwa; linalozungumza kila bangi na kichwa chake limeonekana ni bango zuri halina tatizo. Mimi sielewi nini maana yake. Kwa mtazamo wa kawaida mimi mshamba ningehisi tuacheni tupumue ni bango moja zuri sana ambalo linanikumbusha kwamba ukichoka upumue, lakini nashangaa kwao ni kero.

Bango lililoandikwa kila bangi na kichwa chake ni bango zuri limeambiwa kaeni muendelee kuzungumza. Hii ni dhahiri Mhe. Mwenyekiti, inaashiria mwelekeo mbaya. Hatuwezi kuongoza nchi katika mtazamo wa upendeleo, kama maskani zile hatuziruhusu basi naomba tuondoshe lakini kama vijana tumewaruhusu kuwakusanya maana yake tutumie utaratibu wa haki na kuondosha upendeleo ili tusisababishe mgongano.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora alisema hapa Barazani kwamba suala la uajiri wa sekta za Muungano limepatiwa ufumbuzi. Sasa mimi naomba nichangie eneo hilo na nasema kwamba bado hakuna ufumbuzi kuna malalamiko mengi ambayo kwa kweli yanaleta ishara mbaya.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa sera ile ya uajiri taasisi za Muungano kuna makubaliano kwamba Zanzibar itapatiwa asilimia 25 za ajira na wenzetu Tanzania Bara watapatiwa asilimia 75 za ajira. Sasa nimefanya utafiti mdogo nimegundua kwamba mwaka jana kwenye sekta ya Jeshi waliajiriwa karibu vijana 2000, asilimia 25 maana yake Zanzibar tumepata 500, lakini takwimu

ambazo zipo samahani mwaka huu tumepata chini ya waajiriwa 100 hata wale 500 hawakufika. Sasa hii ni kuonesha kwamba bado kuna matatizo katika sekta za Muungano kwa suala zima la uajiri. Lakini tukiangalia kambi ya Mafinga walioajiriwa ni vijana 2000, Zanzibar pale wapo 125 na Maktopora kuna vijana walioajiriwa lakini wako chini ya watu 500. Kwa hivyo, tuiambie tu serikali kwamba bado sekta ya ajira kwa mambo ya Muungano hakuna usawa na kwa hivyo, Mhe. Waziri wewe ndiye mratibu wa mambo ya Muungano, wizara yako utwambie kwa nini mmekubaliana kwamba Zanzibar ipate asilimia 25 lakini bado makubaliano hayo hayalindwi. Ni lazima atwambie kwamba tayari kero hii ya Muungano imeondoka na tuko salama.

Mhe. Mwenyekiti, kuna vijana wetu wa JKT ambao wameondoshwa hapa kwa ajili ya matayarisho ya kujiunga na Jeshi. Mhe. Mwenyekiti, tumegundua vile vile kambi ya Aljoro, vijana ambao Wazanzibari wana elimu ya diploma na *degree* ni vijana 11, lakini pale amechukuliwa kijana mmoja tu. Wenzetu wa Tanzania Bara katika kambi hiyo kuna vijana 21 lakini wameajiriwa vijana 17. Bado tunasisitiza kwamba utaratibu wa ajira kwenye sekta za Muungano haujakuwa halali na bado Wazanzibari wananyanyaswa na hii sio fursa nzuri kwa masuala ya Muungano.

Suala jengine naomba Mhe. Waziri atwambie kwamba iwapo suala hilo wamelimaliza tupatiwe takwimu ili turidhike kwamba kweli serikali inazingatia ile asilimia 25 katika maeneo yafuatayo. Tuambiwe kuna watumishi wangapi Wizara ya Mambo ya Ndani ambao ni Wazanzibari na kuzingatia ile asilimia 25 ambayo tumekubaliana. Vile vile kuna watumishi wangapi katika Wizara ya Mambo ya Nje ikiwa ni pamoja na ubalozi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba vile vile Mhe. Waziri atwambie kuna watumishi wangapi wa *BOT* ambao ni kutoka Zanzibar. Kwa sababu ukurasa wa 257 hadi 261 wa kitabu ambacho tumepewa hivi asubuhi ukiangalia wale maafisa wa ngazi za juu kati ya maafisa 46 nina hakika hawazidi maafisa wane ambao ni Wazanzibari. Sasa serikali inatuambia wananchi kwamba tumekubaliana na kero zimeondoka wanakusudia kutwambia nini.

Mhe. Mwenyekiti, nieleze mchango wangu niseme tu kwamba mimi ninaendelea kuishauri serikali kwamba si busara katika hii hali tuliyonayo, tayari serikali imeanzisha mfumo wa Katiba mpya na tuko katika hatua ya pili nadhani bado serikali inaendelea kuzungumza kero za Muungano. Mimi ningeomba kwa mara nyengine kuwa acheni tabia hii ya kutafuta kero za umma, waachieni wananchi katika hatua ya Baraza la Katiba na katika hatua ya Mabunge ya Katiba na hatimaye watapiga kura ya maoni kuamua mfumo wa Muungano wanaoutaka. Badala ya kuchukuana juzi hapa iliondoka ndege nzima kama si mbili kuelekea katika *program* za Muungano, ni kuharibu mali

za umma kwa nini hatuwaachii wananchi sasa? Kwa sababu serikali imeshindwa kutatua miaka 50, nadhani serikali sasa waachieni wananchi watatue kwa kupitia utaratibu ambao serikali imeweka kwa kupitia hii Tume ya Katiba ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba serikali lazima iwe makini, wananchi wanajiuliza naomba nichukue mfano mdogo tu kwamba, bandari yetu imezungumzwa kujengwa jengo la abiria zaidi ya miaka 10 nyuma, serikali imeshindwa kujenga banda la abiria. Lakini mfanyabiashara mmoja Bakhresa tu miezi mitatu amebadilisha bandari kama kwamba ni miaka mia. Kile ni kigezo kwamba serikali haina utendaji makini, haiwezekani kabisa Mhe. Mwenyekiti, kwamba miaka 40 ya uhuru wetu karibu ya 50 serikali imeshindwa kutengeneza mazingira mazuri pale bandarini lakini mfanyabiashara miezi mitatu ametengeneza mazingira ambayo leo kama ulikuwa Pemba miezi mitatu minne ukija pale huamini kama ni Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nashauri kwa sababu tumedumaa kila mwaka Bakhresa atoe mradi mmoja atusaidie, nashauri kwa sababu serikali tumeshindwa na kwa sababu yeye yuko tayari kusaidia basi kila mwaka serikali imtafutie mradi mmoja atusaidie kwa sababu sisi wenyewe tumeshindwa. Haiwezekani wala kuingia akilini kwamba mfanyabiashara miezi mitatu anafanya jambo zuri la kihistoria lakini serikali miaka 50 tumeshindwa. Kupitia nafasi hii Mhe. Mwenyekiti, basi niombe kwamba irudi ihsani mfanyabiashara huyu apatiwe eneo pale bandarini la kujenga ofisi, ametujengea maeneo mazuri na bila shaka hakuna fidia atakayopewa lakini serikali imeshindwa kumpatia sehemu ndogo ya kujenga ofisi kama ofisi ya kampuni yake kwa ajili ya kushughulikia suala zima la kampuni yake na masuala mazima ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri hili alifanyie kazi kwa ajili ya kumsaidia ili tusimvunje moyo pale ambapo anakusudia kufanya mengine.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kusema tu kwamba bajeti hii sisi kama Wawakilishi tutaunga mkono kwa sababu inaongozwa na Makamu wa Pili wa Rais. Lakini hoja hii itakwenda sambamba na majibu ya serikali, kwa nini wameshindwa kuchukua hatua kwenye ripoti nne ambazo Baraza hili wamepitisha na tumetumia fedha nyingi, hebu Mhe. Waziri atupe siri hasa kwa nini wanashindwa. Tunadhani kuchukua hatua kwa mbadhirifu kuna kupotoka au kuna tatizo gani tusaidiwe tujue, maana isijekuwa tunadai kuchukua hatua kumbe kuchukua hatua kwa mali ya serikali ni dhambi, tusaidie Mhe. Waziri tatizo nini hasa au kuna watu yanawagusa haya matatizo.

Tusaidiwe Mhe. Mwenyekiti, tatizo nini maana isijekuwa sisi Wawakilishi tunalazimisha chukueni hatua kumbe mna kikwazo kikawa kinawasumbua, tujue kama kuna kikwazo kama cha dhambi au kukasirika sisi tutawaachia twende hivi hivi, lakini kama hakuna sababu ya msingi hebu tuchukueni, vyenginevyo mnatufanyia watendaji wafanye jeuri na kwa taarifa yako Mhe. Waziri kadri wakinyamaza kimya ndio watu wanakula fedha zinapotea. Mimi nimekuwa nikisema kwamba hata aje Rais gani hapa hata atoke mbinguni mpya kwa utaratibu huu wa kulinda watu wanaotumia fedha za umma vibaya hakuna Rais atayefanikiwa kufikia malengo kama ilivyokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo Mhe. Waziri akitoa ufafanuzi wa vifungu na hoja zangu nitaunga mkono.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii lakini pia nimshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wa wizara kwa kututayarishia bajeti hii, kazi hii waliyoifanya ni kazi kubwa na ni nzuri kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitajali sana muda wako ili na wenzangu wapate kuchangia kwa sababu naona mengi wenzangu waliotangulia wameanza kunifilisi, lakini nitaanza kugusa kwenye hiki kitabu kikubwa kidogo. Kuna maeneo nitahitaji ufafanuzi nianzie na hapo kabla sijaingia katika kitabu chake cha hotuba.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaanza na kwenye fungu la 0003 Afisi Kuu Pemba, niende kwenye kifungu nambari 22 0400 gharama za mafuta na vilainishi kwenye kasma nambari 220409, uondoshaji wa takataka. Nahitaji maelezo katika hili kwa sababu naona tangu mwaka juzi hapa kuna taka hazijaondoshwa na hazijesha. Mwaka juzi kwenye bajeti ya mwaka 2011/12 shilingi milioni laki tatu, 2012/13 kuna shilingi milioni kumi laki nane na mwaka 2013/14 kuna shilingi milioni kumi laki mbili. Nilikuwa nahitaji ufafanuzi katika eneo hilo.

Nikisogea nisogee tena huko huko Pemba katika kifungu 311200 ununuzi wa mashine na zana kwenye kasma nambari 311203 ununuzi wa Honda. Naona kila mwaka hapa Mhe. Waziri ametuwekea ananunua Honda, ameanza kununua shilingi milioni mbili laki tano, akaja akanunua shilingi milioni tatu na sasa ana shilingi milioni kumi laki nne. Labda mara hii inaonekana ya kuruka kidogo itakuwa hiyo.

Nikiondoka hapo Mhe. Mwenyekiti, nasogea mbele katika Idara ya Mipango, Sera na Utafiti 0401 Unguja, hiyo au ndio Makao Makuu wanavyoita, niende kwenye fungu 220500 vifaa na huduma za ofisi, kwenye kasma 220517 utayarishaji wa mpango na bajeti pametengwa shilingi milioni kumi laki tisa na hamsini elfu, nilikuwa naomba ufafanuzi katika eneo hilo.

Lakini nisogee mbele tena kwenye fungu 263100 Ruzuku. Pana kasma mbili hapa, kasma 26166 huduma za utafiti shilingi 36,982,000, nilikuwa naomba ufafanuzi wake katika hiyo na 263178 ushauri nasaha pana shilingi 52,500,000/ nayo vile vile naomba ufafanuzi katika matumizi ya fungu hilo.

Halafu nisogee kwenye fungu 311200 ununuzi wa mashine na zana kasma 311202, ununuzi wa gari. Mwaka jana kulikuwa kuna ununuzi wa gari shilingi 55 milioni na mwaka huu kuna 60 milioni kwa ajili ya ununuzi wa gari. Sasa hili nilikuwa naomba maelezo.

Nikitoka hapo nisogee kwenye Idara ya Uendeshaji na Utumishi fungu lake 0501, nisogee kwenye fungu 220100 gharama za vifaa na huduma za mawasiliano kwenye kasma 220108 huduma za mtandao shilingi 16 milioni.

Mhe. Mwenyekiti, anisaidie tena kwenye fungu 220600 samani za ofisi, kasma 220603 ununuzi wa samani viti na makabati ambapo mwaka jana kulikuwa kuna shilingi 200 milioni kwa ajili ya shughuli hiyo lakini na mwaka huu kuna shilingi 102 milioni. Sasa kidogo naona mwaka jana zilinunuliwa za *low quality* sana zimekufa zote na mwaka huu zinaundwa nyengine au vipi naomba waziri atakuja kutusaidia ufafanuzi katika hilo. Kwenye fungu 220700 matengenezo ya ofisi,niende kwenye kasma 220702 matengenezo makubwa ya majengo. Mwaka jana kulikuwa kuna shilingi 31 na mara hii kuna shilingi 152,579,000. Mhe. Mwenyekiti, naomba ufafanuzi kama mwaka jana tumefanya matengenezo hayo makubwa na mwaka huu tuna matengenezo mengine makubwa, sasa kama nyumba ni mbovu bora tukajenga kabisa kuliko kuendelea kufanya matengenezo tu.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwenye fungu 0701 Idara ya Huduma za Makamu wa Pili. Fungu hili mimi nataka ufafanuzi wake kwa ujumla kabisa kwa sababu naona limenona mno. Mwaka jana jumla ya fungu lilikuwa lina shilingi 365,223,000 lakini mwaka huu zinaombwa shs.780,034,000; mara mbili ya zile za mwaka jana. Sasa mimi nataka kuona sababu za msingi kuombwa kwa fungu hili ambapo limekuwa kubwa mno kuliko lilivyoombwa mwaka jana, sijui kuna kipi kilichozidi. Mhe. Waziri naomba sana utakapokuja unisaidie maelezo ambayo yatasaidia kuweza kukuidhinishia fedha hizi.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka huko kwenye uchanganuzi wa vifungu sasa niingie kwenye kitabu cha hotuba cha Mhe. Waziri nianzie kwenye ukurasa wa saba kifungu 14 ambapo panazungumzia masuala ya Muungano. Mhe. Mwenyekiti, mimi kidogo nimepata wasiwasi, kwa sababu kila siku zikienda kwenye masuala haya yanaonekana yanabadilika na mara hii Mhe. Waziri kaja na neno jipya changamoto limeondoka lile neno kero. Zamani akitwambia kero za Muungano ngapi zimetatuliwa, ngapi bado, ngapi zinaondolewa lakini naona mara hii kaja na *style* mpya anaziita changamoto, kwenye miaka hii 50 ya Muungano huu zimekuwa changamoto. Sasa sijui zitakuwa 'pevumoto' baada ya miaka mingapi. Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiria hili Mhe. Waziri aje atueleze vizuri kuzigeuza kutoka kero mpaka akaziita changamoto sasa.

Lakini mimi labda nirejee katika hili kidogo kama ambavyo Mhe. Omar Ali Shehe alizungumzia kero hizi hata ilikuwa nisimwambie tena sasa hivi kwa sababu tuko katika mchakato wa Katiba mpya. Sasa madhali tuko katika mchakato wa Katiba mpya hakuna haja ya kuanza kushughulikia hizo kwa sababu zote zitaingia kwenye Katiba mpya, kama kero, changamoto, pevumoto, tukienda kwenye Katiba mpya pale tutatengeneza mambo ambayo sasa tutaanza kuitumia ile Katiba mpya na ninafikiria *Inshaallah* mwakani tunaanza na kitu hicho. Sasa kama kulikuwa kuna fungu la matumizi kwa ajili ya suala hili na mambo mengine mimi nafikiria Mhe. Waziri masuala haya aweke pembeni aendelee na utayarishaji wa Katiba mpya tujipange vizuri katika hilo tuende mbele, tusianze kushughulikia masuala haya naona sasa hivi haya kama yanapitwa na wakati. Kwa hivyo, Mhe. Waziri nafikiri kama kuna fedha ambazo ametenga kwa ajili ya shughuli hizi nafikiria hizi tuziondoshe moja kwa moja tuende tu kwenye mchakato wa Katiba mpya tupate Katiba yenye muafaka na nchi yetu, na watu wetu, kwa maslahi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu wamezungumzia mambo mengi hapa lakini mimi nitagusa gusa kidogo ili muda wako nisiutupe mwingi na wenzangu wapate nafasi. Nisogee kwenye ukurasa wa 12 kwenye kifungu cha 27, Uwezeshaji wananchi kiuchumi na kuongeza fursa za ajira.

Mhe. Waziri hapa amezungumzia namna serikali inavyojitahidi katika kufanya hivyo, kuwawezesha wananchi kiuchumi, kuongeza fursa ya ajira hasa kwa vijana. Mimi nilikuwa nataka kujua tu Mhe. Waziri zaidi katika hili akija aje atueleze hapa ametengeneza ajira ngapi hasa kwa vijana hawa, au kama suala hili ataiachia Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika basi aje atuelezei. Mimi nilitaka kujua hasa hizo ajira ambazo ametengeneza kwa ajili ya vijana wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikisogea mbele tena hapo hapo ukurasa wa 13 tu, kwenye sekta ya huduma za jamii. Mimi nataka nigusie kidogo kama wenzangu walivyoligusia suala la maji. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, hili suala ni tatizo bado, amezungumza hapa kidogo najua na Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati atakuja kulizungumza mwenyewe, lakini hasa bado tatizo la maji ni kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuna maeneo sasa hivi maji ya mfereji wameyasahau kabisa hayapo, kuna maeneo sisi tulikuwa tunapata maji kipindi cha kabla ya kuambiwa kuna ule mradi wa Wajapani, mradi ule ambao uko katika Mkoa wa Mjini/Magharibi tulitegemea utakuwa ni suluhisho la tatizo hili, lakini cha kusikitisha sana Mhe. Mwenyekiti, mradi ule umekuwa kama ndio umeongeza lile tatizo kuwa sugu zaidi. Wale ambao walikuwa wakipata maji kwa wiki mara moja sasa hawapati kabisa, waliokuwa wakipata kwa miezi miwili sasa ndio wameshasahau. Mimi mwenyewe naishi katika maeneo ambayo maji nilikuwa nikipata kwa kipindi hicho lakini kwa sasa maji yale yametoweka kabisa. Kwa hivyo, Mhe. Waziri anapotwambia serikali imejipanga, inafanya nini, ametoa maelezo mengi hapa na pesa nyingi kazitaja zilizotumika, lakini kwa kweli mimi naona suala hili bado halijafikiwa muafaka.

Mhe. Mwenyekiti, nisogee tena hapo hapo kwenye huduma za jamii katika suala la kuchangia huduma za afya. Mhe. Waziri ametueleza hapa kuanzia mwaka jana alianza kutangaza kwenye bajeti yake namna Rais wa Zanzibar alivyotoa maelezo yake kwamba kutakuwa hakuna kuchangia huduma ya afya kwa akinamama wajawazito. Lakini Mhe. Mwenyekiti, nataka nimwambie Mhe. Waziri nasikitika sana kwamba akinamama bado wanaendelea kuchangia huduma za afya.

Mimi katika jimbo langu ninayo Hospitali ya Kivunge, ina wodi nzima ya akinamama lakini kama tutatoka sasa hivi Mhe. Waziri ukawakuta wale waliolazwa pale watakwambia huduma wanachangia, maana kuchangia sio kumlipa yule daktari tu lakini kama unapokwenda pale hakuna kifaa hata kimoja kila kitu ununue ndio kuchangia kwenyewe huko na huku tuliambiwa kwamba huduma hii itakuwa haichangiwi tena. Sasa hebu Mhe. Waziri atuambie kuchangia kwenyewe kumekusudiwa vipi, kwamba kutomlipa yule daktari tu huduma nyengine ununue au kuchangia huku kulikuwaje. Maana yake inaonekana sisi wengine labda tafsiri hatuitambui vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nisogee mbele kidogo ametaja katika ukurasa wa 16 kifungu cha 38 migogoro ya ardhi. Mhe. Mwenyekiti, kama utakumbuka mwaka jana katika kipindi cha bajeti kama hiki nililizungumza sana suala hili katika wizara hii na Mhe. Waziri akatuahidi kwamba atakapokuja Waziri wa

Ardhi basi tataweza kuunda hata kamati teule. Kwa sababu nilimuomba yeye tuunde kamati teule katika ofisi yake, lakini akaomba tusogee kwenye kamati ya kisekta.

Nakumbuka wizara ile tulikubaliana hapa tukaunda kamati teule kwa ajili ya migogoro ya ardhi, hii nilikuwa nataka kujua sijui kamati ile tumefikia wapi. Kwa sababu sasa hivi ni mwaka mzima lakini ripoti hapa haijaja wala hatuna taarifa yoyote, sasa sijui atatwambia vipi Mhe. Waziri katika hili.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye ukurasa wa 19 kifungu cha 47, madawa ya kulevya. Mhe. Mwenyekiti, mimi kidogo napata wasi wasi katika suala hili. Kila tukisikiliza serikali katika suala hili inalalamika sana juu ya mambo haya, kwanza wanakubali kwamba hivi vitu vipo. Ikiwa wizara hii, ikiwa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ndio inayoshughulika na masuala hayo,wote wanakubaliana lakini namna ya kuyatekeleza matatizo haya. Kwa sababu madawa kwa kweli yanawaumiza vijana wetu kweli kweli Mhe. Mwenyekiti, lakini sioni ule usimamizi wa serikali katika suala hili kuhakikisha kwamba hivi vitu vinatokomezwa. Kwa sababu hivi vitu si vya siri viko dhahiri kabisa, ukimuuliza mtoto mdogo wapi panapouzwa unga siku hizi atakwambia nyumba ile pale, mtoto mdogo tu wa makamo mwenye kuweza kusema basi atakwambia nyumba ile pale inauzwa unga au fulani yule anauza unga.

Sasa serikali sijui inachelea nini kushughulikia vitu hivi, kila ikija hapa inatupa taarifa, maelezo lakini utekelezaji tunaona unasuasua katika hili. Hapa ndio watu wanapopata shaka sasa, ndio pale utakuta kuna baadhi kuna watu wanasema inaonekana wazito wamo katika hili na wazito wenyewe tunaambiwa sisi viongozi maana na mimi ni kiongozi. Sasa tusiwachelee watu wasiseme jamani tufanyeni kazi, kama serikali iko *serious* hasa katika kuhakikisha inatokomeza suala hili linawezekana. Kwa sababu haya mambo hayafanywi siri yashakuwa yako dhahiri kila kitu kinajulikana sasa hivi, muuzaji anajulikana, mtumiaji anajulikana, mletaji anajulikana. Lakini serikali inawakamata sana wale watumiaji zaidi, kila siku ukienda mahkamani kule ukizitizama zile kesi zilizokuwepo ni za watumiaji zaidi kuliko za wasafirishaji, wale waletaji au wauzaji.

Sasa kama hao waletaji hawashughulikiwi wanakwenda kushughulikiwa watumiaji itakuwa mnawaonea. Kwa hivyo, wasiwaletee halafu muone watumie. Basi Serikali ijidhatiti katika kuzuia kuhakikisha kwamba hichi kitu hakiingii katika nchi yetu. Kwa sababu jambo mkilitaka linakuwa, linawezekana na Serikali ina mkono mrefu kwa nini hapa kidogo inakuwa pagumu mmekaa mmeweka udhibiti kwenye magendo ya karafuu mmeunda

mpaka tume nzito nzito na tumetoa mamilioni ya pesa katika kuhakikisha kwamba magendo yale yasifanyike.

Lakini kwenye hili Serikali inachelea kitu gani, kwa nini inakuwa nzito katika kufanya maamuzi kwenye jambo hili. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri akija hapa atueleze mikakati hasa ya Serikali katika kuhakikisha kwamba jambo hili linatokomezwa.

Mhe. Mwenyekiti, nisogee kwenye ukurasa wa 22....

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe una dakika tano za ziada.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Aah! Mhe. Mwenyekiti, bado nimeanza na dakika 20 tupeane nafasi, tutumie ile kanuni ya 58 kifungu 6 ndicho nnachotumia. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana katika hili sitaki kubishana na kiti chako. Lakini tupe nafasi kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 22 sehemu ya 54 Utawala Bora. Nilikuwa nataka nigusie kidogo hapo kwa sababu Serikali yetu inazungumzia dhana ya Utawala Bora. Lakini mimi kila nikitizama naona kile ninachokisema na kilichomo ndani ya roho ni vitu viwili tofauti. Maana tukiitizama rushwa Mhe. Mwenyekiti, inatia kichefu chefu. Napenda kuungana na Utawala Bora katika kitu ambacho kinapigwa vita kwa nguvu kabisa ni rushwa anapofika pahala mwananchi pahala ambapo yeye huenda akapewa haki yake lakini haki ile hawezi kuipata mpaka kwa kutoa rushwa.

Mhe. Mwenyekiti, tumefika mahala pabaya kwa sababu maeneo mengi ambayo panatakiwa patolewe haki. Haki haipatikani mpaka kwa kutoa kitu kidogo. Nina hofu sana nchi yetu itakuja kugeuzwa kama nyimbo ya ule muimbaji wa Kenya aloimba nchi ya kitu kidogo. Sasa tusije kuingia na sisi sasa Zanzibar ni nchi ya kidogo, maana yake mpaka utoe kitu kidogo ndio uweze kupata haki yako. Nina hofu sana tusije kufika huko Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hiyo, nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri, wa Sekta yupo mwenyewe anasikia lakini ambaye anashughulika na usimamizi wa hii Serikali mwenyewe Makamo pia yupo tunataka tumwambie kwamba Mhe. Makamo tumwambie kwamba huku kuna tatizo rushwa bado inawasumbuwa watu wetu huko, tunakuomba sana Mhe. Makamo watu wetu wanapata tabu sana tunapata malalamiko mengi sana kwa wananchi wetu juu ya rushwa haki haipatikani huko kama mtu hakutoa kitu kidogo ni tatizo Mhe. Mwenyekiti hili, nakuomba sana utusaidie katika hili.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kujali muda wako sasa naomba nisogee kwenye ukurasa wa 51 moja kwa moja kwenye Ofisi ya Baraza la Wawakilishi. Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Wawakilishi mimi nilikuwa kuna mambo kidogo nataka niyazungumze hapa. Wizara hii ndio msimamizi kwa mujibu wa hii hotuba aliyotuwekea Mhe. Waziri hapa anaonekana yeye ndie msimamizi katika hii Ofisi yaani iko chini ya mamlaka yake pale.

Lakini mimi nilikuwa nataka nimuulize Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri kwamba utakumbuka hapa tumeunda Kamati teule nyingi sana ipo Kamati teule juu ya mambo hapa kuna Kamati teule kwenye habari za *ZECO*, juu ya suala la Ardhi, Baraza la Manispaa. Tuanzie ile ya mwanzo juu ya mambo mbali mbali ambayo imeleta taarifa yake hapa katika Baraza taarifa ile ilikataliwa na Baraza ililtewa taarifa ya utekelezaji baada ya yale maagizo ya Baraza lakini ilikataliwa na Baraza hapa.

Sasa kulikuja na maneno hapa kwamba tutarudi tuzungumze tena halafu tuone ili tuweze kuyafanyia kazi. kamati ilikaa mara moja lakini mpaka leo hatujapata jawabu lolote, sasa hii kwa kweli mimi hatulitendei haki Baraza. Serikali halitendei haki Baraza katika hili, Baraza linatoa maagizo lakini inaonekana Serikali inakwepa majukumu yao. Katika hili Mhe. Mwenyekiti, nakuomba sana Mhe. Waziri uje na maelezo ya kutosha juu ya uwajibikaji wa Serikali katika kadhia hizi za vitu vya kamati.

Hapo kwanza mimi naodosha shilingi yangu Mhe. Waziri siungi mkono hotuba hii nakuondeshea shilingi katika hili mpaka uje unipe maelezo ya kutosha juu ya kadhia zilizopita. Kamati zote tulizoziweka hapa. Kamati ziko karibu nne nataka nione utekelezaji wa ripoti hizi. Kwa sababu ripoti ilemetwa Barazani ilikataa ni kitendo cha aibu kwa Serikali, lakini sijui kama wenyewe mnajua hilo au vipi maana naona mmekaa kimnya mpaka leo inangojea. Sisi tuunde kamati tukuleteeni halafu hakuna mnachokifanya, tunakaa kama tunaimba tu tunatumia fedha za wananchi hapa hakuna kinachofanyika.

Mhe. Waziri nakuomba sana sitoipitisha bajeti yako kama huna maelezo ya kutosha juu ya ripoti hizi. Nakuomba sana Mhe. Makamo unistahamilie. Mimi nakuona kiongozi wangu nakuheshimu sana kabisa, lakini naiona bado serikali haijakuwa makini katika hili. Mnapewa maagizo mnachukuwa lakini utelezaji unakuwa mzito. Kwa hiyo nakuomba sana hili.

Mhe. Mwenyekiti, kuna kitu nilikuwa nakizungumza hapa kabla haijaanza mijadala ya leo juu ya Wajumbe kwamba wako wengi kuchangia, na muda hautoshi. Kwa hivyo, Wajumbe wengine wanaandika kwa maandishi. Mimi nilikuwa nataka ufafauzi kidogo Mhe. Mwenyekiti, Wajumbe wanapoandika

kwa maandishi au michango yao kwa maandishi anaichukuwa Waziri anakwenda nayo Mhe. Waziri huja na kusema tu hapa nimepokea michango kutoka kwa Wajumbe fulani wamechangia kwa maandishi.

Hivyo ile kumbukumbu ya Baraza inapakana vipi, mana haya maneno tunayoyazungumza katika chombo hiki yanawekwa kwenye kumbukumbu *hansard* huko. Sasa ile michango ambayo inachangiwa kwa maandishi kumbukumbu zake zinawekwa wapi. Hebu kidogo tupate ufafunuzi katika hili. Maana yake ninapokuwa mimi nimechangia halafu Mhe. Waziri anasema kwamba nitamjibu kwa maandishi wako Mawaziri humu na mwaka jana tumeambiwa hapa tutajibiwa kwa maandishi, mimi nina wizara mbili hapa nilipeleka michango yangu kwa maandishi nikaambiwa nitajibiwa na mna maswali ndani ya ile michango, lakini mpaka hii leo ninapozungumzia hapa majibu hayo hayajaja, sijui yamekomea kwenye Ofisi ya Katibu wa Baraza au vipi.

Kwa hiyo, mwaka huu nimeamua kwa makusudi kama sikupata majibu yangu yale ya mwaka jana ya Bajeti za Wizara zile mimi hapa itakuwa vigumu kuzipitisha. Kwa sababu siwezi kuwa napitisha hiki yale majibu ya awali pia sikuyapata, hilo litakuwa gumu.

Kwa hiyo, na hili nilikuwa naomba Mhe. Waziri utakapokuja uje utupe ufafanuzi tunapochangia kwa maandishi kumbukumbu zinakuweko wapi hizi za Baraza zinawekwa wapi hizi kumbukumbu zake. Maana yake Mhe. Waziri anakabidhiwa maandishi yale na michango yetu unachukuliwa, lakini hapa Ofisini ukiuliza hakuna kitu. Unapouliza majibu yangu yako wapi unaambiwa sisi hatuna maswali yako. Sasa itakuwaje kumbe inakuwa kama mnatufanyia mchezo, sisi tunaandika tunakupeni mnaondoka nayo tu. Halafu hakuna jawabu linalokuja hapa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hilo mimi siiungi mkono hotuba hii kwanza mpaka nitakapopata majibu haya nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kupata nafasi hii ambayo nitachangia kwa ufupi sana Bajeti hii ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa mwaka wa Fedha 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuanza naomba nianze kwa kuzungumza kuhusu Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ambayo kwa ufupi tunaita *ZEC* na kwa kuanza huko naomba moja kwa moja nianze kwa kifungu cha 102 kilioko kwenye ukurasa wa 49 ambacho kama ifuatavyo:

Tume ya Uchaguzi wa Zanzibar ni chombo kilichoanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ibara ya 119(1) na Sheria namba 9 ya mwaka 1992 ya Tume ya Uchaguzi ili kuendeleza demokrasia kwa njia ya uchaguzi. Tume ina majukumu yafuatayo:-

i) Usimamizi mzima wa mienendo ya jumla katika Uchaguzi wa Rais, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani.
ii) Kukuza na kuratibu Elimu ya wapiga Kura
iii) Kusimamia ukataji wa mipaka ya Majimbo ya Uchaguzi Zanzibar.
iv) Kuendeleza daftari la kudumu la Wapiga Kura.
v) Usimamizi wa Kura ya Maoni. Hiyo ndio Tume ya Uchaguzi pamoja na majukumu yake.

Mhe. Mwenyekiti, tukiendelea katika ukurasa wa 50 wa kitabu hichi hichi cha bajeti kifungu 105 kimeelezwa kuwa:

Katika mwaka wa Fedha 2013/2014 Tume ya Uchaguzi imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

i) Kuanza maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 ambao umeshaanza.
ii) Kupitia mipaka, majina na idadi ya Majimbo ya Uchaguzi ya Zanzibar.
iii) Kuendeleza Kura ya Maoni 2014 kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Uchaguzi.
iv) Kuimarisha huduma za Ofisi na kadhalika na mambo mengineyo.

Mhe. Mwenyekiti, tukisema Katiba ya Zanzibar kifungu 119 kifungu kidogo cha 12,13 na 14 kwa ruhusa yako naomba nisome ikiwa kinaeleza kama ifuatavyo:

Kifungu kidogo cha 12 kinaeeleza kuwa katika kutekeleza Madaraka yake yaani hiyo Tume ya Uchaguzi na kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii Tume ya Uchaguzi haitalazimika kufuata amri au maagizo ya mtu yeyote au Idara yoyote ya Serikali au maoni ya Chama cha Siasa.

Ina maana hapa inakwenda moja kwa moja bila ya kuingiliwa na chombo chochote cha hapa Zanzibar. Na sehemu ndogo ya 13 ukurasa huo wa 85 imeelezwa kuwa hakuna mahakama yoyote itayokuwa na mamlaka ya kuchunguza jambo lolote litakalotendwa na Tume ya Uchaguzi katika kuteleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii. Ukienda kifungu kidogo cha 14 na kifungu hicho hicho cha 119 kinasema kuwa: Katika utelezaji wa madaraka yake kwa mujibu wa Katiba hii Tume ya Uchaguzi Zanzibar itashaurina mara kwa mara na Tume ya Uchaguzi ya

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hapa haina mshauri, hapa haina muelekezi lakini yanamaliziana na Tume ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mhe. Mwenyekiti, nimesema vifungu hivi makusudi kwa sababu nataka ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti, nikiangalia kifungu cha 11 ukurasa wa 5 kifungu hichi cha kitabu chetu cha bajeti kinaeeleza kuwa:

Tume ya Uchaguzi wa Zanzibar imeanza matayarisho ya kulipitia Daftari la Kudumu la wapiga Kura kuandikishwa wapiga kura wapya na kuwaondoa wale wote ambao wamepoteza sifa ya kuwa wapiga kura kwa mujibu wa sheria. Aidha katika uwandikishaji huu wananchi waliopoteza vitambulisho vyao vya kupigiwa kura wataweza kupatiwa vitambulisho vipya, huko kwengine sitaki tuendelee kwa sababu ya wakati.

Mhe. Mwenyekiti, tukimaliza hapo naomba kwa makusudi kabisa tufungue Katiba ya Zanzibar na itakuwa ni ukurasa 3 kifungu cha 7 sehemu ya (1) na sehemu ya (2) kama ifuatavyo:-

Wakati daftari la kudumu la wapiga kura limo katika zoezini pamoja na kuandikishwa wapiga kura wapya Katiba inatueleza kuwa.

1) Kila Mzanzibari aliyetimiza umri wa miaka 18 anayo haki ya kupiga kura katika uchaguzi unaofanywa Zanzibar na wananchi.
2) Baraza la Wawakilishi linaweza kutunga sheria ya kuweka masharti yanayoweza kuzuia Mzanzibari asitumie haki yake ya kupiga kura kutokana na yoyote kati ya sababu zifuatazo yaani Mzanzibari huyo awe :

(a) Kuwa na Uraia wa nchi nyengine
(b) kuwa na Ugonjwa wa akili uliothibitishwa na Mahakama Kuu.
(c) Mzanzibari huyo kutiwa hatiani kwa kuendelea kutumikia adhabu kwa kosa la jiani katika Chuo cha Mafunzo isipokuwa kwamba mtu aliekuwa yuko rumande, sheria hii haimgusi, na mwisho.
(d) Mzanzibari huo awe amekosa au ameshindwa kuthibitisha au kutoa kitambulisho cha umri, urai au uandikishwaji kama mpiga kura.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijatoa maelezo yangu naomba nimalizie kwa kifungu cha nne cha Katiba ukurasa wa kwanza kinachosema kwamba:

Katiba hii ni Katiba ya Zanzibar na itakuwa na nguvu za kisheria nchini kote na isipokuwa kutokana na kifungu cha 80 ambacho hapa hakitahusika ikiwa sheria yoyote inayotafautiana na Katiba. Basi Katiba hii ndio itakayokuwa na nguvu za kisheria na hiyo itakuwa batili kwa kiwango kile ambacho kinahitalafiana.

Mhe. Mwenyekiti, nimesema yote haya kwa sababu moja. Mhe. Mwenyekiti, uchaguzi tunafanya hapa kila baada ya miaka mitano na uchaguzi huu ni uchaguzi wa Zanzibar na uchaguzi wa Muungano na Uchaguzi huu wanaotaka kupiga kura ni Wazanzibari kwa Uchaguzi wa Zanzibari na Watazania kwa Uchaguzi wa Muungano.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa kifungu namba 7 .3 ukurasa wa 3 wa Katiba ya Zanzibar na kwa kifungu cha 4 ambacho ndicho chenye mamlaka ya mwisho na hatuna sheria itakayopinga sheria iliyomo katika hii. Nazungumza kwa masikitiko makubwa yanayoendelea katika Daftari la kudumu la Kupiga kura.

Kwanza Mhe. Mwenyekiti, tujue kwamba mtu yeyote ambae ni Mzanzibari keshatimia umri wa miaka 18 anayo haki ya kuwa mpiga kura na anayo haki ya kupiga kura, na sheria zimewekwa vifungu kwa vifungu ambapo atapoteza haki yake hiyo na ikiwa kilichomo humu ndicho chenye uamuzi wa mwisho Katiba hii ndio yenye mamlaka sasa kuna mambo ambayo yananiumiza.

Kwanza Mhe. Mwenyekiti, huko nyuma watu wengi walipiga kura na walikuwa na vipande vya kupiga kura. Lakini uchaguzi huu uliofanywa awamu hii uchaguzi Mkuu uliopita kwa masikitiko makubwa kuna watu maelfu waliachwa wakati wana vitambulisho vya kupiga kura ati hawakusajiliwa tena kwa sababu ya kutokuwa na cheti cha kuzaliwa.

Kwa hivyo, hili kwanza nataka ufafanuzi wa kina na imenitisha hata juzi katika uchaguzi wa Chambani kuna watu hawapigi kura Zanzibar. Lakini wapiga kura wa Jamhuri ya Muungano walikuwa na vitambulisho vyao na wakakoseshwa kupiga kura katika uchaguzi mdogo wa Bunge uliopita inasikitisha.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi leo naomba hasa nipewe ufafanuzi kwa nini Wazanzibari tunakoseshwa haki yetu ya kikatiba ya kupiga kura na cheti cha kuzaliwa hakikutiwa kama ni lazima, na ikiwa ni Katiba ndio yenye mamlaka ya mwisho. Hii Tume ya Muungano inatumia kifungu gani ambacho kinakiuka Katiba ya Zanzibar mpaka watu hawa wakakoseshwa haki zao. Na imeshaanza hata hivi sasa daftari kufanyiwa marekebisho huko kuna watu wana haki ya kupiga kura na hawapewi haki hiyo ya kupiga kura nataka maelezo ni Katiba au Tume ndio ina mamlaka ya kumuandisha Mzanziabri kama mpiga kura hilo ni moja.

Halafu jengine ilikwaje watu wakapewa vitambulisho vya kupiga kura wakapiga kura katika awamu zilizopita ikawa hawakupata tena katika awamu hii. Wakati katiba inasema kama mtu anacho kitambulisho cha kupiga kura ni

sheria gani iliyokiuka Katiba hii ikiwa watu hawa ambao ni kwa maelfu ambao ushahidi wake uchaguzi uliopita huu ulikuwa unawapiga kura kidogo zaidi kuliko ule wa nyuma yake.

Jengine ninalotaka kuuliza Mhe. Mwenyekiti, migogoro tunayoipata kuwa ni lazima upite kwa Sheha ukachukuwe barua uende ukapate kitambulisho cha Mzanzibari mkaazi. Mimi nilikuwa mkali hata tukafatana na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kila wilaya na kutoa tamko jamani Masheha hawana mamlaka ya kumzuia mtu yeyote asipate haki yake ya kwenda kuomba kitambulisho. Hata Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba alisema kuwa Masheha wangu nawaheshimu sana. Lakini kwa hili tutagombana akija mtu mpeni akikwama ni huko huko.

Lakini mimi katika jimbo langu nna watu wengi wanakwenda kuomba barua kwa Sheha kwenda kuomba kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi, lakini Sheha anawaambia mimi nitawapeleka kwa Mkuu wa wilaya, eti kwa sababu hawana cheti cha kuzaliwa. Kuna wengine wameshaolewa na wameshazaa watoto mpaka wanne Sheha anawambiwa kama huna barua kutoka huko pia nikupokee hapa wakati yeye kaja juzi mimi sikuchukuwi.

Kwa hivyo, wanakoseshwa hivi hivi na nasikitika si malaika ambaye kateremeshwa na Mwenyezi Mungu ana makosa chungu nzima sijasikia hata Sheha mmoja kuchukuliwa hatua. Kwa hivyo je, Serikali ina mpango maalum wa hawa masheha kuona kwamba kuwa watu wanakosa haki yao, naomba nijibiwe.

Jengine sasa naingia kwenye Sensa ya Watu na Makaazi kutokana na wakati ulivyo. Mhe. Mwenyekiti, Sensa ya Watu na Makaazi imo katika kifungu cha 41 ukurasa wa 17 na 18 wa kitabu chetu cha Bajeti. Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki cha 41 kinaeleza kama ifuatavyo:-

Matokeo ya awali ya sensa yalizinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzani Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete mnamo tarehe 31 Disemba mwaka jana na yalionesha kwamba Watanzania tuko 44,928,923 na katika hao watu 43,625,354 hawa ni Watanzania ambao wanaishi Tanganyika na watu 1,303,569 hawa ni Wazanzibari.

Vile vile katika sensa hii tukitizama kitabu cha Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais anayeshughulikia Mambo ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ameongeza kuwa katika Wazanzibari hawa 1,303,569 watu wanaoishi katika kisiwa cha Unguja ni 8, 966,721 ambayo ni asilimia 69 ya Wazanzibari wote waliohesabiwa au watu wote waliohesabiwa na wananchi kisiwani Pemba

ambao ni asilimia 31 ni 4,600.868. Lakini Mkoa wa Magharabi una asilimia 46 ya wakaazi hao laki tano tisini na tatu mia sita na sabini na nane.

Mhe. Mwenyekiti, katika kitabu cha bajeti cha Mhe. Waziri wa Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo kifungu cha 31 ukurasa wa 20. Kilisema kwamba:

Idadi imekuwa wastani wa asilimia 2.8 kwa mwaka, tokea mwaka wa 2002. Na kwa hali ambayo inahitaji kudhibitiwa na jitihada ya kudhibiti ifanywe hii ndio ushauri wa Mhe. Waziri katika kitabu chake cha Bajeti ni kwa idadi hii ni kubwa idadi inaongezeka kwa asilimia 2.8 kwa kila mwaka toka mwaka 2002 na kuwa idadi hii inahitaji kudhibitiwa na jitihada ya kudhibiti ifanywe. Ni kauli nzuri sana kwa sababu kweli tunaingiliwa kupita kiasi tuna wageni ambao hawajulikani walipotoka Watanzania na wasiokuwa Watanzania idadi hii inaharibu takwimu zetu.

Lakini ukiangalia kitabu cha Bajeti cha Ofisi wa Makamo wa Pili wa Rais hichi kifungu chake cha 42 ukurasa wa 18 kimeeleza kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa zingatia muda.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: (anaendelea) nazingatia muda lakini leo natoa mambo makubwa naomba uniachie.

Mhe. Mwenyekiti, ni kuwa kitabu cha Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kitabu kimeeleza kuwa idadi hii ni kubwa na kwamba Serikali ijitayarishe kulingana na hii kadiri inavyoongezeka. Lakini kakubali kuwa idadi ni kubwa.
Sasa nasema hivyo Mhe. Mwenyekiti, naomba univumilie kwa sababu tukifungua kifungu cha 120 ukurasa wa 85. Sasa Mhe. Mwenyekiti, idadi imeongezeka tena imeongezeka kwa hali ya juu kabisa, na kuna mpango huu ambao sasa hivi unaendelea tunasikia kuwa kuna ukataji wa Majimbo nasema tunasikia na ukataji wa majimbo huu utazingatia idadi ya watu walivyo katika majimbo hayo na kuwa Tume ikaona kuwa hii idadi inalingana. Mhe. Mwenyekiti, watu wameongezeka na wameongezeka wengi na hasa kisiwani Unguja ikiwa manung'uniko haya yanayotolewa ni ya kweli sina ushahidi kuongezwa majimbo kisiwani Unguja tu kwa sababu ya watu wameongezeka wengi. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kuwa Tume inakuwa inakata Majimbo kutokana na idadi ya watu lakini ningeliomba Tume ikate majimbo kutokana na idadi ya watu wanaopiga kura.

Kwa kuongeza majimbo Unguja siku zote tukapunguza Pemba, Pemba hakuna makosa kuwa hakuna watu wengi kutakana na ufukara tulionao, kwa sababu bado Serikali haijawa na uwezo wa kukiendesha kisiwa cha Pemba

kikawa kina mambo ya maendeleo kama kisiwa cha Unguja. Tuachiwe kama ilivyo maumbile yetu lakini isiwe uzoefu wetu wa kutokuwa na maendeleo na kukosa kufikia kwa watu wengi pia tunaomba isitokee hivyo ikiwa ni sababu ya sisi kupunguzwa majimbo na kuongezwa majimbo huku. Kwa kufanya hivyo nikuivunja demokrasia.

Mhe. Mwenyekiti, suala kama hili lilijitokeza na mwenzetu masikini keshakufa lakini mimi Mhe. Said Ali Mbarouk na Mhe. Marehemu Ahmed Seif tulipinga moja kwa moja katika kipindi kile kukatwa majimbo, kwa sababu tulikwishapata mnong'onong'o kama huu na kwa Pemba kukapunguzwa majimbo baada ya 21 yakawa 8 na huku baada ya 29 yakawa 32. Huu si mtindo mzuri ni mtindo unaokiuka demokrasia Tume iangalie japokuwa inashauriana sana Tume ya Muungano. Lakini iangalie kutenda haki kwa maslahi ya Wazanzibari wote tusifanye mambo kisiasa mwisho tukaja kuona kuwa tumeleta mambo ambayo hayafahamiki yatakayoleta mgogoro baina ya Pemba na Unguja kwa kuwa haki haitendeki kitu ambacho kitatufikisha pabaya, naomba serikali isije ikatupeleka huko.

Mhe. Mwenyekiti, naomba dakika kumi kwa sababu ya masuala ya Muungano.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, zingatia muda.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Ahsante. Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 14 kwenye ukurasa wa 7, kinaeleza kwamba Muungano wetu umeshatimia miaka 49. Mimi nakubali na kuwa ikifika tarehe 26/04/2014 itakuwa ni miaka 50 na kuna sherehe kubwa ya aina yake. Sisi tunatakiwa tujivunie Muungano huu kutimiza hiyo miaka 50. Mimi nasema Wazanzibari tujivunie Muungano huu kutimiza miaka 50 kwa sababu tumefikwa na matatizo makubwa.

Kuna matendo chungu nzima ya Muungano tokea enzi na enzi, tokea Waziri Kiongozi wa kwanza katika nchi hii kafukuzwa kwa sababu ya Muungano, alipotaka kujua Serikali ya Tanganyika ilipo. Ilikwenda hivyo hivyo mpaka hapa tulipo. Kwa hivyo, mimi nawapongeza sana Wazanzibari kwa kuweza kuvumilia mashaka yote ya Muungano mpaka ikafika miaka hii.

Pili, nawapongeza kwa kuustahamilia Muungano pamoja kasoro zote zilizokuwepo. Vile vile nawapongeza kwa kuuchukulia Muungano katika hali hii ilivyo. Lakini kitabu kimesema kuna kero za Muungano hizi zinanung'unikiwa na watu kutoka upande wa pili wa Muungano; yaani Tanganyika na pia wa Zanzibar. Naomba kujua, mimi ninavyojua manung'uniko ni yale yanayotoka Zanzibar tu ambayo tunayaita kero. Je,

Mhe. Waziri aniambie ni manung'uniko gani ya wenzetu wa Tanganyika wanaonung'unikia Muungano huu kama tunavyonung'unikia sisi.

Halafu jengine Mhe. Mwenyekiti, ni kuwa kuna changamoto za Muungano

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, muda wako umemalizika.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Kwa hivyo, kama muda umemalizika, namalizia kwa masikitiko ni kwamba Mhe. Mwenyekiti, tumepata rasimu ya Katiba mpya hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Tume ya Katiba iliyoteuliwa na Mhe. Rais ni tume nzito sana ya wataalamu tena wenye vyeo na kutoka vyama mbali mbali. Tume hii imepita Tanzania nzima na tume hii imechukua maoni ya watu wote na kutokana na maoni imeleta mapendekezo ambayo ni lazima yeheshimiwe.

Mhe. Mwenyekiti, ukifungua ukurasa wa mwanzo tu, inaeleza kuwa Tanzania ni Muungano wa nchi mbili, sio kama ilivyo Katiba ya Muungano. Sasa hii tume iheshimiwe kwa sababu hata Rais kuwa ndiye kiongozi mkuu wa chama cha CCM, ndiye Amir Jeshi Mkuu na ndio kiongozi mkuu wa serikali, kayakubali matokeo haya yaliyoletwa.

Mhe. Mwenyekiti: Tunakuomba umalizie.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Ninamalizia kuwa waheshimiwa ili tufanikiwe tufuate maneno aliyoeleza Makamu wa Pili wa Rais katika kitabu chake cha bajeti, tujue kuwa hii nafasi ni muhimu sana. Hii ni nafasi ambayo sio rahisi kutokea tena. Mwenyezi Mungu atujaalie rasimu hii tuweze kuijadili ili tuzipeleke Zanzibar na Tanganyika pale tunapotaka. Lakini sasa inavyoonekana baada ya kazi yote kufanywa hii, kuna kila mtu analeta mambo yake binafsi kwa faida zake, kwa faida ya chama chake na kadhalika ambapo katika kitabu hiki cha bajeti hakuna nafasi Mhe. Waziri kaeleza kwa urefu kuwa jamani hapa tuwache mtu kujinufaisha kisiasa na kibinafsi na kadhalika. Tuangalie maslahi ya nchi.

Kwa hivyo, ushauri wangu Mhe. Mwenyekiti, kwa vile umenipa wakati mfupi nasema hivi waheshimiwa sisi wenyewe kwanza tuwe kitu kimoja, kwa sababu hii imeletwa kwa sote sio kwa chama wala sio kwa watu binafsi, wala taasisi fulani. Tuyaangalie yaliomo humu halafu tuwasaidie wenzetu wa Baraza la Katiba la Wilaya, yale ambayo yanataka marekebisho yafanywe marekebisho kwa maslahi ya Zanzibar na watu wake. Sasa wale wenzangu ambao kidogo hawajakiamini kuwa hiki kitabu kinatoka kwa wataalamu, naomba waje huko tushirikiane na *Inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu tutafika pale tunapokwenda.

Mhe. Mwenyekiti, ushauri wangu Mwenyezi Mungu akitujaalia tukafika pahala ambapo Zanzibar itakuwa na mamlaka yake kamili na Tanganyika itakuwa na mamlaka yake kamili

Mhe. Mwenyekiti: Tunaomba umalize.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Na Serikali ya Muungano ambayo itakuwa na mamlaka yake hivyo ndivyo tunavyotaka. Nashukuru. *(Makofi).*

Mhe. Ussi Jecha Simai: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, juu ya makadirio na mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti, niungane na wenzangu na mimi kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima wa afya, lakini pia kwa kutuwezesha kuweza kuyajadili mambo yetu kwa maslahi ya wananchi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi nisiwe mwizi wa fadhila nimshukuru Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Waziri pamoja na watendaji wote wa wizara hii.

UTARATIBU

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia kwa utulivu, mheshimiwa alikuwa akikufanyia hivi na hivi na ukanikataza. Ulinikataza kwa amri yake au kwa sababu ya nini. Maana nilikuwa nikimuona kila nilipokuwa nikitaka kuchangia anakufanyia hivi na hivi, halafu unaniambia maliza ni kwa amri yake au ni kwa ruhusa yako, naomba hivyo tu.

Halafu iko haki ya Mhe. Mwakilishi kumuingilia mwakilishi mwingine wakati anachangia.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe ambaye umeuliza swali. Kwanza nataka nikufahamishe kwamba kiti hiki hakiongozwi na taarifa ya mtu ambaye yuko huko. Pili, hakuna utaratibu wa kisheria unaomruhusu mjumbe yeyote wa Baraza la Wawakilishi kumuingilia mjumbe mwenziwe wakati anapokuwa anatoa mchango husika kwa hoja husika. Mhe. Ussi Jecha Simai tuendelee.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Mimi naungana na wenzangu kwa kuwapongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Waziri

pamoja na watendaji wote wa wizara hii, kwa maandalizi mazuri ya kitabu hiki cha bajeti au bajeti kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya shukrani zangu hizo. Mimi sitotumia muda mwingi, nina mambo kama manne tu na nitayazungumza kwa haraka.

Kwanza naipongeza wizara kwa kile kipindi chao kizuri cha kuwahamisha watumishi wote wa Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, kutoka pale Saateni na kuwapeleka kule Maruhubi ambako ni kuzuri sana ukilinganisha na pale walipokuwepo awali. Pia kwa kununua vifaa mbali mbali vya matumizi kwa ajili ya kuendesha idara hii.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nitachangia katika Idara ya Kukabiliana na Maafa. Nimeona wana jitihada nzuri, wamepanga mipango yao mingi. Lakini mimi ningeishauri serikali pamoja na mambo mengi ambayo atayafanya katika idara hii, basi wangefanya utaratibu wa kutafuta angalau baadhi ya vifaa vya uokozi. Kwa mfano hasa wangetafuta maboti angalau mawili, kwa bajeti hii inayokuja wakayaweka katika sehemu zetu za bandari, ili yaweze kutusaidia pale panapoweza kutokea maafa basi waweze kulitatua hili tatizo kwa haraka.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naingia katika Idara za Huduma za Makamu wa Pili wa Rais. Mhe. Mwenyekiti, nataka nitumie kanuni ya 98(6), kifungu cha (a) na (c). Katika kifungu 0701 ambacho kinazungumzia Idara ya Huduma za Makamu wa Pili wa Rais. Mhe. Mwenyekiti hapa natangaza nia yangu ya kuzuwia fungu hili ambalo lina fedha zaidi ya shilingi milioni 780, na sababu zangu kubwa ni kwamba kiongozi mkuu wa shughuli za serikali katika Baraza hili ni Makamu wa Pili wa Rais, ambapo Mhe. Rais amemteuwa huyu kwa niaba ya wananchi wa Zanzibar. Sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambao ni Wawakilishi wa wananchi, kwa muda mrefu tumekuwa tukilalamikia baadhi ya watendaji ambao sio waaminifu.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti za kamati mbali mbali zimezungumzwa hapa kwamba zimefanya kazi na kubainisha mambo tofauti juu ya baadhi ya watendaji ambao sio waaminifu, lakini tunaona kuwa serikali mpaka hivi sasa haitaki kuchukua hatua. Hapa tunatumia Katiba ya nchi. Kuna vifungu mbali mbali kama kifungu cha 10 kimezungumzia juu ya masuala ya kupinga masuala ya rushwa na vitu vyengine. Utumiaji mbaya wa madaraka umezungumzwa humo dhidi ya umma.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, hadi hivi sasa serikali hii kweli haitaki kutusikia lakini kuna ilani ya uchaguzi wa CCM ambayo pia inaweza kutuongoza katika kukamilisha mambo yetu katika nchi hii, inapinga moja kwa moja kwamba moja kati ya mambo muhimu ambayo ilani ya CCM imezungumza,

basi ni suala la kuondosha ubadhirifu wa mali ya umma, vitendo vya rushwa na mambo mengine yamekatazwa moja kwa moja na sisi ilani hii ndio tunayoifuata na kuitekeleza, akiwemo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, yeye ni kiongozi mkubwa sana ambaye anatakiwa aisimamie.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kama mwakilishi ambaye natoka katika Chama cha Mapinduzi, naona faraja kubwa sana endapo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais leo ama kesho itakapopitishwa bajeti hii atasimama kutujibu hoja zetu hizi. Je, hadi hivi sasa serikali imechukua hatua gani, tunataka tumsikie sauti yake yeye kama kiongozi mkuu wa shughuli za serikali, atueleze leo hapa, tuna hamu kumuona anasimama anatueleza juu ya namna gani serikali imechukua hatua.

Mhe. Waziri tunamshukuru sana mara nyingi amekuwa akijibu hizi hoja, tunataka yeye kama kiongozi mkuu katika Baraza hili basi leo atueleze ni hatua gani ambayo serikali imechukua dhidi ya watu ambao wametuhumiwa katika kufanya mambo ya ubadhirifu wa fedha za wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo nitazungumza ni katika Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali ambapo kifungu cha 1901, Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kazi nyingi au mambo mengi ambayo imejipangia idara hii, katika mwaka wa fedha 2012/2013 imekuwa ikifuatilia utekelezaji wa ahadi za viongozi wakuu wa kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, katika lile ambalo tuna ahadi nyingi na za zamani za Viongozi Wakuu wa Kitaifa katika Jimbo langu la Chaani. Mwaka 2008 Mhe. Rais mstaafu Dk. Karume, aliwaahidi wananchi wangu wa Shehia ya Moga kwamba watachimbiwa kisima cha maji. Lakini mwaka 2010 wakati wa kampeni Mhe. Rais Dk. Shein aliwaahidi tena kwamba atawachimbia kile kisima cha maji.

Katika utawala wa Dk. Shein sasa hivi tumeingia nusu muhula, tuna miaka miwili na nusu, tukipitisha bajeti hii tuna miaka miwili na nusu ahadi hiyo bado haijatekelezwa hadi hivi sasa. Lakini serikali nayo haijatueleza lolote juu ya utekelezaji wa hizi ahadi za viongozi wakuu wa kitaifa, ikiwemo ahadi hii ya Moga. Kwa hivyo, hapa napo mimi nitakuwa mgumu sana na nina nia ya kuzuia fungu hili hadi nipate maelezo mengine.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, pia katika mwaka 2010 Mhe. Rais Dk. Shein aliahidi uchimbaji wa kisima katika katika eneo langu pale Shehia ya Kinyasini, lakini hadi hivi sasa bado hatujaona suala hili kwamba linafanyiwa kazi na linatekelezwa vipi. Kwa hivyo, mimi katika bajeti hii nitazuwia vifungu vyangu viwili kama nilivyozungumza, Idara ya Huduma ya Makamu

wa Pili wa Rais na Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali, hadi nipate maelezo yenye kutosheleza ambayo pia yanawatia moyo wananchi wangu wa Jimbo la Chaani kwa bajeti hii tunayoingia keshokutwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nakushukuru sana, ahsante sana.*(Makofi).*

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia kidogo bajeti hii ya Wizara ya Makamu wa Pili wa Rais. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu na kumpongeza Mhe. Waziri kwa kutuletea bajeti hii ya Wizara ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nizungumzie suala zima ambalo linahusu Idara ya Maafa. Mhe. Mwenyekiti, katika kitabu hiki ambacho amezungumza Mhe. Waziri alizungumzia mikakati ambayo ipo katika kukabiliana na Idara ya Maafa katika ukurasa wa 41 ambapo kuna mipango na mikakati katika kupambana na kujitayarisha na masuala ya maafa wakati pale yanapofika.

Mhe. Mwenyekiti, idara hii ya maafa katika kutoa mafunzo kwa muda mrefu na muda mfupi kwa wafanyakazi ambao wanatayarishwa kupewa mafunzo ni wafanyakazi 8. Mimi Mhe. Mwenyekiti, ningependekeza kwamba kutolewe mafunzo kwa vijana wetu ili wakati yanapotokea maafa basi waweze kusaidia na kuondoa yale ambayo yaliyotokea katika kipindi kilichopita, katika masuala mbali mbali ya majanga ya meli ambayo yalitokea katika taifa letu hili.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa 42 kuhusu Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa. Mhe. Mwenyekiti, tumepanga mikakati mbali mbali ya kusherehekea miaka 50 ya Mapinduzi matukufu ya mwaka 1964. Naipongeza sana serikali kwa kujipanga vizuri katika kuadhimisha sherehe zetu hizi ambazo zitakuwa ni historia kwa nchi yetu hii, kwa kutimia miaka 50 ya Mapinduzi matukufu ya mwaka 1964.

Mhe. Mwenyekiti, historia kwa wale ambao watakuwa wanatimia miaka 50 na wale ambao sisi tunaelekea huko katika miaka ya 50 tutakuwa na fursa kubwa ya historia ya nchi yetu kwa watoto wetu ambao ndio watakuwa viongozi wa baadae katika kuliongoza na kuiongoza nchi yetu hii katika misingi iliyo bora, kwa kuzingatia kwamba sherehe hizi ndizo zilizotufanya sisi leo hapa tupo katika Baraza lako tukufu hili, tukiwa wazalendo Wazanzibari na Watanzania ambao tunajidai na tunaongoza nchi yetu hii mbele ya jemedari Dk. Ali Mohamed Shein. Haya yote ni matunda ambayo yametokana na wazee wetu na leo hii tuko hapa tukiwa katika mikakati na mipango ya kusheherekea miaka 50 ya Mapinduzi matukufu ya mwaka 1964

Mhe. Mwenyekiti, mengi yamezungumzwa katika Baraza letu hili tukufu, kila mjumbe amezungumza yale aliyoyataka. Hivi punde Mhe. Mwenyekiti, mjadala ulitaka kuharibika baada ya mjumbe kutaka kuingiliwa au kuwa na wasi wasi na mjumbe mwengine. Haya yote Mhe. Mwenyekiti, yanatokana na kutokufahamu, kutokuelewa na kutokujua faida ya Mapinduzi Matukufu na Muungano wetu tulionao, ambapo mwaka 2014 ndio tunafikisha miaka 50 tukijaaliwa.

Mhe. Mwenyekiti, Muungano wetu ambao umetufikisha hapa katika kutujenga kwenye umoja, mshikamano na upendo tulionao wa Watanganyika na Wazanzibari. Haya yote yalitokana na upendo, uzalendo na kuthamini uzalendo wetu kwa viongozi wetu waliotangulia na kutufanya sisi leo hii kuwa wamoja, wenye mshikamamo katika Serikali yetu ya Umoja wa Kitaifa. Haya nadhani ni wajibu wetu sisi kuyaenzi na kuyaendeleza. Halikadhalika tuuendeleze Muungano wetu kwa faida yetu sote.

Mhe. Mwenyekiti, nimethubu kuzungumza haya kwa sababu sisi wenyewe viongozi wetu wakuu wako baadhi yao kwa kweli wanaturejesha nyuma kwa kutopotosha na kuelekea katika kuuondoa umoja wetu na mshikamamo tuliokuwa nao.

Mhe. Mwenyekiti, nazungumza hili kwa masikitiko niliyokuwanayo, kwa sababu kuna viongozi wetu baadhi ambao wako katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa, kwa kutumia madaraka waliyonayo na kutumia madaraka ya vyama vyao wanapokuwa katika sehemu nyengine ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, yaani nakusudia Tanganyika wamekuwa wakiuunga mkono Muungano wetu huu, lakini wanapokuwa hapa katika visiwa vyetu basi wana ulani na kuupiga vita. Hii sio tabia nzuri kwa sababu hatuelekei kule ambako tunakotaka na kuendeleza umoja na mshikamano wetu tuliona, kwa sababu kiongozi huyo huyo anathubuku kusema na kuwasemea Wazanzibari kuukataa Muungano, hili ni jambo la kusikitisha sana Mhe. Mwenyekiti. Anapokuwa katika Jamhuri au katika ardhi na sehemu nyengine ya Jamhuri ya Muungano basi anautetea Muungano, lakini anapokuwa hapa anasema tuukatae Muungano. Tumuelewe vipi, hili ni jambo la kusikitisha sana. Ni jambo la kusikitisha na hatuelekei katika mustakabali mzuri wa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nina umri wa miaka 45. Miaka 45 sio mdogo, nafahamu, ninaelewa na ninajua. Kiongozi wetu mwenye umri wa miaka kama 60 au 65 anatuelekeza katika mustakabali ambao sio mzuri. Mimi nathubutu kusema kwamba kwa sababu humu ndani sote ni wajibu wetu kuwaelekeza wananchi wetu katika mustakabali mzuri, sio kukaa na kuanza kufanya mambo yanayotuelekeza katika hali ambayo sio nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, hili ni jambo la kusikitisha sana na imenibidi niliseme kwa sababu nimechemshwa. Sote ni Watanzania, sote ni Wazanzibari na sote ni wazalendo, hakuna Mpemba wala hakuna Muunguja na hakuna Mtabora wala hakuna Mshinyanga. Sote ni Watanzania na sote ni wamoja. Kwa hiyvo, tukianza kusema hivi na vile tutafika mahali nchi hii itakuwa kama Somali na nchi nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, historia ya Somali wanatoka mbali. Mhe. Mwenyekiti, mwaka 2006 nilibahatika kwenda katika nchi ya Rwanda, ambapo nchi hii walipitia katika migogoro mbali mbali. Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu, niseme hali ya Rwanda

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe tungekuomba zaidi uingie kwenye bajeti yetu.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, niache nipumue. Mheshimiwa nakuomba niache nikohowe. Naeleza kutokana na uchungu na lazima tuwe wamoja, lazima tupendane ili kuirudisha amani ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, unapofika Rwanda suala la ukabila, suala la kutengana halipo, wameshikana wamekuwa wamoja na wanapendana. Sasa leo viongozi wetu. Mhe. Mwenyekiti, kiongozi wa pili wa nchi hii kusimama kuwasemea Wazanzibari, asemee chama chake, asiwasemee Wazanzibari katika kuusemea Muungano wetu.

Mhe. Mwenyekiti, mwenye mamlaka ya kuwasemea Wazanzibari ni Rais peke yake, asemee chama chake na hao wengine wasemee chama chao wasiwasemee wenzao wengine. Kila mmoja na chama chake na kila mmoja na mapenzi yake na kila mmoja na maamuzi yake, sote tuko katika kuulinda na kuuendeleza Muungano wetu, kwa sababu umetuletea faida, umetuletea umoja, umetuletea mshikamano, upendo na udugu tulionao. Ni lazima tuseme mheshimiwa tusidanganyane, tutakuja kuwaweka wananchi wetu katika hali iliyokuwa mbaya. Watakujakuwa kama Wasomali au Wasudani, yatakuja kutokea kama yaliyotokea Rwanda. Mhe. Mwenyekiti, tusiangalie mambo haya kimasihara. Mhe. Mwenyekiti, viongozi ndio dira ya mambo yote, sasa leo kiongozi anasimama anapotosha, hili sio jambo zuri kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nazungumza haya kwa uchungu na kwa kuipenda nchi yangu na kuwapenda Wazanzibari wenzangu na Watanzania wenzangu. Mhe. Mwenyekiti, nawahakikishieni kwamba Muungano huu hauvunjiki na tutaendelea milele na milele.

Mhe. Mwenyekiti, kwa vile nimesimama na nilikuwa sijajipanga vizuri. Lakini yale ambayo nilikuwa nimekusudia nimeyasema na mmenisikia na Wazanzibari na Watanzania wamenisikia. Yule ambaye hautaki Muungano wetu huu, basi akae pembeni, atuwache tuendelee na Muungano wetu, ili tuishi kwa amani na upendo tulionao.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono kwa asilimia mia moja *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atatujaalia. *(Makofi).*

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii kuweza kuchangia hotuba ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ya Makadirio ya Mapato na Matumzi ya Fedha kwa mwaka 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema sitaki nirudishe kilio matangani, kwani naamini aliyekwishakufa ndio kishakufa hasikii tena huyo. Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaingia katika sekta ya elimu, katika ukurasa wa 15.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri katika hotuba yake hii alisema kwamba kwa upande wa sekta ya elimu, serikali inaendelea na mipango yake ya kuwapatia vijana elimu bora na kujenga skuli mpya na za kisasa za wilaya na kujenga maabara. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hayo nakubaliana na Mhe. Waziri, lakini lengo ni kupanga mipango mizuri ya kuwapatia vijana wetu walimu walio watendaji na ambao wana uwezo wa kuwasomesha vijana wetu na kutupatia elimu iliyo bora.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, tukumbuke kwamba kiwango cha elimu Zanzibar kimeshuka kwa kiasi fulani, hii yote ni kwa sababu ya kukosa walimu walio na uwezo wa kutusomeshea watoto. Watoto wanaosomeshwa hawana elimu kutokana na kusomeshwa na walimu waliokuwa hawana uwezo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aliangalie sana suala la kuwaajiri walimu, waajiriwe walimu wenye uwezo na ambao hawana itikadi na watakaoweza kutusomeshea watoto ili kurudisha kiwango cha elimu katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile tuwache itikadi zetu za kuwaajiri walimu waliokuwa hawana uwezo, hili ni tatizo kubwa sana kwa nchi yetu. Kumuajiri mtu kwa maslahi yake yeye, sio maslahi ya mtu ni maslahi yake yeye na hili ni tatizo kubwa Mhe. Mwenyekiti. Tuwaangalie watoto wetu sasa hivi na elimu yetu ilivyo Zanzibar, elimu imeshuka, watoto wanazurura, watoto hawasomi kutokana na uajiri uliokuwa mbovu. Mtu anaajiriwa ambaye hajafikia kiwango cha kusomesha watoto wetu, anaajiriwa mtu wa darasa la tisa hajafikia kusomesha watoto wetu.Yule ambaye ni darasa la 12 pengine anakwenda kule darasa la 16, anakwenda pale ajira ni ndogo haajiriwi kabisa.

Hii ni kutokana na itikadi zetu. Mhe. Mwenyekiti, suala hili namuomba Mhe. Waziri aliangalie sana.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, katika hiyo ajira kuna walimu ambao wameajiriwa tangu mwaka 1995 au mwaka 2000, lakini mishahara yao ni midogo kuliko walimu walioajiriwa mwaka 2010 au 2011, yaani hawa mishahara yao inakuwa juu zaidi. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti aliangalie suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba nizungumzie kuhusu suala la migogoro ya ardhi. Kwa kweli migogoro ya ardhi hichi ni kitendawili kikubwa ambacho hakina mfumbuzi mpaka hii leo. Hivi sasa inafika mpaka watu kugombana, yaani ndugu hawazikani au hawaelewani ama kuhasimiana tatizo la migogoro ya ardhi. Suala hili si kwamba linakuja kwa Mhe. Waziri hata na sisi Wawakilishi linatujia pia, kwa sababu anatoka mtu anakuja kutupa lawama zake na wewe huna jinsi vya kumtatulia. Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, suala hili la migogoro aliangalie sana, kwani linaweza kutuletea athari katika nchi yetu.

Nikiendelea na mchango wangu naomba sasa nizungumzie kuhusu suala la mapambano dhidi ya madawa ya kulevya. Kwanza naomba niipongeze Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na halafu nimpongeze Mhe. Waziri, Katibu pamoja na watendaji wake kwa kupewa uwezo na Mwenyezi Mungu kupambana na suala hili la madawa ya kulevya, suala hili limepungua kwa kiasi fulani.

Mhe. Mwenyekiti, kupungua kwa suala hili isiwe ndio sababu ya kulidharau pia nimuombe Mhe. Waziri pamoja na serikali kwa kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, licha ya kupungua kwa matatizo haya ya madawa ya kulevya na watu wetu wanaotumia madawa haya ya kulevya. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri pamoja na serikali kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, wapige vita wale wanaoingiza haya madawa ya kulevya, kwa sababu madawa ya kulevya ndiyo yanayotuletea athari katika nchi yetu na watoto wetu na ikiwa madawa haya hayakuingizwa naamini hakuna mtu yeyote atakayetumia madawa haya.

Sasa niende kwenye suala la afya. Kwa kweli macho yetu yote tunaangalia kwenye suala hili, kwa sababu kutokana na matatizo yetu wananchi au binadamu kila mmoja anaangalia afya iko vipi. Mhe. Mwenyekiti, suala la afya liangaliwe kwa kina. Kwa mfano, tukiangalia hospitali zetu ambazo hivi sasa zimepewa majina makubwa kama vile kuna Hospitali ya Rufaa, Hospitali ya Wilaya, Hospitali za Mikoa, yaani hospitali hizi zimepewa majina, lakini ukiangalia utendaji wake ni mdogo, pia dawa kidogo na hata wagonjwa walioko kule ni matatizo matupu.

Mhe. Mwenyekiti, kitanda wanalala wagonjwa watatu au wanne na wengine utakutia wagonjwa wako chini wanagaragara, kweli hospitali hii ndio ya kuitwa ya rufaa. Kwa kweli suala hili naomba liangaliwe vizuri.

Vile vile naomba nizungumzie kuhusu suala la uwezeshaji wananchi kiuchumi kifungu cha 12. Mhe. Mwenyekiti, masuala ya uwezeshaji kiuchumi na kukuza ajira ni miongoni mwa mambo yanayopewa kipaumbele na serikali na kutekeleza mipango mbali mbali inayolenga kuwezesha wananchi kiuchumi hususan wenye kipato cha chini na kumudu maisha yao ya kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli jambo hili naungana nalo lakini ni vyema tuliangalie suala la uwezeshaji na tuangalie jinsi ya mikopo inavyotolewa na watu wanaopewa. Kwa hivyo, kuhusiana na suala hili ni vizuri serikali ikajipanga na tuangalie ile mikopo jinsi inavyotolewa inatolewa vipi pamoja na kupewa elimu wale wanaopewa mikopo, kwa ajili ya kuweza kuitumia vizuri, kwa sababu vipo vikundi vya ushirika ambavyo vinapata mikopo lakini hawana elimu.

Kwa maana hiyo, naomba suala hili liangaliwe vizuri Mhe. Mwenyekiti, namna ya kutoa mikopo pamoja na utaratibu wa kuitumia, kwani wakati mwengine mtu anachukua mkopo na kurejesha ni tatizo, kwa sababu hana elimu ya mkopo na hata ile ya ushirika. Hivyo, naiomba serikali kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, iliangalie sana jambo hili ili lisitokezee. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba nije kwenye kitabu kikubwa ukurasa wa 68 211202 kuhusu ununuzi wa sare. Kwa kweli hapa Mhe. Mwenyekiti, naona kuna shilingi 1,600,000/= kwa mwaka 2011/2012 na mwaka 2012 kuna shilingi 5,000,000/=. Sasa namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, wakati atakapokuja kutoa ufafanuzi basi hapa aje anisaidie maelezo zaidi.

Vile vile kwenye ukusara huo huo kifungu cha 211110 posho maalum, mwaka 2011/2012 kuna shilingi 23,644,340/= na ukiendelea kuna shilingi 40,000,000/=, pia hapa namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, wakati atakapokuja kufanya majumuisho anisaidie maelezo zaidi.

Katika ukurasa wa 66 kifungu cha 220402 kuhusu gharama za *diesel* mwaka 2011 kuna shilingi 2,000,000/= na mwaka 2012 kuna shilingi 8,000,000/= pia katika hili namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, wakati atakapokuja kufanya majumuisho anisaidie maelezi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, ahsante nashukuru na mimi kwa kunipa fursa hii ya kuzungumza machache kuhusu bajeti hii.

Kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Makamo wa Pili wa Rais kwa hekma, busara pamoja na anavyotuongoza vizuri katika Baraza hili. Pia nimshukuru Mhe. Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pamoja na watendaji wake wote kwa kazi zao nzuri ambazo wanazifanya kwa kutuletea bajeti hii. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, nianze mchango kwenye ukurasa wa 7 kuhusu masuala ya muungano. Kwanza nianze kuchukua fursa hii kuipongeza Tume ya Marekebisho ya Katiba kwa kuratibu maoni ya wananchi ambayo ni kazi kubwa tena nzuri walioifanya ya kuchukua maoni ya wananchi. Kwa kweli nataka nitoe pongezi za dhati kwamba walichukua maoni ya kila mtu ambaye aliyatoa na yalithamini na kufanyiwa kazi yakapelekwa yanakohusika. Kwa hivyo, sasa tunakwenda kwenye mchakato wa pili kuhusu Mabaraza ya Katiba. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kuwaomba wananchi wa Zanzibar waweze kutoa maoni mazuri ambayo ya kuiboresha Rasimu ya Katiba hii, ili yakidhi matarajio ya wananchi. Kwa hivyo, maoni mazuri yatapatikana kwanza kwa kuweza kuthaminiana, yaani kila mtu kuthamini maoni ya mwenzake. Pili tuweze kuilinda amani yetu, kwani amani hii ikitoweka itakuwa hakuna wa kuweza kuirejesha. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, kupitia hili naomba nitoe wito kwa vijana, hivyo nawaomba vijana watulie na waweze kutoa maoni yao katika hali nzuri tena ya utulivu, bila ya kuhatarisha amani yetu, lakini pia wakijua wao ndio warithi wetu wa nchi hii, kwa hivyo waweze kutulia ili tutakapoondoka sisi wazazi wao hapa, basi wajue kama hii nchi ni ya kwao na wao ndio viongozi ambao tunaowatarajia. Kwa maana hiyo, waachie mambo ya papara pamoja na jazba na hayo hayatatusaidia. Vile vile nitoe wito wangu kwa akina mama wenzangu kwamba tusikubali kurubuniwa kuipoteza amani ya nchi hii ambayo ikitoweka madhara yake makubwa yatakuwa ni kwa wanawake na watoto. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, niwaombe sana wanawake kuwa watulivu ili amani hii tuendelee kuijenga katika nchi yetu na tukijua mbuyu hizi zinakaangwa, lakini zikiwiva wenye meno tutakuwa ni sisi wanawake na watoto wetu, kwani hatutamuona mwanamme hata mmoja kubali ikitokea vurugu wanaume watatukimbia na sisi ndio tutakaobaki na watoto wetu tukihangaika huku na huku. Kwa hivyo, niwaombe sana akinamama wenzangu kupitia kwako Mhe.

Mwenyekiti, kwamba waweze kutulia na kuwa watulivu na nafasi hii tuliyoipata basi tuweze kuitumia vizuri. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije kwenye ukurasa wa 19 ambapo kuna masuala ya watu wenye ulemavu. Kwa kweli serikali lazima izingatie haki za watu wenye ulemavu kwa kuwapatia mahitaji yao mbali mbali na huduma, ili waweze kufikia malengo yao, wito kwa wananchi waweze kufichua watoto wenye ulemavu kwa ajili ya kupatiwa haki zao za msinigi ikiwemo elimu. *(Makofi)*

Sasa niende kwenye ukurasa wa 21 ambapo Mhe. Waziri katika kitabu chake ametuelezea hapa kuhusu jinsia na watoto. Mhe. Mwenyekiti, naishukuru serikali kwa kutujengea uwezo akinamama kushiriki kwenye nafasi za utoaji wa maamuzi. Vile vile nichukue fursa hii kumuomba sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kumshauri vyema Mhe. Rais, ili aweze kuongeza nafasi hizi za wanawake ambao wenye uwezo katika nafasi za utendaji, kwa ajili ya kuweza kumsaidia Mhe. Rais kwamba tukijua kuwa wanawake na wala hakuna anayeweza kupinga kuwa wanawake Mwenyezi Mungu ametushushia imani, waaminifu, woga wa kuiba fedha za serikali. Kwa maana hiyo, naamini Mhe. Makamo wa Pili wa Rais akimshauri vizuri kwamba wanawake waendelee kuwapa nafasi, basi tunaweza tukajenga mustakbali mzuri wa serikali yetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nadhani hakuna atakayepinga mawazo yangu haya, kwa sababu niseme mwanamme yeyote ambaye amefikia mafanikio mazuri basi ubavuni kwake yuko mwanamke mwenye hekma na busara ambaye anamshauri vizuri. *(Vicheko/Makofi).*

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye ukurasa wa 29 kuhusu Idara ya Mipango Sera na Utafiti. Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nimuombe Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kuiangalia idara hii kwamba ndio kiungo muhimu kabisa, kwa hivyo idara kama hizi kwenye mawiza kuna upungufu wa wataalamu. Pia nimuombe Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba idara hizi aweze kuziingizia fedha vizuri ili ziweze kufanya majukumu yake kama ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, katika idara hii wakati tunapokuwa na mipango mbali mbali ya serikali, basi ni lazima tuzingatie kwani serikali ina majukumu mengi pamoja na mipango yake yote ya serikali inazingatia kuwapelekea huduma bora wananchi wake. Lakini utakuta wakati mipango inapopangwa serikali inakosa kuzingatia kwenye miradi ile inayoipelekea jamii kuzingatia kuwa mmoja kutouathiri mwengine.

Kwa mfano, kwenye Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, utakuta kuna ujenzi wa barabara basi naiomba serikali iwe inazingatia kwa sababu barabara huwa inajengwa kwa thamani kubwa na fedha nyingi, lakini utaona pale pale baada ya siku tatu tu inawezekana akaja mwenye huduma ya maji akawa anataka kuwapelekea maji wananchi wake, basi utaona barabara ile kaivunja kwa muda mdogo sana. Kutokana na hali hiyo, naiomba serikali kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, wakati mipango ya serikali inapopangwa basi iwe ni ya muda mrefu na yenye kuzingatia mambo mengi.

Niende kwenye ukurasa wa 33 katika Idara ya Kuratibu Shughuli za Serikali. Mhe. Mwenyekiti, niiombe idara hii kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kufuatilia kwa makini ahadi za viongozi wetu wakuu wa kitaifa kwa sababu ya kuwajengea heshima kubwa viongozi wetu hawa, kwa sababu ahadi zao zisipotekelezwa ina maana wengine wanafika kuondoka kwenye madaraka bila ahadi zao hizi kutekelezwa na wala hili si jambo la heshima kwa viongozi wetu. Kwa hivyo, naiomba idara hii iweze kuzifuatilia kwa karibu ahadi za viongozi wetu wakuu na kuzitekeleza kwa wakati muafaka ambapo kiongozi yule anakuwa madarakani.

Sasa naomba nizungumzie kuhusu Tume ya Uchaguzi Zanzibar kwenye ukurasa 49. Kwanza niipongeze tume kwa kazi zake nzuri inazozifanya, pia tume hii iendelee kuwapatia elimu wananchi katika uandishi wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ambapo watu wengi wanakuwa wanajizonga, hivyo ni vyema kuendelea kutoa elimu. Sambamba na hili waendelee kutoa elimu ya wapiga kura wakati unapofika ili wananchi waweze kutumia haki yao ya msingi vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, kuna kiongozi juzi alisema hapa kama labda hii tume ina miaka mingi ndio hiyo kwa hiyo tu, kwa nini kusiwe na mabadiliko. Lakini mimi nasema hii yote nimpongeze Mhe. Rais na imeonekana utendaji wake ni mzuri na kama utendaji ukiwa mbovu huwezi kuaminiwa kiasi hicho chote. Kwa kweli hii inatupa ushahidi kwa sababu kuna kiongozi ambaye anayegombea Urais tangu wakati wa chama kimoja na mpaka leo anaendelea kugombea Urais, je tuseme hakuna mwengine mwenye uwezo? Lakini ni kwa sababu watu wamemuamini. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, tume hii tuendelee kuiamini kwa sababu bado inaendelea kufanya kazi vizuri. *(Makofi).*

Katika ukurasa wa 17 ambao unazungumzia kuhusu Sensa ya Watu na Makaazi. Mhe. Mwenyekiti, hapa nina masikitiko kidogo kwa sababu tunajua wakati wa sensa, basi kulikuwa na watu ambao hawakuweza kujitokeza kwenye zoezi hili jambo ambalo linarudisha nyuma mipango ya serikali. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, wakati

atakapokuja kufanya majumuisho, basi aweze kutumia fursa hiyo kwa ajili ya kuzidi kuwaelekeza wananchi wetu wasije wakaona labda wanadhulumiwa, lakini kumbe wanajidhulumu wao wenyewe kwa kukosa kuzitumia haki zao za msingi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niseme nashukuru na ninaipongeza na ninaitakia heri bajeti hii iweze kupita kwa salama, tuweze kuwa na mipango mizuri ya serikali.

Baada ya kusema hayo, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kaskazini naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi).*

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kunipa fursa hii ya kuchangia machache kwenye hotuba hii ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2013/2014.

Kwanza naomba nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuleta hotuba yake hii pamoja na watendaji wake ambao wamemsaidia kazi hii na kuweza kuiwasilisha mbele yetu. Kwa kweli sisi kazi yetu kubwa ni kupitia na kuona wapi kuna changamoto na tuweze kuzisawazisha. *(Makofi)*

Nianze mchango moja kwa moja kwenye Ofisi hii ya Makamu wa Pili wa Rais, ambayo ina majukumu mengi na taasisi zake nyingi ambazo zimo ndani ya ofisi hii ikiwemo Ofisi ya Faragha, Idara ya Uendeshaji wa Utumishi, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali, Idara ya Kukabiliana na Maafa, Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa, Idara ya Upigaji Chapa, Ofisi ya Pemba, Tume ya Uchaguzi pamoja na Ofisi yetu hii ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli ofisi hii ina majukumu mazito kwenye taasisi zake hizi mbali mbali na hasa nikenda na Ofisi zile Kuu za Pemba. Kwa kweli ofisi Kuu za Pemba katika taasisi mbali mbali zina kuwa na mapungufu ya hapa na pale kwa kupewa yale mambo muhimu ya kuendesha ofisi hizo. Kwa hivyo, nachukua fursa hii kuiomba serikali kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, na huko Pemba basi ielekeze nguvu zake kwa kiasi kikubwa.

Sasa nataka nizungumzie kuhusu maslahi ya wafanyakazi na hasa kwenye likizo. Kwa kweli kwenye sekta hizi mbali mbali ni kwamba likizo ni jambo la muhimu, mbali na mishahara likizo mtu akisha kufanya kazi kwa muda wa mwaka mmoja anahitaji apate mapumziko. Lakini kwenye vifungu hivi idara nzima kuna shilingi 400,000/=, hivi ni wafanyakazi wangapi watapewa

shilingi 400,000, kwa sababu na hii ni moja ya kumpa moyo mfanyakazi kwamba aweze kujisikia kuwa na yeye ni mfanyakazi na amepata mapumziko, basi aende akapumzike yeye na familia yake.

Mhe. Mwenyekiti, kisheria huko nyuma niliona kwamba ilikuwa mtu anapewa fursa ya kuondoka kwenda likizo wewe na mke wako pamoja na watoto wako wanne. Lakini sasa unakuta kwamba mtu anachukua likizo na anapewa shilingi 30,000/= hivi kweli hata pale shamba atafika na watoto wake wale pamoja na mkewe na hili ni tatizo na hasa kwa wale wafanyakazi ambao ni wengi ambao hawana *skills*, kwa sababu hii ni fursa moja ya kuwaondoshea matatizo ya hapa na pale. *(Makofi)*

Kwa hivyo, kwa mujibu wa sheria ni kwamba mtu anapewa likizo anatembea Afrika ya Mashariki mpaka inapofika meli, yaani inawezekana mpaka Mombasa almuradi ni Afrika ya Mashariki ikiwa hapo nyuma tulipoanza tulikuwa tunapata fursa hiyo na hizi zinaweza kumsaidia. Kwa maana hiyo, utaona fedha nyingi zinatiwa kwenye maeneo kama vile *foods and beverage*.

Mhe. Mwenyekiti, naomba fedha hizi tungezielekeza huko ili na hawa wafanyakazi na wao wakajisikia, kwa sababu mtu unapofanya kazi unachokitegemea ni pale kazini kwao utategemea kwa kiasi kikubwa. Lakini bado unawakuta wafanyakazi wengi wanapata changamoto kama hizi fedha za likizo zinakuwa hazitoki. Kutokana na hali hiyo, nadhani tungepanga utaratibu wa likizo.

Nikiendelea na mchango wangu na wenzangu wamezungmzia sana kwenye suala la muungano na mimi sitaki niende huko kwa sababu tayari wameshalizungumzia sana na kwamba sasa tufike pahala tuchangie hii bajeti na kila mtu amejilabu kwa upande wake.

Sasa naomba niende kwenye ukurasa wa 61 ambako kuna kiambatanisho kinachoonesha hizi kero. Mhe. Mwenyekiti, kero hizi naona nyingi za Zanzibar au tunajivutia kwetu tu, yaani kero hizi zote ni za Zanzibar na wala hakuna kero nyengine zinazozungumzwa katika hapo yaani watu wanapokutana viongozi wetu zinazungumzwa hizi zinazohusu Zanzibar au wenzetu hawana kero hizo kama hawana basi kutakuwa na matatizo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme kwamba hapa kwa mujibu wa kiambatanisho zinaonekana ni kero za Zanzibar na niliwahi kusikia kwamba kuna kero moja ambayo wenzetu wa Tanzania Bara walikuwa wakiilalamikia ni kuhusu kwenye Katiba inaeleza Rais akitoka upande mmoja, basi mara nyengine atoke upande mwengine na wao walikuwa wakiilalamikia kuhusu kwa nini Mzanzibari akaendeshe wananchi ambao kwa kiasi kikubwa sana

Watanzania Bara. Lakini bado sijaiona kwenye hizi kweli wenzetu na wao wanazo kero kama hizo na kwa nini kama yapo yasiorodheshwe kwenye kiambatanisho hichi.

Vile vile suala jengine niseme kwamba ninakwenda moja kwa moja kwenye mchango wangu kwamba tutakapoipitisha bajeti hii, sisi kama Wawakilishi wa wananchi baadae tunataka mafanikio yapatikane. Kwa hivyo, jambo la msingi ni kufuata zile sheria za matumizi na kwa kiasi kikubwa kwamba taasisi zetu zimeonesha kuwa zinakiuka zile taratibu za fedha pamoja na zile sheria za manunuzi.

Mhe. Mwenyekiti, niseme sisi kama Baraza la Wawakilishi hapa tunazo kamati zetu za Baraza za Kudumu, ikiwemo Kamati yangu ya *PAC* ambayo hii ina majukumu ya kuisimamia serikali na nimewahi kusema hapa kwenye Baraza lako tukufu Mhe. Mwenyekiti, tunapofanya mikutano mbali mbali na *PAC's* ambazo tunafanya kubadilishana mawazo na *PAC's* nyengine inaonekana kwamba yale yale ambayo hapa tunazungumza tunayoisimamia serikali na kwa wenzetu yapo pia.

Lakini inaonekana kamati yangu ya *PAC* inapofanya kazi zake, basi inaonekana kama ni utashi wa mtu binafsi. Kweli upo utashi wa mtu mmoja mmoja na mimi hilo sikubaliani nalo na pale tulipokuwepo kwenye vifaa mbali mbali kwa mfano juzi tulikuwa na semina sisi wajumbe pamoja….

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kwa mujibu wa muda tulionao na kwa namna tulivyokuwa tumejipangia kazi zetu bado tunao wachangiaji 14 ambao bado hawajamaliza kuchangia na kwa muongozo wa Spika, shughuli hii ilitakiwa imalizike asubuhi ya leo ili jioni tuendelee kwa majumuisho katika wizara hii kama ambavyo tumekubaliana.

Sasa pamoja na watu 14 ambao wamebaki mimi nilikuwa ninayo maoni na mapendekezo kwamba wale ambao hawajamaliza kuchangia basi tuwaombe sasa wachangie kwa maandishi.

Lakini katika hawa watu 14 waliobakia naomba kutoa nafasi ya upendeleo maalum kwa Mhe. Raya Suleiman Hamad, ili yeye atakapokuja jioni aje kuchangia kwa ajili ya kuwakilisha watu wa jumuia yake na baadaye tumpe nafasi Mhe. Mwanasheria Mkuu, Mhe. Waziri wa Afya na tukimaliza hapo Mhe. Waziri anayehusika na wizara hii, kwa ajili ya kuja kufanya majumuisho ya pamoja. Waheshimiwa Wajumbe, naomba tukubaliane katika hilo. *(Makofi)*

Baada ya maelekezo hayo sasa naomba kuahirisha Baraza hili hadi jioni saa 11:00.

(Saa 7: 00 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 Jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujaendelea na majadiliano jioni ya leo tumepata bahati ya kuwa na wageni, ambao wapo pale katika ukumbi wetu pale juu. Wageni wenyewe ni ujumbe wa madiwani 9. Madiwani hawa wanatoka katika Wilaya ya Mbozi na Momba Mkoani Mbeya. Wageni hawa wamekuja kwa ajili ya masuala ya Tume ya Ukimwi Zanzibar ili kujifunza namna ya kupambana na ugonjwa huo. Niwaombe basi wageni wetu hao wasimame na Waheshimiwa Wajumbe wapate kuwasalimia. Karibuni sana wageni wetu na sasa tuendelee na majadiliano.

Nichukue nafasi hii kwanza kuwashukuru wasaidizi wangu ambao wameendelea na mjadala huu kwa Wizara yetu hii ya Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa alikuwa anaendeleza mjadala huo na ameniwekea taarifa kwamba kuna wachangiaji wapatao watatu hadi wanne ambao nategemea watumie muda vizuri tuweze kupata michango yao na tuweze kupata muda wa kutoa majumuisho kama tulivyokubaliana katika ratiba yetu.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Mhe. Spika, Ahsante kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu (SW) aliyetujaalia kufika katika Baraza letu tukufu kwa mara ya pili. Mheshimiwa mimi nitachangia ukurasa wa 15 sekta ya afya na nitaendelea mpaka nitafika ukurasa wa 19.

Kwanza nawapongeza sana Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais pamoja na Watendaji wake kuwa hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa ni hospitali ya Rufaa. Kuna mkakati wa kujenga hospitali kubwa nayo nzuri ya kisasa Mkoani Pemba ya kuweza kuwahudumia wananchi na kufanya marekebisho katika majengo ya zahanati mbali mbali Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, ninachokiona mimi hatuwezi kwanza kujenga majengo mengine bila ya kurakebisha majengo yetu tuliyonayo. Hospitali ya Mnazi Mmoja kama hospitali ya Rufaa kuna marekebisho makubwa, vifaa mbali mbali vinavyotaka kufanyiwa marekebisho ili viweze kwenda na wakati kuweza kutoa huduma kwa wananchi.

Mhe. Spika, hivi majuzi nilitembelea hospitali ya Mnazi Mmoja kama miezi miwili nilikuwa nina mgonjwa juu ghorofa ya tatu. Kufika pale watoto wale hospitali wakanizuia wakanambia mama kwenye lifti usiingie. Nikawauliza kwa nini nisiingie kwenye lifti. Wakanambia lifti imetengenezwa lakini bado ina matatizo inakwama na haiwezi kufanya kazi. Nikashindwa kwenda kumuona mgonjwa.

Kama hospitali ya rufaa basi tunaomba ifanyiwe marekebisho baadhi ya mambo mbali mbali ili tupate mahitaji kuweza kuendelea kufanya shughuli zile pale, kuanzia vifaa, huduma za wananchi, vipimio vya maradhi mbali mbali, vyote viweze kufanyiwa marekebisho. Mhe. Waziri aweze kufanya mkakati huo kwa makusudi. Kwa sababu kila siku tunachangia mambo haya haya, hata mwaka jana tulichangia mambo haya.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nitaingia kidogo katika ukurasa wa 19 hapa pana masuala ya watu wenye ulemavu. Mimi nashukuru sana serikali, watu wenye ulemavu wamepata msukumo sana kutokea Wizara za serikali na hata katika taasisi na hata katika jumuia zao kuweza kuwapa mafunzo na kuweza kujitambua watu hawa, lakini bado haijakidhi haja. Kwa sababu walemavu, hasa tusiwatizame walemavu waliokuwepo mijini, tuweze kufanya juhudi za makusudi kuwaona walemavu waliyokuwepo vijijini.

Mhe. Spika, siku chache tu nilifanya ziara, niliianzia Mkoani, siku zangu ni kidogo tu nilizokuwa nazo nikarudi Dar-es-Salaam ikawa sikupata kufanya Unguja nilionana na watu wa mawizara tu hapa. Nikaanza Wizara yangu Mkoani, Kengeja mpaka nikaingia Kisiwapanza, nikaja Chake chake, nikapelekwa mwahala mbali mbali, nikapangiwa kuonana na watu wenye ulemavu na pamoja na miradi yao pamoja na wale watu waliokuwa na mazingira magumu. Nikaingia Wete, Micheweni kote huko nimefika kwa kweli watu wenye ulemavu sehemu hizo ni watu waliokuwa na mazingira magumu kikweli kweli. Serikali ifanye mikakati ya makusudi kuweza kuwanyanyua watu hawa kiuchumi, kimaendeleo hata kuweza kujiajiri na sekta nyengine za mbali mbali ya mikono kwa kupata mafunzo kupitia serikalini.

Mhe. Spika, hapa nimeona kuwa watapatiwa huduma kuanzia afya na elimu na mambo mengine. Lakini tulipitisha mwaka 2009 ilipopita ile sera ya watu wenye ulemavu kuwa hapa tuwe na elimu mjumuisho ili tusitenge watu wenye ulemavu tuwe na elimu mjumuisho. Lakini kuna aina za walemavu ambao hawaendi sambamba na elimu mjumuisho wana mazingira mazito watu hawa na wote tunajua.

1. Watu wasioona,
2. Watu wa akili taahira,
3. Watu waliokuwa hawasikii.

Serikali ina mkakati gani wa kuweza kuwawekea vitendea kazi vya kuweza hawa kuwainua kielimu. Kuna vile vipaza sauti vya kuvaa masikioni, bado serikali haijaendana na wakati kuwapatia watoto hawa waliokuwa hawasikii. Kuna hawa watu waliokuwa hawaoni kuna zile mashine zao ndogo za nukta nundu, bado maskuli mengi hamna. Ukienda hawa kwenye elimu mjumuisho wao ndio waliokuwa watu wa mwanzo waliokuwa wanakosa huduma za elimu. Kuna watoto waliokuwa ni watoto taahira, hawa wana watu maalum wa lugha za alama. Je, serikali imetusomeshea watu wa lugha za alama wanatosheleza maskulini. Naomba Mhe. Waziri aweze kuweka juhudi ya kuwasomesha walimu hawa kuweza kuwafundisha watoto wenye ulemavu.

Mhe. Spika, hapo hapo kwenye ukurasa wa 19 hapa kuna dawa za kulevya. Mimi kwanza nashangaa hizi dawa za kulevya huyu anayeleta hizi dawa za kulevya ni nani aliyekuwa hatumjui, hatumuoni? Mheshimiwa leo mimi nakutana na watoto njiani natoka Darajani, nilipotoka hapa nilikwenda kwenye Dispensari moja hapa nilikuwa nakwenda kuchukua dawa. Nimewakuta watoto wanasinzia, naambiwa hao wapo tayari wameshakula unga. Huo unga ukoje? Maana naona sembe linamaliza, mchele unamaliza, sukari inamaliza, unga huu una wingi wa kiasi gani uliokuwa haumaliziki, unatumalizia watoto.

Serikali iweke mkakati maalum wanaolewa wakamatwe, wanaokula unga huu au vidonge hivi wawapeleke kwa wale watu wanaouleta na wao wale wasiuliwe wala wasifungwe kuwa kaja na kibaba akaambiwa aule mpaka awishe ni vitu eti, kwa sababu kama si vitu asingelituletea akatuhujumia watoto kiasi hichi.

Halafu Mhe. Spika, mazingira ya majengo kwenye zahanati, hospitali na maskuli bado hayajaoana na watu wenye ulemavu. Sehemu nyingi ninazozitembelea hazina mazingira rafiki. Tunaomba Mhe. Waziri tubadilishiwe hii sheria ya majenzi iendane na wakati kwa sababu kuna watu wenye ulemavu wengi sana. Mimi nilisema hasa mara moja na nilichangia hapa hapa nikasema hawa wafanyiwe sensa watu wenye ulemavu. Nikaambiwa tayari, naomba tupewe takwimu ni wangapi walemavu waliokuwepo Zanzibar.

Nitatoa mfano mimi mwaka 2005 ndio naingia kwenye Baraza Tukufu, tulikuwa Kikwajuni, lakini jengo hili hili hapa lilipokuwa likijengwa tayari mimi nimeshaingia na tunakuja kulikagua jengo na siku moja kule kule

Kikwajuni nilichangia nikasema jengo linavyojengwa iko siku atatokea mlemavu mwenye mazingira mazito zaidi aliyekuwa hawezi kuhudumia kwenye jengo hili. Mjenzi hakupewa utaratibu hata wa kuweka lifti ya kuibandika nje si lazima aweke ndani.

Alikuja mie hapa Mkurugenzi wangu Bi Abeida, mimi nilijiona ni mzima anapanda juu kuja kuisikiliza bajeti yao. Tunaomba Mhe. Waziri sheria za majenzi zirekebishwe, twende na wakati kwa sababu lifti zinaweza kuingizwa kwenye majumba hata kwa kuzibandika nje watu wakaweza kufikia mwahala wanamokwenda.

Mimi nimpongeze Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Mhe. Makamu wa Pili kaleta bajeti lakini anakumbana na vikwazo vya kuambiwa katika rasimu. Rasimu haiendani na Baraza hili, rasimu tuisubiri kwenye Mabaraza. Rasimu walichaguliwa Tume ambayo inaratibu maoni ya wananchi nchi nzima na tayari imetolewa rasimu. Tusubiri katika Mabaraza watu waweze kutoa maoni yao kwenye Baraza tuweze kuwashawishi, wanawake, wanaume, wazee kila anatakayepata fursa kuingia aweze kujipanga vyema pamoja na watu wake, rasimu zimeshatolewa zisomwe ili waweze kurekebisha rasimu. Palipo na mapungufu waongeze, wanapoona hapa hapafai watuwekee vizuri. Isiwe huyu huyu Waziri wangu hana nafasi, yeye kaleta bajeti hapa hajaleta rasimu. Rasimu iko Bara kaitoa nani, mimi nashangaa. Tusubiri rasimu ifike siku zake tuweze kutoa maoni yetu katika rasimu ya mabadiliko ya Katiba. Tusimkwaze Waziri, tusimtie kitumbojoto Waziri. Yeye kaitia humu kwa sababu tayari imeshaandikwa na inapitishwa ni wajibu wake kuiweka katika kitabu cha bajeti lakini yeye atakawapa majibu gani na rasimu bado ipo inafanyiwa kazi ili tupate rasimu nyengine itakayokuja kupata hiyo Katiba. *(Makofi)*

Halafu sisi kama Wawakilishi na Wabunge bado sisi tuna mwanya mkubwa sana kwa sababu tunaingia katika Bunge la Katiba, hapo sisi tuna mchango mkubwa. Sasa ikiwa ni taasisi na tayari mabaraza yameshaundwa Waheshimiwa naomba tusubiri na tuwashajihishe watu wetu waweze kuingia kwenye mabaraza kuweza kutoa ufafanuzi katika rasimu iliyotolewa na Tume Mheshimiwa. Mimi sitaki niwatolee ufafanuzi, muisome Katiba mutoe ufafanuzi. Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwanza na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema tukakutana saa hizi hapa. Lakini pia naomba kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi kutoa kidogo ufafanuzi wa suala ambalo limetajwa hapa kwa hamasa sana. Ni vizuri nikalitolea maelezo ili na wananchi wasikie vilivyo.

Mhe. Spika nimelazimika kutoa mchango wangu huu baada Mhe. Mshimba wakati akichangia hotuba ya bajeti ya Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais aliituhumu sana wizara ya Afya juu ya ununuzi na matumizi ya dawa hii ya *Insulin* ya aina *WOCKHARDT LIMITED YA INDIA.* Kati ya mengi aliyotuhumu ni pamoja na lawama kwamba Wizara imeinunua dawa hiyo kwa bei ya juu na kuacha ile iliyo rahisi ambayo hua inatolewa bure na Shirika la DANIDA.

Mhe. Mshimba amesema mengi zaidi ya tuhuma hizi kwa kurudia dhana ya rushwa katika ununuzi wa vifaa vya saratani (*cancer*) na kwamba hadi sasa hakupewa jibu la kutosheleza juu ya dhana yake hiyo. Ameituhumu Wizara kwamba kuna baadhi ya watendaji ndani ya ununuzi wa vifaa hivyo kumefanyika kwa wahusika kupewa rushwa na hata akataja kima cha dola elfu kumi.

Mhe. Spika, tuhuma hii ni nzito sana na kanuni za Baraza zinaagiza Mjumbe anapotuhumu kwa uhakika wa aina hii hutakiwa atoe uthibitisho. Nadhani Mhe. Spika, si vibaya ukamuagiza Mjumbe kuleta uthibitisho huo wa rushwa.

Mhe. Spika, Mhe. Mshimba aliendelea kutulaumu sana juu ya hali ilivyo ya hospitali ya Mnazi Mmoja na kusema kwamba ni ajabu sana kuwa hospitali hiyo kuitwa ya rufaa wakati hata mashuka ya kufanyiwa upasuaji wagonjwa kwenye chumba cha upasuaji hakuna. Mashuka yapo ya kutosha na yamenunuliwa kwa dhamira hiyo.

Mhe. Mshimba alikuwa na hamasa kubwa alipokuwa akieleza udhaifu wa utendaji wa wizara hii kiasi kwamba alichanganya mambo yenye kuhusu na yasiyohusu hoja ya bajeti iliyokuwepo mbele ya Baraza. Katika kuchanganya huko aliamua hatoipitisha bajeti ya Wizara yetu ya Afya kabla hata haijawekwa hoja katika meza yako Mhe. Spika.

Mhe. Spika, bila ya kinyongo wala dharau wala dhana mbaya namuomba nimshukuru sana Mhe. Mshimba kwa kulileta suala la *insulin,* maana nilishamuona katika TVZ akilishupalia kwa hamasa kubwa wakati wa mkutano wa wagonjwa wa kisukari uliofanyika tarehe 2/6/2013 hapo Skuli ya Haile-Selassie. Nilikuwa na matumaini makubwa kwamba baada ya mkutano ule Mhe. Mshimba angekuja kutafuta taarifa za upande wa pili kwa Wizara ya Afya na kwisha akapima katika kufanya maamuzi yake juu ya ukweli au uongo wa hoja aliyobeba na kuifikisha Barazani. Kwa sababu hakufanya hivyo nalazimika kueleza suala hili huku nikitegemea kwamba wananchi wote wanaonisikiliza na wao pia wapime ukweli wa hoja hii ambayo inatumiwa kwa kutuchafulia majina yetu.

Mhe. Spika nasikitika sana kwamba suala hili limegeuzwa kua vita vya kibiashara badala ya kua ni suala la tiba na hivyo wizara ya afya kupata lawama zisizostahiki, na kupelekea kuleta kutofahamiana kati ya wale wenye dhamana ya uagiziaji dawa (Afisi ya Mfamasia Mkuu wa Serikali na watumiaji wa dawa ya kisukari yaani, Daktari wa maradhi ya Kisukari Mnazi Mmoja).

Umuhimu wa kulitolea taarifa katika Baraza hili ni kwamba baada ya kubaki kuwa suala la kiwizara wameingia wasiohusika na kulishabikia kama kwamba ni vita baina ya pande mbili hizo. Matokeo yake ni kutuchafulia heshima zetu ambazo baadhi yetu tumezilinda katika maisha yote tuliyoishi kwa hasara kubwa, tukiwa katika utumishi wa serikali na nje ya serikali.

Madhumuni ya taarifa hii Mheshimiwa ni kulieleza suala la Insulin lilivyo na kuwasaidia wananchi wakatae kupotoshwa na kutumiwa kwa maslahi ya watu wengine, na hivyo watuamini kwamba hatuna nia ya kusababisha afya za wagonjwa hao na wengine kuharibika au kusababisha vifo vyao kama linavyoendelea kuelezwa katika mitandao ya kijamii na katika magazeti ya ndani na nje ya nchi

Mhe. Spika yaliyojiri kuhusu insulin. Kwa mujibu wa sera ya dawa ya Zanzibar *(Zanzibar National Medicine Policy 2008)* Mfamasia Mkuu wa Wizara ndie aliepewa madaraka kulinda na kusimamia sera, matumizi na ubora wa dawa za wizara ya afya.

Dawa za wizara huwa zinaagizwa kutoka *Medical Store Dar Es Salaam.* Tumekua na mfumo huo kwa sababu DANIDA, shirika la Denmark ambalo ni wafadhili wetu wakubwa wa wizara ya afya ikiwemo ufadhili wa kununua dawa kutoka ghala hiyo. Dawa tunazopata huko kwa kiasi fulani huwa zinafidiwa *(Sub-sidized)* na hivyo bei yake hua rahisi kuliko zile tunazonunua kwa tenda.

Mhe. Spika, dawa, zinapokua pungufu au hazipo nchini, Mfamasia Mkuu akishatiliwa fedha za ununuzi wa dawa, huomba Bodi ya tenda ya wizara kutangaza tenda kwa mujibu wa sheria iliyopo. Tenda hushughulikiwa na Bodi na aliyeshinda hulazimika kuleta dawa hizo kwa mujibu wa maelezo ya nyaraka za tenda zilivyo

Tenda ya dawa zilizonunuliwa katika kadhia hii ilitolewa baada ya ukosefu mkubwa wa dawa huko MSD ikiwemo hiyo Insulin ya *Novo Nordisk* iliyozoeleka kutumiwa na wagonjwa wetu wa kisukari. Tenda hiyo ilitolewa 20/11/2012, na mzabuni aliyeshinda alitangazwa 5/12/2012 na kati ya dawa zilizokuwemo kwenye orodha ya tenda hiyo ni dawa ya kisukari ya *Insulin.*

Ni vyema ieleweke kwamba tenda iliyotolewa ilikua kwa dawa nyingi zisizopungua 80, moja wapo ikiwa ni *insulin*. *Insulin* haikuagizwa peke yake kama inavyodhaniwa na wahusika, na wala katika orodha wa tenda huwezi kusema unataka insulin ya kampuni fulani vinginevyo ununuzi huo hautakua wa tenda, bali yatakua ni manunuzi ya moja kwa moja.

Yule aliepata tenda hiyo akaleta insulin aina ya *Wockhardt limited* ya India na kuifikisha katika Bohari kuu yetu ya dawa Maruhubi. Alileta *Insulin* ya aina hii baada ya kuikosa ile iliyozoeleka.

Ni pale kitengo cha tiba ya sukari walipokwenda kuchukua dawa huko Bohari kuu Maruhubi, ndipo walipogundua kwamba dawa hiyo si *ya Novo Nordisk* bali ni ya insulin aina ya *wockhardt limited* ya india ambayo kimatumizi katika hospitali ya Mnazi Mmoja ni mpya. Wagonjwa wetu wamezoea kutumia dawa ya *Novo Nordisk*. Daktari wa tiba akakataa kuitumia dawa hii mpya na kufikisha malalamiko yake wizarani na kwingi kwengineko. Mwanzo kukataa kwake kulijielekeza zaidi kwenye dhana kua dawa hii mpya imenunuliwa ghali zaidi kuliko ile iliyozoeleka.

Mhe. Spika, naomba nikuthibishie kwamba kati ya wale aliowaona kisirisiri daktari huyu kuieleza dhana hiyo ni mimi kwani alinifuata nyumbani kwangu akiwa amefuatana na Mr Edi Riyami.

Mhe. Spika, daktari huyu aliwaona viongozi hata wa CUF na kuwaeleza suala hili katika sura ya tuhuma ya manunuzi mabaya na watendaji wa Idara ya Mfamasia wakawa wananuka mitaani kwa kunyooshewa vidole ya ubadhirifu wa manunuzi haya. Kwa hivyo hoja ya awali ya msingi haikua udhaifu wa dawa yenyewe bali ni dhana ya ubadhirifu wa manunuzi.

Nilimuahidi Daktari kwamba nitalifuatilia kujua ukweli huo. Wakati Daktari anaeneza dhana mbaya dhidi ya watendaji wenzake wa wizara, alikua anaendelea kubishana nao kwa maandishi juu ya shaka ya uletwaji wa dawa hiyo kutofuata taratibu za kitaalam, kama vile kutofuata utaratibu wa kusajiliwa na uthibisho wa kitaalam wajumuia za kimataifa juu ya ubora wake. Kwa hivyo hoja ya tuhuma ya ununuzi ikasherehekezwa na taratibu za kitabibu kufuatwa au kutokufuatwa.

Mhe. Spika, hatua ambazo wizara ilizichukua. Mjadala kati ya wasajili, wasimamizi na watumiaji ulizuka kwa sababu ya mazoea ya muda mrefu ya Hospitali hiyo kutumia aina ya dawa ya *Novo Nordisk* kutoka Denmark na kuonekana kwamba wagonjwa wetu wa kisukari ndiyo waliyozowea kuitumia dawa hiyo, na kuzuka mashaka kwamba kubadili dawa hiyo na kutumia aina nyingine ni kukaribisha matatizo kwa wagonjwa wetu. Zaidi ya upya wa

kutumika kwa dawa yenyewe ndipo shaka hii ikasindikizwa na tuhuma ya kwamba dawa hiyo imenunuliwa kwa bei kubwa kuliko hii tuliyozowea kuitumia.

Suala hili liliripotiwa katika kikao cha waziri na wakurugenzi cha kila Jumatatu *(Monday briefing)* , na kujadiliwa tena na wataalam wa fani ya udaktari wa Insulin wa Tanzania akiwemo Dr. Kaushik na Prof. Swai tarehe 12/04/13, kama alivyotaja Mhe. Mshimba.

Mhe. Spika, naomba niwaeleze Waheshimiwa Wajumbe na nimueleze Mhe. Mshimba kwamba hao aliowaeleza hapa kwamba ni mabingwa wa tiba hii "Dr. Kaushik na Prof. Swai niliwaita mimi kutafuta ushauri wa kitabibu, hawakuitwa na Daktari wa Kisukari kama alivyoeleza. Nilipofanya kikao hicho wataalam wa wizara ambao nao ni madaktari kama huyo wa kisukari, akiwemo katibu Mkuu na Mkurugenzi Mkuu, Mkurugenzi wa hospitali ya Mnazi Mmoja na Daktari wetu huyu wa kisukari wote walikuwepo.

Wakati wa mjadala Dr. Kaushik aliulizwa suala la moja kwa moja kwamba "jee wewe kama mtaalam wa tiba hii dawa hii inafaa au haifai kutumia?" Dr. Kaushik ameshindwa kutupa jibu la moja kwa moja kwamba haifai isipokua alisema kwamba baadhi ya nchi kama USA, Uingereza na WHO hawajaithibisha.

Baada ya kikao tulimuomba atuletee ushauri wake kwa maandishi, alikaa kimya hata baada ya kumuhimiza mara mbili. Baadae Dr. Kaushik alikuja na wageni wa Jumuia ya kisukari wa Dunia na baada ya mkutano na wageni hao nikamuomba tena aniletee ripoti yake. Mwishowe aliileta ripo hiyo kwa matandao na wala hakuitia saini, na ndiyo ambayo Mhe. Mshimba aliyopewa na anaitumia kama kwamba ndicho kielelezo cha udhaifu wetu wa kukataa ushauri wa mabingwa.

Mhe. Spika baada ya kupata maelezo ya kitabibu Wizara iliomba tena ushauri kwa wasimamizi wa kusajili dawa wa Serikali ya Muungano na wa hapa kwetu Zanzibar. Wao kwa pamoja walijibu kwamba dawa hii imesajiliwa pande zote mbili za Serikali za Jamhuri ya Muungano, na imethibitishwa kutumika tangu mapema, kwa mara ya kwanza 2005.

Mhe. Spika, dawa hiyo ikasajiliwa tena 2010 baada ya miaka 5 ya usajili wa mwanzo. Mkurugenzi Mkuu wa TFDA, kwa Registration No. TAN.09 036A10 AWOC ya 02/02/2009, na nyingine No. TZ 12h086 ya 07/03/2012. Bwana Hiiti B. Sillo, amekwenda mbali zaidi na kueleza kwamba kabla kuisajili dawa hii walisafiri hadi India kwenye kiwanda chenye kuzalisha dawa hiyo chenye anauani ya*: L-1, Maharashtra Industrial Development*

Cooperation (MIDC), Chikalthana, 431 210, Aurangabad, India na H-14/2 MIDC area, Waluj aurangabada, India, na walipoisajili hapo 2005, walifuata taratibu zote zinazotakiwa kitalaam na kisheria kabla dawa haikuruhusiwa kutumika. Tangu walipoisajili hawakupokea taarifa za madhara yatokanayo na matumizi ya dawa hiyo kupitia mfumo uliowekwa ujuilikanao kama *"pharmaco-vigilance"*. Dawa ikishasajiliwa TFDA huruhusiwa kutumika Zanzibar na lazima iwe na sifa za ubora, usalama na ufanisi kama vilivyo kwenye muongozo wa kusajili dawa za binaadam wa *Serikali (Guideline for Registration of Biological Product 2004,* na muongozo wa kusajili dawa za binaadam wa 2012, (Sifa ni *quality, safety and efficacy*).

Maduka ya dawa ya binafsi na hospitali za binafsi Tanzania na Zanzibar inauzwa na inatumika kama kawaida dawa hiyo isipokua haikuwahi kutumika kwa wagonjwa wanaopata msaada kupitia Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe Spika, wakati majadala wa suala hili unaendelea. Jumuia ya wagonjwa wa kisukari walikuja kuniona na ninasikitika sana kwamba mwenyekiti wa Jumuia hiyo na wajumbe wake wakaanza kunishambulia kwa maneno makali na kunitaka niwaeleze kwa nini tumenunua dawa kwa bei ya ghali wakati dawa rahisi iliachwa. Wakaniuliza huku kwenye tenda bodi kunafanyika nini hata dawa hii ikanunuliwa kwa bei ya ghali.

Niliwajibu kwamba mumekuja kunieleza hamna dawa au dawa tumenunua kwa bei gani. Suala la ughali wa dawa ni suala la kiutawala nyinyi haliwahusu, na niliwashangaa na kuwaambia kwamba haya si maneno yenu, haya mumetumiwa kuja kutupa shindikizo ambalo haliwa husu. Niliwaomba tuonane tena siku mbili baadae ambapo wataalam na watendaji wa wizara walikuwepo.

Mhe. Spika, mjadala na wataalam ulichukua zaidi ya masaa 3 hatimae tukakubaliana kwamba tuzungumze na daktari wao kwani walisema yeye ndiye aliyewakataza wasitumie dawa hiyo. Tukawaambia kwamba tutafanya hivyo katika taratibu za kiwizara na tuliwakabidhi baadhi ya barua za maamuzi yetu. Tuliwaomba sana wasilifikishe suala hili katika vyombo vya habari maana ni suala la kitaalamu wao litakuja kuwapa matatizo.

Mhe. Spika, waliacha ushauri wetu na kutoka nje tu wakamueleza mwandishi wa *Daily News* na siku iliyofuata likaandikwa kwamba watoto wa wagonjwa wa kisukari wanakufa kwa kukosa dawa ya *insulin* wametakiwa watumie dawa iliyo chini ya kiwango cha kimataifa ambao ndio kwanza ipo kwenye majaribio. Mwandishi wa gazeti la *Daily News* akaandika kwamba dawa hiyo ni *sub standard.* Mhe. Spika, Wizara ilitoa *Press Release* kueleza ukweli ulivyo na kuepuka malumbano ya magazeti.

Baada ya kuona Wizara imetoa msimamo wa kwamba dawa hii ina ubora ndipo Jumuiya ya Watu wenye Kisukari ikafanya mkutano wa wagonjwa wote wa kisukari na kutoa azimio la kwamba hawako tayari kutumia dawa hiyo kwa kuwageuza wagonjwa hao kifaa cha majaribio, yaani *pygmies*. Hapo ndipo Mhe. Mshimba alipolibeba dudu ambalo hana utaalam nalo na wala hakufanya hima ya kutuuliza.

Mhe. Spika, katika taratibu zetu za kiwizara, suala hili nililifikisha kwa Baraza la Madaktari pamoja na maelezo yote yanayostahiki katika kikao chao cha tarehe 4/06/2013 daktari wa kisukari na watendaji wa Idara ya Mfamasia Mkuu waliitwa na kila mmoja kutakiwa ajenge hoja zake juu ya ubora wa dawa au udhaifu wa dawa hii. Daktari wa kisukari alishindwa kujenga hoja za msingi kitaalamu na kiutaratibu na hivyo kushauriwa kwamba isingefaa kuchukua masuala ya kitaalamu na kuyafanya ya kibiashara. Alikiri mbele ya kikao hicho kwamba baadhi ya taarifa za dawa hiyo alikuwa hakuzijua mapema na hivyo suala hili lisingefika kiwango hiki cha kusutana yeye na wenzake.

Mhe. Spika, dosari ya kuambiwa kwamba dawa hii ni chini ya kiwango imewaumiza wenye kuzalisha na kuuza biashara hii na walikuwa tayari kufungua mashtaka ya madai katika Mahkama za Tanzania na kudai fidia kwa kuchafuliwa jina la bidhaa yao. Nyaraka za kitaalamu zilizothibitisha ubora wa dawa hizo wametuletea na kwamba WHO ambao ndio huwa inatumiwa vibaya sio inayotoa madaraka ya kutumia au kutotumia dawa hii. WHO wao wameacha matumizi ya dawa na udhibiti wake kwenye taasisi ya udhibiti wa dawa ya nchi husika. Katika sura hii Mhe. Spika, Wizara tumewaomba watuachie tulishughulikie kiwizara badala ya kulipeleka katika vyombo vya sheria.

Mhe. Spika, ushauri wa mabingwa wote hao na ule wa Katibu Mkuu Afya umepewa msimamo kwamba hakuna madhara wa dawa hiyo kutumika ingawa tunahitaji kuwatahadharisha wagonjwa wetu juu ya mabadiliko ya upatikanaji wa dawa tuliyoizoea na aina ya dawa hii mpya kwao. Inafahamika kabisa si jambo geni na wataalamu wa Wizara kwamba si jambo geni dawa kutoka India, ikiuzwa na zile zinazotoka Uingereza na Ujerumani au USA.

Mhe. Spika, hatujawahi kumkataza mgonjwa wala daktari kutumia dawa aliyoizoea au anayopenda, na Jumuiya tuliwashauri kama wana wafadhili wa kuwapatia fedha za kununua hiyo dawa waliyoizoea, sisi tulikuwa tayari kuwapa barua waende MSD wakanunue kama imeshakuwepo kwa bei nafuu tunayouziwa sisi serikali.

Mhe. Spika, tulichokataa na tutaendelea kukataa, Mhe. Spika, ni kulazimishwa kuacha utaratibu wa kiserikali wa kuondosha taratibu za tiba kwa kisingizio cha daktari mmoja kujifanya wakala wa dawa maalum ya maradhi maalum anapokuwa katika kazi kwa maslahi yake binafsi. Kibaya zaidi ni kule kuwatumia wagonjwa na jumuiya zao pamoja na waandishi wa habari kupotosha ukweli kwa maslahi yake. Hali hii inaendelea kwa kuitumia familia yake, marafiki zake kueneza kwa njia ya mitandao taarifa potofu bila ya kutoa sababu za kitaalamu au ushahidi wa tiba. Tabia hii inavunja miiko mikubwa kwa utaalamu na huduma za kitabibu.

Mhe. Spika hali iliyoelezwa katika jamii haipewi sura sahihi na taswira sahihi na hivyo kutuchafulia majina yetu kwa taarifa ambazo wanazozitoa hawana uhakika na wala utaalamu nazo. Mhe. Spika, katika huduma za matibabu ya wagonjwa wanaokwenda nje takriban asilimia 90 huwa tunawapeleka India, na katika miaka ya karibuni wananchi wenyewe kufuata matibabu ya kila aina huko India. Wanapokweda huko hutibiwa na dawa zilizotengenezwa India wakiwemo wale wa kisukari wanaokwenda wenyewe na tunaowapeleka serikali. Ni mawazo ya ajabu kwamba dawa ya kisukari kwa Mzanzibari aliyeko India anakula ya India, yule anaetibiwa Zanzibar anakataliwa kupewa eti tu kwa kuwa anaipata aina nyengine bila kulipia hapo hospitali ya Mnazi Mmoja.

Hivyo nataka muamini Mhe. Spika, kwamba wagonjwa wa kisukari wanapokwenda matibabuni India hufungiwa vifurushi vya dawa ya *Novo Nordisk* na kuagizwa wasile dawa nyengine wanapofika India si suala la kawaida. Je, hoja ni ubora wa dawa au kuna zaidi ya hilo ambalo wagonjwa wa Jumuiya ya Kisukari wamelisema pale kwenye mkutano wa Haile Sellasie na kuandika katika Zanzibar Leo tarehe 4/6/2013 kwamba Kampuni hiyo inayowapa dawa ya *Novo Nordisk* wanawasaidia mambo makubwa zaidi kuliko zile dawa zinazopunguzwa bei. Mwenyekiti wa Jumuiya Hii anasema wakati wa mkutano dawa hiyo ya *Novo Nordisk* ina ubora, na mbali ya ubora huo Kampuni hiyo imekuwa ikitoa misaada mbali mbali ikiwemo kuwasomesha madaktri, kutengeneza kiunganishi, kuwasaidia watoto dawa na mashine za kuisaidia Jumuiya ya Kisukari kifedha wakati wa maadhimisho ya siku ya kisukari duniani limeandika gazeti hilo maneno ya Mwenyekiti.

Mhe. Spika, pamoja na sifa hizo za ubora wa dawa ya *Novo Nordisk* zinazotolewa na mawakala wa Kamupuni hii ya *Novo Nordisk* Wizara inayo barua ya tarehe 12/12/2012 ya kitengo cha usimamizi na uchunguzi wa makampuni ya dawa ya USA iliyosainiwa na Mr. Steven Lee Mr. Steven Lynn aliyoandikiwa Mr. Lars Rebien Sorensen Mkurugenzi Mtendaji na Rais wa Magnodis wa Denmark kuhusu uchunguzi uliofanywa katika kampuni hiyo ya *Novo Nordisk* na kugunduliwa kwamba hata wao hawafuati masharti

ya uzalishaji wa dawa hii ya *insulin* na kutakiwa wajirekebishe na wamebaki bila ya kujitoshelezea maagizo waliyopewa.

Mhe. Spika, tusilazimishwe kusema mambo ya watu ambayo nayo si mazuri kutoa fursa kutuingiza katika migogoro ya kibiashara ya kampuni za dawa. Mhe. Mshimba ajue tu kwamba tumeteuliwa na Rais kulinda uhai wa wananchi sio kuwaua. Na Mhe. Sisi hatutokataza Kampuni ya *Novo Nordisk* au nyengine yoyote kuendelea kuwafanyia madaktari wetu, jumuiya na kitengo cha kisukari mambo mazuri na zaidi ya hivyo. Hayo yanayofanywa Wizara tunayapongeza sana. Hata hivyo ushauri wa wataalamu wa Wizara ya Afya ni kwamba si busara kutegemea dawa ya aina moja kwa sababu pamoja na hoja ya upungufu huko MSD dawa zilizokuwa zimetumika, lolote linaweza kutokea na dawa hii iliyozoeleka ikakosekana kabisa. Suala ni je katika hali kama hiyo ikitokea ndio wagonjwa wa kisukari hawatotafuta dawa mbadala ya ile iliyozoeleka wakaendelea kuishi. Mhe. Nyaraka za mabingwa wa tiba na zile za wasajili dawa hii pamoja na tenda zipo Wizarani na waandishi hawakuziomba kuziona ili wanapotoa taarifa zao waweze kuweka mezania hoja hii.

Mhe. Spika, kama kuna tuhuma za ubadhirifu wa manunuzi wa dawa hiyo, Wizara inaviomba vyombo husika vya serikali kulifanyia uchunguzi stahiki na watakaostahiki na kuharibu mazingira ya ununuzi basi wachukuliwe hatua kama taratibu za serikali zilivyo.

Mhe. Spika, napenda kukushukuru kwa kunistahamilia, naomba kumaliza maelezo yangu kwamba katika sera yetu ya dawa tumeorodhesha aina ya dawa muhimu ambazo zinatumika katika hospitali zetu, tunaiita “Essential Medicines List” hakuna dawa inayoitwa Novo Nordisk isipokua kuna dawa ya “Insulin Plain 100.I.U/ml. inj. Na Insulin, Zinc Suspension 100IU/ml.inj. Tulipotoa tenda tulitumia jina la *insulin* na aliyepewa tenda kaleta dawa ya *insulin* hakuleta dawa ya *Novo Nordisk* kwa sababu kaagiza *insulin* na anaweza akapata *Novo Nordisk* au nyengine.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha na kuwaomba Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waipitishe bajeti ya Makamu wa Pili wa Rais bila kipingamizi. Haya hayahusu kwakwe yanatuhusu sisi. Mimi naiunga mkono asilimia mia moja na zilizobaki zaidi. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, na mimi ninakushukuru sana kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na kabla na mimi sijasahau naomba niunge mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja na naomba Waheshimiwa Wajumbe wenzangu pamoja na marekebisho ya hapa na pale,

lakini tuipitisheni kwa sababu ya kuendeleza na kama ndio msimamzi na mratibu wa shughuli zetu.

Mhe. Spika, kulikuwa na masuala mengi madogo madogo ya hapa na pale kuhusu vitambulisho vya ZAN-ID na Baraza la Manispaa. Naomba nianze kwa Baraza la Manispaa Mhe. Spika, nakumbuka dada yangu Mhe. Asha Bakari alizungumzia suala la Saateni, nikiri kuwa kweli hali haijawa nzuri Mhe. Spika, nimekwenda pale sokoni mwenyewe nimejionea lakini hilo isiwe sababu ya kuwafanya wafanyabiashara wetu wadogo wadogo wahame kule. Bado ninasisitiza kwamba nafasi ipo, hayo mambo madogo madogo tutajitahidi kushirikiana na uongozi wa Baraza la Manispaa tuone kwamba tunaweka sawa. Muhimu sasa hivi tunapanga suala zima la usafiri wa daladala kwa kushirikiana na Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano tuone kama daladala inaifanya kituo cha Saateni au Kinazini zipite kule na ikiyumkini kukihamisha kituo kikubwa kuwa Darajani pale ili kupunguza msongamano.

Sasa kama nilivyosema haya tunayazungumza na tunaendelea nayo na zaidi alinambia Mhe. Waziri kwamba alikuwa hajateua bodi yake ya usafiri sasa ameshaiteua na ameshaipa meno ninafikiri hilo tutalikamilisha mapema iwezekanavyo. Na nizidi kusema ile miundombinu iliyopo pale Saateni sio mibaya kiasi hicho zaidi ni vyoo ambavyo tunataka tuviongeze tu kwa idadi ya watu na ile miundombinu mengine ambayo wenyewe wakija pale tutaijenga. Lakini kwa kweli Mhe. Spika, kwa hali iliyopo Darajani na kipindi tunachokwenda cha Ramadhan na Sikukuu tukiendelea watu waendelee kupanga vitambaa chini, waendelee kufanya biashara chini, hata njia haipitiki tutakanyagana pale. Kwa hivyo ningeomba sana wafanyabiashara wadogo wadogo wafuate haya maagizo au mipango hii ni mipango yetu sote, huu ni mji wetu sote. Tunataka uwe na sura nzuri, uwe na mipango mizuri tusibugurushane wala tusisukumane.

Na nilitoa rai na hiyo tunaifanyia kazi Mhe. Spika, kwamba tumeshapokea maombi mawili ya kujenga *shopping moll* pale Darajani ili tuondoshe wale wafanyakazi kufanya kazi chini pale, lakini tutatizama tumewaachia kazi hiyo wataalam wetu tuone kweli pale panajengeka *shopping moll.* Lazima tuangalie kwanza magari *shopping moll* lazima iwepo *space* kubwa ya magari, yata-*park* wapi magari, tutakwenda vipi. Sasa hilo tunalifanyia kazi lakini na hayo maombi tumeshayapokea tunayajadili pamoja na Wizara ya Fedha ambayo ni dhamana ya wawekezaji, ambao pia pamoja na Wizara ya Majenzi ndio wenye mipango ya miji, lakini pia na Wizara ya Biashara. Kwa hivyo kama serikali tunakamilisha taratibu zote halafu tuandae *cabinet paper* tuone hilo suala litafanikiwa vipi.

Mhe. Spika, kulikuwa na suala zima la ZAN- ID au kitambulisho cha Mzanzibari, watu wengi nao walizungumzia suala hili, mimi nataka kusema Mhe. Spika, suala la msingi kwamba kitambulisho cha Mzanzibari ni haki ya kila Mzanzibari, hilo halina mjadala. Kila Mzanzibari anastahiki apewe kitambulisho cha Mzanzibari lakini muhimu na hilo ndio ninasisitiza afuate taratibu na sheria iliyopo, hii ndio sheria iliyopo hatujaibadili, tuliipitisha hapa hapa. Sasa kama kuna maoni ya kubadilisha sisi kama serikali tutapokea, tutapokea maoni tuyajadili tuyatizame. Lakini tatizo kubwa liliopo utamthibitisha vipi huyu ni Mzanzibari hilo ndio tatizo, tatizo linatokezea hapo, kwamba utasema wewe ninakujua tu umeishi hapa, umezaliwa hapa, uthibitisho mnataka cheti cha kuzaliwa. Sasa cheti cha kuzaliwa aidha unacho, kama huna ukale kiapo kortini ndio uthibitishe ule uraia wako. Sasa nafasi zote hizo zipo lakini Mhe. Spika, tatizo liliopo kwamba kuna wananchi niseme wanapenda sana *shortcut* na hawataki hizo taratibu kuzifuata, wanataka tuzipinde na hiyo kuzipinda kwa kweli haiwezekani.

Mhe. Spika, leo suala la *forgery* nchini mwetu imekuwa kitu cha kawaida, watu wana-*forge* vyeti vya kuzaliwa, wana-*forge* vitambulisho; hicho cha Mzanzibari pia anaki-*forge* au cheti cha kuzaliwa kile apate kitambulisho cha Uzanzibari. Ana-*forge* cheti cha *form* 1V, form V1 hata digrii apate kazi. Hili suala Mheshimiwa lazima Waheshimiwa tusaidiane tulipige vita kwa viwango vikubwa sana. Leo mtu ana-*submit* cheti cha kuzaliwa tarehe ukiangalia tarehe ile ni ya juzi juzi tu hapa, miezi 6 mpaka mwaka mmoja uliopita tarehe ya cheti cha kuzaliwa. Lakini ukiangalia saini yake pale kimetiwa saini marehemu Topiwala amefariki miaka mingi iliyopita. Sasa unaona waziwazi hiki cheti cha ku-*forge* na hivi vingi sana Mheshimiwa. Tumevikamata viko rundo kubwa kabisa, ninafikiri wakati wa *budget speech* yetu tuje tuviweke pale tuone Mheshimwia hivyo vyeti vya *forgery.*

Sasa nasema sisi hatuna pingamizi yoyote ile, hii ni haki ya kila Mzanzibari na sio kupiga kura tu akakate tiketi ya kusafiria, anataka kwenda benki anataka kwenda popote lazima kitambulisho awe nacho, tena anatakiwa atembee nacho. Nakumbuka wengi watu wazima tupo hapa wakati wa kadi ya uraia, kama *passport* ulikuwa unaambiwa utembee nayo mfukoni na vituo vya polisi walikuwa wanakusimamisha hasa makusudi. Wanasimamisha gari halafu wanauliza nataka wote mwenye pasi ya uraia atoe, kama huna anakuteremsha kwenye gari. Sasa si jambo jipya kwa vitambulisho vya Mzanzibari mtu kutembea nacho, lakini kwa bahati nzuri au mbaya huwa kidogo tunaona mtu labda kidogo kile atakipoteza sasa anakiacha nyumbani mpaka atakiwe ndio akilete. Lakini kwa kweli sheria hasa inasema uwe nacho muda wote.

Kwa hivyo Mhe. Spika, nataka kusisitiza tu haki ya kitambulisho cha Mzanzibari ni haki ya kila Mzanzibari lakini aandike pale ambapo anastahiki, tuliwaponda sana masheha wetu tumewatupia lawama kwamba wanawapinga watu si kweli. Nilitoa takwimu nyingi sana hapa kuonesha vitambulisho ambavyo havijachukuliwa.

Nitatoa mfano kama Pemba tulipokwenda kulikuwa na takwimu kama vitambulisho si chini ya vitambulisho 20,000 tukafanya ziara na Waheshimiwa na Masheha na Wakuu wa wilaya kule na Madiwani wote tukaenda kila Wilaya, kila Wilaya tulitembelea tumemaliza Pemba sasa hivi tunafanya ziara hapa Unguja. Kwa hivyo kwa Pemba baada ya ziara ile Mhe. Spika, kwa kweli tumepata mafanikio kwa kiwango fulani, vitambulisho si chini ya 6000 wameshavichukua wenyewe, na bado hivyo viliopo hatuna sasa hakika kweli hawa waliopo Wazanzibari wanastahiki, wakaazi au wanakuja katika kipindi fulani halafu wanaondoka huo ndio mtego uliopo.

Na bahati nzuri kitambulisho kile hasa kimetengenezwa cha kimaifa kabisa huwezi ku-*forge* wala hakuna kwamba utaandika Mkokotoni halafu kesho uende ukaandike kwetu labda Dimani kule. Wewe ukiweka dole lako gumba sura yako ikitokea tu pale wewe uki-*forge* tu utakamatwa. Kwa hivyo kitambulisho kiko *standard* na kila mwaka tunakaguliwa Mhe. Spika, kuona kwamba tuko kwenye *standard*. Nataka kusema tu naomba sana Waheshimiwa tushirikiane tuwaelimishe watu wetu wafahamu ile ni haki ambayo anapaswa mtu apate kwa eneo lile analopaswa. Akienda kinyume ndio anapata matatizo tutawatia watu lawama bure, tumesema mtu yoyote miaka 18 kuendelea lakini pia awe Mtanzania. Ukishakuwa Mtanzania ana-*qualify* kuwanacho. Sasa nataka kusema lakini si kila Mtanzania awe ndio Mzanzibari anastahiki lakini kwa mzanzibari lazima awe mtanzania ni sifa moja hiyo.

Halafu Mhe. Spika, tatizo kubwa linakuja kwenye huu ukaazi katika eneo, tunaomba sana Waheshimiwa watu wetu wanapohamia kwenye maeneo basi achukue karatasi anakotoka shehia ile apeleke kwenye sheria nyengine. Matatizo mengi tunayapata kwamba watu wanakwenda analala akiamka pale hana utambulisho wowote Sheha hamjui kwenye daftari lake la Sheha hayumo, kwa hivyo matatizo mengi yanakuja hapo. Sasa anakuja kudai fursa kwenye eneo lile Sheha anasema mimi simjui. Sasa naomba sana tuelimishe wananchi wetu mtu yoyote anapohama kutoka eneo moja kwenda jengine achukue karatasi huko anakotoka aipeleke anakokwenda. Ninafikiri hayo yatatusaidia sana kuondosha tatizo hili.

Lakini Mhe. Spika, ninachotaka kusema vitambulisho tunavitoa kwa wingi sana wala hakuna tatizo, hakuna khiyana isipokuwa tatizo kwamba zile

taratibu tu naomba sana tuzifuate, kama tunaona kuna kipengele kidogo tukiweke sawa basi sisi kama wizara, kama serikali, tuko tayari kupokea fikra au mawazo tufanye nini lakini sio kurejesha kamba kama inavyosemekana. Na wenyewe tunalalamika kwamba nchi yetu ni kisiwa, kama ni kisiwa tukiachia milango wazi tutavamiwa na watu kweli kweli. Nina swali la kujibu kesho lakini ninaambiwa tumelipunguza, swali lenyewe linahusu watu wangapi wamehusishwa na kudanganya na kupata hivyo vitambulisho vya uzanzibari. Wakenya, Wacomoro, wengine hata watanzania Bara au hawajafika zile siku za kukaa pale au wengine wazanzibari wameondoka lakini wapo nje miaka 30, 35 sasa wanapokuja huku si wakaazi tena wanataka waje wachukue fursa tu sasa hiyo haikubaliki. Sasa kama anakuja atimize miaka 7 basi tunajua huyu kweli sasa hivi keshakuwa Mzanzibari mkaazi tunampa haki zote na kitambulisho tutampa. Kwa hivyo Mhe. Spika, nataka kusisitiza tu kwamba hii ni haki ya kila Mzanzibari na sisi tunasisitiza kwamba kwa mujibu wa sheria na taratibu atapewa kila anayefuata taratibu ziliopo.

Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, kwanza nitangulie kwa kushukuru kwa kunipa na mimi fursa hii ya kuchangia katika hoja hii lakini la pili nitangulie kusema kwamba na mimi naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na naomba wenzangu nao wote waiunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika, mimi naomba kuchangia katika labda maeneo 4 tu tena kwa haraka haraka najua muda umekwenda kidogo. La kwanza ni lile alilozungumza Mheshimiwa sahibu yangu Mwanasheria mkubwa Mhe. Mshimba. Yeye aliuliza swali na alisema hawezi kupitisha hoja hii mpaka ufafanuzi kwa nini kumetumika neno Makamu wakati Katiba inasema Makamo. Lakini najua mimi kwa ufasaha wake kwa uelewa wake alichokitaka kikubwa ni kututanabahisha tu lakini kisheria kosa la kutamka au la kuandika ni jambo ambalo kusema kweli haliathiri maadam haliundi ofisi nyengine ambayo inaleta mkanganyiko.

Nakubaliana na yeye kwamba kweli katika Katiba limetumika neno Makamo lakini baada ya uchambuzi limeonekana ni kosa la uandishi tu lakini neno sahihi ni makamu, ndio ambalo linatumika na tutakapofanya marekebisho hapo baadae ya kuchapisha toleo jipya basi na hili nalo litarekibishwa. Kwa sababu ni la uandishi tu.

La pili Mhe. Spika, lilizungumzwa suala la Utumishi wa Baraza au watumishi wa Baraza. Mimi nadhani suala hili Mhe. Spika, wewe mwenyewe ni shahidi tumelizungumza sana na mimi labda kwa hapa niseme tu Mhe. Spika,

kwamba tumeunda vyombo kwa mujibu wa Katiba; tumeunda Kamisheni ya Utumishi, tumeunda Tume za Utumishi nne, tumepitisha sheria ya utumishi wa umma ambayo inafafanua kila moja kazi ya vyombo hivi. Na bahati nzuri katika kifungu cha 33 kwa mfano kifungu kidogo cha 3 cha sheria ya Utumishi wa Umma kimesema kwamba Tume za Utumishi hizi zote ziliopo ziko huru na hazitoingiliwa na wala hazitofuata maelekezo ya mtu au ya chombo chochote kile. Kwa hivyo mimi naomba Wazungu wana msemo wanasema, *"the principle of being principle is being principle"*. Yaani ukitaka kuwa mtu wa kufuata kanuni basi uwe mtu wa kufuata kanuni, haiwezi kuwa nusu nusu wao wakasema "*the principle of being principle is being principle"*. Kwa hivyo na chombo hiki na sisi ni chombo ambacho juu ya hizi *politics* za hizi taasisi ambazo tumezianzisha. Wajibu wetu kuzisimamia pale tunapoona kwamba utendaji wao hauendani na matarajio ni kuwaelekeza.

Lakini nadhani si vizuri Baraza tukachukua reli ya kuwa chombo cha rufaa wakati sheria tuliyoipitisha wenyewe hatukujipa mamlaka hayo ya rufaa. Wala si vizuri pengine Baraza kujifanya kama ni chama cha wafanyakazi wa Baraza kwa sababu hatukujipa mamlaka hayo mbali ya sheria ambazo tumezipitisha. Utaratibu uko wazi penye makosa tunapoona hayajafanyika vizuri mimi nadhani tutumie njia ziliopo kuweza kurekebisha yale ambayo makosa yametokea. Lakini itakuwa si vizuri hata kidogo kwa kweli kutumia Baraza kulazimisha chombo ambacho kimepewa mamlaka ya kisheria kufanya maamuzi ya kisheria. Pale kilipokosea katika utendaji ni vizuri kusema hapa kimekosea na kirekebishe makosa ambayo yamerekebishwa lakini nadhani si sahihi kuchukua *role* ya kuwa labda *trade union* ya wafanyakazi. Kwa sababu taasisi zote hizi ni zetu na ni wajibu wetu kuzisimamia.

Mhe. Spika, jambo jengine la tatu ambalo nilipenda nilichangie kidogo ni suala la Muungano. Kwanza nitangulie kuipongeza kwa dhati kabisa Tume ya Katiba ambayo imeundwa chini ya Mwenyekiti Bwana Jaji Warioba. Mimi naomba tutazame mazingira ambayo wameyafanyia kazi, na tukubaliane kwamba kusema kweli wamefanya kazi kubwa.Haikuwa rahisi wala haikuwa jambo jepesi kufika pale ambapo walifika na ndani ya muda kusema kweli. Na hapa nichukue fursa ya kumpongeza pia Mhe. Raya, ametukumbusha kwamba hatua iliyopo ni Rasimu, la kwanza Waheshimiwa mimi niwaombe sana tuisome Rasimu. Mimi nimeona kwamba wako watu wengi wanasema, wanatoa hoja, wanatoa fat-wa, lakini ukisikiliza unajua kwamba hiyo rasimu hajaisoma. Kwa hivyo mimi nawaomba sana hii rasimu tuisome, na tuisome vizuri na ile sheria yenyewe ya katiba au ya mchakato wa Katiba.

Mhe. Spika, ninaloomba hapa nikumbushe tu mimi kwamba, jamani katika hatua hii siasa basi, katika hatua hii kusema kweli kinachohitajika ni hoja za kuiboresha au za kuifanya ile rasimu iwe nzuri zaidi. Na si jazba wala si utashi, Mimi naomba tena na nawaomba sana wenzangu na nimuombe kila mwananchi tujiulize kila tukikaa tunajua tunataka nini. Maana Mhe. Spika, hii safari ndio imeanza, bado wengine ukisema watakasirika lakini kama hatujui tunakwenda wapi mimi naomba nirudie *asiyejua anakokwenda ni mzururaji*. Kwa hivyo ni vizuri tusikubali kuwa wazururaji, ni vizuri tuwasaidie wananchi kuunga mustakabali wajue tunakwenda pahala gani. Leo tuko pamoja lakini itafika siku itabidi kila mtu achague anakwenda kushoto au anakwenda kulia, na itakapofika hapo inatisha kuona kwamba ndani ya chombo hichi kinachowakilisha wananchi wetu wa Zanzibar tukianza kuwa na tafauti sisi ya kuonesha kwamba hatujaelewa, hatujafahamu, kusema kweli tukianza sisi kuwa wazururaji wananchi sijui watakuwa kitu gani. Kwa hivyo mimi naomba tujue tunakwenda wapi, tuwasaidie wananchi wanakwenda pahala gani.

Mhe. Spika, na katika hili labda mimi niseme tu hasa niwaombe wananchi, kuna baadhi ya mambo ni vizuri wakayazingatia. Katika hili wazee wetu wana msemo, wanasema *macho si mboni*, unaweza kumuona mtu anaangalia ukafikiria labda anaona, pengine kumbe kaona anachokipenda tu, anaweza akaingia kwenye shimo ukasema ah! Yule si ana macho, lakini watu wanasema *macho si mboni*. Kwa hivyo lazima tujijuwe kwamba kila mtu anachokiangalia halafu tutizame nani wa kumfuata. Lakini mambo matatu haya ambayo nitapenda niyakumbushe au ni vizuri kuyazingatia moja nimeshalisema kujua tunataka nini.

Mhe. Spika, la pili ninaomba tusijipotoshe wala tusikubali kupotoshwa. Mimi nimesikia tokea imeanza hii rasimu kutoka wenzetu katika vyombo mbali mbali wengine wasomi, wengine watu maarufu, hasa kwa upande wa wenzetu wanatoa maneno mengi sana, lakini moja kama na sisi wenyewe hatukuwa makini tunaweza tukapata tatizo nalo ni hili suala la kusema kwamba labda Zanzibar tunadai hichi, au Zanzibar tunadai hichi, hayo ni maneno yanayotumika sana. Mimi ninaomba tuwaache watu waseme lakini sisi wenyewe tujue kwamba Zanzibar hatudai, chochote ambacho kiliingia katika Muungano tukakubali tukiendeshe kwa pamoja tulikiweka amana na tuna haki ya kusema kwamba aah! Sasa tunataka jambo hili tuliondoshe kwa utaratibu huu, hakuna jambo ambalo tunalidai, siku tukidai almasi ya watu kweli tutakuwa tunadai. Lakini jambo ni letu naomba sisi wenyewe tusikubali kupelekwa katika dhana ya kwamba tunadai.

Mhe. Spika, la tatu mimi naomba tusiwatishe na kuwatia fadhaa wananchi, maana haya ni mambo ambayo ninayaona hapo sana katika mjadala huu

tunaoelekea sasa wa rasimu. Fadhaa ya kwanza tunawatia wananchi hasa wenzetu tunawasikia sana wanasema, tena wengine watu wakubwa, wengine watu ambao hutarajii kama watasema hivyo, lakini wanasema Wazanzibari wako wengi Bara, maana ukitoa hoja sasa ya kusema hili lirekebishwe unaonekana kama unataka kuvunja Muungano. Kwa hivyo tusiwatie hofu kwamba mtu asiseme yeye anataka lipi na akisema ikawa nongwa kwamba wewe unataka kuvunja muungano si sahihi, huu mchakato umeletwa ili watu waseme ili turekebishe hizo kasoro. Kwa hivyo tusiwatie hofu kuwaambia Wazanzibari wako wengi, kwa hivyo Muungano ukivunjika itakuwa hivi. Mimi nadhani Bara wako wengi zaidi watu wa nchi nyengine jirani kuliko Wazanzibari, na hatujaungana na nchi hizo hata moja. Mimi naamini Wanyarwanda walioko Tanzania Bara ni wengi zaidi kuliko Wazanzibari, na hakuna mtu anayesema tuungane na Warundi isipokuwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mhe. Spika, vile vile wapo wengine wanasema faida za kiuchumi, kwamba ah! Wazanzibari wamewekeza, wanasema maneno hayo tunasikia kwenye *Television*, tunaona kwenye magazeti, tukijenga misingi hii kusema kweli ni mbaya. Mimi ninavyoamini kwamba Wazanzibari uchumi wanaoumiliki asilimia ni ndogo sana ukilinganisha na nchi nyengine. Kuna watu ndio wanaomiliki migodi, ndio wanaomiliki rasilimali zote kubwa kubwa lakini hatujaungana na nchi hizo sisi, huu ni utaratibu wa kidunia wa kufanya biashara. Lakini wengine wanasema kwamba mchele mtapata wapi, wako pia wanaosema hivyo, lakini Mhe. Spika, ukitoka hapo nje magari yaliyopo nadhani asilimia 99 yanatoka Japan na ukitizama basi labda gari moja linanunua tani kumi za mchele au zaidi, lakini hatuna hofu sisi hatujaungana na Japan wala hatuna hofu ya kusema kwamba siku moja wakikataa gari wasituuzie hii ni biashara, sasa tukiitumia katika misingi hii mimi nadhani tutakuwa tunajenga misingi mibaya ya kujadili jambo letu namna ya kulirekebisha. Maana itakuwa sasa tunajadili kwa ugomvi na hili ni jambo limeletwa tulijadili wala tusitiane hofu wala tusitiane fadhaa wala tusifanye kinyongo katika kujadili hili. Mimi niseme hilo kama wajibu wetu kama viongozi tumepewa dhamana ya kuongoza wananchi katika jambo hili.

Mhe. Spika, la mwisho nimalizie kwa jambo ambalo limeulizwa na Mhe. Raza na pia Mhe. Ismail Jussa kuhusiana na kisiwa cha Latham Island. Kwanza Mhe. Spika, wengi hapa naamini wanasikia tu kisiwa cha Latham, Fungu Mbaraka, Fungu Kizimkazi, lakini niseme tu kwamba kisiwa hichi kipo ni kidogo, kipo umbali wa karibu kilomita 57 kutoka kusini mwa Zanzibar, yaani kutoka Kizimkazi mpaka Latham ni karibu kilomita 57 kwa kwendea kusini na si kikubwa lakini ni muhimu, maana hakizidi upana wa urefu wa mita 320 kwa upana kama mita 160. Na mimi nitangulie kusema kwamba lile ambalo amelizungumza Mhe. Mohammed Raza kwamba kweli

kuna watu walienda kule wakakamatwa na tunamshukuru ni yeye mmoja aliyetusaidia kutupa hizi taarifa na baadaye waliohusika wakatuandikia Serikalini kwamba limetokea jambo hili, na baada ya hapo tukaanza kulifuatilia. Na mimi pia nimshukuru Mhe. Jussa kwamba ni mmoja ambaye ametuunganisha na watu ambao wana taarifa zilizotusaidia kuhusiana na msimamo wa kisheria ya kisiwa hichi cha Zanzibar, nimshukuru sana kwa kweli.

Mhe. Spika, baada ya kupata taarifa hii Serikali iliagiza kwamba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ilifanyie kazi na niseme kwamba kwa umuhimu wa jambo lenyewe mimi binafsi yangu ndio niliyehakikisha kwamba tunalifanyia kazi maana yake ndio niliyekuwa nikienda nikirudi, nikishinda na kufanya utafiti pale *Archives*. Kwanza niishukuru kwa juhudi ya Serikali kuihifadhi ile *Archives* ikawa na kumbukumbu muhimu. Lakini la pili niushukuru uongozi wenyewe wa *Archives* kwa msaada ambao wametupa kupata kumbukumbu sahihi kuhusu suala hili.

Mhe. Spika, taarifa rasmi naamini kwamba Serikali itakapokamilisha kuitayarisha kila Mjumbe atapata taarifa hiyo ambayo itakuwa na maelezo hayo. Lakini kwa ufupi nawaomba niwakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba kisiwa hichi ni cha Zanzibar (Makofi) na kimekuwa rasmi chini ya Zanzibar tokea tarehe 19/10/1898. Na tokeo wakati huo kusema kweli hakujawahi kutokea mzozo wa umiliki wa kisiwa hichi isipokuwa mara moja tu. Mwaka 1910 Wajerumani waliwahi kudai kwamba hichi ni cha kwao, lakini Serikali wakati ule ikawajibu majibu fasaha kabisa kuhusiana na uhalali wa kisiwa hichi kuwa chini ya Mamlaka ya Zanzibar na majibu yale yalipelekwa kwa Serikali ya Ujerumani tarehe 13/4/1911, na yakaelezwa misingi na hata wakaambiwa kwamba ah! Nyinyi wenyewe mwaka 1900 Serikali hapa ilishauri nchi nyengine kuweka maboya haya ya kuongezea meli au minara ya kuongozea meli, katika maeneo ya Zanzibar kikiwemo kisiwa hichi na nyinyi Wajerumani mlipewa taarifa hiyo wala hamkuleta malalamiko kwamba ni cha kwenu, lakini na kwa mujibu wa sheria za kimataifa ni kwamba kisiwa hiki kimekuwa chini ya Zanzibar kwa miaka mingi lakini rasmi ni tokea mwaka 1998. Lakini kwamba kama mna madai mnakitaka njooni tuzungumze, lakini hawakujibu barua hiyo wala hawakuja, wala hawajawahi tena kuleta malalamiko ya kwamba kisiwa hichi labda ni chao au wana madai juu ya kisiwa hichi.

Mhe. Spika, na tokea wakati huo 1911 mpaka leo hakujawahi kutokea malalamiko wala madai ya nchi yoyote wala taifa lolote wala mtu yeyote na kisiwa hichi kimekuwa kikiendeshwa chini ya Zanzibar kwa miaka yote hiyo. Mwaka 1959 kwa kupitia tangazo la kisheria No. 56 na mwaka 1959 kisiwa hichi kilitangazwa na Zanzibar chini ya sheria ya hifadhi ya ndege kuwa ni

hifadhi ya ndege na mpaka leo tangazo hilo halijafutwa, kwa hivyo kwa sheria za Zanzibar mpaka leo kisiwa hichi bado ni hifadhi ya ndege (Makofi).

Mhe. Spika, mwaka 1963 kama alivyoeleza Mhe. Jussa hapa kwamba ni kweli chini ya kifungu cha 136 cha Katiba ya Zanzibar mwaka 1963 kisiwa hichi kilipewa hadhi sawa sawa na Unguja na Pemba, kwa sababu kifungu kile nimesema kwamba Dola ya Zanzibar ni Unguja, Pemba na Latham na visiwa vidogo vidogo. Kwa hivyo kama nilivyotangulia kusema kwamba Serikali inaandaa kwanza mpango wa usimamizi madhubuti, haya yaliyotokea yametutanabahisha na yametukumbusha kwamba kuna haja ya kufanya usimamizi wa kisiwa hichi na hili linaandaliwa na taarifa rasmi ili kila mtu aliyekuwa na wasi wasi apate taarifa hii inaandaliwa na hakika kwamba kila Mjumbe atapata taarifa hii rasmi ya Serikali (Makofi).

Mhe. Spika, niseme tu kwamba kilichotokea au kilichofanywa lakini hatujawahi kupata malalamiko ya Serikali tokea wakati huo wa Tanganyika wala Serikali ya Muungano kuhusiana na umiliki wa kisiwa hichi. Kwa hivyo kwa kuwatoa wasi wasi Waheshimiwa Wawakilishi na wananchi ni kwamba hakuna mzozo kuhusiana na suala hili na hayo niliyoyasema yanaendelea kuandaliwa.
Mhe. Spika, nilisema labda niseme hayo na baada ya kusema hayo niwaombe Waheshimiwa Wajumbe tuipitishe bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, tuwawezeshe wafanye kazi.Naunga mkono hoja. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza niwashukuru Wajumbe kwa kofi hizo na waendelee kuonesha moyo huo huo kuipitisha bajeti yetu hii vizuri kabisa.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Makamu wa Pili wa Rais, kwanza kabisa kabisa naomba kumshkuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia tena uhai na uzima na kutuwezesha kuendelea kufanya shughuli zetu katika Baraza hili tukufu. Aidha Mhe. Spika, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kusimama mbele ya Baraza hili na niendelee kukushukuru kwa namna unavyoliongoza vizuri Baraza letu. Vile vile nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa na Wajumbe wake wote wa kamati ile kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kutoa maoni, mapendekezo na maelekezo mbali mbali ambayo kwa kweli sisi kama Wizara tunayapokea na kwenda kuyafanyia kazi. Aidha niwashukuru sana Wajumbe wote wale waliochangia, waliochangia kwa maneno, waliochangia kwa maandishi, na waliochangia kimya kimya wote wametuchangia nawashukuru sana sana. Na kwa heshima ya kipekee Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, atawataja kwa majina wakati atakapokuja kujumuisha majuisho ya mwisho ya Wizara ya hii.

Mhe. Spika, tumechangiwa karibu na Wajumbe 30 katika Wizara hii, waliochangia kwa maandishi na kwa maneno naamini wote walikuwa na nia njema ya kutukosoa pale ambapo wanahisi pana kosa, na kuturekebisha ili utendaji wa kazi Serikalini uwe mzuri zaidi. Kwetu sisi tunapokea maoni na mapendekezo haya. Aidha nitoe pongezi za kipekee kwa Viongozi wetu Wakuu. Kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, niseme wazi kabisa kabisa Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe viongozi wetu hawa wana mahusiano mazuri, wanafanya kazi zao kwa pamoja, wanaelekezana na kushauriana kwa manufaa ya nchi yetu na hakuna hitilafu yoyote baina ya viongozi wetu hawa watatu, na Mungu awajaalie waendelee na umoja huo.

Mhe. Spika, lazima tukubali kwamba mfumo huu wa Serikali yetu ya Umoja wa Kitaifa ni mfumo mpya kwetu, ndio tunaanza nao, kwa kawaida changamoto za hapa na pale zinajitokeza, lakini changamoto hizo zisiturejeshe nyuma, linapotokea tatizo linarekebishwa tunakwenda mbele, yatatokea tu matatizo katika uhai wa binaadamu, lakini huu ni mwanzo na mimi ninataka niseme tumefikia hatua kubwa ukilinganisha na nchi yetu ya Kiafrika jirani zetu hapa wameliona na wengine mnaona, sina haja ya kutaja nchi lakini mmeona wameanzisha mifumo kama hii na namna gani wamepata tabu zaidi, sisi tumekwenda uzuri, kwa hiyo niwapongeze sana viongozi wetu wakuu hawa na pongezi maalum ziende kwa Rais wetu, Rais wetu amesimama imara, hakuyumba, hasikilizi hili wala lile wala chokochoko zozote anaendesha nchi yetu kwa manufaa ya nchi na watu wake. Kwa hivyo naamini kwamba kila linalofanyika ni kwa maslahi yetu kwa pamoja. Mimi kwa maana hiyo nampongeza sana sana Mhe. Rais, Mwenyezi Mungu azidi kumpa umri yeye na familia yake wazidi kutuongoza. Na rasilimali yetu pekee Wazanzibari ni umoja wetu, amani na utulivu ndio utakaotusaidia sisi kutuondoa hapa tulipo, matatizo yetu sote yanategemea na umoja wetu, tukiuvunja umoja wetu hatuna safari, hilo tulijue.

Mhe. Spika, kwa hivyo jambo la kushabikia sote na kuhakikisha kwamba umoja wetu unakuwepo, tunakaa kwa pamoja, tunasikilizana, mambo madogo madogo yakijitokeza tunayatafutia ufumbuzi wa pamoja, hakuna njia ya mkato isipokuwa tuelewane, tupendane, tushirikiane.

Mhe. Spika, ni wajibu wetu ndani ya Serikali kusikiliza maoni ya Wajumbe wa Baraza hili tukufu na tunafanya hivyo kwa maendeleo ya nchi yetu, wakati wote tunakuwa wasikivu kwa nia ya kuleta mabadiliko. Ni lazima tukubali kwamba dunia ya leo inabadilika kwa kasi ya haraka sana, kwa hivyo hatuna budi sote kwa pamoja tushirikiane ili tuendeleze nchi yetu na nchi haijengwi na Serikali peke yake inajengwa kwa maelewano ya pamoja, Serikali, Sekta

Binafsi na Wananchi wote kila mmoja atimize wajibu wake hapo alipo ili tupige hatua, na mimi sana sana Mhe. Spika, kwa jitihada hizi tutafanikiwa, hakuna njia ya mkato, lazima tufanye kwa bidii ndio matokeo yatokee.

Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe hapa waligusia sana sana suala la uwajibikaji, matumizi mabaya ya fedha za umma, utekelezaji wa maagizo na ushauri wa Baraza la Wawakilishi na Kamati zake na hasa Kamati Teule, maadili ya uongozi na uadilifu wetu na uratibu wa shughuli za Serikali. Nataka niwahakikishie kwamba Mhe. Spika, uendeshaji wa nchi ni namna ya kuyakabili matatizo yanayojitokeza na namna ya kuweka mazingira mazuri ya kuyatatua matatizo hayo, na ndani ya Serikali mambo mengi haya yameanza kwa muda mrefu, tumeyakuta na watakaokuja baada yetu watayakuta na wao watafanya wajibu wao, lakini tunajitahidi kujenga misingi itakayosaidia matokeo yanayotokea sasa yasitokee mbele. Tunajaribu kujenga misingi ya kuhakikisha kwamba tunapiga vita kwa hali yoyote ubadhirifu, tunapiga vita ubaguzi, tunapiga vita kwa hali yoyote jambo lolote baya lisitendeke ndani ya Serikali yetu.

Mhe. Spika, huu ndio msimamo wetu na hatua mbali mbali tunazozichukua malengo na mtazamo wetu huo kuanzishwa kwa Tume ya Utumishi, kuweka taratibu za miundo ya mifumo ya utendaji kazi, kuanzisha mageuzi ya kiutendaji, kuanzishwa kwa utaratibu wa kusikiliza taarifa za Serikali kila miezi mitatu zinazowasilishwa kwa Rais, kuanzishwa mchakato wa kuwa na sheria ya maadili ya viongozi, kuanzishwa sheria ya kupambana na rushwa, kujenga misingi ya utawala bora, kufanya tafiti za utawala bora na vile vile kuondoa kufanya kazi kwa mazoea, nia na madhumuni ni kupambana na ubadhirifu, kuleta mabadiliko katika utendaji wa Serikali. Nia yetu si kumlinda Kiongozi yeyote ambaye anafanya ubadhirifu ndani ya Serikali na ziko hatua za muda mfupi, ziko hatua za muda kwa kati, ziko hatua za muda mrefu na hatua hizo zimeanza na tumeanza kuwashughulikia na wengine kuwaondosha katika nafasi mbali mbali na kuweka watendaji wengine katika wizara na bado vyombo vyetu vinavyofanya uchunguzi na kutafuta mambo mbali mbali kwa ajili ya kuwapeleka Mahakamani na kila mwenye kosa atahukumiwa kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Spika, hatuwezi kumlinda mtu na yako mambo mengi yamefanyika, nikianza kuyataja hapa kwa muda huu tulionao itachukua muda mrefu sana. Lakini nitakachokifanya nitahakikisha nimeliandikia Baraza hili kuleta hatua baada ya hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kuwashughulikia wale wote ambao Baraza hili lilitushauri, hakuna tunachokidharau, tunawaheshimu, tunayapokea, tunayafanyia kazi, tunafanya kazi kwa pamoja. Sote sisi ni wamoja tunafanya kazi moja, na nia yetu ni kuwahudumikia wananchi tuondoke hapa tulipo nchi yetu ilete mabadiliko makubwa ya kiuchumi na

kimaendeleo ndio madhumuni yetu sote hapa, hatuwezi kudharau jambo ambalo mnashauriana kwa nia njema na kutuondoa hapa tulipo. Kwa hivyo ninakuombeni mjue ziko hatua mbali mbali zinachukuliwa ndani ya Serikali na tutazileta hapa na mtazielewa.

Mhe. Spika na Waheshimiwa kiukweli tupo katika hatua mbali mbali za kuimarisha Muungano wetu. Haya yote tunayoyafanya Mhe. Spika, tunayafanya kwa nia njema ili kila upande wa Muungano wetu upate haki iliyo sawa na sahihi. Tutaendelea kushirikiana vizuri kuimarisha umoja wetu, amani na utulivu wa nchi yetu. Yapo mafanikio yaliyopatikana katika Muungano lakini pia yapo matatizo yamejitokeza ndani ya muungano na lazima yashughulikiwe na lazima yaendelezwe. Na njia nzuri na sahihi ya kuondoa matatizo haya ni mchakato wa Katiba. Naamini wananchi watapata nafasi na wameshaanza kuonesha muelekeo mzuri wa kutafuta ufumbuzi wa matatizo yetu ndani ya nchi zetu mbili. Naamini kabisa kabisa katiba mpya itatuwekea mustakbali mzuri wa kuondoa matatizo yaliyopo ya Muungano.

Kwa hivyo, sipendi nirudie mambo ambayo wenzangu wameyasema, nataka nimshukuru sana Mhe. Raya Suleiman Hamad, nimshukuru sana Mwanasheria Mkuu kwa maelezo yake na wengine wote ambao wamechangia hoja hii. Kwa kweli waliyoyaeleza kwamba tumefikia hatua ya pili, tumetoka hatua ya mwanzo ya kutoa maoni ya mchakato wa Katiba, sasa tumekwenda hatua ya pili ya Mabaraza ya Katiba tuwaachie Wajumbe wa Baraza la Katiba watoe maoni.

Mhe. Spika, ni wajibu wetu kuwasaidia wale wajumbe wetu kama tunaona kuna jambo lina kasoro, lina tatizo, tukionana na wajumbe wetu tuwaambie hapa kuna hivi, hapa kuna hivi ili tuondokane na rasimu ambayo itatusaidia kwa maendeleo yetu na vizazi zinavyokuja. Hatuna haja ya kuchukiana, kugombana, kulumbana wala kutukanana, cha msingi hapa ni kushirikiana tukafanya kazi kwa pamoja kwa maslahi ya nchi yetu. Naamini sote lengo letu ni moja, nia yetu ni kuimarisha Zanzibar, ni kuiendeleza Zanzibar, tunajenga nyumba moja tunagombania fito za nini? Kwa hivyo, mimi naamini kabisa tukishirikiana vizuri tutapata suluhu ya matatizo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, ziko hoja mahsusi mbali mbali ambazo Wajumbe wamezieleza na hasa wameeleza sana kuhusu suala la vifungu mbali mbali vya wizarani kwetu, hasa walionesha kuna vifungu vimejitokeza vina mapungufu, kuna vifungu vimejitokeza vina ziada, lakini sababu kuu za msingi zilizopelekea kujitokeza huko si kwa sababu nyengine yoyote ni kwa sababu tumeanza kujenga uelewa ndani ya wizara yetu kujua nini tunakitaka. Pia tunaanza kufahamu mahitaji ya gharama ya hizo shughuli tunazozihitaji.

Kwa hivyo, hii inatokana na uzoefu tunaoendelea kuupata katika kupanga mipango yetu ya kibajeti tukiangalia mwaka uliopita na mwaka unaofuata. Sasa hivi ndio tunaanza ku-*experience practically* kile kinachojitokeza, tunakwenda *per activities* tunajua *unit* hii inahitaji hiki na hiki na ndio maana utakuta hivi. Inawezekana ukaona mwaka huu kuna mapungufu ya kifungu hiki ama kuna ongezeko la kifungu hiki, kilichofanya vile msingi wetu mkubwa ni kwamba kutokana na uzoefu tuliopata ndio ambao umetusaidia kufikia hatua hii.

Vile vile Wizara yetu ya Fedha sisi inajitahidi sana kutuelekeza namna ya kuandaa bajeti kuelekeza kwenye *core function* zetu. Kwa hivyo, matokeo yake ndio haya hapa ambayo Waheshimiwa mmeyaona. Kwa hiyo ni vyema mlivyouliza mkataka kupata ufafanuzi wa baadhi ya vifungu mbali mbali na mimi nitajaribu kueleza kadiri nitakavyoweza kuyaelezea hayo na mengine tutastahamiliana, haina haja ya kupiga buti tukapoteza muda mwingi sana wakati nia yetu ni moja.

Lilijitokeza suala la kifungu cha mafuta katika vifungu vya Ofisi ya Pemba. Ni kweli matumizi ya mafuta yamejitokeza kwa mwaka huu kupungua, ila yamepungua kwa sababu shughuli zile ambazo zilifanywa mwaka jana tulikuwa tunazifanyia Micheweni, hii inahusiana na kuendesha ile gari ya sinema. Kwa hivyo, kiwa vyovyote vile kutoka Chake Chake kwenda Micheweni mafuta yatakuwa yamepanda. Mhe. Ali Salum Haji aliuliza hilo, ukifanyia Chake Chake kunakuwa na upungufu. Mimi nawashukuru vijana wetu kuliona hili maana ingekuwa na wao si waaminifu wangeendelea tu kupandisha asilimia, hatuendi hivyo sasa tunakwenda kutokana na shughuli yenyewe. Kwa hivyo, naamini hii ni moja katika hatua ambayo tunapiga.

Kuhusu kifungu cha viburudishaji. Ni kweli ukitizama hiki kifungu utakiona kimepaa sana, lakini kinavyojitokeza hapa sasa viburudishaji kumewekwa kwenye sehemu moja, zamani ilikuwa utavikuta kwenye kifungu hiki na kifungu hiki, idara hii na idara hii, sasa hivi vinawekwa mahala pamoja na kule Pemba wameweka mahala pamoja. Kwa msingi huo ndio utaona kifungu hiki kimekuja juu zaidi.

Ukija kwenye safari za kikazi kwa kule Pemba utaona zimeongezeka shilingi laki nane na elfu arobaini, mwaka jana ilikuwa ni shilingi 28 milioni, lakini kwa sababu kulikuwa kuna vifungu viwili pale tofauti. Kifungu kimoja mwaka jana kilikuwa na shilingi 26 milioni na kifungu kimoja kilikuwa na shilingi milioni mbili. Sasa kile kifungu kilichokuwa na shilingi milioni mbili kimeongezeka shilingi milioni nane sasa hivi kitakuwa na shilingi milioni kumi, na kile chengine kitakuwa na shilingi 18, 849,000/-. Kwa msingi huo ndio kimeongezeka, hivyo kuongezeka kwake isiwe dhana kwamba ndio

zimeongezeka nyingi sana, zimeongezeka shilingi 840,000/- kutokana na hali halisi ya mabadiliko yanavyokwenda. Kwa hivyo, mambo haya yatakuwa yamejitokeza katika vifungu mbali mbali tutaelezana, tutajibizana kwa kadiri ambavyo itahitaji maelezo zaidi.

Mhe. Spika, kuhusu suala la fedha nyengine ambazo hazikuonekana katika bajeti kwenye buku kubwa lile la maelezo ya Mapato na Matumizi, ni kwamba kwa upande wa Idara ya Maafa. Kuna fedha zinazoonekana shilingi 70 milioni na 270 milioni zinazotoka *UNICEF*, lakini shilingi 439,500,000 ambazo tuliahidiwa na *UNDP* hazionekani pale. Pesa zile hazionekani kwa sababu wenzetu hawa walichelewa kutupa hizi taarifa, wakati tunazipeleka taarifa kuandaliwa kitabu hiki cha bajeti ilikuwa hatujapata idadi hii ya fedha. Idadi hii ya fedha tumeipata baada ya kuandaliwa kitabu cha bajeti, lakini sisi tukaona kwa heshima ni vizuri kuripoti kwenye Baraza hili tukufu. Kwa hivyo, ikionekana kwamba tuziondoe tusiripoti hapa mpaka zitakapokuja lakini matumaini makubwa na hawa wenzetu wanapo *confirm* wanatoa ule udhati wa moyo wao wanatusaidia mara zote *UNDP* na ndio maana tukaona kuna mabadiliko ya namna hiyo.

Vile vile ziliulizwa zile shilingi 4.3 bilioni zinazosaidia kwenye suala zima la Tume ya Uchaguzi kwa ajili ya kuendeshea kura ya maoni. Hizi hazitoki kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hizi wanazitoa wenzetu upande wa Jamhuri ya Muungano kuzileta kwa ajili ya kufanyia kura ya maoni. Kwa hivyo, nazo pia inawezekana hapa ukiziona zinaweza kuwa zimeleta hitilafu. Fedha ambazo zimeonekana moja kwa moja ni zile shilingi 3,364,000,000/- hizi za washirika wa maendeleo ambazo zilitolewa kwa ajili ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, kwa ajili ya kutaalamisha, kujenga uwezo na kadhalika na ile elimu kwa wapiga kura.

Kwa hivyo, msingi wake kwenye suala hili liko namna hiyo, lakini kadiri litakavyokwenda huko mbele kwenye masuala ya mafungu tutajaribu kuelezana na kutoa ufafanuzi zaidi pale Waheshimiwa wakihitaji kupata ufafanuzi zaidi kutokea upande wetu.

Mhe. Spika. Mhe. Makame Mshimba na baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe akiwemo Mhe. Mohammedraza Hassanali na Waheshimiwa wengine walizungumzia sana suala la mapato ya gesi asilia na mapato mengine yanayotokana na Muungano, na wakasema je, sasa tunakwenda kwenye utaratibu mpya mapato yetu haya vipi? Tusijekwenda kwenye utaratibu huu fedha zetu hizi tukazikosa.

Mhe. Spika, nawambia hatuwezi kuzikosa fedha zetu hizi, mtazamo wetu ni kupitia Tume ya Pamoja ya Fedha, haya mambo yote yanajulikana kila haki

yetu lazima tuipate. Mhe. Mwanasheria Mkuu kasema hapa ni haki yetu ni kuichukua wenyewe tu, kwa hivyo tuelezane tupewe haki yetu, lazima tudai haki zetu zote. Kwa hivyo, utaratibu wowote utakaotokea bado haki zetu Zanzibar zipo pale pale na lazima tuzipate. Hawa wenzetu tumekubaliana, sisi tunachokitaka kwenye kamati ya pamoja ile tunawahimiza wenzetu upande wa Tanzania Bara kwamba wamalize nao mapendekezo yao ili *GAC* ifanye kazi na mambo yaende vizuri utekelezaji uanze mara moja. Kwa sababu sisi tunazihitajia sana fedha hizi na inaonekana ni nyingi na Mwenyezi Mungu akitujaalia kwa hali inavyokwenda na wenzetu weshafika hatua kubwa nao kwenye suala hili naamini litapata ufumbuzi.

Kuhusu nyumba iliyoko Afrika ya Kusini. Ni kweli yalikuwepo mazungumzo kwa nia ya kubadilishana nyumba hii iliyoko Afrika ya Kusini na nyumba anayokaa Makamu wa Pili wa Rais pale Dar es Salaam. Lakini utaratibu walioutaka utumike ni wa kutia thamani. Nyumba ya Afrika ya Kusini itiwe thamani na nyumba tunayokaa pale itiwe thamani ionekane bei yake kiasi gani na mabadiliko yenye utaratibu, anayemzidi mwenzake amzidishie ile tafauti si kwamba kulikuwa na mpango tu wa kuitoa au chukua hii na mimi nichukue hii. Taratibu lazima zifuatwe ili tufikie maamuzi mazuri. Na tunafanya hivyo kwa kuona ile nyumba inaharibika tu, kila ikiendelea itaharibika na itapotea kabisa. Kwa hivyo, uamuzi kwamba mahitaji ya nyumba tunahitajia na nyumba tunayo imekaa ili nyumba ile isiharibike basi tunaona utaratibu huo unatusaidia zaidi.

Kuhusu suala la Fungu Mbaraka namshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu amelielezea sina haja ya kutia nukta wala ziada ya aina yoyote, maelezo aliyoyatoa ni sahihi.

Mhe. Spika, kuhusu usahihi wa Sensa. Nataka nimhakikishie Mhe. Ismail Jussa na Waheshimiwa wengine kwamba, wataalamu wetu wamefanya kazi hii vizuri, wameifanya kwa utaalamu wao na uzoefu wao mkubwa walionao na wamekwenda vizuri. Suala kubwa hapa wametumia teknolojia ya kisasa ya kazi za uingizaji wa taarifa na uchambuzi wa taarifa. Teknolojia ile inayojulikana kama *optical mark recognition.* Teknolojia hii inaisaidia sana baadhi ya kusoma dodoso kwa urahisi kulipeleka kwenye kompyuta, sasa kazi ambayo tulifanya huko nyuma tulifanya kwa miezi tisa inaweza kufanywa kwa mwezi mmoja.

Kwa hivyo, hilo ndilo lililotokea. Na taarifa nyengine nyingi zitaendelea kutokea awamu kwa awamu, hakuna nia yoyote ya kupika takwimu, tunajua ndani ya serikali ukipika takwimu unajiumiza mwenyewe, tunachokitaka ni takwimu halisi ili tushughulikie matatizo ya wananchi wetu. Na ndio maana ilikuwa tunahimiza sana watu wajitokeze wajiandikishe kwenye sensa ili

tuweze kuwaelewa walipo na mahitaji yao tuweze kuwahudumia. Kwa hivyo, nataka niwahakikishie Wajumbe kwamba hakuna nia hata kidogo ndani ya serikali ya kupika takwimu.

Kuhusu kero zilizopatiwa ufumbuzi. Mhe. Subeit Khamis Faki na wengine walisema hizi kero zilizopatiwa ni zile ambazo hazina maslahi ya kiuchumi. Nataka niseme Mhe. Spika, mengine lazima tuyashukuru tumepata ufumbuzi na zina maslahi ya kiuchumi.

Utekelezaji wa sheria za haki za binadamu, utekelezaji wa *Multi Shipping Act* una maslahi kiuchumi. Misamaha ya mikopo ya fedha kutoka *IMF* tumepata vitu chungu nzima hapa vya kilimo, magari na kadhalika vya serikali, kwa hivyo yana faida kiuchumi. Uwezo wa Zanzibar kutoka ndani na nje pia faida ya kiuchumi, Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo ule tulilimaliza wenyewe kwa sababu ya kuanzisha Mfuko wetu wa jimbo hapa.

Kodi ya mapato kutokana na *PAYE* ina faida kiuchumi inatusaidia kwenye bajeti yetu. Kwa hivyo haya mambo tulioyamaliza yana faida ya kimsingi kabisa na mengine tunachokitaka yamalizwe haraka, utekelezaji uendelee na maslahi makubwa yapatikane na manufaa ya kila upande wa Muungano wetu na kila chetu tukidai ni haki yetu. Kwa hivyo, naomba tuendelee vizuri na mchakato huu wa Katiba ili yale ambayo yana matatizo basi kupitia mchakato wa Katiba yapatikane majibu.

Kuhusu Waziri wa Muungano kutangaza kuwa Zanzibar ni eneo la ugaidi je, vipi Arusha? Mhe. Spika, suala la ulinzi na usalama liko chini ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na kwa kawaida Waziri kutangaza hutegemea sana taarifa anazozipata kutoka vyombo vyetu vya ulinzi na usalama. Kwa Arusha mpaka sasa bado uchunguzi unaendelea, matokeo bado hayajatolewa, kwa hivyo itakapoyumkinika uchunguzi ule ndio atatangaza kwamba tukio lile ni la usiri gani ndani yake au limefanywa kwa misingi ipi. Lakini mimi ningependa nitoe wito tu, kwamba tujitahidini wananchi wa Zanzibar tusigombane wenyewe kwa wenyewe, tusihujumiane wenyewe kwa wenyewe, tusiumizane wenyewe kwa wenyewe. Tunapofanya haya tutatoa fursa ya wengine kutuumiza, sisi wenyewe tuelewane, na mimi nataka niwahakikishie kwamba Zanzibar ni shwari, ni salama, tunaendelea vizuri.

Mhe. Spika, kuhusu Jeshi la Polisi kufanywa Mkoa. Kwa kweli Zanzibar ina mikoa mitano Jeshi la Polisi halifanywi mkoa. Tatizo liliopo ni uwezo wa kifedha ndani ya Jamhuri ya Muungano wenyewe, mapato yanayopatikana ni kidogo. Sasa hivi kumechukuliwa hatua maalum za kuimarisha Jeshi la Polisi nchini. Kuna utaratibu mpya wa maboresho ya Jeshi la Polisi siku ya semina ile yalielezwa vizuri, nia ni kuimarisha uweledi ndani ya Jeshi la Polisi, ni

kuimarisha zana za kisasa, makaazi bora kwa askari, vituo vya kisasa vya polisi na maslahi mazuri ya askari wetu.

Kwa hiyo, cha msingi hapa tukubali kwamba tatizo liliopo ni uwezo wa kibajeti, lakini tutahakikisha kwamba lazima polisi Zanzibar ipewe mgao maalum kwa sababu inahudumia nchi ya Zanzibar na viongozi wake. Inayo jukumu kubwa la kufanya hivyo ukiiunganisha kwa sababu hakuna udogo wa nchi katika kuwahudumia viongozi, viongozi ni viongozi wana hadhi sawa. Kwa misingi hiyo kwa vyovyote vile lazima Jeshi la Polisi waone umuhimu huo katika migawano yao ya fedha ili Jeshi la Polisi Zanzibar lisiwe na matatizo.

Kuhusu msaada kwa Polisi Jamii. Ni nia ya serikali kabisa kuunga mkono hatua zote za Polisi Jamii. Polisi jamii wanafanya kazi nzuri ya kuhakikisha wanaongeza suala la ulinzi katika maeneo yetu na lazima tuwapongezeni kwa kazi kubwa wanayoifanya. Ni kweli kwamba wana matatizo mengi ambayo wanahitaji kusaidiwa. Serikali kupitia Jeshi la Polisi imeanza kazi ya kusaidia Polisi Jamii na sisi kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kadiri uwezo tutakaokuwanao tutawasaidia wenzetu hao. Lakini ningependa nitoe wito kwa viongozi, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Mawaziri, Sekta Binafsi na wananchi mbali mbali tuwaunge mkono Polisi Jamii wanasaidia sana, wanafanya kazi kubwa sana ya kufanya ulinzi ambao ni kwa usalama wetu sote.

Kwa hivyo, si vibaya tukaanzisha utaratibu maalum hasa sisi viongozi, hata Mhe. Makame Mshimba ameonesha mfano sana kwenye eneo hili kusudi tushirikiane kwa pamoja tuwasaidie wenzetu wa Polisi Jamii. Kwa sababu wana matatizo mengi na mimi naliunga mkono jambo hilo.

Kuhusu suala ambalo alizungumza sana Mhe. Ismail Jussa na Waheshimiwa wengine kuhusu jamii ya Wangazija kudhalilishwa katika kupewa *passport*. Sheria zetu za Uhamiaji haziruhusu ubaguzi wa mwananchi yeyote. Wananchi wote wana haki sawa mbele ya sheria, kwa hivyo huwezi kuwadhalilisha, huwezi kuwabagua na mimi ningeomba sana Mhe. Jussa malalamiko hayo atuletee rasmi serikalini tuyashughulikie. Hatuna nia kabisa ya kumbagua mtu yeyote, haki ni kwa wananchi wote.

Mhe. Spika, kuhusu matumizi ya *diplomatic Passport*. Jambo hili lishapata ufumbuzi, wenye hadhi ya kutumia *diplomatic passport* ni wale ambao wana hadhi inayokubalika kwa mujibu wa sheria na taratibu ziliopo. Wale wote ambao wameshapungukiwa na hadhi hiyo basi hawana haki ya kuendelea kutumia *diplomatic passport*, na tayari wote wamearifiwa na Uhamiaji wamewapelekea taarifa za kuwataka warudishe, sasa asiyerudisha shauri

yake. Maana utatajwa mtandao unatolewa *passport* yako unaipeleka puu, hakirudishwi kitu. Kwa hivyo, utakuja kuadhirika mtu mzima uko safarini au uko wapi ya kutafuta, halafu watu wa meli wanasema aa hiyo sio *passport* yako matatizo yatakukuta wewe kwenye safari. Kwa hivyo, nawaomba sana wale ambao hawana hadhi tena ya kutumia *passport* hizi za *diplomatic* wazirudishe kwani watatolewa kwenye mtandao wasije kumlaumu mtu.

Kuhusu Rasimu ya Katiba mpya tumeshaieleza kwa hivyo maelezo mazuri Mhe. Bi Raya ameyatoa na tulitakiwa tutoe msimamo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar nini maoni yetu kwenye rasimu. Maoni yetu ni maamuzi ya wananchi, wanachokitaka wananchi ndio tunachokitaka serikali, haya maneno tushayasema na tutaendelea kusema, msimamo wetu wa SMZ ni maamuzi ya wananchi wenyewe, maoni ya wananchi ndio sisi tunayaheshimu.

Mhe. Spika, kuhusu suala la uratibu wa serikali mimi nipokee ushauri, niupokee ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wajumbe mbali mbali. Ni kweli yapo matatizo katika suala la Uratibu. Ni kweli watendaji wetu wana mapungufu ya hapa na pale lakini lazima tuwape pongezi na kazi wanazozifanya. Wanafanya kazi nyingi sana kabisa, kuratibu mambo mengi na kwa kweli wanahitaji kupewa mafunzo zaidi, kutaalamishwa zaidi ili kujenga uelewa mkubwa, wanajitahidi kufanya kazi zao mambo ni mengi sana kwenye shughuli za uratibu ni moja katika Idara ambayo ina wafanyakazi kidogo na ina shughuli nyingi, inahitaji kupewa msukumo ili iweze kutoa utendaji uliotukuka, utendaji unaostahiki.

Kwa hivyo niseme tu, tunayapokea mashauri ambayo Waheshimiwa mmetupa ili tukayafanyie kazi na ili tuweze kutoa utendaji wenye viwango, wenye ubora ili kukidhi mahitaji yenu Waheshimiwa na yenye kukidhi mahitaji ya wananchi. Msimamo wetu ni kuendesha serikali ambayo inahudumia wananchi kwa vizuri zaidi. Azma hii yote ni kufanya jambo lenye urasimu, inapotokea hiyo ni kwa sababu tu ya bahati mbaya lakini nia yetu ni kuhakikisha kwamba tunatoa huduma vizuri kwa wananchi wetu.

Kuhusu mfumo wa Uandishi wa bajeti. Nataka tuupokee ushauri huo ili kuwa na uwiano mzuri wa kitaasisi, mfumo wetu wa kiuandishi ulingane na ili u-*simplify* katika kusoma bajeti zetu Waheshimiwa wetu wazifahamu vizuri, na kila penye mapungufu tunapoambiwa sisi tunakubali. Lakini nataka niseme kwamba uandishi wetu wa bajeti kila mwaka unabadilika huwa sio huo huo, tunajaribu kuhakikisha kila jipya na zuri tunaweza kujifunza kutoka hapa Barazani, tunajifunza kutoka kwa wenzetu na mahala pengine tunafanya hivyo ili kila mwaka tuendelee kuwa na bajeti nzuri zaidi. Na nasema wazi kabisa kwamba sisi siku zote tuko tayari kupokea ushauri, mapendekezo kutoka kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu.

Mhe. Spika, kuhusu Miswada ya Sheria kufikishwa Barazani. Hii wakati mwengine inatokea sana kwa sababu sasa hivi tungependa kabisa tusije na sheria unakaa baada ya mwezi mmoja miwili kuna kasoro fulani. Sasa hivi Baraza hili limetuelekeza kwamba sheria yoyote ipitie kwa wadau, ipitie hatua mbali mbali wakati mwengine inachelewa na wakati mwengine pia kunakuwa na mapungufu ya fedha. Lakini nataka nipokee ushauri kwamba nitajitahidi sana kuhakikisha miswada hii ya sheria tunaifanyia kazi ili ziweze kuwa sheria nzuri zilizokamilika ambazo zitakidhi haja ya mahitaji yetu. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa kwamba tutafanya kila jitihada jambo hilo lifanyike.

Kuhusu ukubwa wa serikali naamini mwenye mamlaka anayeunda serikali amesikia maneno haya maana yametoka kwenye Baraza hili yeye ndiye mwenye uamuzi wa kujua ukubwa na udogo wa serikali. Lakini naamini alifanya hivyo kukidhi haja ya kisiasa, haja ya kijamii, haja ya mfumo mpya ya kuanzisha mfumo mpya tuliouanzisha wa Umoja wa Kitaifa, hakufanya tu, atakuwa amefikiri sana katika uamuzi huo. Lakini Mhe. Rais yeye ameyasikia mawazo hayo na yeye ndiye mwenye mamlaka ya maamuzi hayo. Lakini mimi nampongeza sana kwa uamuzi huo na Inshaallah aendelee kumuona na kubakia katika wizara hii.

Kuhusu Makamu wa Pili wa Rais kukasimiwa madaraka. Madaraka Mhe. Spika, ya Makamu wa Pili wa Rais yamo ndani ya Katiba yanaeleza vizuri katika Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 toleo la kumi kifungu cha 39 kinaeleza kazi za Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais ndio watakaokuwa wasaidizi wakuu wa Rais. Kwa hivyo, naamini mamlaka yao yako hapa kwa mujibu wa Katiba.

Kuhusu suala la *TASAF*. Ni kweli miradi ya *TASAF* ipo mengine ambayo haikufanya vizuri, lakini ipo ambayo imefanya vizuri. Sisi tumefanya tathmini ya miradi ya *TASAF* tumeona mapungufu na tumeona mafanikio. Kwa kweli ni vizuri kuendelea nayo miradi ya *TASAF* na ndio maana hata hao wenzetu wa Benki ya Dunia wameona kazi nzuri iliyofanywa kwenye miradi ya *TASAF* na ndio maana wakakubali tuje na *TASAF III*. *TASAF III* msingi wake mkubwa ni kushughulikia kaya zilizo maskini ili kujenga uwezo zaidi.

Kwa hivyo, yale mapungufu ambayo yametokea katika *TASAF* huko nyuma sasa tutajaribu kuchukua kila hatua kurekebisha mapungufu hayo na kujenga msingi wa kuweka miradi hii endelevu kuweza kusaidia wananchi wetu. Sio nia ya serikali kuona fedha hizi zinatumika vibaya, nia ni fedha hizi kutumika vizuri. Tutafanya kila jitihada ya kuhakikisha kwamba udhibiti unakuwa mkubwa, mafanikio yanatokea na zile sekta husika zinalea ile miradi inayoanzishwa. Tatizo kubwa kwa sasa ni kwamba hakukuwa na mpango

madhubuti wa kulea miradi baada ya ufadhili, hivyo tunasema lazima tuweke utaratibu baada ya ufadhili miradi ilelewe na sekta husika ili miradi hii ilete tija kwa wananchi.

Kuhusu uletaji wa kuku nchini. Ni kweli jambo hili linaleta ushindani mkubwa kwenye soko la ndani, lakini jambo la msingi hapa ni kuwawezesha wananchi wetu waweze kuzalisha kuku bora, waweze kufanya vizuri katika kuzalisha na bidhaa nyengine zikiwemo za mboga mboga. Jambo kubwa litalofanya ku-*control* hili ni mbinu ya kodi, iko mbinu ya kodi inatumika ili kuku hawa bei yao nayo iwe juu iweze kushindana katika soko la ndani. Kadiri tutakavyoweza kuzalisha zaidi kodi tutazipandisha zaidi ili kupunguza uingiaji wa kuku kutoka nje. Ni nia ya kusaidia wananchi wetu.

Kuhusu Soko la Saateni Mhe. Asha Bakari amezungumzia sana hili, mapungufu yaliyopo tutayachukua tuyapeleke kwa Baraza la Manispaa ili wayafanyie kazi. Lakini juu ya hivyo wao hivi sasa wanachukua hatua mbali mbali za kutaka kuanza kuezeka mabanda yanayovuja, kuwa na miundombinu ya uhakika ya maji, kuwa na vyoo vya kutosha na pia kufanya tathmini ya kujua wale wafanyabiashara walioko pale ili kuwe na utaratibu mzuri wa kuwaratibu na kusaidiana nao ili mambo yaende vizuri. Naamini ushauri wake utasaidia sana katika kuendeleza shughuli hizi.

Mhe. Spika, kuhusu suala la KMKM kuchangishwa fedha hili nitalipeleka kwenye Wizara husika na waziri wa sekta yupo ataitolea ufafanuzi wakati wa hotuba yake ya bajeti.

Kuhusu taarifa za Kamati Teule nilieleza mwanzo kwamba hatuna nia kabisa na tunayo makabrasaha mengi ya mambo yaliyofanyika. Kwa hivyo, naomba Waheshimiwa mtuamini kwamba tunalifanyia kazi jambo hili na hatuna nia kuwa sio wasikivu, bali ni wasikivu na nia yetu ni kujenga mazingira mazuri ya watumishi wazuri na kujenga serikali ambayo itatoa huduma zinazohitajika.

Madawa ya Kulevya Mhe. Waziri mwenye sekta amesikia atapokuja hapa ataeleza kwa kina hatua zinazochukuliwa. Lakini nataka niseme tu kwa kifupi, katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita kutoka Julai 2012 mpaka Juni 2013 watu 22 wa makosa ya madawa ya kulevya wamekamatwa wakiwemo 21 wanaume na mwanamke mmoja. Kesi zinaendelea na ni kweli kwamba kubwa hapa ni kuwashughulikia wale waletaji kutafuta kila namna tukawashughulikia hawa, kwa sababu hawa ndio chanzo kikubwa cha tatizo. Kwa hivyo, serikali itaendelea kujipanga kuhakikisha kwamba hawa wanaoitwa *mapapaa* au wanaofanya njia moja au mbili kuingiza madawa ili

waweze kushikwa na kutiwa mikononi na hatua za kisheria zichukue mkondo wake.

Kuhusu suala la mazingira Mhe. Waziri muhusika amenisikia na naamini atalifanyia kazi. Kuhusu migogoro ya Ardhi Mhe. Waziri wa Ardhi mwenye Sekta amesikia na naamini atakapokuja hapa wakati akiwasilisha Hotuba yake ya Bajeti ataeleza vizuri alivyojipanga katika kulitatua tatizo hili.

Lakini jambo kubwa Serikali sasa hivi inachukua jitihada kubwa katika kuhakikisha kwamba kusajili ardhi na tunaamini kwamba Usajili wa Ardhi utasaidia sana katika kuondoa migogoro, na vile vile kwa viongozi na wahusika wote na watendani ambao wana jukumu la kusimamia mambo ya ardhi wawe wasafi, waadilifu na kufanya kazi zao kwa mujibu wa sheria hili litatusaidia sana. Na wale ambao watashindwa kufanya hivyo Mhe. Waziri yupo pale anasikia na watendaji wake watachukua hatua zinazofaa.

Kuhusu uongozi wa *ZBC* Mhe. Waziri wa Habari yupo amemsikia Mhe. Hamad Masoud naamini ushauri wake ataupokea ataufanyia kazi ili aupeleke kunakohusika.

Kuhusu Ajira ya Watu wenye Ulemavu suala la ajira kwa watu wenye ulemavu linahitaji kukamilika na utafiti unaendelea kufanywa unaohusu masuala yote ya Utumishi. Utafiti huu utaainisha masuala mbali mbali yakiwemo idadi ya watu wenye ulemavu walioajiriwa kwenye Sekta binafsi na Sekta ya Umma na taarifa hiyo itatolewa baada ya kukamilika utafiti huo.

Ni kweli kabisa wenzetu wana kila haki ya kupewa haki zao na pale ambapo pana mapungufu ni wajibu wetu kujirekebisha ili mapungufu hayo yaondoke tuweze kuhakikisha kwamba wenzetu hawa wasitengwe kwa sababu ya ulemavu wao na wapewe haki zote za msingi zinazostahiki na Serikali itachukua kila hatua kuhakikisha kwamba yanakwenda sawia kwa upande wao.

Mhe. Spika, kuhusu Sheria ya Utawala wa Baraza la Wawakilishi. Serikali siku zote haina tatizo na jambo hili na tulikubaliana kwamba Baraza lenyewe limejipa kazi ya kujifunza na kutafuta uzoefu katika nchi mbali mbali ili uzoefu huo uje kutumika katika kiwanja kwa Sheria za Utawala wa Baraza la Wawakilishi. Kwa hiyo sisi kama ni Serikali tunalosubiri ni mapendekezo ya kazi iliyofanywa tuletewe kushikirikiana na wenzetu kazi ianze sisi hatuna matatizo kabisa.

Jambo la msingi tuweze kujua tu na naamini Baraza hili litajua hali yetu ya uchumi katika kupanga Bajeti zetu tutapanga kutokana na hali halisi ilivyo.

Kuhusu matengenezo ya jengo hili ushauri naupokea ni wajibu wetu kufanya kila njia jengo hili litengenezwe katika kasoro zilizoanza kujitokeza ziondoke.

Kuhusu Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali nataka nikuhakikishie mama Asha Bakari Makame na wenzake kwamba hatua zinaendelea vizuri baadhi ya mitambo imewasili, ukarabati wa jengo unakwenda vizuri pale Maruhubi maana Disemba haitofika mitambo itafungwa na kazi itaanza ili tuwe na kiwanda kipya cha kupiga chapa.

Mhe. Spika, kuhusu maslahi ya wafanyakazi tunayashughulikia na madeni ya muda mrefu pale kiwandani. Lakini kila mwaka tunaweka fungu la kupunguza matatizo ya maslahi ya wafanyakazi ili wapate haki zao. Kuhusu kupanga kada zao za kazi, wanapangiwa hivyo lakini wakati mwengine wengine uwezo wao walionao mdogo kiutendaji inabidi watangenezewe utaratibu wanaoweza kufanya hizo kazi. Ilimradi nitajaribu kila namna kusaidiana ili wafanyakazi wetu waweze kutimiza wajibu wao na kwa ufupi kila ushauri wa Baraza hili sisi tunaupokea.

Kuhusu Idara ya Sherehe na Maadhimisho, kuhusu kujenga kituo cha kumbukumbu cha Kiongozi wetu Mzee Karume jitihada zinafanywa, na nataka nilihakikishie Baraza hili tukufu kwamba si muda mrefu tutafika hatua ya kujenga kituo maalum cha kukumbukumbu cha kuenzi taarifa za viongozi wetu wa kitafia. Hivi sasa tunafanya kazi kubwa ya kukusanya taarifa mbali mbali, maandalizi yanakwenda vizuri. Naamini hali itakuwa nzuri na siku moja tutakuwa na nyumba ya kumbukumbu ya Mzee Karume.

Kuhusu kutoa Elimu juu ya Malengo ya Mapinduzi kupitia vyombo vya habari na makongamano. Mambo hayo yamo katika mpango wetu wa maadhimisho ya sherehe za miaka 50. Kwa hiyo, kamati inayoshughulikia mambo haya imeshapewa kazi hiyo ya kuandaa makongamano, warsha, mijadala, maelezo ya kwenye *television* na kadhalika. Kwa hivyo, mambo yote hayo yanapokelewa na tunawashukuru Wajumbe kwa kuzidi kututanabahisha lakini nia na madhumuni ni haya haya niliyoyasema, na tunatarajia kwamba uzinduzi rasmi utafanyika tarehe 15 Agosti mwaka 2013 kutoka hapo ni kusonga mbele tu.

Kuhusu Idara ya kukubiliana na Maafa jitihada mbali mbali zinachukuliwa katika kuhakikisha kwamba tuwe na zana za kisasa na tuwe na mambo mazuri ya kuweza kukabiliana na maafa pamoja na kujenga maghala kuwa na vifaa na kadhalika. Jitihada zinafanyika tunajua tuna mapungufu makubwa katika suala zima la vifaa vya uokozi. Tunazungumza na wenzetu mbali mbali na tamaa imeanza kuonesha nzuri.

Wenzetu wa *UNDP* wameanza kutusaidia katika kutafuta mshauri muelekezi wa kufanya tathmini ya mahitaji yetu kujua nini tunakihitajia, na ndugu zetu wa Oman tayari wameshatupa msaada wa kupeleka watu kuwa- *train* kule, na vile vile wako tayari kutusaidia katika vifaa. Kwa hivyo, naamini katika eneo hili pia tutapiga hatua nzuri zaidi.

Tume ya Uchaguzi maelezo mengi yametolewa nia yetu ni kuendesha Uchaguzi Huru na wa Haki, na watu wote wapate haki zao za msingi za kupiga kura. Kwa hivyo, lolote lile ambalo Waheshimiwa mnatoa ushauri hapa sisi tuna wajibu mkubwa kulifanyia kazi ili kuhakikisha kwamba kasoro ndogo ndogo zinaondoka na Tume inafanya kazi zake vizuri sana. Lakini nataka niseme kwamba Tume yetu hii imeonesha maendeleo ya kuendesha chaguzi kwa vizuri. Hata hii jana tu kumefanyika uchaguzi katika Wadi ya Ng'ombeni na matokeo mmeyasikia na hakuna aliyelalamika maana yake Tume hii inaendesha uchaguzi vizuri wa haki na huru. Hata uchaguzi wa Kura ya Maoni sote tumeisifu Tume yetu imefanya kazi nzuri.

Kwa hiyo, cha msingi ni kushirikiana na kuwa wakweli katika kila jambo hili linaonekana lina kasoro basi hakuna shaka yoyote tunalitatua na kulipatia majibu sahihi. Hakuna namna yoyote ile ya kwamba Tume hii inampendelea huyu au yule nia ni kwamba Tume ifanye kazi zake kwa mujibu wa sheria na mambo yaende vizuri.

Hivi karibuni lilitokea tatizo na Wajumbe wengi walisema kuhusiana kwamba *NEC* imeanzisha Rasimu bila kuishirikisha *ZEC.* Ukweli mimi niseme sio kosa la *NEC* mambo haya yanaanzishwa na Tume inayoshughulikia kuratibu masuala ya mchakato wa Katiba. Kwa hiyo, inapofikia hatua zozote kama Tume inaarifu *NEC* ilikuwa wakati huo huo wawaarifu na *ZEC* tukawa na utaratibu mzuri wa kufanya mambo yetu kwa pamoja. Lakini hili tatizo linatokana na ile sheria yenyewe ile sheria ndio iliyofanya Tume ya Kukusanya Maoni isiwataarifu *ZEC.*

Lakini baada ya yaliyotokea na kuwasiliana na wenzetu *NEC* wamewasiliana na *ZEC* na tokea majuzi *ZEC* walikuwa huko katika kila eneo ambalo *ZEC* wameona lingefaa kuingizwa basi wenzetu wale wamekubali. Kwa hivyo, cha msingi tuingojee hiyo Rasimu itakapokuja tuletewe Serikalini tuitizame kwenye SMZ kama tukiiona haikidhi haja tutawaambia wenzetu kwamba Rasimu hii hatukubaliani nayo.

Lakini maoni vijana wetu wa *ZEC* wamekwenda wameshirikiana na *NEC* naamini pengine majibu mazuri yatatokea. Sisi tusubiri hiyo Rasimu watakuja nayo na wakati wa kujuilishwa Serikali watujuilishe tujue wapi mapungufu yapo. Sisi tuliwaambia sana wenzetu wa *ZEC* linapotokea jambo kama hili ni

vyema iitaarifu Serikali mapema kama kuna hatua za kuchukua zichukuliwe mapema.

Kwa hiyo, sasa kwa sababu mchakato umeanza na tayari sasa wenzetu wa *ZEC* na walikuweko huko na leo watakuwa wamerudi basi kwa taarifa za awali za simu wamesema kila walilolitaka limekwenda vizuri mpaka sasa. Kwa hivyo, tungojee tupate taarifa vizuri zaidi.

Kuhusu kuandaa Elimu ya Uraia ya Wapiga kura mapema. Kwa kweli kwenye ile elimu inayohusiana na Tume ya Uchaguzi kazi hiyo Tume ya Uchaguzi itafanya. Lakini mamlaka ya kutoa Elimu ya Uraia kwa mujibu wa taratibu zilizopo ni taasisi nyengine kama vile Wizara ya Utawala Bora, *NGOs* na kadhalika. Kwa hiyo, Tume wanashughulika na mambo yanayohusu kura sio Elimu ya Uraia, Elimu ya Uraia watafanya wanaohusika, Tume watafanya kazi zao zinazohusiana na mambo ya Uchaguzi na hasa hasa kwa kuwa wamepata ahadi kubwa ya kupata fedha za kufanya shughuli hizo naamini mambo yatakwenda vizuri kwa matayarisho yote na hivi sasa kama mlivyosikia katika daftari la kudumu la wapiga kura yamefikiwa hatua nzuri na tarehe 29 mwezi huu wataanza rasmi.

Kuna suala moja ambalo limejitokeza sana linahusu Sekretarieti. Nataka niseme kwanza Mkurugenzi huyu wa Tume aliyopo ameanza kuwa Mkurugenzi 2006 sio muda mrefu na huyu ameajiriwa na taratibu za kisheria na anafanya kazi zake kwa mujibu wa sheria. Pale ambapo kutaonekana kuna upungufu kwa mujibu wa sheria hakutimiza wajibu wake ndipo hapo anatakiwa kuwajibishwa.

Lakini kama ametekeleza mambo yake kwa mujibu wa sheria mimi natoa huduma zilizo sahihi anafanya wajibu wake wa Utumishi kwa mujibu wa sheria, kama kuna mapungufu basi yawe mapungufu na sheria na hivi sasa tunafanya jitihada vile vile za kuleta mabadiliko ya sheria. Na sheria ya Rasimu sasa hivi iko kwa Makatibu Wakuu karibuni Mwenyezi Mungu akitujaalia uhai basi itakuja hapa tutaizungumza na itapita kabla ya Uchaguzi wa mwaka 2015. Cha msingi nasema tena hapa ni kuelewana wenyewe tukaondosha kasoro zilizopo. Mambo madogo madogo haya yasitushughulishe yakatusababishia kugombana na kutafautiana wakati ziko njia za kutatua matatizo kwa njia nzuri kabisa.

Kuhusu watu ambao amesema kwamba kuna watu elfu tatu. Mhe. Subeit Khamis Faki alizungumzia watu elfu mbili mia nane walikuwa na vitambulisho lakini hawapati haki ya kupiga kura na waliwahi kupiga kura katika uchaguzi wa mwaka 1995 na uchaguzi wa 2000. Niseme tu kwamba

jumla ya watu wote waliotakiwa kujiorodhesha walikuwa ni watu elfu tatu mia tatu na thamanini na saba na watu hawa wanajulikana na Tume.

Watu hao ndio walitakiwa waende wakachukue vitambulisho kwenye Ofisi ya Vitambulisho, na waliojitokeza kwenda kuchukua ni mia nne ishirinia na tisa na kama katika watu elfu tatu na mia tatu thamanini na saba kuna mtu ana tatizo nyeti la kupata kitambulisho aende akamuone Mkurugenzi wa Tume yeye ata-*facilitate* kuhakikisha kitambulisho chake anakipata kwa taratibu na sheria zilizowekwa. Haina tatizo hata kidogo hiyo ni watu wenyewe wamaeshatangaziwa mara nyingi hawakwenda wenyewe tatizo tunawapaka matope bure hawa watendaji wetu wakati mwengine kwa mambo yetu wenyewe, tangazo limetoka wamekwenda watu mia nne na ishirini na tisa waliokwenda wote kwenye Idara ya Vitambulisho wamepewa vitambulisho vyao na wamo kwenye daftari la kudumu.

Sasa katika watu elfu tatu mia tatu thamanini na saba nizumgumze nae leo kwa simu Mkurugenzi akanambia watu hao keshawaambia waende na hawakujitokeza waliojitokeza ni hawa na yoyoto yule katika hao ana shida aende amuone Mkurugenzi tatizo lake litashughulikiwa. Kwa hiyo, mambo mengine jamani wenzetu hawafiki hapa tuwe aste aste tusiwadunde kiasi ambacho tukawavunja moyo.
Mhe. Spika, kwa sababu ya muda na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ana mengi ya kueleza ikiwa lipo lolote ambalo pia tumelisahau naomba Waheshimiwa watusamehe. Lakini siku zote tupo watuulize tutawatolea ufafanuzi usiokuwa wa leo leo tena *time* hii ya Magharibi kuwahi ili tuweze kumaliza Bajeti yetu vizuri ili tushirikiane kujenga nchi yetu.
Mhe. Spika, na mimi naunga mkono hoja mia kwa mia. Baada ya hayo Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Mhe. Waziri tunakushukuru na wewe baada ya ufafanuzi huo hatimaye ukaunga mkono hoja. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. (*Makofi*).

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, awali ya yote na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima nikasimama mbele ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na mimi kufanya majumuisho ya Hotuba hii ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Spika, lakini kwanza nitoe pole kwa wenzetu waliofiwa na wazee wao jamaa na marafiki.

Kwanza nimpe pole Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad Makamu wa kwanza wa Rais kwa kufiwa na kaka yake. Pili nitoe pole za dhati kabisa kwa Mhe.

Hamad Masoud kwa kufiwa na mama yake mzazi. Tatu nitoe pole kwa Mhe. Amina Iddi Mabrouk na yeye kwa kufiwa na mama yake mzazi, pia nitoe pole sana kwa kufariki kwa Mbunge wa Chambani Mhe. Salim Hemed Khamis. Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu wote mahali pema peponi. Amin.

Pia nimpongeze Mhe.Yussuf Salim Hussein kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge mpya wa Jimbo la Chambani.

Mhe. Spika, namshukuru sana Mhe. Mohammed Aboud Mohammed Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mchango wake mkubwa aliotoa ikiwa ni sehemu ya majumuisho ya hotuba ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Lakini pia niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa michango yao mizuri kwa hotuba hii na nina hakika kwamba michango hiyo imetolewa kwa nia safi kwa nia thabiti ili kutusaidia kufanya kazi zetu vizuri kwa ufanisi kama waswahili wanavyosema siku zote mtazamaji ndiye anayeona walioko uwanjani wanacheza vipi isipokuwa wachezaji wenyewe hawajioni.

Sasa michango yote hii ya Waheshimiwa Wawakilishi imetudhihirishia kwamba wametuangalia wametuona tunavyocheza na kwa hivyo wamejaribu kiasi wanavyoweza kututoa makosa. Tunashukuru sana.

Mhe. Spika, Hotuba ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais imechangiwa na Waheshimiwa Wawakilishi jumla yao 31. Na kwa heshima sana niwataje waliochangia kwa kusema na wale pia waliochangia kwa maandishi. Waliochangia kwa kusema walikuwa 22 na waliochangia kwa maandishi walikuwa 9. Waliochangia kwa kusema walikuwa kama hivi ifuatavyo:-

1.Mhe. Hamza Hassan Juma - (Mwenyekiti wa Kamti ya kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa na Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura).
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe Asha Bakari Makame
4. Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedali
5. Mhe. Subeit Khamis Faki
6. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
7. Mhe. Ali Salum Haji
8. Mhe. Hamad Masoud Hamad
9. Mhe. Omar Ali Shehe
10. Mhe. Hija Hassan Hija
11. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa
12. Mhe. Salum Abdalla Hamad
13. Mhe. Ussi Jecha Simai

14 Mhe. Nassor Salim Ali
15. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
16. Mhe. Panya Ali Abdalla
17. Mhe. Fatm Mbarouk Said
18. Mhe. Raya Suleiman Hamad
19. Mhe. Juma Duni Haji
20. Mhe. Mwinyi Haji Makame
21. Mhe. Othman Masoud Othman
22. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed.

Waliochangia kwa maandishi walikuwa ni Waheshimiwa:-

1. Mhe BikameYussuf Hamad
2. Mhe. Marina Joel Thomas
3. Mhe. Kazija Khamis Kona
4. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa
5. Mhe. Wanu Hafidh Ameir
7. Mhe. Ashura Sharif Ali
8. Mhe. Shadya Mohd Suleiman
9. Mhe. Mgeni Hassan Juma
10. Mhe. Salma Mohd Ali

Wote hawa Mhe. Spika nawashukuru sana kwa michango yao yote waliyotoa.

Mhe. Spika, kama nilivyosema Mhe. Mohammed Aboud karibu amemaliza michango yote iliyotolewa na Wahehimiwa Wawakilishi.

Mimi nitakuwa na michango michache sana, kuna suala la ubadhirifu limezungumzwa sana hapa ubadhirifu wa mali za umma na kwamba Serikali inafanya nini. Mimi niseme tu nachukia sana ubadhirifu Serikalini. Na kila tunapopata habari tunachukua hatua kuhakikisha kwamba hatua za kisheria na hatua za kinidhamu zinachukuliwa ili kukomesha suala la ubadhirufu wa mali za umma Serikalini.

Nataka nitoe mfano mmoja tu kwamba hivi karibuni Waziri mmoja alinijia akanieleza tatizo la ubadhirifu uliotokea katika ofisi yake tukazungumza na nikampa maelekezo. Kwa hivyo, kila ninapopata taarifa hizi lazima nitoe maelekezo na namna ya kulishughulikia tatizo hili kisheria na vile vile kinidhamu. Nategemea hiyo hatua inachukuliwa. Kwa hivyo, sisi Serikalini hatupendi, tunafikiria kwamba labda Serikali inawakingia kifua baadhi ya watendaji hapa mimi ni mmoja ninayechukia sana ubadhirifu na tutajitahidi kuchukua kila aina ya hatua na hatutomvumilia mtendaji yoyote yule ambaye atabainika kuvuruga au kufanya ubadhirifu wa mali za umma.

Lakini pia limekuja swali hapa ni nani msimiaji wa nidhamu Serikalini. Niseme tu kwamba Serikali yote ina dhamana ya kusimamia nidhamu Serikalini. Lakini kuna mgawanyo wa madaraka mawaziri wote wana wajibu wa kusimamia nidhamu ya watendaji wao. Kwa sababu hili si jukumu la mtu mmoja tu asimamie nidhamu ya Serikali nzima tumegawanywa mawaziri wana wajibu huo na pale ambapo itaonekana Waziri ataona tatizo kubwa analileta kwangu, na mimi kama msimamizi mkuu wa shughuli za Serikali nitaweza kushirikiana na Rais hatua gani tuchukue dhidi ya mtendaji yoyote yule ambaye amefanya.

Kwa hivyo, mimi nawasihi sana Mawaziri pale ambapo mtendaji hakuonesha nidhamu ameonesha ubadhirifu amefanya utovu wa nidhamu basi tuje tuzungumze tuone namna gani tunaweza kulishughulikia. Na mimi kama ni mshauri Mkuu wa Mhe. Rais nitakwenda kushauriana naye tuone na yeye atachukua hatua gani. Lakini niseme tu hatutomvumilia mtu yoyote ambaye analeta utovu wa nidhamu Serikalini.

Mhe. Spika, mambo yamezungumzwa na jambo kubwa lililozungumzwa kila mmoja humu ni suala la Muungano. Nimshukuru sana Mhe. Raya Suleiman Hamad kwa sababu jambo hili humu hatuna kauli. Sasa hili tunawaachia wananchi wenyewe kupitia mabaraza yao watoe kauli zao na mawazo yao. Humu tumesema mengi kuhusu Muungano lakini humu ndani hatuwezi kufanya kitu, kauli ziko kwa wananchi wetu kupitia kwenye Mabaraza yao.

Mategemeo yangu kwamba wananchi wajitokeze kwenye mabaraza yao wazungumze suala la Muungamo na mambo mengine. Maana ile Rasimu sio Muungano peke yake tu. Kuna mambo mengi yote tuyazungumze na kama alivyosema Mhe. Mwanasheria Mkuu tunakwenda wapi tunataka nini basi tuyaseme humu kwenye Baraza.

Mhe. Spika, pia Wajumbe walizungumzia juu ya suala la rushwa. Kweli rushwa ni adui wa haki, sisi sote humu tuna dhamana ya kusimamia suala hili lisitendeke. tumepitisha sheria hapa ya kudhibiti rushwa na tuisimamie sheria hii sote kwa pamoja ili kuhakikisha kuwa tunailetea mafanikio nchi yetu.

Nyumba ya SMZ iliyopo Afrika ya Kusini tayari nimelitolea ufafanuzi. Lakini pia nataka kufanya marekebisho madogo kwamba awali kweli ilikuwa nyumba hiyo tuibadilishe na nyumba ambayo anakaa Makamu wa Pili wa Rais Dar- es Salam. Lakini baadaye Mhe. Rais akaja na wazo jengine kwamba tubadilishane na nyumba ambayo sasa hivi inatumika kama Ofisi ya SMZ.

Kwa hivyo, Mhe. Omar Ali Shehe aliposema yeye hakubaliani kwa sababu nyumba ile iko *prime area* kwa kweli hata Dar - es Salam iko kwenye *prime area* kwa sababu iko karibu na Ikulu pale hakuna matatizo. Kwa sababu wazo la kwanza kabisa ilikuwa nyumba ile tuiuze, tuwauzie SMT, kwa sababu kwa kule labda Ubalozi wataitumia. Lakini Mhe. Rais akasema kwa nini tuuziane, kwani sisi hatuna haja ya kujenga Dar es Salaam. Kwa hivyo, tukakubaliana kwamba nyumba ile sasa hivi tufanye utaratibu wa kubadilishana, wenzetu wa SMT wachukue ile ya Afrika ya Kusini na sisi tuchukue ile ya Dar es Salaam ambayo sasa hivi inatumika kama Ofisi ya SMZ. Lakini bado mambo hayajakamilika na ile nyumba kule Afrika ya Kusini inazidi kuharibika na sisi tumeshindwa kuitengeneza kwa hali tuliyokuwanayo sasa. Kwa hivyo, kila mmoja atatengeneza yake, SMT tukishakabidhiana watatengeneza yao na sisi tutatengeneza yetu pale Dar es Salaam.

Swali kubwa jengine lililojitokeza hapa ambalo lilizungumzwa na Mhe. Asha Bakari Makame ni suala la viongozi wakuu wa SMZ, uhusiano wao ukoje. Mhe. Spika, kama alivyosema Mhe. Mohammed Aboud. Uhusiano wa Viongozi Wakuu wa Serikali ya SMZ kwenye Mfumo wa Umoja wa Kitaifa ni mzuri, una masikilizano makubwa ndani ya serikali. Tunakaa kwenye BLM tunazungumza na tunapitisha mambo yetu kwa salama na amani kabisa, tunacheka, tunafurahi na mambo yetu tunapitisha vizuri.

Kwa hivyo, uhusiano wa viongozi wakuu ndani ya serikali ni mzuri sana. Tatizo letu liko kwenye viriri, tukiwa kwenye majukwaa hapo ndipo matatizo yanapotokea na wananchi wetu tunawatia wasi wasi, hivi viongozi wetu wakoje.

Mhe. Mansoor Yussuf Himidi alipokuwa akichangia amesema tunaitana majina, tunakaa kwenye viriri kule tunaitana majina ya ajabu ajabu. Kweli, mimi nimeshaitwa majina mengi tu, na nikapewa vyeo vingi tu na vyeo vyengine hata havipo katika itifaki ya diplomasia pia nimepewa. Barabarani huko jina langu limeshageuzwa sasa, nikitajwa jina huko, utasikia *laanatullah*. Sasa mimi nasema ni lazima hili tuliepuke, kama kweli tunataka tuwe na mfumo huu wa umoja wa kitaifa kuanzia juu mpaka chini basi haya mambo ya viriri kuanzia juu mpaka chini ni lazima tuyaepuke. Maana tukianza kupeana majina hatufiki mbali na yale tuliyoyakimbia basi tutarudi huko huko.

Kama tulikuwa hatuuziani vitu katika maduka tutarudia kule kule, kama tulikuwa hatuendeani kwenye maziko tutarudi kule kule. Sasa kuna tija gani, kuna tija ya kusemana kwenye viriri bure bila hata sababu ya msingi. Tuelewe kwamba tulichounganisha ni serikali, lakini vyama kila mmoja ana chake, na kila chama kina sera zake. Sasa kama mimi nitasema sera zangu zitakuudhi

wewe bure tu, kila mmoja ana haki ya kutangaza sera ya chama chake hiyo ndiyo demokrasia. Lakini leo mmoja akitangaza sera hii basi imekuwa kelele na kupeana majina, kitu gani tunachogombea. Maana leo mimi nikiuliza hivi jamani nimekosa nini hasa mpaka napewa majina mengi ya ajabu ajabu. Ingekuwa hayo majina yanachuna basi ningekuwa nimeshachunika ngozi sasa hivi.*(Makofi).*

Mhe. Spika, lakini niseme tu kwamba jamani sisi ndio wahimili wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa sote kwa umoja wetu, kuanzia juu mpaka chini. Kwa hivyo, mambo ambayo yanaweza kutuharibia umoja wetu huu basi tuyaepuke, moja wapo ni kutukanana kwenye viriri. Mimi naamini hakuna hata mkutano mmoja wa CUF wa hadhara jina langu pale lisitokee. Nimewakosa nini?*(Makofi).*

Tatizo langu mimi siwezi kumrudishia mtu ninaheshimu nafasi yangu. Kwa hivyo, nawaachia tu waseme, lakini nawaambia hili halitupeleki mahali, tutarudi kule kule tunakotoka tunakokukataa. Tumeshakataa tusirudi kule. Kwa hivyo, kama tumejenga Serikali ya Umoja wa Kitaifa, basi sote tuamini kwa dhati, wala hakuna haja ya kutuhumiana kwamba huyu hivi, dhana siku zote ni madhambi kumdhania mwenzako yuko hivi.

Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu, naomba sana.

Mhe. Spika: Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, nikuombe radhi muda unayoyomea. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, karibu.

KUONGEZA MUDA WA BARAZA

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa muda ulio mbele yetu hautoshi kumaliza shughuli iliyo mbele yetu, kwa hivyo Mhe. Spika, naomba Baraza lako tukufu liweke kando kanuni ya muda, ili tuweze kukamilisha utaratibu ulio mbele yetu wa kupitisha bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda. *(Makofi).*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Mhe. Makamu wa Pili wa Rais endelea.

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, la mwisho tu niendelee kutoa wasia wangu, tufanye kazi kwa ushirikiano, tufanye kazi kama wamoja kuendesha nchi yetu. Sisi wanasiasa ndio tunaosababisha vurugu, na vurugu ikitokea ndani ya nchi yetu mambo mengi tutayakosa, kwanza sisi tutakimbilia wapi. Tujiulize vurugu zitaleta tija gani, hakuna tija. Tutawakosesha wananchi wetu kuishi kwa vizuri, tutawakosesha wananchi wetu kufanya biashara zao bila ya sababu za msingi.*(Makofi).*

Kwa hivyo, mimi niseme tu Mhe. Spika, kwamba uhusiano wa viongozi ndani ya serikali ni mzuri, lakini mambo haya yanaharibiwa tukikaa kwenye viriri. Sijui pana shetani gani pale, tuache, tukikaa kwenye viriri hebu tuzungumze sera za vyama vyetu si basi!*(Makofi).*

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa na sasa hoja hii tuiamuwe. Niwahoji basi, wale wanaokubaliana na hoja ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka 2013/2014 wanyanyue mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda. *(Makofi).*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza lako limejadili na kuikubali hotuba ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya matumizi ili kupitisha vifungu vya matumizi ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 05 - OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS

Kifungu 0501	Idara ya Uendeshaji na Utumishi	38,000,000
Kifungu 0601	Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa	6,000,000
Kifungu 0801	Idara ya Upigaji Chapa na Mpigaji Chapa Mkuu wa Serikali	500,000,000
Jumla ya Fungu		**544,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 05 - OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS

Kifungu 0003 - Afisi Kuu Pemba

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Bismillahi Rahman Rahim. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ndio mara ya kwanza nasimama naomba uniruhusu kwa dakika moja, nitoe shukrani zangu za dhati kabisa kwa ufafanuzi wote uliotolewa, kuanzia Mhe. Mwanasheria Mkuu, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na mwisho mwenyewe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

Mimi nimefarijika sana Mhe. Mwenyekiti, hasa baada ya Makamu wa Pili wa Rais kusimama, kwa sababu utaratibu niliouzoea katika mabunge mengi ya Jumuiya ya Madola ni kwamba Kiongozi wa Shughuli za Serikali mara nyingi katika bajeti yake huwa anasimamia mwenyewe. Mwaka wa mwanzo alisimama mwenyewe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, lakini hapa katikati akabadilisha taratibu, ikawa anakuja kusoma hotuba Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, sio tatizo kwa heshima ya uzee wake na nafasi yake na hadhi yake.

Lakini leo angalau katupa heshima katika kufanya majumuisho na yeye katia baraka zake, imekipa hadhi chombo chetu. Nataka nimuhakikishie Mhe. Balozi kwamba tumethamini na tunaheshimu sana heshima ambayo kakipa chombo hiki leo.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba nipate maelezo na katika hili niseme kwamba namuhakikishia bajeti yake Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Mohammed Aboud kwamba itapita tu. Lakini ni wajibu wetu kutaka maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia nilisema kwamba kuna vifungu vingi, lakini nikasema nikivitaja kimoja kimoja itaweza kutuwia kazi kubwa sana ya kutojadili hotuba tukajadili vifungu. Kwa hivyo, nikamwambia Mhe. Waziri awe na maelezo ya kutosha tutakapotaka maelezo atupe. Mhe. Mwenyekiti, katika hili mimi naomba maelezo yangu kwenye Ofisi Kuu Pemba, lakini naomba niseme hapa ili iwe na kwa sehemu nyengine zote, isipokuwa kama kuna sehemu ya lazima sana basi nitasimama tena kwa vifungu, kwamba bado mimi nilikuwa nikisema mwaka jana kuna matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba katika kifungu cha *vote* mwanzo pale, mishahara ya fedha taslim. 211100, halafu kuna kifungu kidogo cha 2111110 posho maalum hizi. Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba maelezo kwa sababu fungu hili lina Shs. 44,238,000 ambalo ni tofauti na fungu la mwaka jana Shs. 32,638,000. Sasa maelezo ambayo tulikuwa tukipatiwa katika miaka mbali

mbali kuwa posho hili linaambatana na marupurupu ya mshahara ya mtu husika anayeongoza ofisi ile na linakwenda na mshahara. Sasa najiuliza, huku juu kwenye mishahara na waajiriwa wa kudumu wa serikali, kwenye fungu hilo hilo pana Shs.141,072,000, ambapo mwaka jana ilikuwa ni Shs. 140,562,000. Kwa hivyo, pana tofauti ya kama Shs. 500,000 mpaka 600,000 tu katika mishahara. Lakini fungu la posho maalum limechupa kutoka Shs. 32,000,000 mpaka Shs. 44,000,000 ni tofauti ya shilingi 12 milioni, pana nini hapa Mhe. Mwenyekiti? Nataka niliulize hili kwa sababu nilikuwa namuonesha rafiki yangu hapa Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwamba hili tumeanza kulihoji sisi na hata Bara sasa wanahoji katika Bunge.

Mhe. Mwenyekiti, ninalo gazeti la *Citizen* hapa la juzi, kuna vifungu kama vilivyokuwa vikihojiwa katika Bunge sasa baada ya sisi kuanzisha utaratibu kama huu. Kwa hivyo, nilikuwa naomba tusaidiwe maelezo ya kifungu hicho na vile vile katika fungu hilo, kwa sababu ni fungu moja kwa pamoja, nipatiwe maelezo katika ile *vote* ya 220700 inayohusu matengenezo ya ofisi, kuna matengenezo makubwa pale kwenye 220702 katika ukurasa wa 56, matengenezo makubwa ya majengo kuna Shs. 70,000,000 wakati mwaka jana ilikuwa ni Shs.15,000,000 milioni katika fungu hili la Ofisi Kuu Pemba, nilikuwa naomba maelezo katika vifungu hivyo Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa maelezo ya Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi hizi posho zote zinasimamiwa mahala pamoja hizi posho maalum. Kwa hivyo, kwa kule Pemba maana yake ni kwamba lazima kutakuwa na nyongeza ya namna hiyo, haikuwa tena kwenye sehemu nyengine zinasimamiwa mahala pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, ukitizama sasa hivi kuna huu utaratibu mpya ambao unakwenda kutokana na daraja ya kila mmoja, kwa hivyo ndio maana kiwango hiki kimepanda kutoka 32 milioni, zikaja 44 milioni. Hayo ndio maelezo ambayo naweza kuyazungumza Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ile hoja nyengine ya kuhusu matengenezo ya ofisi. Kuna hoja mbili.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Ismail Jussa, naomba urudie hoja ya pili iko katika kifungu gani.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Katika ukurasa huo wa 56 unaofuata kwenye matengenezo makubwa ya majengo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti kule Pemba tunajenga uzio wa kuzuia ile ofisi. Ukienda pale ukitizama Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, utaikuta iko chini ya bonde. Tumeanza kujenga ukuta kwa chini na atakayekwenda ataona kwamba kuna maporomoko yanatokea. Niliahidi tokea mapema kuzuia yale maporomoko, lakini wakati huo huo uzio ule pia tunajenga na ghala ya kuhifadhia vifaa vya maafa, ndio maana ikafikia kiwango hicho cha milioni 70. Tukienda pale tutaona kuta kubwa tunalijenga na pia kutakuwa kuna ghala ya kuhifadhia vitu vya maafa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, hili la matengenezo makubwa nashukuru kwa maelezo nayapokea, nadhani kamati inayohusika itayafuatilia zaidi utekelezaji wake. Lakini hili la posho maalum bado maelezo ya Waziri hayakunitosheleza kwa bahati mbaya Mhe. Mwenyekiti. kwa sababu kama nilivyosema hapa na hili ni vizuri serikali ikajifunza.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tunakumbuka maelezo tuliyopewa mwaka juzi na mwaka jana na tunategemea kwamba maelezo yale ni thabiti. Sasa tulipokuwa tukipewa maelezo, nakumbuka katika ule msimamo wa mara moja Mheshimiwa mwenyewe mwenye bajeti, Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwamba mafunzo haya ya posho maalum, zile posho ambazo zinakwenda kwa watu maalum ambao ni viongozi. Kwa mfano mawaziri, makatibu wakuu, wakurugenzi na zinaambatana na nafasi zao. Kwa hivyo, hizi kwa ninavyoona mimi zinatakiwa ziwe *fixed*, kwa sababu marupurupu yale kama hakujaongezeka mishahara na haya mara nyingi yanatolewa kulingana na asilimia ya mishahara yao. Sasa kama hawa hawajabadilika na idadi yao ni ile ile na hatujakusikia kama kumeundwa ofisi mpya, na kwa Ofisi Kuu Pemba zaidi, kwa sababu wanaohusika na kutengeneza hii ni Afisa Mdhamini.

Sasa hebu nipewe maelezo zaidi ya kina Mhe. Mwenyekiti, katika hili ni kwamba kwa nini kwenye mishahara bado iko vile vile laki tano, laki sita lakini kwenye posho maalum pana nyongeza ya milioni 12? Naomba maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa tumeanzisha utaratibu maalum wa kutoa hizi posho maalum, na kwa kuwa idara ya huduma kule Pemba pia wameingizwa kwenye kifungu hiki hiki. Kwa hivyo, wale wafanyakazi wa Idara ya Huduma yetu wanapata posho lao maalum kwa kupitia fungu hili, ndio maana hiki kiwango cha fedha kimeongezeka Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, nia ni kutokana na utaratibu mpya wa Utumishi na taratibu za ongezeko la mishahara na posho ndio maana imefika hivi, kwa hivyo sio

njia nyengine yoyote zaidi ni matumizi ambayo yapo katika uhalali wa utaratibu wa kuendesha shughuli za serikali.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, mimi sasa hivi kidogo nimemuelewa. Lakini naomba aniweke sawa ili niliruhusu fungu hili liendelee. Nataka maelezo tu kwamba Idara ya Huduma za Makamu wa Pili ina fungu lake. Hili naomba atuweke sawa kwa jumla na serikali, kwamba tunavyoelewa sisi tunaopitisha mafungu hapa Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba tukiipitishia idara inahudumia Unguja na Pemba. Nitakuja katika wizara husika, na katika kupitisha mafungu haya Mheshimiwa kwenye kamati tulizozana, kwa sababu kila tukiambiwa kwamba idara inahudumia kote Unguja na Pemba, haihudumii Unguja peke yake. Lakini sasa inapokuwa na fungu kama hili kwa Ofisi ya Huduma za Makamu wa Pili wa Rais ikawa limewekwa kwa Unguja tu, lakini kwa Pemba likawa linatumika la Ofisi Kuu Pemba, linatutatiza.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina tatizo, kwa sababu najua baadae kutakuwa na kamati itafuatilia na kwa hivyo niko tayari kuliruhusu, lakini hebu anipe maelezo. Kwa nini mafungu haya hayakai katika idara zake zinazohusika? Kwa sababu haya ndio yanayotuletea matatizo kwa Pemba katika utumiaji wa fedha za serikali, tukija kupitia wizara moja moja nitakuja kuliuliza kwa kina hili Mhe. Mwenyekiti. Kuna tatizo kubwa sana la ugavi wa fedha kwa upande wa Ofisi Kuu Pemba za kila wizara. Sasa kwa nini kwa bajeti ambayo inahudumia posho maalum ya viongozi. Mimi naikubali kama ni Ofisi ya Idara ya Huduma za Makamu wa Pili wa Rais, kwa nini isikae kule iwekwe katika Ofisi Kuu Pemba kwa maana ya kwamba ya fedha zinazosimamiwa na Afisa Mdhamini pale, ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Kwanza namshukuru hiyo hatua aliyokwishafikia pia sio ndogo kwangu. Lakini ningependa tu nimueleweshe Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwamba kwa kuwa Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba, kwa utaratibu wetu sisi kwenye suala hili, na kwa sababu ofisi ya faragha ukiitizama sana ipo Unguja na nilisema *activity* za Pemba ni vizuri zikasimamiwa huko Pemba wenyewe. Kwenye eneo hili ndio maana hawa wahudumu wa idara ya huduma wakawepo kwenye fungu hili, ni kwa sababu ya utaratibu tu kwamba sasa hivi tumekubaliana kwenye serikali, kwamba zile shughuli za Pemba zijisimamie wenyewe kwa Pemba. Ukitizama idara ya faragha *nature* yake hasa inakuwa ni pale alipo mwenyewe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Wakati mwengine wahudumu hawa hawa hutoa pia huduma kwa viongozi wengine wanapokuwepo Pemba na ukitizama utaona pengine mafungu ya viongozi wengine na kwa sababu wanajenga nguvu kwenda kutoa huduma zile kwa viongozi wanaokuwepo pale.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee, lakini kwa sababu nina *mike* mkononi nikuambie kwamba hali ya hewa kidogo ndani ya jengo inaanza kunichokesha mapema kabla hatujaingia kwenye vifungu, nadhani kuna tatizo la *AC*, nafikiri tumezungumza na watendaji. Baada ya kupata hali ya hewa ya *AC*, ili kumfanya Mhe. Mohammed Aboud aweze kujibu vizuri vifungu vyetu, naomba tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi ya kupata ufafanuzi wa baadhi ya mafungu hapa ambayo nilimuuliza Mhe. Waziri wakati nilipokuwa nachangia, lakini naona katika ufafanuzi sikuyasikia vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye kasma hii ya 220400 gharama za mafuta na vilainisho, niende kwenye kifungu 220404 gharama za vilainishaji, imetengwa hapa milioni 1.2. Lakini nikiteremka chini kwenye fungu hili la 220800 kuhusu matengenezo ya zana. Kuna fungu 220803 ya matengenezo ya magari, sasa ukiliangalia hili fungu Mhe. Mwenyekiti, huku limeshawekwa la vilainishaji, lakini huku kwengine kuna matengenezo ya magari. Vilainishaji maana yake ni girisi na *oil*, lakini huku kwengine unapeleka gari kwenye matengenezo yote kule, sasa fungu hili ni la kitu gani. Nilikuwa nataka kujua hapa, maana kule umeshalipeleka gari kufanyiwa *service* maana yake vitu vyote vinafanyiwa huduma, mambo ya *oil* na kutiwa girisi huku kwenye fungu la matengenezo. Lakini huku kumetengwa tena fedha kwa ajili ya vilainishaji. Nataka kujua hivi vifungu ni vya kazi gani sasa, kama huku tayari unapeleka *service* kwa kawaida gari yako, *oil* inamwagwa na girisi inawekwa. Hoja yangu ni kwamba fungu hili nahisi halina kazi kuwekwa hapa. Naomba ufafanuzi kutoka kwa Mhe.Waziri.

Lakini kuna fungu jengine hapo hapo la 220409 kutoka kwenye vilainishaji kuja chini kuhusu uondoshaji wa takataka. Mhe. Mwenyekiti, hapa naomba kupata ufafanuzi, kwa sababu kila mwaka naona kunatengwa fedha kwa ajili ya uondoshaji wa takataka, sasa nataka kuelewa ni kitu gani hichi, uondoshaji wa takataka maana najua kazi hii ya kusafishwa huwa inafanywa na Manispaa. Mhe. Mwenyekiti, naomba ufafanuzi kwenye hili.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tupate maelezo, lakini kimsingi hoja alitumia Mhe. Ismail Jussa Ladhu katika fungu hili na ilikuwa imebakia hoja tu. kwa hivyo, tusaidie maelezo kwa hiyo ya mambo ya vilainishaji na hiyo nyengine tena basi.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais naomba kidogo nimsaidie Mhe. Mjumbe kama ifuatavyo. Kwa

kweli sio kama kila gari inapoharibika inakwenda kufanyiwa *service* na sio kila gari inapohitaji *service* inakwenda kufanyiwa matengenezo tukubaliane hapo kwanza.

Kwa hivyo, *lubricant* inahitajika pale gari inapofanyiwa *service* na gari inakuwa ni nzima, lakini tuna kawaida ya kufanya *service* kila mwaka unapofika au miezi 6 inategemea na gari matumizi yake. Kwa mfano, magari ya mizigo au daladala ni vizuri kuyafanyia *service* kila baada ya miezi 6 na pale inahitajika *lubricant*.

Lakini gari zetu za kawaida hizi *private* hizi unaendesha na kurudi kazini miezi 12 *service* inatosha. Kwa maana hiyo, vifaa na matengenezo ni pale unaponunua vifaa, gari inawezekana *plug* imekufa au taa zimekufa au *diskette* imekufa ama *engine* imenoki sasa pale ndio unafanyia matengenezo gari na zile fedha inabidi zitoke kwenye vifungu hivi.

Nadhani Mhe. Mbarouk Wadi Mussa yeye ni shahidi anayo gari anaendesha kuna wakati ndugu yangu anapeleka gari kwa ajili ya kufanyiwa *service* tu, pia wakati mwengine gari yake anaipeleka sio kufanyiwa *service* isipokuwa ni kufanyiwa matengenezo. Kwa hivyo, nataka atafautishe hivi vifungu viwili tumevitafautisha kwa nia safi kabisa kwa sababu ya kujua *service* zitakwenda pale na matengenezo yatakuja huku. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, naona maelezo yanatosha tuendelee.

Kifungu 03	-	Ofisi Kuu Pemba	452,817,000/=
Kifungu 0401	-	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ahsante nilikuwa katika kuwapa fursa wenzangu kwa sababu niko peke yangu, naamini nitatumia vizuri fursa hii. Mhe. Mwenyekiti, bado niko pale pale kwenye posho maalum katika idara hii na *vote* itakuwa ni 211110 posho maalum (*special allowance*).

Mhe. Mwenyekiti, tuanze na mwaka jana ilikuwa ni shilingi milioni 3,160,000/= na mwaka huu imekuwa ni shilingi milioni 15,198,000/=, lakini kwenye mishahara na ninajenga hoja yangu Mhe. Mwenyekiti pale pale katika dhana nzima kwamba posho maalum tunavyoarifiwa kwamba linakwenda pamoja na mshahara yaani liwe *fix*.

Sasa kwenye mshahara *vote* 211101 mishahara ya waajiriwa wa kudumu wa serikali *civil servants*, bajeti ya mwaka huu imepungua na mwaka jana ilikuwa ni 52,906,000/= na mwaka huu imekuwa 47,892,000/=. Lakini posho

maalum ambazo zilipaswa zifuatane nazo hizi zimechupa kutoka shilingi milioni 3 hadi milioni 15, naomba maelezo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, hii inatokana na utaratibu wa sasa ambao umeweka mambo katika ubayana wake. Kwa msingi huo ndio kumeanzishwa utaratibu huo wa watu kuwa na posho maalum kutokana na kazi zao wanazozifanya.

Vile vile ni utaratibu ambao umewekwa, ili kuwa na posho maalum kwa wale wanaostahiki. Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba nyongeza na mapungufu yanategemea uhalisia baada kuendesha shughuli zenyewe. Kwa mfano, anasema mshahara mwaka jana umekua na sasa umepungua, lakini unapopungua kuna watu sasa waliokwenda kwenye Idara ya Utumishi ndio maana inapungua, lakini suala la posho maalum linakuwepo kwa sababu sasa utaratibu umeanzishwa na posho maalum zipo zinazowahusu wahusika na ndio maana tukawa tunacho kiwango hichi cha fedha Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru, lakini mimi naomba katika kusaidiana kabla sijaeleza hoja yangu, kwa sababu nafikiri tutapata tabu sana kwa fungu hili kwa kila pahala na leo tunaianza hii Ofisi ya Makamu wa Pili, ambapo ni ya mwanzo tunaingia kwenye vifungu, lakini hali hii itakuja kuendelea katika kila wizara.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani ni vyema tukamuangalia mwenye *policy* Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa sababu serikali ndio inajibu kwa pamoja basi atusaidie.

Kwa hivyo, hizi posho maalum ni za watu gani na zina-*cover* maeneo gani? Basi nafikiri tukilielewa hilo ndipo tutaweza kuelewa vizuri hii hoja, kwa sababu hivi tunavyokwenda Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema sisi tunachukua maneno tunapoyapata kutoka mwaka juzi au mwaka jana kwamba hizi ni za Mkurugenzi au Katibu Mkuu ama Waziri ambazo zinaambatana na mshahara wake, yaani zinawekwa pale posho ya mafuta, viburudishaji vinaambatana na nafasi yake.

Sasa utaratibu uliokuja kwa mara ya pili Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais anatuambia kutokana na utaratibu uliokubaliwa sasa na huo utaratibu hatuelezi na sisi hatuwezi kuujua. Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi kama mpitishaji sitapitisha kitu ambacho sikielewi.

Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri mwenye sera kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba fungu hili katika bajeti ya posho maalum lina-*cover* maeneo gani, kwa sababu kuna maposho mengine pia humu yamo

ambayo yanahusika ikiwa ya *overtime* au kamati na vikao, kushika wadhifa yapo. Sasa haya ya posho maalum hebu atueleze kwa kina yanahusika na nini Mhe. Mwenyekiti, ili turidhike vyenginevyo, itakuwa tunapiga mapanga hapa na kumbe hatujaridhika nayo tu maelezo yake. Kwa hivyo, naomba maelezo kwa Waziri mwenye dhamana hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, waziri mwenye sera kwa upande wa maposho ni Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora, lakini kwa sababu Mhe. Mjumbe ameniona mimi mpiga kura wake ninafaa basi acha nisaidie tu. *(Vicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ni hivi posho maalum, yaani posho ambayo wanayopata viongozi wale wateuliwa kwa maana ya posho ya mafuta, lakini kuna posho wanapata madereva wa viongozi, *secretaries* wa viongozi, watumishi wa viongozi na hawa wote wanapewa posho maalum na zote zinatakiwa ziwepo hapa.

Kwa mfano, kama hivi sasa viongozi tupo hapa madereva wetu wanatuendesha bila ya kujali wakati, *secretaries* wanaweza kuwepo afisini bila ya kujali wakati au *weekend* na hawa wote wana posho maalum ambazo zote zinakuwepo hapa.

Lakini kwa mara nyengine naomba kwamba mwenye mamlaka haya ni Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora na sio Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima bado sijaridhika na ninakiheshimu sana kiti chako.

Mhe. Mwenyekiti, nilitaka nielezwe na tayari nimeyapata na sasa yatatusaidia mimi na wenzangu huko tunakokwenda. Sasa kama ni hoja ni hiyo, basi ndipo ninapojenga ile hoja yangu niliyosema kwamba posho maalum iko katika kila idara.

Kwa hivyo, ninavyochukulia mimi kwamba ikiwa ni ya Kiongozi wa Pili wa Rais na wale wanaowahudumia, yaani wale ambao watakuwa fungu lao la mshahara liko kwenye idara inayohusika, kwa hiyo na posho yao maalum inakwenda pale pale, kwa sababu liko katika kila idara hili.

Sasa hoja yangu na kama unakumbuka Mhe. Mwenyekiti, nilipoanza idara hii kwamba lile fungu la mishahara limeshuka kutoka milioni 52,906,000/= hadi milioni 47,892,000/=. Kwa hiyo, hawa bila ya shaka watakuwa wanahudumia

Idara ya Mipango Sera na Utafiti, kwa sababu Mkubwa wa Ofisi ya Makamu wa Pili iko Idara ya Faragha kuna posho maalum na wengine ambao wako kwenye Idara ya Utumishi na Uendeshaji iko posho maalum na hii inahudumia Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.

Kutokana na hali hiyo, ndio maana nikauliza ikiwa fungu la mishahara ambalo ndilo linalo-*determine* vile vile posho zao maalum ikiwa *secretary* wake au dereva wake wote wako hapa. Sasa kwa nini fungu la mshahara liporomoke na lakini fungu la posho maalum liongezeke? *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, labda niweke wazi zaidi, tunauliza haya kwa sababu tunapokwenda kwenye Kamati tunagundua mambo. Mhe. Mwenyekiti, kuna watu humu na ikifika wizara zao tutawataja, yaani kuna wakubwa wanachukua posho yake ya mafuta kwenye posho maalum, lakini bado anatumia mafuta ya wizara na wako hao na ikifika katika wizara zao tutawataja kwa majina humu Mhe. Mwenyekiti.

Sasa ndio maana ninahoji fungu hili kwa sababu hili linatupa mashaka, kwamba watu wanarudufisha tu gharama hizi na ndio maana kama nilivyosema sikuhoji *overtime* nahoji hawa kwa sababu hivi ndivyo tulivyopewa maelezo na Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, kwamba linaambatana na mshahara.

Hivyo, kama linaambatana na mshahara kwa nini mshahara unaporomoka na unahudumia Wakurugenzi, ikiwa ni dereva wake au *secretary* wake, lakini kwenye posho maalum lipande na hiyo sera ya kuongeza maposho hayo imeanzishwa lini ambayo sisi hatujui na nadhani Mhe. Waziri labda atueleze hapa, hivyo naomba maelezo Mhe. Mwenyekiti kama si hivyo nitaona nitoe hoja na wenzangu wanikubalie kwamba posho hii tuikate na irudi shilingi milioni 3,000,000/= kama ilivyokuwa mwaka jana. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi kuhusu kifungu kinachoelezea posho maalum ambalo mwaka jana lilikuwa shilingi milioni 3,160,000/= na mwaka huu kiko shilingi milioni 15,198,000/=.

Ukweli usiofichika ni kwamba mwaka jana baadhi ya watumishi wa idara hii walilipwa posho hili maalum kutoka fungu la Idara ya Uendeshaji na Utumishi, kwa sababu idara hii bado ilikuwa haikupanga posho na kwa sababu matokeo ya kuwapa maposho wafanyakazi kama tulivyosema ni kwamba wizara yangu ilikuwa na kazi ya kupitia nani anastahiki kulipwa posho na yupi hastahiki. Kwa hivyo, hii inayoonekana kasoro huku ni kwa

sababu hawa mwaka jana walibebwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi, ambayo ipo pale Makao Makuu.

Vile vile ukiangalia hapa utakuta kwamba kwenye posho maalum (*special allowance*) mwaka huu kwenye Idara ya Uendeshaji na Utumishi limeshuka kutoka 161,827/= mpaka 126,000/=. *(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ikifika idara hiyo tutaihoji nayo Utumishi na Uendeshaji, lakini mimi bado nang'ang'ania hapa hapa kwenye Mipango, Sera na Utafiti. Mhe. Mwenyekiti, bajeti ninavyofahamu mimi na haya maelezo kwamba tuna-*improve* siku hizi yanaletwa kila mwaka, kwamba tunajipanga vizuri na tunaelewa.

Naomba hoja yangu ieleweke Mhe. Mwenyekiti na wala sio kama ni ya ukaidi, nia ya kuzilinda fedha za walipa kodi wa nchi hii, ambao wanakwenda hospitali hakuna dawa, watoto wanakwenda skuli hakuna madeski, lakini fedha kwenye posho maalum zinakuwa kama hivi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, idara hii ili tufahamike sasa turudi mwaka juzi 2011/2012 ilipangiwa milioni 8,653,000/= na juu ukitizama mshahara ulikuwa milioni 64,878,000/= kuna *fluctuation* za ajabu ajabu Mhe. Mwenyekiti kwamba vile viwango haviendani na mshahara unaporomoka kila mwaka, ukitizama *trend* ilikuwa milioni 64, imekuja milioni 52 na mwaka huu imekuwa milioni 47, lakini posho maalum linacheza lilikuwa milioni 8, likaja milioni 3 na sasa limekuja milioni 15.

Sasa kama hoja ya Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora ni sahihi kwamba walikuwa hawajajipanga vipi mwaka juzi lilikuwa milioni 8 na halafu mwaka jana likashuka. Kwa kweli mimi ninavyoamini ni kwamba walijipanga vizuri zaidi wakajua hawahitaji milioni 8 na wakaweka za uhalisia ni milioni 3 sasa mwaka huu zimeongezeka zimekuwa milioni 15.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti nasema ili nisiendelee kupoteza muda mimi nadhani maelezo yake hayatoshelezi basi mimi nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wenzangu kwamba tuwawekee milioni 3 kama ilivyokuwa mwaka jana zinatosha na nyengine ziende zikahudumie mambo mengine. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, maelezo zaidi, lakini kwanza namshukuru Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa maelezo yao.

Mhe. Mwenyekiti, hapa tunazungumzia milioni 15 kama ni posho maalum kwa wafanyakazi wote ambao wako chini ya idara hii, sasa tukipima kazi za mwaka mzima Mhe. Mwenyekiti pamoja na kuangalia na uzito wa kazi zenyewe na Waheshimiwa kila wakati wanataka kazi zifanyike kwa wakati, tena vizuri. Kwa maana hiyo, ndio maana serikali iliweka utaratibu wa kuweka *standards* kwenye malipo ya wafanyakazi.

Kwa msingi huo hawa walivyo wakweli walipokuwa hawahitaji walikwenda milioni 3, sasa kutokana na mabadiliko ya mishahara na ajira mpya wote hawa ambao wako kwenye idara hii malipo yao kwa mwaka mzima milioni 15, basi Mhe. Mjumbe nafikiri ni vyema akaelewa uzito huo. Kweli fedha ni nyingi za umma, lakini tutazame utendaji kazi wa mwaka mzima na wafanyakazi ambao wako katika Idara hii ya Mipango, Sera na Utafiti. *(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, maelezo ya mawaziri hayanitoshelezi hayasaidii, bado yanajikita au yanazunguka pale pale tu. Mimi nadhani ndiyo yale tunayosema hapa kwamba tunawasaidia wao, kwa sababu mara nyingi mambo haya yanakuwepo kwa watendaji na tukisema tunaambiwa hatu-*appreciate* mambo wanayofanya watendaji na kila wakati tunawalaumu. Lakini kama nilivyosema haya maelezo yanakuja kuombewa bajeti hapa walipaswa wajue.

Mhe. Mwenyekiti, tunazo *options* mbili kwa sababu sitaki kuzuia Kamati hii ya Matumizi ikakamwa hapa. Moja tukubaliane tulikate lirejee kama lilivyokuwa mwaka jana milioni 3 au kwa sababu naiamini Kamati hii ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa na ninamuamini Mwenyekiti wake, kwa sababu ndio kwanza tunaanza basi niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wenzangu tulikubali lakini kwa masharti na hiyo ni *option* ya pili.

Kwa hivyo, leo tunapitisha na tukijaalia lakini kesho tuletewe *break down* yake hii, kwa sasa hili itakuwa tumelishtukiza na hili wajiandae na wengi wote, tuletewe *break down* yake hizi milioni 15 anastahiki nani na kila mmoja anapata kiasi gani na halafu tuone kama nilivyosema msingi wake wa hoja unaendelea na asilimia ya mshahara.

Mhe. Mwenyekiti, maelezo ya Mhe. Waziri yatakuja kuwazonga, kwani serikali inawajibika kwa pamoja kama ulisema tumerekebisha viwango vya mishahara haiwezi kuwa vya Idara ya Mipango, Sera na Utafiti moja tu katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, isipokuwa vinakuwa vina-*apply equally* katika wizara pamoja na idara zote.

Sasa tutakuja kuona huko mbele kwamba kila idara au wizara imejipangia kivyake vyake tu. Mhe. Mwenyekiti, nasema nalikubali tuendelee *option* ya pili ama tulikate, lakini tuje tupewe *break down* na ihalalishwe, na naomba nimsaidie Mhe. Waziri na haya si posho ya kufanyia kazi tu walituambia wao, kwamba hizi ni posho zinazoendana na mshahara wa mtu, yaani yale marupurupu na aliyataja Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwamba ni yale ya mafuta na pengine viburudishaji vyake inategemea mhusika wa idara ile.

Kwa hivyo, haya hayategemei kwa nani, isipokuwa yanatakiwa yawe *fixed* kwa mwaka mzima kwa kila mwaka. Mhe. Mwenyekiti, nikubali tuendelee, lakini tugaiwe *photocopies* na kila Mhe. Mjumbe aipate ile *break down* yake inapatikana vipi, ili tujue na baadaye tuje tuitumie kwa kila wizara na kila idara inayokuja huko siku za mbele.

Baada ya hayo, Mhe. Mwenyekiti nasema tuendelee, ahsante sana.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, ahsante wakati nilipokuwa nikichangia nukta iliyonipa mashaka zaidi katika masuala ya vifungu na nilitoa kasoro tofauti, kama vile nilitoa kasoro baadhi ya vifungu kuzidi na vyengine vimeshuka.

Sasa katika fungu hili la posho maalum. Kwa bahati Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wakati alipokuwa akichangia hapa alielezea kwamba posho hili mwaka jana limesahauliwa baadhi ya maeneo na wakachuma fedha nyingi kutoka eneo jengine kwa ajili ya kuwalipa wale wafanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, langu liko tofauti kidogo la mchango wa Mhe. Ismail Jussa Ladhu kuna baadhi ya kada ambazo wanastahiki kupata posho maalum, yaani wasaidizi wa mawaziri, mwaka jana fungu lao limesahauliwa kabisa na wala hawakupata kuchukuliwa fungu lao kutoka sehemu nyengine na wao wakapewa kama walivyochukuliwa hawa wengine.

Kwa hivyo, kwenye fungu hili nataka kujua Mhe. Mwenyekiti na hofu yangu ni kwamba Mhe. Waziri asijekuwa mwaka huu amelisahau na wale watu wakaanza kuteseka tena, kwa hiyo labda tuelezwe katika kuweka sawa wale wasaidizi, yaani madereva mwaka huu fungu lake katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais limeekwa au vipi Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, tatizo la *echo* bado lipo na Mhe. Mjumbe alipokuwa akisema sauti yake aliinyanyua juu kama vile ilivyokuwa Mhe. Ismail Jussa Ladhu

alivyokuwa hanisikii, basi naomba kidogo Mhe. Mwenyekiti arudie tena Mhe. Mjumbe. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, rejea hoja.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, nasema kwamba katika kifungu hichi cha posho maalum Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora wakati alipokuwa akitoa ufafanuzi alielezea kwamba kifungu hichi wakati wa bajeti ya mwaka jana kuna baadhi ya kifungu kilisahauliwa na wakahaulisha kutoa kifungu kwenda kifungu chengine kwa ajili ya kuwalipa watu wanaostahiki kuwalipa posho maalum.

Lakini miongoni mwa watu wanaostahiki ni wasaidizi wa mawaziri, sasa wao hawakuchukuliwa kifungu chengine na kulipwa haki yao kwa sababu ndani ya bajeti ilikuwa hamna. Kwa hivyo, hofu yangu nataka kumuuliza Mhe. Waziri kwamba mwaka huu wale waliosahauliwa mwaka jana na pengine hawakupata mwaka huu hakuwasahau na posho lao lipo kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka niseme kwamba ni kweli katika watu waliopewa maposho mwaka jana ni wasaidizi wa mawaziri hawakuwemo na wala hawakupangiwa posho hilo.

Sasa ninachotaka kusema ni kwamba wasaidizi hawa wa mawaziri safari hii tunayo nia ya kuwapangia maposho kama walivyo *secretaries*, matarishi, watu wa masjala na wengi wengineo. Kwa hivyo, fungu lao la nyongeza ya posho hizi, kwa sababu hizi ni posho mpya kwao na wala hazimo katika wafanyakazi ambao hivi sasa wanalipwa, isipokuwa nyongeza ile ipo kwenye lile fungu la bilioni 15.5 la nyongeza zote za maposho na mishahara ambayo itatolewa kwa mwaka huu wa fedha 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, kwa hiyo kwa kifupi imezingatiwa.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, ahsante na baada ya maelezo ya Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora nimeridhika na wafanyakazi wameshafurahi, basi tuendelee. *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu naielekeza kwenye kifungu kidogo cha 263178 ukusara wa 59 kuhusu ushauri nasaha. Kwa kweli mwaka juzi ilikuwa ni 500,000/=, mwaka jana bila ya shaka masuala ya UKIMWI ilionekana hamna labda na fedha haikutengwa, lakini mara hii tumetenga milioni 52,500,000/= Mhe. Mwenyekiti naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, hii ina-*reflect* kutokana na fedha hizi za *Global Fund* na hii ni kwa nia ya kusimamia mradi mzima huu kwa sababu hili jambo linaratibiwa na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pamoja na Wizara nyengine kwa sababu kuna fedha ambazo zitafika karibu dola milioni 5.8 za Malaria na pia za TB ni dola milioni 5.8 vile vile kuna dola kama laki 2 ambapo Serikali ya Zanzibar imetakiwa kutoa asilimia 20. Kwa hivyo, hapa tumeweka milioni 52, ili ziweze kukidhi haja yenyewe, yaani tunasimamia kwa wizara zote za serikali kwenye suala hili la kuratibu fedha hizo ambazo nimezitaja.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, maelezo ya Waziri ni matamu sana, lakini nataka aendelee kunielimisha kwamba masuala ya UKIMWI tumeyaweka kwenye Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na kila mwaka hutoa mamilioni ya fedha na mwaka jana nakumbuka tulikubaliana kwamba kwa sababu yeye ndiye mratibu Ofisi ile ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia Tume ya UKIMWI, basi tulishauri hizi fedha ziende kule kwa ajili ya kupunguza matatizo.

Sasa Mhe. Waziri akisema kwamba bado anaratibu na kule kuna tume nzima ambayo ina mamilioni ya fedha na hizi fedha hazikuingia kwenye fungu la maendeleo bado sijapata maelezo ya kutosha kuhusu fedha hizi. Mhe. Mwenyekiti, naomba azidi kunielimisha kwa maslahi ya wizara yake pamoja na wananchi kwa jumla.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kazi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ni pamoja na kuratibu hata kwenye neema pia tukiwa tunaanza ku-*question* kuratibu kupatikana kwa neema kidogo naona tutakuwa tunajirudisha nyuma, kwa sababu ni utaratibu tu wa serikali. Kwa hivyo, fedha hizi zinaratibiwa ile miradi inayofadhiliwa na Mfuko wa Dunia, kwa ajili ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria.

Sasa fedha zimepatikana na tumeweka milioni 52 ziweze kuratibu shughuli hii kwa ajili ya serikali na wala sioni kosa letu liko wapi, kupata fedha hizi tukaratibu kwa fedha hizi maana anazungumzia zaidi ya dola milioni 11 na sisi fedha hizo tunaratibu tu zitakwenda kwa wahusika na wala haziguswi na sisi, lakini kwa sababu ni uratibu basi ni utaratibu uliofanywa na serikali pamoja na wafadhili wenyewe ndio ukafikia hatua hiyo. Kwa hivyo, sijui nieleze vipi kimiujiza mpaka Mhe. Mjumbe anaweza kufahamu, lakini huo ndio ukweli halisi.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, kwa hakika usiku unaingia, lakini tuko katika kuwajibika. Sehemu hii ni ya ruzuku na hoja yangu ni kwamba hapa ni ushauri nasaha na sio kuratibu, kama amekusudia ndio yeye

anaratibu kwa maana ya kufanya *follow-up* kwenye wizara zote za serikali basi ningeshawishika.

Lakini anafanya ushauri nasaha ndani ya idara moja tu, si kwamba anaratibu shughuli nzima ya UKIMWI ya taifa, isipokuwa ni ushauri na nasaha kwenye Idara moja ya Mipango, kwamba wale wafanyakazi wa Idara ya Mipango, Mkurugenzi na timu yake wanapewa ushauri nasaha kwa milioni 52 na sio kuratibu kwa masuala ya UKIMWI kwa wizara mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kwa ushauri nasaha tu ndani ya idara moja ya mipango nadhani ni fedha nyingi. Sasa atuambie ni uratibu au ni ushauri nasaha wa Idara ya Mipango kuhusu masuala ya UKIMWI.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, mimi ninamuelewa Mhe. Mjumbe analotaka kulisikia na pia nafahamu Mhe. Waziri anachokielezea. Kwa kweli Mhe. Mjumbe anapata tabu kidogo akiona kwamba shughuli za UKIMWI ziko chini ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na hapa masuala ya ushauri nasaha au uratibu uko chini ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Kuna utekelezaji wa miradi inayohusiana na masuala ya ukimwi ambayo inakwenda moja kwa moja kwa walengwa. Zile ni shughuli ambazo zipo chini ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Tunapokuja katika Ofisi zetu moja moja ni dhahiri kwamba tunapaswa kutoa ushauri nasaha kwa wafanyakazi wetu ndani ya maofisi yetu.

Lakini vile vile Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, ndiyo inayoratibu shughuli zote za serikali hata kama shughuli zile zipo kwa Makamu wa Kwanza au Rais mwenyewe au Rais mwenyewe au zipo Wizara ya Fedha. Sasa kwa masuala haya uratibu anao yeye, utekelezaji wa programu zenyewe zote za ukimwi ndio zipo chini ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Sasa hapa mimi nadhani tuweze kutofautisha haya mawili, sasa kama kuna Kiswahili chengine cha kuzungumza basi nitashindwa kutoa maelezo zaidi ili nikaweza kufahamika. Ufahamu wangu ni huo kwamba hawa Makamu wa Pili wa Rais ndio waratibu wa shughuli zote zikiwemo zile shughuli za ukimwi lakini vile vile Makamu wa Kwanza wa Rais ni watekelezaji wa programu zote zinazohusika na masuala ya ukimwi.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, hapa mimi nina hoja mbili, kama serikali imekubaliana kwamba Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais iwe inaratibu shughuli za mipango, fungu la Makamu wa Kwanza wa Rais

kwenye Tume ya Ukimwi, gharama zote za uratibu tufute ili ubakie na utekelezaji wa miradi.

La si hivyo nashawishika kabisa tubakishe milioni 10 za ushauri nasaha kwenye Idara na 40 ziende sehemu nyengine kwa ajili ya maendeleo. Hata kama Wizara hii hii lakini hatuwezi kutenga milioni 52 kwa ushauri nasaha kwa idara moja tu. Kwa hivyo tukubaliane Serikali ishauriane Mawaziri wawili, tubakishe milioni 2 wenzangu wananambia za ushauri nasaha ili 50 ziende sehemu nyengine. Hata kama ni Wizara hii hii lakini iende Idara nyengine.

Au tukubaliane kwamba uratibu utoke kwenye Tume ya Ukimwi iende kwenye Ofisi hii nakubaliana na hilo. Kwa hiyo naomba maelezo hayo ili tuweze kuamua hatua ya mwisho. Si hivyo Mhe. Mwenyekiti, tuende kwenye kura ili tumalizane.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, napenda Mhe. Hija Hassan Hija aelewe kwamba hapa tunazungumzia *activities* inayohusu malaria, kifua kikuu na ukimwi. Suala lenyewe ni kwamba sisi tunakuwa waratibu tu wa kushughulikia lile suala la fedha za *Global Fund*, fedha hizo hiyo miradi yenyewe itakwenda kwa wenyewe wahusika na wala huko kwetu hazitopita. Sisi tunaratibu ili ku-*facilitate* hizi *project* ziwezekane.

Msingi wenyewe hii kuwepo milioni 52 sio kwa kimaana hasa ili jina la ushauri nasaha lipo tu hapa, lakini hazikutumika kwa sababu ya ushauri nasaha. Hizi sana zitatumika zaidi. Huo ushauri nasaha kwetu sisi kwa Wizara zitabakia hizo hizo laki tano. Hizo fedha takriban hazitoshi hata hizo milioni 52 zenyewe kwa ku-*facilitate* kwa sababu inatakiwa ipatikane 20% huko mbele kuna dola laki mbili nyengine *extra* 20% *almost 45 dollars* ukizibadilisha kwa TSh zipo zaidi ya milioni 60.

Maana yake itabidi hata hayo mafungu huko mbele ya safari utakapokamilika huo mradi lazima zitoke ili suala liendelee vizuri. Suala ninalozungumza hapa hatuzungumzii ukimwi peke yake, tunazungumzia Ukimwi, Kifua kikuu, tunazungumza TB, kuna fedha hizi zaidi ya dola milioni 11. Sasa sioni tunashinda nini, ikiwa tuache fedha hizi kwa sababu ya milioni 52 sawa lakini ninachokizungumzia hapa hizi zina - *facilitate* hizi pesa nyengine hawa wameachiwa kama waratibu kufanya shughuli za uratibu. Hapo hakuna hoja ya kushindana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi navutika kwamba hizi pesa tuziache, lakini kule ndio zinakopatikana kazi za kufuatilia za Kamati. Sasa kamati tuifanye kazi

hiyo, tuone fedha hizi zimetumikaje ili tuweze kuhakikisha kama matumizi yamekwenda ndivyo. Nadhani tuendelee.

MUONGOZO

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu mara nyingi hushughulika na kuchunguza fedha za aina hiyo. Nataka nilihakikishie Baraza lako Tukufu kwamba kifungu hiki takriban kipo katika mawizara yote suala la *councelling* kuhusu HIV. Na mimi nataka nikuthibitishie kwamba takriban hizi ni fedha tu hutengwa kwa ajili ya wakubwa kufanya wanavyotaka wao wenyiwao, wala hazitumiki hata hizo milioni mbili hazitumiki. Nataka nikuhakikishie Mwenyekiti, kama tuwaachie bora tuwaachie milioni mbili kulikoni kuwaachia kazi hizi.

Hizi ni fedha ambazo takriban *department* zote zipo kwa ajili ya HIV *councelling* lakini hazitumika kama tunavyoziidhinisha katika Baraza hili. Nashauri matumizi ya fedha yachungwe Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, hapa wao wangeangalia je, sisi tunazungumzia suala la *councelling* au tunazungumzia suala zima la uratibu wa kupata fedha kwa ajili ya utekelezaji. Kama ni *councelling* hizi sisi laki tano zinatosha, hizi nyengine *almost* kwa sababu ya kuratibu hii miradi. Mimi nakubaliana na hoja yake kamati ije ifuatilie ione kama kutatokea tatizo lolote. Kwa sababu hiyo *commitment* ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hii imo katika hatua nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninachokitaka iundwe kamati ya aina yoyote ije isimamie hizi fedha hizi zitatumika kuzitumia sisi kwenye masuala ya *councelling* ya ukimwi ama zitatumika katika ku - *facilitate* hizi. Ama vyengine basi mtu achukue dhamana kama tunapata fedha hizi zitoke mfukoni mwake ili ku - *facilitate* hizi pesa tupate ndio suala la msingi tu hilo Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Muongozo umeshakuwa tayari kwamba kamati inapata shughuli zake kwa namna ya kufuatilia shughuli kama hizi kwa hivyo kamati zinazohusika kwa kila eneo kwa kila *ministry* basi watafuatilia pesa hizi namna ya matumizi yake, tuendelee.

Kifungu 0401	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	295,240,000

Kifungu 0501

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naomba kwa sababu nipo peke yangu mpaka sasa hivi naomba nitumie hoja mbili. Ya kwanza inayohusu fedha na naomba niende katika ukurasa wa 61 fungu 220700 Matengenezo ya Ofisi Nyumba. Nakwenda katika Ofisi ndogo kupata *break down* zake mbili. Kuna matengenezo madogo ya ofisi ni ishirini na nne milioni laki nne sabini na moja elfu na ishirini. Lakini kuna matengenezo makubwa ya majengo mia moja hamsini na mbili milioni laki tano sabini na tisa elfu. Nilikuwa nataka maelezo ya fungu hilo.

Lakini ukienda kwenye matumizi hapa nataka nimshukuru Mhe. Waziri hili kalijibu vizuri katika majumuisho yake. Naomba nitumie fungu hili kumtaka atoe kauli rasmi ya serikali ndogo tu juu ya suala la Wazanzibari wenye asili ya Kingazija kwa sababu Idara ya Utumishi na uendeshaji ina fungu pia la Mheshimiwa hilo la mshahara wake. Kwa hivyo nina haki ya kuhoji Sera hapa Mhe. Mwenyekiti.

Suala hili nashukuru kwamba kwa maelezo aliyonipa nataka tu atoe kauli badala ya pale aliyoitoa ya jumla kataka mimi nimpelekee kesi ambazo zinazohusika nitampelekea kama ni sera. Kwa sababu nisitumie vibanda vya Idara ya Uhamiaji wa kuadhibu jumuia nzima hii kwa sababu tu pengine kuna kesi moja au mbili ukataka kauli ya serikali ya kisera kwamba Wazanzibari wenye asili ya Kingazija wana haki sawa na ni raia wa Zanzibar kama raia wengine wowote wa Zanzibar na kama kuna mtu mmoja mmoja ana tatizo lisimamie hivyo lakini wasiadhibiwe kwa sababu ya asili yao. Hayo hayo Mhe. Mwenyekiti, nashukuru.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, sisi tulikuwa tunajenga ofisi yetu na bado tunadaiwa kwenye matengenezo makubwa kwa hiyo ni sehemu ya kulipia madeni ambayo ofisi inadaiwa kwa majengo ambayo yamefanyika. Matengenezo madogo madogo hii inatokea kwenye kazi zile za kwa kweli haziwezi kuepukika na zinajitokeza.

Mimi nataka nimuhakikishie tu Mhe. Jussa kwamba kadri anavyozungumza hapa ndio kadri anavyotupa macho ya kuona zaidi ya kufuatilia kila hatua tunachoambiwa na watendaji wetu ili tuweze ku- *break down* vizuri, haya yote kwa kuhakikisha kwamba fedha za umma zinatumika ipasavyo. Wala sisi hatuoni kwamba wanatubughudhi wanapohoji wala hatuoni tabu, ni vyema kadri inavyosemwa sisi tunapata kujenga uelewa zaidi ya kujua nini kinafanyika. Lakini maelezo ya majengo ni hayo.

Kuhusu maelezo ya ndugu zetu Wangazija. Nasikitika sana Mhe. Spika, kurudia kutaja jamii ambayo miye ipo karibu yangu sana. Maana mimi

shangazi yangu ameolewa na Wangazija, wamezaliwa Mzee Himidi Msoma alimuoa shangazi yangu, wale kina Buruhani, kina Salum Msoma, Abdulghani na wengine ni ndugu zangu. Kwa hivyo nikisikia kutajwa tajwa kitu kama hichi kinanisikitisha. Nasema sisi tumefanya Mapinduzi Zanzibar kwa ajili ya kujenga umoja sio kumbagua mtu yoyote. Sisi ni watu wamoja tunatakiwa tutoe huduma kwa wote sawa bila ya ubaguzi wa aina yoyote ndio utaratibu ambao tumekubaliana mbele ya sheria wala hakuna huyu ndiye, huyu siye, sote ni watu wamoja. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naomba nilianze na hili la Wazanzibari wenzangu wenye asili ya Kingazija. Mhe. Mwenyekiti, nafurahi na kauli yake na nategemea kwa kauli hii suala hili la Idara ya Uhamiaji kuwaadhibu, kuwatesa na kuwadhalilisha wenye asili ya Kingazija litakoma kuanzia leo.

Mhe. Mwenyekiti, nilivyoambiwa nimeletwa mara hii kwa sababu tangu zamani linazungumzwa hilo. Kwa sababu uraia mpaka hivi tunavyozungumza bado ni suala la Muungano. Na bahati nzuri Zanzibar na Tanganyika kabla ya kuungana zote zilikuwa chini ya Muingereza kwa hivyo Sheria zake wa uraia zilikuwa zinafanana. Lakini cha ajabu wananchi wenye asili ya Kingazija waliokuwepo Bara hawabughudhiwi lakini hapa Zanzibar ndio Idara ya Uhamiaji inawabughudhi na kuwadhalilisha. Kwa hivyo nashukuru kwamba leo Waziri katoa kauli na naamini Inshallah kuanzia kesho watatembea wakiwa wana haki kama wale wengine wowote na lile tatizo la kuwa wanasafiri na wanawanyang'anya paspoti zao, wakawabughudhi wengine wakawazuilia paspoti kwa muda zaidi ya mwaka hilo litakoma. Nashukuru kwa kauli yake Waziri nategemea kwamba litakomeshwa.

Narudi kwenye fungu la matumizi Mhe. Mwenyekiti, kwa jumla nataka kusema nimeyapokea vizuri maelezo ya Mhe. Muhammed Aboud (Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais). Na mimi nampenda Mhe. Muhammed Aboud kwa uungwana wake kwamba kakiri kwamba tukifanya hivi tunawasaidia wao. Kwa hilo Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaruhusu kwamba tuendelee nataka kuyaunganisha na yale maelezo aliyokuwa kayatoa Mhe. Makamo wa Pili wa Rais mzee wangu Balozi Seif Ali Iddi, alipozungumzia suala zima la kusimamia nidhamu katika serikali. Na mimi nilizungumza nilitaka nijue nani anayemamlaka ya nidhamu katika mchango wangu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nawakumbusha tena mawaziri kwa sababu hili linaleta malalamiko sana Katiba yetu ibara ya 50(1) imeweka wazi madaraka ya Waziri na kwa faida ya kifungu hicho naomba nikisome kinasema kwamba:

"Pale Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais au waziri yeyote mwengine anapokuwa na dhamana ya Wizara yoyote ya serikali, atakuwa ndiye kiongozi na Msimamizi Mkuu na bila ya kuathiri masharti yoyote ya usimamizi. Katibu Mkuu ambaye afisi yake itakuwa ni ya Utumishi wa Serikali vatakuwa ndio Afisa Mtendaji Mkuu wa Wizara"

Kwa hivyo mawaziri hawa wana haki ya kuwahoji hawa Mhe. Mwenyekiti, wengine tunasikia sisi na tunapata tabu kama wanasiasa wenzangu tukiwa katika Baraza hili, kwamba unapokwenda kuhoji unaambiwa hili silijui kwa sababu watendaji wananambia sio mamlaka yangu.

Kwa hivyo nasema sisi kama tunaona mimi Mhe. Mwenyekiti, si mtu wa mahesabu naamini na Waziri akipewa nafasi ya kuwapitia hawa kabla hajaleta hapa atapata kuwagundua hawa. Kwa hivyo niwaombe tu, nayapokea maneno ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, hasa yale mawaidha yake mazuri kwamba basi kabla ya kuleta hapa hebu na wao wajiridhishe kwanza, unapoona kuna mchupo mkubwa kama huu wa mfuko, wawahoji Mhe. Mwenyekiti, tusingoje mpaka tukafika hapa. VAT inasema msimamizi ni Katibu Mkuu lakini anayetuomba fedha ni Waziri, kwa hivyo hapa yeye ndiye anayebeba jukumu hapa.

Kwa hiyo naliomba liendelee fungu hili la matumizi haya ya matengenezo ya Afisi kwamba sharti na wao watayatizama kwa makini. Na sisi kamati zetu zitakapokwenda huko tutakwenda kuhoji. Niwaombe Mawaziri pale tunapokaa katika Kamati tukawahoji watendaji wao tena wao mawaziri wasiwe wakali wakaghadhibika kwenda kuwahoji watendaji wao wakawa wanawatetea, watuache tufanye kazi zetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya Mhe. Mwenyekiti, nasema tuendelee, Ahsante sana.

Kifungu 0501 Idara ya Uendeshaji ya Utumishi 148,080,000

Kifungu 0601 Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, hapa sitaki maelezo ninachotaka ni kutahadharisha tu katika ukurasa wa 64 fungu la matumizi mengineyo 282100, kwenye sherehe za kitaifa yaani ni *vote* 28211 sherehe za kitaifa imetengewa bilioni mbili. Mhe. Mwenyekiti, lakini hapo hapo chini pana kumbukumbu za viongozi wa Kitaifa ambao kwa maarifa yangu ya Zanzibar ni moja tu ya kumkumbuka muasisi wa Mapinduzi marehemu Mzee Abeid Amani Karume. Sasa hapa nilitaka kutoa indhari tu kwamba katika maelezo tuliambiwa kwamba Sherehe ya Mapinduzi imetengewa bilioni moja,

lakini hapa zimeandikwa bilioni mbili sijui kama zina *cover* na sherehe nyengine.

Lakini kwa vyovyote iwavyo sikusudii kutaka maelezo kwa sasa najua fungu la sheria ni kubwa na hasa kwa sherehe za miaka 50. Nilitakiwa maelezo siku ya bajeti, Waziri wa Fedha alinitolea maelezo mazuri. Nilitaka kumtahadharisha tu kwamba ili katika matumizi Mawaziri wawe waangalifu. Kwa sababu katika mafungu kama haya huku mara unaambiwa kumetoka bilioni moja lakini katika mafungu unaona bilioni mbili ndipo unapata wajanja ndio wanafanya mambo yao.

Kwa hiyo nilikuwa nasema hili tu Mheshimiwa alitizame vizuri Waziri muhusika na tujue kwamba fedha hizi zinakwenda kutumika kwa shughuli zilizokusudiwa. Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, tuendelee ahsante sana.

Kifungu 0601 Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa 2,189,103,000

Kifungu 0701 Idara ya Huduma

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilimuomba Mhe. Waziri aje anifafanulie kwenye mwaka 2012/2013 kuna shilingi milioni nane na mwaka huu kuna shilingi milioni kumi na nne, matengenezo ya magari. Chengine kuna kifungu 221102 Mafunzo ya ndani, kuna shilingi milioni 15 mwaka wa 2012 /2013 na mwaka 2013/2014 kuna shilingi milioni tano, laki mbili na hamsini niliomba Mhe. Waziri anifafanulie. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba vile vifungu avitaje taratibu ili niweze kuvifahamu vizuri.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye kasma kifungu 220803 Matengenezo ya Magari ukurasa wa 67, mwaka 2012/2013 kuna shilingi milioni nane na mwaka 2013/2014 kuna shilingi milioni 14 hapa nimuulize Mhe. Waziri ni kitu gani kilichosababisha kupanga hadi kufikia shilingi milioni 14.

Vile vile kuna kifungu kasma 221102 Mafunzo ya Ndani kuna shilingi milioni 15 mwaka 2012/2013 na mwaka 2013/2014 kuna shilingi milioni tano laki mbili na hamsini. Hapa sijui ni kitu gani kilichobidi hapa kushusha kufikia milioni tano mia mbili na hamsini. Naomba Mhe. Waziri anifafanulie.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, hapo ukitizama inajieleza kama ilivyosema unatizama na zile *activities* zenyewe, matengenezo ya magari kwa mwaka nzima milioni 14. Kwa sababu sasa hivi Mheshimiwa kwenye utaratibu wetu wa bajeti tumeweka kwa utaratibu wa kuwasilisha serikalini ambayo inatutaka tusiumize kifungu hichi ukabana kifungu hichi. Kwa hivyo hapa tumekwenda kwenye uhalisia wake kwa msingi wa kuwa na milioni 14. Huko nyuma unaweza kuwa na milioni nane lakini ukawa umekibana kifungu chengine, sasa utaratibu haukubaliki ina maana uje na yale makadirio yenye uhalisia ndio sababu yenyewe.

Na hicho chengine kuwa kikubwa au kuwa kidogo msingi wake ni huo huo kwamba sasa baada ya uzoefu tumeona pengine matumizi ya mwaka uliokwisha yamekuwa hayahitajiki kiasi hicho, tumekwenda kwa kile kinachohusika. Hii maana yake ni kuonesha kwamba na watendaji nao wamekuwa makini, pale penye nyingi na panahitaji ndogo wanakwenda kwenye kidogo na pale penye kidogo panahitaji nyingi wanakwenda kwenye nyingi. Maelezo ni hayo Mhe. Mwenyeki.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwenye Idara ya Huduma za Makamu wa Pili wa Rais nilikuwa nataka maelezo yale, nafikiri sasa hivi hoja yangu itaeleweka zaidi. Nina mambo mawili; la kwanza kuna ile *vote* yangu ipo ukurasa wa 65 ninayoipenda posho maalum 211110. Naomba nieleweke kwamba hii haimridhishi Makamu wa Pili kwa sababu yeye ana fungu lake mbali linalohusu ofisi yake ya faragha, imetoka kutoka milioni thalathini na tisa laki mbili kumi na sita elfu kwa mwaka jana, mwaka huu ni thamanini na nne milioni laki tano, kumi na moja elfu ni zaidi ya mara mbili Mhe. Mwenyekiti, wakati kama nilivyosema nikilihamisha na fungu la mishahara tofauti ni milioni moja, mwaka jana ilikuwa milioni mia moja hamsini na sita mwaka huu mia moja hamsini na saba milioni. Kuna tofauti kama milioni moja tu hapa.

Lakini kwenye posho maalum tofauti ni zaidi ya mara mbili kutoka thalathini na tisa milioni laki mbili kumi na sita elfu hadi thamanini na nne milioni laki tano kumi na moja elfu. Mwanzo Mhe. Waziri alitwambia kwamba Idara ya Mipango, Sera na Utafiti linajumuisha watu wote na nikamwambia itakuja kumzonga kwa sababu ile Idara fungu hili lipo. Sasa nilikuwa naomba maelezo ya fungu hilo. Lakini mimi nilikuwa naomba na maelezo ya fungu la pili isipokuwa kama mwenzangu ana fungu niko tayari kumuachia kwa sababu tuliitoa kwenye semina kwamba tuachiane, asiseme mtu mmoja tu. Kwa hivyo kama mwenzangu ana fungu anataka kulihoji naomba nisilitumie

miye nimpe fursa. Lakini kama hana nitumie fursa ya pili kabisa. Kwa sababu hoja zinazoruhusiwa ni tatu, sasa kama hayupo mwengine nimalizie ya tatu kabisa.

Mhe. Spika: Kwa kweli ni moja tu unayoruhusika nyengine mbili atachukua Mhe. Mwanajuma hapo nyuma yako.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, naomba nimsaidie kidogo Mwakilishi wangu Mhe. Jussa maelezo yake kama ifuatavyo.

Ofisi ya Faragha ya Makamu wa Pili wa Rais na hii posho ambayo anayoiuliza Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwanza posho hii maalum inajumuisha yale maposho ambayo niliyomwambia kama anayakumbuka. Lakini *on top* katika eneo hili hapa pana posho nyeti kwa wafanyakazi wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Ofisi ya faragha na Ofisi nyengine za Makamu wa Pili wa Rais zilizopo pale Makao Makuu. Mwaka jana kupitia Wizara ya Utumishi ilitoa *secular* kwamba zile posho zote tunazisimamisha ili tuzichunguze kwanza uhalali wake na upeo wake. Na kwa zile posho ambazo zimekubalika zitarudi tena mwaka huu. Moja ya posho ambayo tuliyoisimamisha mwaka jana ilikuwa ni hii posho nyeti. Kwa hivyo mwaka jana ndio maana ukakuta tumeweka thalathini na tisa mwaka huu thamanini na nne, posho hii tumeirudisha. Nadhani Mhe. Hamza Hassan Juma wakati alipokuwa Waziri pale kaikuta posho nyeti pale ipo. Mhe. Shamuhuna alipokuwa Waziri na mimi ndio Katibu Mkuu ndio ilipoanzishwa posho hii nyeti.

Kwa hivyo nataka nimwambie kwamba hapa kuna na posho nyeti kwa watendaji waliomo mle ndani ambayo tumeirudisha mwaka huu ndio kwa maana kuna milioni thamanini na nne pamoja na watendaji wapya walioongezeka.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, maelezo ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo hayakuniridhisha, kama ilisitishwa mwaka jana ningeliiona na ya mwaka juzi linalingana na hili la mwaka huu kabla ya kusitishwa. Lakini mwaka juzi ni thalathini na nne milioni laki mbili kumi na tisa elfu. Mwaka jana limeongezeka kidogo kuliko mwaka juzi, thalathini na tisa milioni laki mbili kumi na sita elfu. Pana nyongeza ya takriban milioni tano na elfu tatu, mwaka huu thamanini milioni.

Ningelielewa kidogo tena sio kwa maneno kwa takwimu kwamba hawa wafanyakazi wa ofisi ya faragha wameongezeka mara mbili kuliko

walivyokuwa, kama walikuwa kumi mwaka huu wamekuwa 20 nitaweza kuikubali kidogo. Lakini kama ni hivyo na kama nyongeza ya watumishi na fungu la mshahara lingepanda, lakini fungu la mshahara ofisi ya faragha tofauti milioni moja, fungu la posho maalum tena hilo hilo posho nyeti ambalo lilikuwepo miaka yote kama wamesitisha mwaka jana wanavyotwambia wao. Mwaka juzi ilionekana hapa hesabu Mheshimiwa haziendani na maelezo tunayopewa, tunaomba maelezo Mheshimiwa hizi nyongeza za takriban 45 milioni za nini?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mheshimiwa naomba niongezee maelezo kilichosababisha kuvimba kwa posho hizi safari hii kwamba tumezifanyia mapitio hizi posho. Kwa hivyo pamoja na maelezo ambayo ameeleza Mhe. Waziri wa Nchi Fedha ni kwamba kwanza tulisimamisha kwa ajili ya kuzipitia upya na kuona uhalali wa hizi posho wenyewe zinalipwa kwa nani na hao watu wanaoandikiwa posho hizi wapo au hawapo. Hiyo kazi tumeifanya na baada ya kwisha kujiridhisha kwamba hawa watu wanaostahiki kulipwa posho hizi ndio maana tumeziongeza sambamba na wale watumishi katika Ofisi ya faragha ambao wameajiriwa wapya katika mwaka huu, posho zao pia zimesababisha hiki kifungu kivimbe. Hayo ndio maelezo ya ziada baada ya maelezo ambayo ameyatoa Mhe. Waziri wa Nchi Fedha.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti baada ya maelezo mazuri ya Waziri wa Nchi Fedha na Waziri wa Nchi Utumishi, nimuongezee Mhe. Jussa haya yafuatayo.

Mheshimiwa kwa kuwa nia yetu safi, na nia yetu sote hapa ni kuhakikisha kila aina ya matumizi mabaya yasimamishwe ili matumizi yatumike vizuri. Mimi nataka nimuhakikishie tu Mheshimiwa kwamba tunaweza kesho au keshokutwa tukazileta *break down* zote za haya anayoyazungumza tukayapitisha kwa Waheshimiwa Wajumbe wakajua kwamba kwa nini fungu hili likafikia 84,000,000. Kwa sababu ni fedha ambazo zimeshakubalika na ziko kwenye taratibu na huko mwanzo mara hii wamefanya kazi kubwa sana watu wa utumishi, wamekuja ofisini kwetu wamemtazama kila aliopo wakajua idadi ya watu, nani anahitaji kulipwa kiasi gani ndio maana hiyo *break down* ikaja. Kwa hivyo mimi nataka nimuhakikishie Mhe. Jussa atuachie tuendelee na shughuli halafu tulete *break down* kwa viongozi hapa waone wajumbe hiki ndicho kilichofanyika kwenye posho nyeti. Kwa sababu Mheshimiwa ukweli tusingependa na mtu mwengine akose haki yake, tunachotaka tuendeshe serikali vizuri na kila mmoja apate haki yake. Wala vile vile hatupendi ionekane tunaongeza fedha tuupe mzigo ambazo hazina mahitaji kwa serikali. Kwa hivyo ningeomba tu Mhe. Jussa atukubalie halafu tumletee hizi *break down* kwenye maeneo ambayo ana wasiwasi nayo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti kama nilivyosema awali kwa sababu ninamuamini Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na maelezo yake yameonesha nia njema kufuatiliwa nakubali kwamba afuatiliwe, ninamuomba pia afuatilie kwenye safari za ofisi na matengenezo ya ofisi katika kifungu hicho hicho. Lakini baada ya hayo nakubali kwamba afuatilie halafu aje atupe maelezo kwa sisi kwa ujumla wetu au Kamati inayohusika. Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti nasema tuendelee. Ahsante.

Kifungu 0701	Idara ya Huduma za Makamu wa Pili wa Rais	780,034,000
Kifungu 0801	Idara ya Upigaji Chapa na Mpigaji Chapa Mkuu wa Serikali	546,868,000
Kifungu 1901	Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali ya	

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti kwanza nataka nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa ufafanuzi mzuri alioutoa katika maelezo yake lakini vile vile nimpongeze Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kukohoa maana yake katoa ufafanuzi mmoja tu lakini sote tumeuelewa na sisi kama viongozi tunamwambia Mhe. Makamu wa Pili wa Rais tumekusikia na tutajirekebisha na tutafanya kazi kwa mashirikiano kama unavyotuongoza.

Mhe. Mwenyekiti baada ya kusema hayo nilikuwa nataka kidogo tu katika Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti kama tunavyoelewa kwamba Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ndio kiongozi wa shughuli zote za serikali na Afisi yetu ya Baraza la Wawakilishi iko chini ya usimamizi wake. Sasa Mhe. Mwenyekiti tumekuwa tukizungumza katika vikao mbali mbali na vikao vyenyewe tunazungumzia suala la maslahi ya watumishi wa Baraza. Na kama Katiba ya Zanzibar inavyosema kifungu cha 77 mabano (1), (2), (3) mpaka (4) kimetupa nguvu na mamlaka ya kuweza kufanya shughuli hiyo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza si ungojee Baraza.

Mhe. Hamza Hassan Juma: *No*, najaribu kutoa ufafanuzi halafu ndio nakuja katika hiyo hoja yangu.

Mhe. Mwenyekiti: Njoo kwenye Baraza. Ni hivi hoja yako inahusu watumishi wa Baraza tungojee eneo la Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Unajua uratibu wa shughuli zote si ndio fungu hili Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Ngojea kwenye Baraza.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Mhe. Mwenyekiti nilipokuwa nikichangia..

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mheshimiwa kwa sababu sina wasiwasi na fungu la Baraza la Wawakilishi, hoja yangu Mheshimiwa nimesimamia katika uratibu, kwa sababu katika kusimamia shughuli za serikali Baraza linaingiliwa ndio katika ile uratibu, hii ndio hoja yangu ilipo. Sasa nikija kuzuia kwenye fungu la Baraza fungu la Baraza nimeshalikubali sina tatizo nalo, fungu la Baraza kama lilivyo sina tatizo nalo.

Mhe. Mwenyekiti: Hebu malizia hoja yako tuyasikie maelezo.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Kwa sababu nikizuia fungu la Baraza inaonesha kuna kifungu sijaridhika nacho lakini fungu la Baraza sina tatizo nalo. Lakini sasa kuna maamuzi ambayo tuliyopitisha kama Baraza ambayo maamuzi hayo tumeyapitisha mpaka katika lile fungu tutakalolipitisha la Baraza, lakini bado utekelezaji wake unaingiliwa kati, jambo ambalo si sahihi Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti naomba kidogo mimi nitanukuu hiki kifungu cha 77 (3) kinasema ‘Muundo na taratibu za Tume ya Utumishi wa Baraza utakuwa kama unatakavyoelezwa na sheria hii itakayotungwa kwa madhumuni hayo.’ Mhe. Mwenyekiti, tumezungumza katika vikao mbali mbali vya Kamati ya Uongozi na ikafika pahala Mhe. Mwenyekiti, kutokana na maingiliano ya Mamlaka yetu ya chombo chetu cha Baraza, Tume ya Utumishi tukakubaliana na Mawaziri, Waziri wa Katiba na Sheria tukazungumza naye na tukakubaliana kwamba kuna kifungu kifanyiwe utaratibu wa kufanyiwa marekebisho.

Lakini pamoja na hayo Mhe. Mwenyekiti sitaki niseme ya ndani zaidi lakini tulipofanya ziara ya kujitambulisha kwamba tulifanya ziara na kuangalia Mabunge ya wenzetu yanavyofanya kazi Mhe. Mwenyekiti, tulipata busara kwa Mhe. Rais na alitwambia kama kuna maeneo kwa sababu tulimueleza tuliyoyaona kwa wenzetu na haja ambayo tunayoitaka akatueleza kama kuna maeneo tunahitaji lazima turekebishe Katiba, basi kaeni na Waziri wa Sheria na Katiba na Mwanasheria Mkuu tubadilishe vifungu vya Katiba. Lakini kama kuna maeneo mnaweza mkayafanyia kazi bila ya kufanya marekebisho ya Katiba mnaweza mkafanya hivyo na ndio maana tukaingiza mpaka suala la Ofisi ya Mhe. Mwenyekiti, ambayo ilikuwa haina hadhi ya Spika.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, hapa nataka kueleza *concern* yangu kwamba serikali inaliingilia Baraza la Wawakilishi na hii si sahihi Mhe. Mwenyekiti. Tume ya Utumishi ya Baraza ina mamlaka kamili na tunataka uhuru wa Baraza la Wawakilishi, lina mamlaka yake kamili na serikali inaona mamlaka yao na

Baraza la Wawakilishi lina mamlaka yake kamili na serikali na wao ina mamlaka yao na Baraza la Wawakilishi tuna mamlaka yetu. Sasa katika eneo hili Mhe. Spika, na kwa kuwa Mhe. Waziri sasa hivi amewatetea wafanyakazi wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, mimi ningefurahi sana kama kwamba kulikuwa kuna maposho nyeti walikuwa hawapatiwi wamerejeshewa watazidi kufanya kazi. Sasa serikali mnatetea wenu, sisi tushindwe kutetea wetu hiyo imetokea wapi?

Mhe. Mwenyekiti kwa hivyo mimi kitu ambacho ninachokiona, wenzangu wamesema wanasubiri Ofisi ya Utumishi ya Umma, mimi sisubiri huko, Kiongozi na mratibu wa shughuli za serikali yupo hapa na hii bajeti tutakayoipitisha hapa Mhe. Mwenyekiti, hilo fungu tunalolizungumza tumeshalipitisha humu. Sasa leo je Waziri atakuja kukataa bajeti ambayo kaipitisha yeye mwenyewe. Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki kuja kusumbuana na rafiki yangu, mwalimu wangu sahibu wangu Mhe. Haji Omar Kheri. Mimi nitakaa hapa na ninaamini Mhe. Waziri, Ofisi ya Makamu wa Pili hana tatizo na eneo hili, sasa hebu turuhusuni tuendelee nalo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili: Mhe. Mwenyekiti kwa sababu sisi kama alivyosema tunazungumza lugha moja wala hatukuja hapa kuvutana. Lakini kwa sababu kwanza mimi nikatae kwamba serikali inaingilia shughuli za Baraza la Wawakilishi, serikali inaheshimu sana shughuli za Baraza la Wawakilishi. Lakini kila jambo linaendeshwa kwa sheria na ndio maana tukasema kwa huu utendaji tulionao sasa wa Baraza basi tunahitaji kufanya marekebisho ya sheria ya Baraza lenyewe. Na wakati nafanya majumuisho hapa tulisema kabisa kwamba serikali haina tatizo kuwa na sheria ya utawala ya Baraza. Kilichotokea tukasema ili kuwe na sheria nzuri basi tujifunze kutoka mabunge mengine ya nchi mbali mbali na Mhe. Hamza anaijua hatua ambayo tunaendelea nayo.

Sasa kwa kuwa yote hayo tunayafanya kwa sababu hatutaki tuingilie uhuru wa Baraza la Wawakilishi. Lakini kwenye suala la uratibu sisi kazi yetu ni kuratibu hatukatai kuratibu, hata siku moja hatujakataa kuratibu. Lakini mambo ya mishahara maposho yapo kwenye eneo la fungu la Baraza la Wawakilishi, hapa hatujazungumzia hata siku moja Mwakilishi wa Baraza kwenye fungu zima hili. Mhe. Mwenyekiti ikiwa tutazungumza hapa itakuwa kidogo tumeonewa. Kwa sababu utaratibu hapa ukitafuta katika vifungu vyote hivi vinasema kuratibu na sisi hatukatai kuratibu. Na fedha zitakazoingiliwa za Baraza tumuulize Katibu hapa kama ipo siku Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imetumia hata shilingi moja ya Baraza au na uwezo wa kugusa moja kwa moja kwenye *account* yao. Kwa hivyo tukigusa hapo kwenye Uratibu ni kama kwamba kwa kweli tutakuwa hatukutendea haki Idara hii Mhe. Mwenyekiti. Naomba tukifika kwenye fungu la Baraza lizungumzwe.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti mimi nadhani Mhe. Waziri katetea tu Idara yake ya Uratibu lakini hakutetea ile hoja yangu. Sasa mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti ili hili suala tusilifanye likawa kubwa kwa sababu kuna idara au kuna taasisi mbele ya serikali ambayo inaingilia muhimili huu ambao tayari umeshafanya maamuzi yake. Sasa kama serikali ndio inaratibu, kwa sababu kama Idara hii ndio inaratibu shughuli zote za Wizara. Kwa hivyo ina maana kama kuna Wizara inaingilia mamlaka basi hapa ilikuwa awaambie msiingilie mamlaka ya Baraza hasa yaliyokwishaamuliwa.

Sasa kwa sababu Mheshimiwa unajua tatizo unaogopa kuja kupigwa kiguu cha nyuma nikaja nikasubiri kwenye fungu la Baraza kwa sababu nitaulizwa hapa tatizo lako liko wapi fungu gani hulitaki? Mafungu yote ninayataka na nimeyapitisha. Sasa huku katika uratibu, uratibu maana yake Mhe. Makamu wa Pili wa Rais mimi Mhe. Mwenyekiti, huwa ninamuona Mhe. Waziri Mkuu kule Pinda akiona kuna Wizara inaleta tabu kidogo huingilia kati akawaambia bwana Waziri hebu usiingilie mamlaka ya mwenzako. Sasa mimi nadhani basi mimi sitaki kumsimamisha Balozi lakini alau Mhe. Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais amwambie basi Waziri mwenzake usiingilie mamlaka yangu, mimi nafikiri hapo tutaelewana lakini bila ya hivyo Mhe. Mwenyekiti nikija nikizuia fungu la Baraza la Wawakilishi nitakuwa sikuridhika nalo, kitu ambacho si sahihi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti mimi huridhika sana na maelezo ya Mhe. Hamza kwa sababu ni mwenzangu tumetoka mbali tunazungumza mengi na Kiswahili chetu tunaelewana. Na pindipo ikitokea aina yoyote ile ya kuingiliwa kwenye mamlaka yangu kwenye Wizara yangu basi mwenzangu nitamnong'oneza nitamwambia hapa umepita nje ya mstari. Kwa hivyo pale itakapotokea hivyo nitafanya hivyo. Lakini nataka nimuhakikishie Mhe. Hamza kwamba hoja zake tumezisikia, tutazifuatilia lakini kwa hapa si mahala muafaka pa kupazuia, ninachomuomba kwamba maneno haya yamesikilikana, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ameyasikia, Ofisi yetu imesikia basi tuendelee basi akijua kwamba jambo hili mimi na yeye tunalifahamu kwa kina na sote tuna imani na watumishi wa Baraza letu la Wawakilishi, tungependa kila haki yao waipate lakini kwa utaratibu mzuri wa kisheria na kanuni zilizopo ili kila mmoja aweze kuridhika. Hata mimi ni sehemu yangu Mhe. Mwenyekiti siku zote ningependa wafanyakazi wa Baraza wapate maslahi yao sawa sawa, kwa sababu ni sehemu ambayo inanigusa kwa njia moja au nyengine. Kwanza tunakutana kila asubuhi hapa lakini tunafanya kazi pamoja. Kwa hivyo nisingependa hata kidogo iwe kuna mtetezi mwengine zaidi ya mimi kwa wafanyakazi wa Baraza. Kwa hivyo mimi naomba Mwenyekiti na Mhe. Hamza aturuhusu tuendelee tukiamini kwa pamoja tunashirikiana haki za wafanyakazi wetu zipatikane.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi ninafikiri tuendelee na hatua tulizojipangia kuhusu *research* yetu ambayo tutakaa pamoja na hatimae nakumbuka hata kwenye kamati zetu za uongozi tulikubaliana kwamba suala la marekebisho linaweza likafanywa ama kwa mswada wa Mjumbe au serikali ikawasilisha mswada huo. Kwa hivyo tukusanye yale tuliyoyasoma halafu baadae nini tunaweza tukafanya na kuuboresha mswada ambao uko mbele ya meza yetu. Hapa mimi nadhani tuendelee.

Kifungu 1901

Mhe. Ussi Jecha Simai: Mhe. Mwenyekiti nilipokuwa nikichangia hotuba hii au bajeti hii nilikumbushia juu ya ahadi 3 ambazo zilitolewa kwa nyakati tofauti katika Jimbo langu ahadi za viongozi wakuu wa Kitaifa. Kuna ya mwaka 2008 ambayo ilitolewa na Rais mstaafu Mhe. Dr. Karume lakini ahadi nyengine katika uchimbaji wa kisima Moga na kuna ahadi mwaka 2010 ilitolewa na Dr. Shein Rais wa Zanzibar na ahadi nyengine ilitolewa Kinyasini na Mhe. Dr. Shein. Nilitaka kupata maelezo lini ahadi hizo zitatekelezwa ili wananchi wangu wajue kwamba serikali yao haiwadanganyi.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili Rais: Mhe. Mwenyekiti ni kweli kiongozi wetu hutoa ahadi na kwa nia njema kabisa ya kushughulikia matatizo ya wananchi ili wananchi waweze kupata sulhu ya matatizo mbali mbali yanayojitokeza katika maeneo yao. Ni kweli kabisa kuna ahadi ya Mhe. Rais wetu katika maeneo ambayo Mheshimiwa ameeleza lakini napenda nimuhakikishie kwamba kipindi cha utawala wa Mhe. Shein ni miaka 5 na katika mtu mmoja mkweli, muungwana anayetekeleza ahadi zake ni Dr. Shein, sisi wajibu wetu tutamkumbusha kuhusu jambo hili na vile vile sekta zinazohusika tutazikumbushia ili utekelezaji uende vizuri na matatizo haya yasitokee.

Na kuhusu ahadi ya Mhe. Karume tutafuatilia ili serikali ni endelevu yeye ni Rais mstaafu kwa vyovyote akitoa ahadi hizo ametoa kama Rais tutafuatilia ili tuone namna gani tutapata ufumbuzi wa tatizo hili. Naomba kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba jambo lolote ambalo Marais wetu wameyatolea ahadi yatatekelezwa, atupe muda tuyatekeleze kwa wasaa.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Mhe. Spika, tangu niwe Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi hii ni bajeti ya tatu yaani ni bajeti ya tatu hii hapa sasa hivi. Na kila siku ninapouliza swali hili naambiwa bajeti ijayo, bajeti ijayo. Kwa hesabu niliyonayo tumebakisha bajeti mbili kabla kumalizika muhula huu tulionao.

Mhe. Mwenyekiti mimi ningelimuomba Mhe. Waziri anambie basi angalau ahadi moja kati ya ahadi 3 zile pale lini zitatekelezwa katika Jimbo langu kwa sababu wananchi wangu wanapata shida sana katika suala la maji na sina njia hiyo. Fedha ambazo ninazipata kupitia mfuko wa Jimbo hazitoshelezi kabisa kuchimba kisima. Kwa hivyo nakuomba Mhe. unijulishe angalau ahadi moja katika hizi lini nitatekelezewa na serikali?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mheshimiwa kwa kuwa kuna mradi mkubwa wa uchimbaji wa visima vya maji na hivi karibuni ndugu zetu wa *Ras el khaima* wametuongezea visima vingine vipya karibu 50. Kwa hivyo ningemuomba Mheshimiwa nisimpe ahadi lini lakini iwe katika maeneo ya mpango wa utekelezaji basi na eneo la Moga nitazungumza na Mhe. Waziri aone uwezekano wa namna gani ahadi hii inatekelezwa. Kwa kuwa ni kauli ya Rais na sisi tungependa kabisa kabisa kuweka heshima ya Rais wetu, na kama nilivyosema Rais wetu huyu hana jambo hata moja analolisema akawa halikumbuki anajua. Kwa hivyo nataka nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba utekelezaji utafanyika na kama nilivyosema awali kwa kuwa kipindi cha Mhe. Rais ni miaka 5 basi uone na ustahamili katika miradi inayoendelea tutakaa na wenzetu wa Wizara husika inayosimamia mambo ya maji kulitafutia ufumbuzi tatizo hili. Mhe. Mwenyekiti naomba kueleza hayo.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Mheshimiwa tuendelee.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti ninayo ya mafungu lakini kwa sababu ya umuhimu wa sera na mafunzo kwa Idara hii ninamuachia atatafuta mengine atizame mambo mengine nitampa pembeni. Lakini ninachotaka kumwambia moja ya sera katika Idara ya Uratibu nilizungumzia sana masuala ya Muungano, na mimi tofauti na wenzangu mimi sikuingia katika rasimu, lakini badala yake nilizungumzia utaratibu mzima wa suala zima hili la namna ya kufikia kupata muafaka wa kitaifa juu ya hatma ya muungano na haki zetu.

Sasa mimi nilizungumzia suala moja Mhe. Mwenyekiti, suala la jinsi gani kuhakikisha haki za Zanzibar zinalindwa katika utaratibu huu tunaoufuata hatimae kufika huko tunakotaka kufika. Na nilizungumzia kwamba kuna rasimu ya sheria ya kura ya maoni yaani *referendum act* ya mwaka 2013 ambayo tulipata taarifa na najua hata kamati inayohusika imeambiwa hivyo kwamba upande wa Zanzibar hasa imetoa taarifa kwenye Tume ya Uchaguzi kwamba haikuwa imeshirikishwa ipasavyo. Sasa Mhe. Waziri alipokuwa akijibu hoja hapa katwambia kwamba wala kosa si la Tume ya Taifa ya Uchaguzi mimi nakubaliana nae, lakini yeye kasema kwamba waliohusika hasa walipaswa kuwa ni Tume ya Mabadiliko ya Katiba mimi hata hilo sina hakika nalo Mhe. Mwenyekiti kwamba ni Tume ya Mabadiliko ya Katiba,

kwamba ni Tume ya Mabadiliko ya Katiba ama ni serikali ya Jamhuri ya Muungano kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Sasa Mhe. Mwenyekiti, rasimu niliyonayo mimi ni ya Mswada wa Sheria ya kura ya maoni *the referendum act* ya 2013. Katika *draft* inaonekana aliyeitangaza ni bwana mmoja anaitwa Ombeni Sefue, *Sectretary to the Cabinet* Katibu Mkuu Kiongozi wa Jamhuri ya Muungano.

Sasa nataka anieleze na nihakikishiwe tu na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa sababu wale wanasimamia uratibu, kwamba mimi ningependelea mambo haya yote kwa sababu hapa Mhe. Mwenyekiti hata sisi hatuwezi kujua mambo kama itavyokuwa inajua Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wetu wa Zanzibar, sasa nilitaka nipewe kauli tu kwamba je, wamerekebisha watwambie haya yamefanyiwa kazi? Na kwamba je wameweka indhari hiyo kwamba kuanzia sasa halitapokea chochote wala hatutokubali chochote ambacho Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wetu haikushirikishwa katika kuandaa rasimu hizo? Kujiridhisha tuone kwamba haki za Zanzibar zimelindwa. Kwa sababu hofu moja Mhe. Mwenyekiti ni kwamba mna mambo humu yalimo sasa yanakwenda kinyume hata yale ya sheria na mabadiliko ya katiba ambayo kuipata mpaka kupata muafaka imekuwa kazi kubwa sana.

Sasa nilikuwa nataka kauli ya Waziri kwamba hili limezungumzwa na limefikia wapi tusizungumze tu kwamba lawama Tume ya Mabadiliko ya Katiba ama ni ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi ni suala zima la haki zetu za Zanzibar je, Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar imeshirikishwa? Inatambua rasimu hii iliyoletwa? Imejiridhisha, inatambua kwamba haki zetu zimelindwa? Nilikuwa nataka kauli hiyo Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, mimi wakati wowote huwa mkweli katika kueleza mambo haya yanayohusu nchi yetu. Hili moja katika tatizo kwa sababu tatizo hili wenzetu hawakutuarifu rasmi kwa upande wa Jamhuri ya Muungano. Na sisi tulilipata wakati kamati ilipokutana na Wizara yetu ndio kamati walitueleza kwamba watumishi wa ZEC waliwalalamikia wao kwamba hizi taarifa hawakuelezwa mapema. Lakini vile vile na watendaji wetu hawakuchukua hatua ya kututaarifu mara zilipokuja hizo taarifa. Na ndio maana tukawa jambo hili ndani ya serikali hawakulitambua rasmi.

Lakini juzi baada ya kuwasiliana na Tume yetu ya Uchaguzi Zanzibar na baada ya mualiko uliokuja rasmi wa NEC kwenda kukaa nao pamoja na wenzao ZEC na maelezo niliyoyapata ya hawa ambao kesho tutapata kuonana rasmi na Mkurugenzi wa Tume, alinieleza kwamba wamefikia mahala pazuri na sasa baada ya kwisha kukubaliana kati ya wao ZEC na NEC jambo hili litazungumzwa kiserikali na walitegemea kwamba hiyo rasimu tutaletewa na

sisi Zanzibar kama kutakuwa na mabadiliko yoyote, tutaweza kuichangia na kuifanyia mabadiliko kama tunahitaji kufanya hivyo. Lakini wenzetu wa ZEC kwa sasa wameridhika na hatua iliyofikia. Na kwa sababu bado hawajatukabidhi rasmi siwezi kuzungumza lolote na kumtaarifu Mwanasheria Mkuu mpaka tutapopata hayo mazungumzo rasmi kesho kutokana na Mkurugenzi wa Tume halafu tutamuwasilishia Mwanasheria Mkuu na hizo hatua tukizipata kwa undani zaidi ndio tutaweza kulitolea ufafanuzi wa kutosha.

Kwa leo niseme hayo tu ambayo ndio naweza kueleza Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti kwanza ninamshukuru sana Mhe. Mohammed Aboud Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kama alivyosema kakubali kuwa muwazi na ninamuomba aendelee kwa sababu mambo haya yanaingia katika historia Mheshimiwa. Unaweza ukalifumbia jicho jambo hapa kwa utaratibu wa kutaka kustiristiri mambo kesho historia ikaja ikatuhukumu vibaya sana. Kwa hivyo ninamshukuru sana kwa hilo. Na ninafurahi hii hatua iliyofikiwa. Naiomba tu serikali itizame kwa makini kwa sababu kama nilivyosema sheria ya mabadiliko ya katiba iliweka utaratibu hata namna ya uendeshaji wa kura ya maoni juu ya Katiba hii. Sheria hii imeweka utaratibu sasa wa kuendesha kura ya maoni ile moja katika *schedule* nyongeza yake. Kwa hivyo ni muhimu sana kujiridhisha kwa sababu kuna vifungu ambavyo vimo katika mswada huu au rasimu hii inapingana na sheria ya mabadiliko ya Katiba na mara nyengine vifungu vilivyomo kwenye mswada na vilivyomo katika nyongeza vinapingana vile vile rasimu moja ya mswada. Na hapa pana suala la hatma ya nchi yetu. Kwa hivyo inapokea maneno mazuri ni matumaini yangu kwamba serikali ya Mapinduzi Zanzibar tuna imani nayo tunaamini viongozi wake, tunamuamini Mwanasheria Mkuu wetu wataipitia kwa kina kuridhika kwamba haki za Zanzibar zitalindwa.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti naomba tuendelee. Ahsante.

Kifungu 1901		Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ	397,530,000
Kifungu 2001	-	Idara ya Maafa	262,528,000
Jumla ya Fungu			**5,929,000.000**

FUNGU 16 BARAZA LA WAWAKILISHI

Kifungu 0201	-	Utawala Unguja

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa ninatoa mchango wangu nilimuomba Mhe. Waziri, aje atusaidie hapa namna ya utaratibu wa michango yetu tunayoichangia kwa maandishi ni namna gani inawekwa kumbukumbu zake kwenye *hansard* nilimuuliza hilo lakini sikupata majibu, hebu naomba Mhe. Waziri, kama una ufafanuzi katika hili utusaidie.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli, Mhe. Mtando aliniuliza suali hilo na kwa sababu makaratasi yalikuwa mengi na muda pale ulikuwa umeshakuwa juu kwa hivyo naomba radhi sana. Ni kweli Mhe. Mwakilishi, alitaka kujua kwamba namna gani hii michango ya maandishi inavyoweza kuwekwa katika *hansard* zetu. Na ni kweli tumefanya makosa, inaonekana hatukuiratibu sawa sawa suala hili la *hansard* za maandishi. Lakini kwa sasa tutaweka utaratibu, itabidi tutoe kopi, sisi tuna wajibu kwa upande wa Serikali na ile *original* tuweze kuikabidhi kwa Katibu wa Baraza ili hii yote michango ya maandishi iweze kuwemo katika *hansard*, na kule Bungeni wanafanya hivyo. Kwa hiyo na sisi tunaweza kufanya hivyo. Kwa hivyo Mhe. Mbarouk naomba radhi lakini tutaweka utaratibu kwa kushirikiana na Ofisi ya Baraza ili kuwepo na *hansard* kwa hoja ambazo zitatolewa kwa maandishi.

Na hapa ningependa Mhe, Mwenyekiti, nitoe wito kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza kwa sababu wengine huandika naunga mkono hoja na kusaini tu hawaelezi vizuri, kwa hivyo wajue itajitokeza namna hiyo hiyo tu katika *hansard*, basi baada ya maelezo hayo Mhe. Mbarouk nakushukuru kwa kunikumbusha na nakuomba radhi sana.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakubaliana na maelezo ya Mhe. Waziri, tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 0201	Utawala Unguja	12,189,864,000/=
Kifungu 0301	Ofisi Kuu Pemba	2,662,136,000/=
Jumla ya Fungu		**14,852,000,000/=**

FUNGU 30 - TUME YA UCHAGUZI - ZANZIBAR

Kifungu 0201 - Utawala Unguja

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, hapa pana hadithi ya ajabu kidogo, ninaomba nitenguliwe kitendawili hichi kwa Waziri mwenye dhamana ya utawala. Kwenye *vote* 2111000, mishahara ya fedha taslimu. Katika kifungu kidogo 211101 mishahara na waajiriwa wa kudumu wa Serikali *civil servants* pana 179,045,800/=, lakini kwenye 211110 posho

maalumu inaambatana hapo hapo imekuwa *copy and paste* vile vile 179,045,800/= nataka kabla sijampa mji anitegulie kitendawili Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa na sisi ni binaadamu si kwamba yote haya tunaweza kuyaona, na nadhani mwenzangu Mhe. Jussa naamini ameliona hivi sasa hivi, kama angeliona mapema angepata nafasi ya kuniambia mapema tukalifuatilia na kutoa taarifa vizuri. Kwa sababu ya hali ilivyo namuomba Mhe. Jussa, anipe muda niendelee kulifuatilia wakati tunaendelea na vifungu vyengine naamini nitampa majibu vizuri baadae, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, sina maelezo ya ziada hivi sasa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza ninaomba nihitilafiane na kaka yangu sikuliona sasa hivi, kama atakumbuka nimwambie tu, mimi huwa na kawaida ya kupitia mafungu haya kabla hata sijatoa mchango wangu hupitia kabisa mafungu haya, lakini ninakumbuka nilimwambia kwamba kwa sababu ni mengi nikiyachambua moja moja katika mchango sitachangia hotuba yake, kwa hivyo nilimwambia ajitayarishe kwa yote ambayo aliyasimamia yeye na nilitaja lakini nilimsaidia kumtajia kwamba hasa vifungu vya posho maalumu, vya viburudishaji. Kwa hivyo sijaibua kipya ambacho sikukitaja. Kwa hivyo ninataka nimuhakikishie kwamba nimekiona, na kwa kumsaidia nimwambie afungue na Pemba kuna tafauti nafikiri ya milioni mbili kama sikosei, lakini kuna hali hiyo hiyo kwamba hapa pana kitu cha ajabu katika Tume ya Uchaguzi, hatujafika lakini natoa mlinganisho kwa sababu nikifika nisisimame tena, kwa sababu amesema atafuatilia mwenyewe, lakini utakuta kuna 63,000,000/=, na posho maalum 65,000,000/= kwa Pemba, yaani posho maalumu limezidiwa na mishahara kwa 2,00,000/= kwa Pemba.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, nataka kumwambia tu Mhe. Waziri, hapa kwamba ni ajabu hasa na hasa katika lile fungu la Utawala wa Unguja kwamba mishahara ya Tume ya Uchaguzi na posho maalumu maana utakuta nambari kwa nambari imekopiwa vile vile imewekwa inaleta masuali mengi sana, na mimi nina shaka moja tu kwamba tukimuachia ndio tutakuwa tumepitisha hapa, sasa sisi tutajiridhisha vipi kama kupitia katika Kamati, kama kupitia *PAC* watajuilishwa mimi sina tatizo, lakini nasema hii imenipa mashaka makubwa sana, na katika vyombo hivi Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo ya ajabu ajabu sana katika mahesabu, kama ilivyokuwa katika Tume ya Ukimwi, ikifika wakati na hatujapata habari yao nao lakini kwa jumla kuna mambo mengi Mhe. Mwenyekiti katika mambo haya na hili ni mfano dhahiri kwa jinsi gani fedha zinavyobandikwa bandikwa nambari tu lakini hazioani katika matumizi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo namridhia Mhe. Waziri wa Nchi, najua na yeye kama alivyosema kawa mkweli tuendelee lakini naomba afuatilie na Kamati mbili ya Sekta, Kamati ya Viongozi wa Kitaifa na Mahesabu ya Serikali PAC afuatilie katika masuala haya, Ahsante sana.

Kifungu 0201	Utawala wa Unguja	799,700,000/=
kifungu 0301	Ofisi Kuu Pemba	187,003,000/=
Jumla ya Fungu		**987,000,000/=**

FUNGU 05 - AFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS

Kifungu 0801	Idara ya Upigaji chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali	2,500,000,000/=
kifungu 1901	Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ	

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nikiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti, pamoja na kwamba nilikuwepo safarini China, lakini namshukuru sana Mhe. Makamo wangu Mwenyekiti Mhe. Salmin Awadh Salmin, nilimuuliza jinsi mulivyoipitia bajeti ya Serikali kama Kamati ya Wenyeviti na akanipa maelezo ya kutosha. Lakini leo nilipokuja kuangalia fungu maelezo ambayo yaliyopitishwa katika Kamati ya Wenyeviti, ni tafauti na yaliyoandikwa katika kitabu chako cha bajeti. Sasa fungu kwenye kitabu changu limefutika lakini kinasomeka 730003 miradi midogo midogo ya wananchi, huo ndio uhai wa wananchi wetu huko Majimboni.

Mhe. Mwenyekiti, bajeti ya mwaka huu ilikuwa 760,000,000/=, na 750,000,000/= ni fedha ambazo moja moja zitakwenda kuwahudumia wananchi kutatua matatizo madogo madogo, sasa Kamati ya Wenyeviti, iliomba kutokana na matatizo mbali mbali ya majimboni kwetu fedha hizi bado zinakuwa kidogo na mahitaji ya wananchi yanakuwa ni mengi, sasa Kamati ya Wenyeviti, ilimuomba Mhe. Waziri anayeshughulikia masuala ya fedha na uchumi kuongeza fungu hili kutoka 15,000,000/= kuja 20,000,000/= ambapo tulitegemea ingekuja karibu 1,000,000,000/=, lakini leo naona fungu hili limejirudia tena, sasa je, ile ahadi ya Waheshimiwa Wenyeviti, ile hoja yao Serikali haikuzingatia, na kama imezingatia basi mimi nafikiri hapa kunahitajika marekebisho. Mhe. Mwenyekiti, naomba ufafanuzi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, hoja ya Mhe. Hamza, Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti, ni ya msingi kabisa na mimi kama ni Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha wala siipingi hoja yake kwa sababu ninajua kwamba fedha hizi zinakwenda kuwasaidia wananchi wetu katika maeneo yetu, wala sipingi. Kinachotukwaza ni kwamba muda ambao aliouzungumza na hali ya mapato

kama utakumbuka bajeti yangu nilieleza kiwango cha fedha ambacho ni nakisi na nikasema kwamba kiwango kile kinatakiwa kizibwe kwa utaratibu ambao nimeueleza kwenye bajeti. Suala hili namuomba Mhe. Hamza pamoja na Waheshimiwa Wawakilishi watuachie, tulizingatie katika bajeti ya mwakani nadhani Mungu akitujaalia uhai na uzima sote tutakuwepo hapa bado tunaendelea tukiwa hai tutalizingatia na ataona matunda yake *inshallah* na wala asitaharuki, bajeti ya mwakani atustahamilie.

UTARATIBU

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, najua Mhe. Mwenyekiti, unapoambiwa jambo kuliwasilisha kama lilivyo wakati mwengine linakuwa na shida kidogo, unaweza kuwasilisha vyengine. Nilimwabia Mwenyekiti wangu kwamba tulipokaa kwenye Kamati ya Wenyeviti, fungu hili tulipitisha 1,000,000,000/= sio 760,000,000/=, sasa kama kulikuwa na mabadiliko basi Mhe. Waziri wa Fedha alikuwa arudi kwenye Kamati ya Wenyeviti, na sio kama tumeomba, tokea mwanzo hili lili-*appear* fedha hizo 1,000,000,000/= na tukahisi kwamba ile ahadi ya Mhe. Rais ya kusema kila mwaka ataongeza 5,000,000/= tukaona imetimia. Sasa tumekuja kushangaa kuona kwamba kwenye fungu halisi limejitokeza hili, sio kwamba tuliomba ni bajeti ambayo ilikuja kwenye Kamati ya Wenyeviti na tumeiona na tumekubaliana nayo, lakini imekuja kubadilika kwenye maeneo haya. Kwa hiyo huo ndio uhalisia wenyewe kwamba tokea mwanzo na ndio tumeipitisha hiyo kwenye Kamati ya Wenyeviti, hivyo tumetegemea kwa kuwa tumeshaipitia kwenye Kamati ya Wenyeviti, tukasema *ok* iende na hapa ingejitokeza kama hivyo ilivyo, lakini kinyume chake imepunguzwa.

Mhe. Mwenyekiti, hata ukiangalia jina lenyewe pia limebadilishwa kwa sababu sisi hatuchukui fedha kutokana na miradi midogo midogo ya wananchi, hata jina hili linaonekana limebadilishwa, kifungu sio hichi cha miradi midogo midogo ya wananchi, hili limekuja kwa jina la CDF, kwa hivyo Mhe. Waziri wa Fedha, akubali kwamba fedha zilizoletwa tuliopitia kwenye Kamati ya Wenyeviti ni 1,000,000,000/= ambapo kila Jimbo litapata 20,000,000/= katika bajeti hii, ndivyo tulivyopitisha. Sasa kama anakuja kutuomba baadae ilikuwa arudi kwenye Kamati ya Wenyeviti atuambie kwamba kutokana na hali iko hivi na hivi, sisi tunatetea kile tulichokuwa tumekipitisha. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli ninamuheshimu sana Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Fedha, kikao ambacho mimi nilikuwepo na *notes* zangu huwa sizitupi, nina *notes* za mwaka jana za bajeti na mwaka juzi za bajeti, sikumbuki kupitisha 1,000,000,000/= nina *notes* zangu sikumbuki kupitisha

1,000,000,000/= inawezekana ame- *quote* kitu sicho, nilichokipitisha ni 760,000,000/= lakini hapa inawezekana kwamba hili jina tulibadilishe kwa sababu ya kubadilika kwa sheria, inawezekana Mwenyekiti wangu ame-*quote* kitu tafauti na *notes* zangu ninazo, na Mhe. Mwenyekiti naweza nikakukabidhi kesho ukaziona, inawezekana ka-*quote* kitu tafauti.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, nadhani tufike pahala tuelewane kama *notes* anazo na sisi tunazo, tutakwenda kuangalia kama ni 760,000,000/= akubali kwamba zitabakia 760,000,000/= lakini pia akubali kwamba ikiwa kwenye *notes* zetu zime-*appear* 1,000,000,000/= basi akubali tunapitisha fedha hizo, kwa sababu na mimi *notes* pia ninazo zote.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza maelezo zaidi sina, mimi ninachokikumbuka ni fedha hizo 760,000,000/= ndio maelezo yangu, na wala sina uwezo wa kupunguza hizi. Tulipokuwa tunazungumza na kupitisha hivi vitabu vilikuwa tayari viko kwenye *draft form*, hichi kitabu hakikutengenezwa upya kilikuwa kwenye *draft form* tayari, wala mimi sina uwezo wa kuvipunguza wakati ishachapishwa. Sasa sijui kama ame-*quote figure* ambayo siyo.

Mhe. Mwenyekiti: nafikiri cha kufanya ni tu-*cross check* kwa pande zote mbili tuone hii itafikia wapi, lakini kwa hapa hatuna suala la kusema tufanye nini, tu- *cross check* ili tuhakikishe ukweli ni vipi, lakini kilichopo itabidi tukipitishe, maana kuna fungu kuu hapa, sasa kama hatukupitisha maana yake hili pia tutakuwa hatuwezi tukapitisha, lakini tu-*cross check.*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, amejaribu kutumia busara zake na akatuahidi basi mwakani tutafurahi, sasa kwa kuwa Wenyeviti wangu katika *notes* zao na kwa bahati nzuri wenyeviti wangu wapo saba, kwa hiyo *notes* saba zimeandika bilioni moja moja, sasa Mhe. Waziri *note book* yake ni moja, kwa hivyo ina maana tukirudi tena kwenye hoja ina maana sisi tutamshinda, sasa kutumia busara na mimi naamini Serikali yetu na tunamshukuru sana Mhe. Rais tulimuomba akaanza kutupa mwaka jana milioni kumi, na mwaka huu anatukatia milioni kumi na tano. Kwa hivyo basi tunaomba hiyo mwakani Mhe. Waziri, ninaomba ukubali deni, kwamba baada ya ile kuongeza ishirini ije ishirini na tano, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, kama si fedha hizi za miradi midogo midogo Mhe. Mwenyekiti, Ramadhani kusingekalika mitaani kwetu, magari ya maji Serikali hawana ya kutosha lakini tunajitahidi kuchimba visima usiku na mchana, pamoja na hivyo vitakavyokuja kuchimbwa na Serikali, basi na vyetu sisi tutaendelea kuchimba kwa fedha hizi hizi.

Mhe. Mwenyekiti, fedha hizi tumefanya utafiti kwa kutafuta fedha hizi ni mimi na wewe, tulikwenda Kenya. Kenya wenzetu Mhe. Spika, sisi leo tunabuburushana kwa milioni kumi na tano kwa mwaka, Kenya wenzetu milioni ishirini na tano za Kenya kwa mwezi, milioni ishirini na tano za Kenya, ukifanya mahesabu si chini ya milioni hamsini au arubaini na tano kwa mwezi, na tumeona miradi chungu nzima ambayo imefanywa na Wabunge wa Kenya kupitia fedha hizi za mfuko wa maendeleo. Sasa mimi naomba Mhe. Waziri mimi najua ni mtu msikivu na ana nia njema sana, naamini na sisi tutajitahidi kuendelea kumuonesha yale maeneo ambayo fedha zinavuja ili zijae, ili hiyo mwakani aje atufanyie hiyo *double*. Mhe. Mwenyekiti tuendelee.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Hamza, Mhe. Salmin, wote hao ni wenzangu, na mimi kazi yangu ni kutafuta fedha kwa ajili ya nchi yetu wala sina ubakhili wala sina khiyana. Lakini nataka nimwambie Mhe. Hamza na Waheshimiwa Wawakilishi wengine ni kwamba tukianza kulinganisha Kenya na kwetu ukubwa wa majimbo nayo tuulinganishe. Tanzania Bara tu kuna baadhi ya majimbo wanapata milioni mia na kitu, lakini kwa kwetu sisi Zanzibar huko huko Bungeni wanapata shilingi milioni ishirini na nne ishirini na tano, mimi nilikuwepo kule Bungeni kuna baadhi ya majimbo wanapata mia na *CDF* zao na sisi hapa tunapewa milioni ishirini. Sikatai hali yetu ya uchumi kila itakapokuwa tutaangalia maslahi ya watu wetu na tutaangalia maslahi ya majimbo yetu. Mimi nakubaliana sana na Mhe. Hamza na Waheshimiwa wengine wote tuwe tunauangalia uchumi wetu, hali ya uchumi ikiwa nzuri nadhani Mhe. Makamu wa Pili wa Rais yupo hapa, Mhe. Spika, wewe mwenyewe upo hapa, nitamshauri Mhe. Rais mimi napata maelekezo tu. Lakini kuji-*commit* hapa kwangu mimi nadhani mwakani tuje tuangalie angalau milioni ishirini badala ya ishirini na tano. Lakini tukifanya uzuri na uchumi ukiinuka nadhani Mhe. Spika, na Makamu wa Pili ni watu wazuri tu mshaurini Rais mimi nipewe maelekezo tu nipewe *cheque* basi sina ziada.

kifungu 1901 - Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ 840,000,000/=
kifungu 2021

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nilipochangia nilimtanabahisha Mhe. Waziri kwamba katika kitabu chake cha bajeti ukurasa wa 59 ya hotuba yake, vile viwango ambavyo alituomba tumuidhinishie havilingani na viwango ambavyo vipo katika buku hili la makadirio ya mapato na matumizi. Katika majumuisho yake nafurahi kwamba kakiri kwamba kuna hitilafu hiyo ambayo amesema imesababishwa na mabadiliko ya siku za mwishoni. Sasa nilikuwa nataka maelezo tu kwanza moja tunapitisha 340,000,000/= zilizomo katika buku hili ama tunapitisha

779,500,000/= zilizomo ndani ya kitabu. Lakini mbali ya kutaka maelezo hayo juu ya fungu lipi linasimama, pia nilimwambia na akanipa maelezo ya jumla kwamba uzoefu wetu katika maafa mawili makubwa yaliyotokea ya ajali za meli, inaonesha kajikita zaidi katika kufanya semina na warsha na sera na makongamano, lakini hivi vifaa hasa vya kufanyia kazi za uokozi katika maafa hatuna, na tukatoa mfano vikosi vyetu vya SMZ vilijitahidi sana siku ile pale na vifaa vilikuwa hakuna. Sasa nilikuwa nataka kujua kwamba haya mafungu haya hizi za wafadhili na hiyo michango ya Serikali zinakwenda kufanya shughuli gani?

Mhe. Mwenyekiti, lakini la pili ninaendelea kukumbusha kwamba tunapitisha zipi katika fungu la matumizi tunapitisha 779,500,000/= zilizomo humu au tunapitisha 340,000,000/= ambazo zimo katika kitabu hichi na kama tunapitisha zilizokuwemo humu zinaingiaje baadaye katika buku hili la matumizi. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze hili la kwa nini ni semina na zisiwe ni vifaa. Hii hasa inatokana na utaratibu wenyewe unaoanzia kwa mle ambamo tunaomba zile fedha. Kwa kuwa washauri wetu waelekezi hawa kuna maeneo inabidi wafanye hizo semina na hizo fedha zinazotolewa zinatolewa *specific* kwa ajili ya kufanyia hizo shughuli za ushauri, na katika huo ushauri mnakuwemo hizo semina na kupata michango. Ndio maana ukakuta suala sana linajitokeza kwenye semina, na kwamba tulivyosema hawa washauri ndio wanakuja sasa kututengenezea tathmini na kutuwekea utaratibu wa mahitaji tunayohitaji kwa ajili ya sasa kwenda kwa wafadhili na marafiki zetu ili kuwaambia mahitaji yetu ni haya, kwa hiyo tuko kwenye *process* ya kufikia huko kwenye vifaa kwa maana ya kuwa na *document* halisi ndio *process* yake inapita hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia katika mikutano mbali mbali hii ya kimataifa inayohusu mambo ya maafa yako hayo mambo maalum ambayo yanatutaka kutoa elimu kwa kupitia hizo semina na makongamano. Kwa hiyo hawa wanaosaidia elimu tunaomba fedha hizo misingi hiyo. Lakini sasa kuhusu kwa nini fedha hapa kipo kiwango hichi na hakipo kile kiwango kamili. Niseme tena kwamba kwa maana hiyo tukubaliane tuipitishe kwa kiwango kilichopo kwenye hili buku la mapato na matumizi wakati huo huo taarifa Wajumbe ikishawafikia tuendelee kuwafuata wenzetu wa *UNDP* na watakapotupa mchango wao itakuwa ni msaada kwetu kwa kufanyia shughuli zetu zinazohusiana na maafa na hizo zitakuwa sasa tumesaidiwa kwa sababu jambo la kusaidiwa ni vizuri tukalitaarifu Baraza, lakini kwa kuwa sasa hawakuwahi kutuletea taarifa hizi mapema iwezekanavyo msingi wangu ni kwamba fedha zilizokuwa *reported* hapa ni hizi 340,000,000/=, sasa msingi huo tukipitisha kwa 340,000,000/= sisi tutaendelea na mazungumzo na

wenzetu wa *UNDP* tutapewa hizo fedha ikubalike tu katika Serikali kwamba kunakuja fedha hizo na Waheshimiwa Wawakilishi waelewe kwamba zitakuja fedha hizo kupitia *UNDP*, lakini hapa tupitishe hichi ambacho kimo kwenye bajeti.

Halidhalika Mhe. Mwenyekiti, hata zile ambazo ziko kwenye Tume ya Uchaguzi, kule ukitizama na Tume ya Uchaguzi utakuta bilioni 3.6 hivi zile zinazotoka *SMT* kwa sababu nazo hawakututaarifu na mapema zikaonekana hapa nazo vile hazimo kwenye bajeti yetu. Kwa hivyo ningeliomba tupitishe kwa mujibu yaliyomo kwenye bajeti na haya maelekezo mengine yatapojitokeza tutataarifu wenzetu wa Wizara ya Fedha na tutawa-*brief* wahusika wengine kwamba zimepatikana fedha hizi kwa ajili ya kazi kadhaa, lakini ni vizuri kuripoti kwa Baraza hili na kuelewa kinachoendelea.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti kwa maelezo hayo kusema hapa tutashughulikia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, tuendelee na hilo la Idara ya Maafa na maelezo yake nimeyapokea lakini nimtahadharishe tena tu kwamba tujitahidi sana, kwa sababu hizi fedha tunaomba sisi na tukiziomba tunaziomba kutokana na mahitaji yetu, sasa isiwe tu kwamba kipaumbele cha watendaji wetu ni semina, warsha na makongamano tu, lakini na yale mengine mimi naamini kabisa tukijenga hoja kama kweli tutahitaji vifaa basi kama wanaweza kutusaidia katika kujenga uwezo, maana huo uwezo tunaojengea Mhe. Mwenyekiti, hautotusaidia kupata vifaa vya kufanyia kazi baadaye. Kwa hivyo, nilikuwa nasema wafanye uwiano mzuri katika maombi yao ya fedha na mie mie naweza pia kujenga hoja vipi katika zile fedha ambazo tushaahidiwa wakaweza kuzitenga baadhi zikatumika kwa kununulia vifaa. Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, tuendelee nangojea Tume ya Uchaguzi ikifika nitayazungumzia huko.

Kifungu 2001	Idara ya Maafa	340,000,000/=
Jumla ya Fungu		**3,680,000,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumzi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 16 - BARAZA LA WAWAKILISHI

Kifungu 0201	Utawala Unguja	697,536,000/=
Jumla ya Fungu		**697,536,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumzi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 39 - TUME YA UCHAGUZI ZANZIBAR

Kifungu 0201 Utawala Unguja

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa jumla hapa kidogo nataka ufafanuzi. Kwenye kitabu cha bajeti ambacho Mhe. Waziri alikisoma kuna fedha ambazo zimetengwa shilingi 80,000,000 kwa ajili ya mapitio ya majimbo, shilingi 4.4 bilioni kwa ajili ya kura ya maoni ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, shilingi 220 milioni kwa ajili ya kufanya maandalizi ya uchaguzi mkuu. Sasa kwenye mafungu hayo shilingi 80,000,000 na shilingi 220,000,000 nimeziona kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina maana yake zimetoka kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina Fungu 45 kwenye kitabu cha pili.

Lakini hizi shilingi 4.4 bilioni ambazo ni uratibu wa shughuli za kura ya maoni kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hatukuziona popote zaidi ya kitabu hiki cha bajeti ya Mhe. Waziri. Sasa sielewi kama ni Mfuko Mkuu wa Hazina zimeingia huko au ziko kwenye *capital* au kwenye *recurrent*. Sasa naomba maelezo ya Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, anavyosema Mhe. Hija Hassan Hija ni sahihi, na kwa sababu na hapa vile vile lilitokea tatizo la wenzetu kutwambia katika dakika za mwisho, kwa hivyo ule utaratibu wa kutaarifu mapema wenzetu wa Wizara ya Fedha haukufanyika. Kwa msingi huo basi, tupitishe hili fungu ambalo lipo rasmi na limo kwenye kitabu na lile fungu jengine basi hapo wakati utapofika taratibu zitatumika kwa sababu zinatoka katika mfuko wa SMT tutawasiliana na wenzetu wa Wizara ya Fedha tuweke utaratibu utakaowezesha ili shughuli yetu ya kura ya maoni iweze kufanyika.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nimeelewa lakini *reference* zetu sisi nadhani ni lile fungu la bajeti. Sasa kitabu kikubwa sijui Wizara ya Fedha itatuwekea vipi sawa. Kwa sababu maandishi hayaendi sambamba na kitabu ambacho kimekuwa ni kumbukumbu. Sasa namuomba Mhe. Waziri labda anielekeze tu *reference* iwe ipi, *reference* iwe ile ya hotuba yake ya bajeti ambayo anayo yeye shilingi 4.4 bilioni au *reference* tuweke hili fungu kubwa la bajeti ambalo limeangaliwa na Idara ya Bajeti yenyewe ambalo kuwa ndio husika kwa ajili ya bajeti hii?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ni utaratibu ule ule wa uaminifu na kutokana na maelekezo ya Baraza letu hili kwamba mambo tunayoyafanya tuyaseme. Pia tulikuwa na woga wetu kwamba tusingeripoti halafu tukapata fedha hizo zikatumika vile vile ingekuja *query* baadae.

Kwa vyovyote vile masuala bado yatakuwepo, lakini sisi kile ambacho tumewaambia ilibifi tukieleze lakini kwa ufupi wenzetu wa Wizara ya Fedha watambue hiki kilichoandikwa hapa. Kwa hivyo tuendeleeni na kilichoandikwa hapa na hizo za kura ya maoni pale taratibu zikikamilika basi siku zote nafikiri wazee wa Wizara ya Fedha hawa watatupa taratibu za kuweza kuzipokea fedha hizo na kutuwekea utaratibu wa kuzitumia kwa mujibu wa malengo yenyewe na wakati huo huo Baraza litakuwa limeelewa kwamba kuna fedha zitatumika kwa ajili ya kufanyia kura ya maoni. Kwa sababu kama hatukuwa na fedha hizo maana yake kura ya maoni Zanzibar haiwezi kufanywa. Sote tunajua umuhimu wa Katiba na hali iliyofikia, mahitaji tunaoyafanya na kila siku tunazungumzia kutafuta ufumbuzi wa kuwa matatizo yanayojitokeza katika Muungano wetu.

Mhe. Mwenyekiti, moja ya njia ya kutafuta ufumbuzi huo ni kufanya kura ya maoni ili wananchi waweze kukamilisha maoni yao kwa usahihi wa kidemokrasia. Kwa hivyo, ni suala la kulitaarifu Baraza likaelewa kwamba upo utaratibu wa namna hiyo. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee kwa sababu sina wasi wasi na Tume nilikuwa nataka hili fungu tulielewe tu liko wapi. Kwa hivyo naomba tuendelee.

Kifungu 0201	Utawala Unguja	3,594,000,000/=
Jumla ya Fungu		**3,594,000,000/=**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

TAARIFA

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, UIchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, kufuatia kidogo kauli mbili tofauti baina yangu na Mwenyekiti wangu kuhusiana na miradi, fedha kwa ajili ya majimbo, kwa heshima yako naomba nikukabidhi ripoti yangu hii niliyoiwasilisha kwenye kikao na humu ndani kuna *figure* ambayo nimeitamka. Naomba Katibu uje uchukue umkabidhi Mhe. Mwenyekiti, ili kwa upande wangu yatakuwa yamekwisha kwamba sina dhamana tena ya kumletea Mhe. Mwenyekiti ripoti yangu. Naomba Katibu mkabidhi Mhe. Mwenyekiti, hii.

Mhe. Mwenyekiti: Hebu isome hiyo *figure* yenyewe.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: *Figure* niliyonayo hapa ni shilingi 760,000,000/-. Kwa hivyo, namuomba

Katibu na Mwenyekiti wangu naye atawasilisha ya kwake kama ndio ile ile niliyompa au nimempa nyengine hii ndio ripoti yangu 760 milioni.

Mhe. Mwenyekiti: Maelezo ni yale yale kwamba hali ya uchumi itapoimarika itazingatia suala hili. Kwa hivyo tunarejesha Baraza.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwahoji baada ya kazi nzuri sana mliyoifanya, wale wanaokubaliana na makadirio haya wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni kwa kazi kubwa mliyoifanya, imekwenda vizuri kwa utulivu na hakuna ziada zaidi ya sasa niakhirishe kikao hiki hadi kesho tarehe 25 saa tatu barabara za asubuhi.

(Saa 4:10 usiku Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 25/06/2013 saa 3:00 asubuhi)